# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 23 Mei, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. HAMISI S. TALETALE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu. *(Makofi)*

Sasa namwita Mheshimiwa Joseph Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, pamoja na uwekezaji mkubwa sana wa Serikali kwenye sekta ya elimu, matokeo ukiyaangalia kwa mfano wale wanaosajiliwa wa darasa la kwanza, wale wanaomaliza darasa la saba wanakuwa wachache. Kuna wanafunzi ambao hawamalizi darasa la saba, halafu ukiangalia wanaoanza *form one* na wanaomaliza *form four,* wale wanaomaliza *form four* kuna wanafunzi hapo katikati wanaacha shule hawamalizi shule ukiacha wale wanaofariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba wale wanaoanza shule angalau wote wanamaliza shule ukiacha wale wanaofariki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kwenye sekta ya elimu Serikali imefanya uwekezaji mkubwa wa kujenga miundombinu na ni kutoka ngazi ya awali mpaka vyuo vikuu na tumeanza kushuhudia watoto wengi wa Kitanzania wanapata nafasi za kusoma kwenye ngazi hizi husika na nikiri kwamba idadi ya wanafunzi wanaosajiliwa kuanza masomo siyo sawa na idadi ya wanafunzi wanaomaliza masomo kwenye ngazi hizo iwe ni elimu ya msingi hata sekondari na hasa sekondari ya kidato cha kwanza mpaka cha nne, ila kidato cha tano na sita kuna unafuu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tunaendelea na kuimarisha mahudhurio ya vijana wetu kwenye ngazi hizi zote kwa mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, tunaendelea kuzungumza na jamii yetu na hasa wazazi kuhakikisha kwamba kila mzazi anasimamia mahudhurio ya mtoto wake kwenda shule, kuingia darasani, lakini anaporudi lazima afuatilie mwenendo wa masomo ya mtoto huyu ili ajiridhishe kama mwanafunzi alishaenda shuleni. Bado kwenye ngazi za sekondari ambako pia vijana wetu wana umri ule ambao ni kati ya miaka 12 na kuendelea huku tunaimarisha na ujenzi wa mabweni pamoja na hosteli kwa ajili ya wavulana na wasichana waweze kulala huko huko shule, wasome hapo, wacheze pale pia na huduma nyingine na usimamizi wa maadili yao uweze kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua tuna utoro ambao pia unajitokeza ikiwemo tatizo la mimba kwa wasichana wetu kwa kujenga mabweni itasaidia zaidi kuhakikisha kwamba tunawalinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mkakati huu tunaoendelea nao tunaendelea kuimarisha pia hata sheria tulizonazo za kudhibiti utoro kwa vijana wetu na hasa kwa wazazi ambao wana wajibu wa kumlea mtoto huyu. Tumetoa maelekezo kwenye ngazi ya halmashauri za wilaya ambako ndio kuna shule za msingi na sekondari, tumetoa maelekezo kwenye ngazi ya mkoa kufanya ufuatiliaji na tumeimarisha pia ukaguzi kupitia

taasisi yetu ile ya ukaguzi ambayo sasa hivi inaitwa Udhibiti Ubora. Moja kati ya jukumu ambalo anatakiwa kulifanya ni kuhoji idadi ya wanafunzi waliosajiliwa, waliopo darasani na hawapati sababu za kwa nini hakuna vijana wengine darasani kulingana na usajili ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi tunazoendelea nazo tunaamini kwamba utoro utapungua na kuona kuwa wanafunzi waliosajiliwa angalau iweze kufikia zaidi ya 95% mpaka 98% ya wanaomaliza shule kwa sababu tunajua yako matatizo ya vifo na matatizo mengine ambayo huwezi kuyazuia na kwa hiyo, kazi hiyo inaendelea na kwa maelekezo tuliyoyatoa kwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kusimamia kwenye ngazi zao tunaamini hatua hii itaenda vizuri, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Noah Mollel.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa unayofanya ya kupambana na ubadhirifu wa mali za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwepo na urasimu na usumbufu wa utoaji wa huduma kwa wananchi kwa baadhi ya taasisi za Serikali jambo linalopelekea kuashiria kuwepo kwa dalili za rushwa na kupunguza imani ya wananchi kwa taasisi hizo na Serikali kwa ujumla, je, nini kauli na mkakati wa Serikali katika kukabiliana na hali hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lemburis Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba rushwa ni adui wa haki na inachangia sana kudhorotesha maendeleo pale ambapo vitendo hivi vinaendelea, lakini pia kutenda rushwa ni kosa la kijinai na ziko sheria zinabana wale wote wanaojihusisha na utoaji na upokeaji wa rushwa hapa nchini. Tunayo taasisi inayosimamia na kupambana na rushwa hapa nchini ambayo ni TAKUKURU.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAKUKURU imeunda sheria na sheria tunazo. Waheshimiwa Wabunge mmeshiriki katika kuimarisha na kutunga sheria hizi na wasimamizi wote kwenye taasisi iwe za umma au binafsi wanapaswa pia kupambana dhidi ya wale wote wanaoomba na kupokea rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali katika hili kwanza ni kusimamia taasisi zetu na kuimarisha sheria hii mahali panapoombwa rushwa. Rushwa mara nyingi ni kitendo cha mtu mmoja mmoja au vikundi vichache haviwezi kuharibu sura ya taasisi na hasa taasisi ikisimamia jambo hili kutoka mahali taasisi ilipo.

Kwa hiyo, mkakati wetu ni kuimarisha sheria, lakini kusimamia sheria na kuchukua hatua kali dhidi ya wale wanaojihusisha na ulaji rushwa na kupokea rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka niwahakikishie kwamba, Serikali inaendelea kusimamia eneo hili na kukemea vikali na kuchukua hatua dhidi ya wala rushwa na wapokeaji rushwa kwa sababu rushwa ni moja kati ya jambo linalochangia sana kudhorotesha maendeleo kwa jamii na hasa katika utoaji wa huduma kwenye maeneo yetu ya taasisi ambayo yanatoa huduma hizi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali itaendelea kutoa elimu kwa jamii ya kila mmoja kuhakikisha kuwa anakuwa mlinzi wa wale wote ambao wanatenda matendo hayo ya ulaji rushwa na kuchukua hatua pale ambako rushwa imeonekana dhahiri.

Baada ya uchunguzi ukibaini hatua kali zinatolewa, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edwin Swalle.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia inabadilika sana katika mambo ya uchumi, teknolojia na sayansi nakadhalika na sisi kama Taifa pia tumepiga hatua kubwa sana katika mambo mengi ya sayansi, uchumi na ustawi wa jamii, lakini tumekuwa na sheria nyingi za muda mrefu na sera za muda mrefu kama Taifa ambazo baadhi yake zimepitwa na wakati. Kwa mfano, tumekuwa na Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Viwanda ya Taifa ya mwaka 1967, tumekuwa na Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda ya mwaka 1979 na sheria nyingine nyingi na sera za miaka ya 1970 na 1980 ambazo nyingi zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni upi mpango wa Serikali wa kuhuisha hizi sheria nyingi na sera ziendane na hali ya sasa ya nchi yetu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Swalle, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri, kubwa mnayoifanya ya kufanya mapitio na kupitisha sheria zetu hapa Bungeni na ninyi ni mashahidi Serikali yetu imekuwa ikileta mabadiliko ya sheria mbalimbali, kanuni na tunazipitisha. Tunashukuru kwa sababu mnaendelea kutushauri Serikali kwenye maeneo ambayo mnagundua kwamba kuna udhaifu na kuweza kukazia kwa kuweka sheria na kuimarisha uwekaji wa kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko kazi inaendelea ndani ya Serikali kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na ile Tume yetu ya Marekebisho ya Sheria kufanya mapitio ya sheria zote ambazo zinaonekana zimepitwa na wakati kama ambavyo Mheshimiwa ameeleza. Zoezi hili linapitia maeneo yote ya kisekta ili kuona kuwa pale ambapo kuna udhaifu wa sheria katika utendaji wake tunachukua, tunaorodhesha na kuifanyia kazi na kupitia Kamati ya Bunge ambayo pia inashughulikia masuala ya sheria na yenyewe pia inatuongoza kwa sheria zote zilizopitwa na wakati kwenye sekta mbalimbali na kuziorodhesha na kuzileta hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie kwamba Serikali tupo tayari kupokea sheria zote ambazo zinaonekana zimepitwa na wakati katika utekelezaji ili tuweze kufanya marekebisho na sisi tunaendelea na tunashukuru kwa ushirikiano ambao mnatupa Waheshimiwa Wabunge kufanya mapitio haya ya sheria, kupitia kazi inayoendelea sasa na kama kuna sheria ambazo zimepitwa na wakati basi tunakaribisha maeneo hayo ili tuweze kuongeza kwenye orodha ya sheria ambazo zimepitwa na wakati ili tuweze kuzifanyia kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipatia niweze kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Desemba, 2021 Serikali yetu ya Tanzania iliingia makubaliano na nchi nne ambazo zinazunguka Ziwa Tanganyika kwa ajili ya kupumzisha Ziwa Tanganyika kutokana na athari za uvuvi haramu na azimio hilo walikubaliana kwamba kila tarehe 15 Mei tutapumzisha hilo ziwa mpaka tarehe 15 Agosti, lakini Bunge lako Tukufu tarehe 14 Mei tuliazimia kwamba na tamko la Wizara kwamba waende kutekeleza hilo agizo, lakini mpaka sasa nazungumza ndani ya Bunge lako Tukufu ni nchi mbili kati ya nne ambazo zinatekeleza hilo agizo kutokana na sababu tofauti ikiwemo mafuriko na nchi yetu pia tumepata mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu hatuoni sasa kwa kuwa agizo hilo halijatekelezeka na nchi nne na wanaoumia ni Watanzania na wao wamepata mafuriko na wanategemea uvuvi kama uchumi wao. Hamwoni kuna haja ya kusitisha hili jambo sasa mkakae tena ili mwone namna bora kutekeleza azimio hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Tanganyika ni kweli linatoa huduma za uvuvi na hata usafiri wa nchi nne ambazo ni Tanzania, Burundi, Kongo na Zambia. Nchi hizi kwa pamoja tunayo mahusiano ya kidiplomasia ambayo tunayaweka pia mikataba mbalimbali ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kwa kutumia ziwa hili na kwa maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameeleza maana yake inagusa maeneo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameshauri Serikali kwa namna yake kwamba upo umuhimu wa kupitia sheria hii na utekelezaji wake ambao pia tunakubaliana kwa pamoja, basi nataka nichukue maeneo haya ambayo nitafanya ufuatiliaji wa maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge amebaini ili tuweze kuitisha vikao vyetu vya kidiplomasia kwenye hizi nchi nne, tufanye mapitio ya makubaliano tuliyoyaweka, tuone mapungufu na hayo maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge amebainisha nayo tutayaweka kwenye orodha, halafu tuzungumze kupitia utaratibu tuliojiwekea na kuweka utaratibu mpya na kuweka msisitizo thabiti wa namna ya kushughulikia changamoto zilizopo kwa sasa, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Asia Abdulkarimu.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha watoto wote wa kitanzania wanapata elimu aliamua watoto wa kike waliopata ujauzito waweze kurejea shuleni, licha watoto wa kike kurejea shuleni aliamua kuendeleza programu mbalimbali zitakazowasaidia watoto waliopata ujauzito, lakini zoezi hili limekuwa likisuasua sana.

Je, ni mpango upi wa Serikali kuleta sheria Bungeni ili kufanya marekebisho na jambo hili lisiwe la hiyari liwe la lazima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa najibu swali la awali lililokuwa linazungumzia suala la utoro, nilidokeza kidogo kwamba kuna eneo ambalo tunalipitia ambalo lina kasoro. Wanafunzi wanaoingia na wanaomaliza ni tofauti, tuna kundi la watoto wetu wa kike ambao pia hukwama katikati kwa kupata ujauzito. Nataka kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye katika kipindi chake cha uongozi wa miaka hii mitatu kati ya mambo makubwa ambayo ameyafanya ni kuelekeza watoto wote wa kike waliopata ujauzito lazima utaratibu ufanyike warudi shuleni na waendelee na masomo yao ili waweze kufikia ndoto zao walizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa tunaendelea na utekelezaji huu, sasa hivi Wizara ya Elimu inafanya mapitio ya Sera yake ya Elimu. Moja kati ya maeneo ambayo tunayaweka na kuyafanyia kazi ni pamoja na kuimarisha maelekezo ambayo yatakwenda kutunga sheria yake na kanuni za namna ya watoto waliopata

ujauzito wakaacha shule, kurudi shuleni. Sasa hilo halitakuwa ni matakwa ya mtu, itakuwa ni matakwa ya kisheria pamoja na kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kulifanyia kazi kupitia mabadiliko ya Sera ya Elimu ambayo inaendelea kwa sasa na moja kati ya vipengele vitakuwa ni hivyo. Kwa hiyo, tunaamini mabinti zetu wanaopata ujauzito ambao hata sasa wakipata ujauzito mamlaka za mikoa na wilaya zinaendelea kufuatilia mienendo hii na kuwarudisha shuleni, lakini muhimu zaidi ni pale ambako tunaenda kuweka sheria ili jambo hili lisiwe hiyari ya mtu yeyote kulitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote niwahakikishie kwamba mabinti zetu kwenye maeneo yetu wale wanaopata ujauzito watapata nafasi ya kuendelea na masomo yao ili waweze kukamilisha ndoto zao na waweze kuendelea na ngazi zao za masomo kwa maslahi ya Taifa letu, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukuaji wa sekta ya elimu na ongezeko la shule binafsi kumepelekea ongezeko la huduma ya usafiri kwa wanafunzi kupitia mabasi maalumu na tumeona kwamba kuna athari nyingi. Je, Serikali haioni haja ya kutunga sheria inayolinda usalama kwa magari yote yanayosafirisha wanafunzi nchini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nancy, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo sheria za vyombo vya usalama vyote, vyombo vyote vya moto ikiwemo na mabasi yanayobeba wanafunzi. Sheria hizi zinatakiwa kufuatwa kwa ajili ya usalama wa abiria wakiwemo watoto wetu, lakini kwenye eneo hili la mabasi ya wanafunzi tumeongeza kanuni ambazo zinawabana wamiliki wa shule kuimarisha mabasi yao na yaweze kutambulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, lazima tuwe na dereva ambaye ana sifa ya kuendesha mabasi ya abiria na kubeba vijana wetu na pili, mabasi hayo ya wanafunzi tumelazimika kuyawekea kanuni ya kwamba lazima yapakwe rangi ya njano ili popote linapopita lazima lijulikane kwamba hili ni basi la shule na liwe na maandishi makubwa ubavuni na mbele ikionesha kwamba ni basi la wanafunzi *(school bus)* na tumeanza kuona utekelezaji huo unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado tunajua tuna shule zina watoto wa kike na wavulana kila inapofanya safari basi hili kwenda kuwafuata wanafunzi na kuwapeleka shule ni lazima liwe na walezi wawili, mwanamme na mwanamke kwa ajili ya usalama wa watoto wetu na panapotokea dharura kama ni ya mtoto wa kike basi yule mlezi wa kike atafanya hivyo na hata wanapowapeleka likizo ni lazima wanafunzi hao wasindikizwe mpaka wawakabidhi kwa wazazi wao. Kwa hiyo, eneo hili tunaenda kulisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa ambayo inafanywa sasa ni kufanya mapitio kwa kuwa na vikao vya pamoja kati ya Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI na wadau waliowekeza kwenye sekta ya elimu na Serikali imetoa fursa kwa Watanzania kuwekeza kwenye sekta ya elimu na tumepata mafanikio makubwa. Tuna shule za awali, shule za msingi na shule za sekondari nyingi za sekta binafsi na tunaendelea kufuatilia masharti yote ambayo tumeyaweka kwenye vyombo hivi vya usafiri kwa usalama wa watoto wetu, lakini kwa sheria zote zinazosimamia vyombo vya moto kwa ajili ya usalama wa abiria wetu ambao wanatumia mabasi haya, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Stella Simon Fiyao.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya hifadhi hawana elimu ya kutosha kuhusu sheria inayowakataza kuingia katika maeneo ya hifadhi kwa shughuli mbalimbali zikiwemo za kiuchumi, ikiwemo kurina asali kwa njia ya asili, kuokota kuni, kuchunga mifugo na mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu hii imepelekea wananchi wengi wanapoingia kukumbwa na kukutana na adha mbalimbali, lakini sababu hii imepelekea wananchi kuingia katika migogoro na mapambano mara kwa mara ambayo yamepelekea madhara makubwa ikiwemo wananchi kuumizwa, wengine kuuawa, wengine kupotea katika maeneo ya hifadhi na mambo mbalimbali na wengine kuumizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua mpango wa Serikali ni upi kutoa elimu kwa umma wote wa Watanzania ili waweze kufahamu vizuri sheria hizi, lakini pia wananchi wawe ni sehemu ya kulinda maeneo ya hifadhi ili kuepusha haya mambo ambayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara? Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Fiyao, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wanaoishi kando kando ya maeneo yote yaliyohifadhiwa kisheria. Wamekuwa wakisaidia ulinzi mbali ya changamoto zilizojitokeza, lakini kazi yao Serikali tunaiona na tunakiri kwamba wanao mchango mkubwa wa uhifadhi kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi hawa wanaoishi kando kando ya hifadhi kwa lengo la kupunguza migogoro kwa kiasi kikubwa kati ya wananchi wenye matamanio ya kufanya shughuli za kijamii, lakini pia pamoja na wahifadhi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo sasa tunafanya kwanza tunaimarisha kuweka alama kwenye mipaka iliyowekwa kisheria kwa kuweka *beacon* na sasa tumesema *beacon* zetu ziwe ndefu, halafu tupake rangi nyeupe kiasi cha kwamba inaweza kuonekana kwa umbali. Tumeanza kazi hiyo eneo la Loliondo kule Wilayani Ngorongoro tumeweka *beacon* ndefu na zinaonekana na ni rahisi pia na hata watumiaji kuona kwamba hapa ni ukomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, tunaendelea kutoa elimu kwa kushirikiana na zile Kamati za Mazingira za kila Kijiji na Serikali za Vijiji juu ya uhifadhi, pia na mipaka yetu na kwamba wao sasa nawapa nguvu ya kusimamia kwenye maeneo yao. Kwa hiyo, kwa njia hii ya kutoa elimu ambayo pia tunahusisha vyombo vya habari, *television* na redio katika kuwakumbusha wananchi hii tunaendelea nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kazi nyingine ambayo tunaifanya ni kuhakikisha kuwa tunajenga mahusiano ya karibu kabisa kati ya wananchi na wahifadhi wawe wanazungumza lugha moja pale ambapo kunakuwa na changamoto ya aina yoyote ile ya uhifadhi kwenye mbuga zetu au maeneo yote yaliyohifadhiwa. Kwa kufanya hilo wanajenga mahusiano ya kulinda kwenye mipaka yetu ambayo pia tumeshaweka na alama na tunaendelea na kazi hiyo, lakini pale ambapo kunatokea tatizo basi tunazungumza pamoja kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia hili, Mheshimiwa Mbunge ameeleza kwamba liko tatizo huko na sisi tunakiri kwamba yako matatizo baadhi ya maeneo. Nitoe wito kwa wahifadhi wote wanaolinda maeneo yaliyohifadhiwa kisheria kuendelea kujenga mshikamano na wananchi na Serikali za Vijiji kwenye maeneo yao, kujenga tabia ya kuzungumza pamoja pale ambapo tatizo

linatokea badala ya kuchukua hatua ambazo wakati mwingine zinaleta madhara na kuleta usumbufu Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaamini sasa Wizara husika ya Maliasili na Utalii ambayo ina maeneo haya ya uhifadhi, lakini pia hata halmashauri zetu ambazo zina misitu yake ya uhifadhi wote hawa waandae utaratibu ambao unaweza kukutanisha wananchi na wahifadhi wetu na kutoa elimu ya jumla kwa lengo la kusimamia hifadhi zetu na maeneo yote yaliyohifadhiwa ili yalete manufaa, hata wananchi walioko kando kando ya misitu nao wafaidike na uwepo wa maeneo hayo yote yaliyohifadhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zaytun Swai.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Bunge limekuwa likitunga sheria mbalimbali na kukasimu kwa Mamlaka za Serikali utungaji wa kanuni za sheria husika. Mheshimiwa Waziri Mkuu kanuni hizi zimekuwa zikitungwa bila kushirikisha wadau na hivyo kusababisha taharuki wakati wa utekelezaji wake, kwa mfano tu hivi karibuni kwenye sekta ya utalii nchi nzima kumekuwa na taharuki baada ya kuanzisha tozo mpya ya waongoza watalii kuingia mbugani, lakini vilevile kuendelea kutoza leseni kwa dola kinyume na matamko mbalimbali ya Serikali. Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusu jambo hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Swai alirudie tena swali lake nipate kulielewa vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Swai, rudia swali lako polepole acha jazba.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Bunge limekuwa likitunga sheria mbalimbali na kukasimu kwa Mamlaka za Serikali husika utungaji wa kanuni za sheria hizo.

Utungaji wa kanuni umekuwa ukifanyika bila kushirikisha wadau na hivyo kusababisha taharuki wakati wa utekelezaji wa kanuni hizo. Kwa mfano tu Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi karibuni katika sekta ya utalii kumekuwa na taharuki kubwa nchi nzima ambapo wamewekewa tozo mpya ya kuwaongoza watalii kuingia mbugani *(park fees),* lakini vilevile wameendelea kutozwa leseni zao kwa dola kinyume na matamko mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusu jambo hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Swai, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Arusha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kulishukuru Bunge lako Tukufu ambalo wakati wote limekuwa likifanya kazi ya kutunga sheria, lakini pia sheria hizi zimekasimiwa pia kwa Serikali kupitia taasisi husika katika kutengeneza kanuni mbalimbali ambazo zinakwenda kwa ajili ya utekelezaji. Mheshimiwa Mbunge ameeleza kwamba ziko sheria ambazo pia zinazalisha kanuni ambazo katika utekelezaji wake zinaleta mgongano kutoeleweka, lakini malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utungaji wa sheria na utengenezaji wa kanuni ili sheria iweze kutumika ni kitendo kinachofanyika kwa kushirikisha. Tunashirikisha wadau walaji wa sekta hiyo kama ni sekta ya elimu huwa tuna utaratibu wa kuwaita wadau wa elimu kuweza kuimarisha sheria na kanuni zake ili tuweze kukubaliana zinapokwenda kwenye utekelezaji kusiwe na changamoto za kuzidi kiasi.

Kwa hiyo, tutaendelea kushirikisha wadau katika sekta ambayo tumeanza kuiweka sheria na inahitaji kuweka kanuni ili kuondoa malalamiko tunapoanza kuzitumia. Endapo hatua zote hizi zimepitiwa, sheria imetungwa ndani ya Bunge mmekasimu kwa Serikali tunatengenezea kanuni ambazo pia tumewashirikisha

wadau na inaonekana kwenye matumizi yake kuna shida ambayo bado haijatatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tumefungua milango kuleta sheria hizo na kanuni hizo ili tufanye mapitio tena kwa pamoja na niwaahidi wadau ambao tunafanya nao kazi kuendelea kuwashirikisha katika kutengeneza kanuni ambazo zitaendelea kutumika ili zinapotumika zilete maslahi kwa waweka kanuni, lakini pia kwa watumiaji wa kanuni hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niendelee kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali milango yake iko wazi kujulisha kanuni ambazo utekelezaji wake bado unashida. Vilevile nitoe wito kwa wadau wasisite kutuletea kanuni ambazo zinaleta ukakasi katika kutumia sheria hizo na zinaleta tatizo katika matumizi ili tuweze kufanya mapitio na marekebisho twende tukazitumie ili pande zote tuweze kunufaika nazo. Kwa sisi wasimamizi lakini pia na watekelezaji wa sheria hizo, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana huyo ndiyo msemaji wa mwisho. *(Makofi)*

Hiyo inaitwa majibu kwa viwango, ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Francis Ndulane.

Na. 416

**Ujenzi wa Vituo vya Afya - Kilwa Kaskazini**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kujenga Vituo vya Afya Kata za Kandawale, Kibata, Namanyuni, Mingumbi na Kirojumbi – Kilwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2023/2024 Serikali imepeleka jumla ya shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali ya wilaya, ujenzi wa vituo viwili vya afya na ukamilishaji wa maboma 12 ya zahanati katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Kilwa itatenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Kandawale. Aidha, Kata za Kibata, Namanyuni, Mingumbi na Kinjumbi zitajengewa vituo vya afya kwa awamu kwa kuzingatia mahitaji na vigezo vilivyoainishwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningeomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Kata ya Kandawale ni kata ya kimakakati ambayo imeorodheshwa kupewa fedha za ruzuku ya Serikali Kuu ya maendeleo ili iweze kukamilika. Je, ni lini fedha hizo zitafika ili zikiungana na shilingi milioni 100 za halmashauri ziweze kukamilisha kituo hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tumekuwa na mfumo wa *MUSE* ambao umeanza kutumika hivi karibuni, umefanya malipo kwa miezi sita sasa ya fedha za Mfuko wa Jimbo na fedha za *MSD* zisilipwe jumla ya shilingi milioni 848 katika Wilaya ya Kilwa.

Je, Serikali imejipanga vipi kutukwamua na malipo haya ili shughuli za ununuzi wa vifaa tiba, dawa pamoja na umaliziaji wa Kituo cha Afya cha Chumo uweze kukamilika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini kwa namna ambavyo amefuatilia sana ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya kimkakati ya Kandawale. Ni kweli tulishakiingiza kituo cha afya katika Kata ya Kandawale kwenye mpango wa vituo vya afya vya kimkakati na nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kufanya utaratibu wa kutafuta fedha na kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha mapema iwezekanavyo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kandawale. Kwa hiyo, halmashauri itatenga shilingi milioni 100 kama sehemu ya utekelezaji wa mradi huo na Serikali Kuu tutaendelea kutekeleza kwa kupeleka fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto ya Mfumo wa *MUSE* katika malipo na Serikali inatambua changamoto hiyo na inaifanyia kazi. Kwa hiyo, sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutawasiliana na Wizara ya Fedha - Hazina ili tuweze kuongeza *speed* ya kushughulikia changamoto hiyo ili malipo ya fedha za dawa, Mfuko wa Jimbo na malipo mengine yaweze kwenda vizuri na kuboresha huduma kwa wananchi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali ya nyongeza yawe mafupi leo ni Alhamis tuna nusu saa tu ya maswali. Mheshimiwa Samweli, ajiandae Mheshimiwa Amar.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, je, Serikali itapeleka lini fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Balangdalalu na Hidet ambayo nimeshaiomba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaweka mpango wa ukamilishaji wa vituo vya afya na hatimaye kujenga vituo vya afya ambavyo vimeainishwa na nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutapeleka katika kata hiyo ambayo umeiainisha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa kuwa Jimbo la Nyang'hwale lina kata 15 na kata hizo zinapata huduma ya *x-ray* kwenye Hospitali ya Wilaya pale Kharumwa. Kata saba ziko mbali na huduma hiyo zaidi ya kilometa 30 mpaka 60. Kata hizo ni Shabaka, Kaboha, Busolwa, Nyang'hwale, Nyijundu, Nyabulanda na Mwingiro.

Je, Serikali haioni haja sasa ya kutenga fedha kununua *x-ray* na kwenda kuwafungia katika kituo cha afya kilicho katikati kinaitwa Kituo cha Afya Nyang'hwale na je, Serikali iko tayari?

**NAIBU SPIKA:** Waziri jibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko tayari na nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale atuletee taarifa rasmi ya mahitaji ya mashine ya *x-ray* na kama jengo lipo ili tuweze kupeleka kifaa hicho katika kituo hicho cha afya.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Mtemvu.

Na. 417

**Kituo cha Afya Kata ya Kibamba**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kituo cha afya katika Kata ya Kibamba?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kujenga vituo vya afya katika kata za kimkakati kote nchini ikiwemo Jimbo la Kibamba. Katika kipindi cha mwaka 2022/2023 Jimbo la Kibamba lilipelekewa shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya vya Goba na Amani. Ujenzi wa vituo hivyo umekamilika na vituo vinatoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo itatenga shilingi milioni 252 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Kibamba, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa majibu yake hayo mazuri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa hapa Bungeni tayari nimeshajibiwa changamoto ya maboma ya Saranga na King'azi, maelekezo ya Serikali ni kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imalizie majengo hayo haraka ndani ya miezi sita; na kwa kuwa, Kata hii ya Kibamba ni ya kimkakati na wananchi wake wengi zaidi ya 70,000 wa Kiluvya, Gogoni, Kibamba, Kibwegere, wa Hondogo na wa maeneo ya Luguruni, wote hawa hawana huduma yenye hadhi ya kituo cha afya.

Je, Serikali hamuoni mnayo sababu kwenye fedha zilizotengwa mwaka huu 2024/2025 za vituo vya afya na yenyewe mkazielekeza ndani ya kata hiyo ya kimkakati ili wananchi wapate huduma ya kituo cha afya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nashukuru kwa fedha shilingi bilioni 1.1 kwa Kituo cha Afya Goba, lakini na kupandisha hadhi Zahanati ya Amani pale Kwembe kuwa kituo cha afya, naishukuru sana Serikali lakini kwa kupandisha hadhi hivyo imesababisha kuwe na uhaba wa watumishi.

Je, Serikali hamwoni kuna haja ya kupeleka watumishi kama maombi yetu ya Halmashauri ya Wilaya ya Manispaa ya Ubungo yalivyoletwa katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI?

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mtemvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na maombi ya Kituo cha Afya cha Saranga alishauliza hapa mara kadhaa na mimi nikiwa na yeye tuliongea na Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo Ndugu Kagurumjuli tulikubaliana na Mkurugenzi ameweka *commitment* ndani ya miezi sita kama tulivyokubaliana Kituo cha Afya cha Saranga kitakuwa kimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumsisitiza tena Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo kuhakikisha anatekeleza makubaliano hayo.

Pili, kuhusiana na uhitaji wa watumishi, ni kweli kwamba Serikali imefanya kazi kubwa. Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kusogeza huduma za vituo vya afya karibu na wananchi kikiwemo Kituo cha Afya cha Goba na hiki cha Amani amekipandisha hadhi. Nikuhakikishie katika vibali vya ajira ambavyo vitatangazwa hivi karibuni tutahakikisha tunawapa

kipaumbele Halmashauri ya Ubungo na Jimbo la Kibamba kupata watumishi wa kutosha kwa ajili ya vituo hivi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Mpengele kina umri wa miaka saba sasa hakina jengo la *OPD*. Ni lini Serikali itatupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa *OPD* katika Kituo cha Afya cha Mpengele?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimsisitize Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale kwamba maelekezo ya Serikali wanatakiwa kutenga mapato ya ndani kuanza ujenzi wa majengo muhimu ya huduma za afya yakiwemo majengo ya *OPD*. Kwa hiyo, kituo hicho cha afya tunatarajia tuone Mkurugenzi ametenga fedha kwenye mapato ya ndani, lakini pale ambapo mapato ya ndani hayatatosheleza tupate taarifa rasmi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kuongeza nguvu na kukamilisha vituo hivyo.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Gulamali.

Na. 418

**Ujenzi wa Madarasa Shule za Msingi Manonga**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa madarasa Shule za Msingi Ikunguipina, Izimbili, Mwina, Itibula, Ndembezi, Chapela na Bulangamilwa – Manonga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa madarasa katika shule mbalimbali za msingi nchini kufuatia kuongezeka kwa mahitaji yanayotokana na ongezeko la wanafunzi. Tathmini iliyofanyika mwaka 2022/2023 ilibaini uwepo wa uhitaji wa shule mpya na nyongeza ya madarasa katika halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Serikali kupitia Mradi wa *BOOST* imejenga shule mpya 302 na kuongeza madarasa 3,350 ambapo katika Jimbo la Manonga shilingi milioni 543.9 zilitumwa kujenga shule moja mpya ya msingi ya mkondo mmoja katika eneo la Kiloleli, vyumba sita vya madarasa na matundu matatu ya vyoo kwenye Shule za Msingi Selegeyi na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024 Jimbo la Manonga litapelekewa shilingi milioni 238.4 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba nane vya madarasa na matundu 12 ya vyoo katika Shule za Msingi Igumila na Nyandekwa. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kutenga na kupeleka fedha kwenye shule nyingine zenye uhitaji zaidi wa miundombinu kwenye Jimbo la Manonga na majimbo yote nchini kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na napenda kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shule ambazo tumezitaja kwa maana ya Shule za Izimbili, Ikunguipina, Mwina, Itibula, Ndembezi, Chapela na Bulangamilwa ni shule ambazo zina madarasa manne na nyingine zina madarasa sita, katika majibu

ya Mheshimiwa Naibu Waziri hajaonesha kupeleka fedha katika hizi shule.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kuongeza madarasa katika hizi shule ili kupunguza msongamano wa wanafunzi katika hizo shule?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itafanya *operation* ya ujenzi wa vyoo katika shule zote za msingi nchi nzima ili kuhakikisha kwamba watoto wetu wanakuwa na maisha bora katika elimu zao za msingi? Ahsante.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lini Serikali...

**NAIBU SPIKA:** Subiri, Mheshimiwa Waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ana hoja za msingi sana na ninampongeza kwa kutetea wananchi wake, lakini naomba nimfahamishe kupitia Programu ya *BOOST* ambayo ni programu ya kuboresha elimu ya awali na elimu ya msingi, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za msingi, lakini na ujenzi wa madarasa. Kwa mfano, kama mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 230 kwa ajili ya shule mpya 302, madarasa 2,942 pamoja na ujenzi wa matundu ya vyoo 11,297.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama vile Serikali ambavyo imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha miundombinu na hasa katika shule zetu za msingi ili kupunguza msongamano. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge awamu hii tayari alishapewa shilingi milioni 543.9 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa shule zake chache na katika awamu inayokuja

tutaweka kipaumbele kutazama shule ambazo amezitaja ambazo na zenyewe zina uhitaji wa kuongezewa madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili kuhusu ujenzi wa vyoo, pamoja na kwamba Serikali kupitia miradi yake mbalimbali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwa ajili ya kuboresha mazingira na ujenzi wa vyoo katika shule zetu, lakini pia naomba nitumie fursa hii kukumbusha halmashauri wajibu wao wa msingi, wa kutenga fedha kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya kujenga miundombinu muhimu kama hii ya vyoo kwenye shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali pamoja na kutenga fedha, lakini pia kuna jukumu la halmashauri kuhakikisha na wenyewe wanatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hii muhimu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itakarabati na kuongeza madarasa mapya katika shule kongwe zenye hali mbaya zilizopo katika Jimbo la Newala Vijijini? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024 Serikali ina mpango wa kufanya marekebisho katika shule kongwe 50. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wakati wa utekelezaji au wakati wa kuhakikisha mgao huu unafika kwenda kwenye shule mbalimbali tutaiangalia Newala kwa jicho la kipekee.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kunambi.

Na 419

**Ujenzi wa Madaraja – Mlimba**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Madaraja ya Chiwachiwa, Mbasa, Isago na Mfuji – Mlimba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali kupitia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* imekamilisha kazi ya usanifu wa Madaraja ya Chiwachiwa, Mbasa, Isago na Mfuji – Mlimba ambapo jumla ya shilingi bilioni 4.5 zinahitajika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Madaraja ya Chiwachiwa, Mbasa, Isago na Mfuji katika Jimbo la Mlimba, fedha zitakapopatikana ujenzi utaaanza mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Madaraja haya ya Chiwachiwa, Mbasa, Isago na Mfuji ni madaraja yaliyojengwa kwa mbao na magogo na kutokana na mvua hizi za *El-Nino* madaraja yote haya yameharibika na hayawezi kupitika kwa sasa. Nini mpango wa Serikali wa kuyakarabati madaraja haya yaweze kupitika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Naibu Waziri uko tayari kuambatana nami kwenda Jimbo la Mlimba kushuhudia madhara haya? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge amekuwa ni mtetezi mkubwa sana wa wananchi wake na hasa kwenye masuala ya miundombinu muhimu ya barabara. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba Madaraja haya ya Chiwachiwa, Mbasa, Isago na Mpuji yanajengwa kwa viwango vikubwa zaidi na vya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tayari tathmini na usanifu umeshafanyika, Serikali inaendelea kutafuta fedha na kuhakikisha kwamba inakuja kujenga madaraja haya na yawe ni madaraja ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusiana na mimi kuambatana naye kwenda jimboni kwake kwenda kuona madhara makubwa ya mvua kwenye miundombinu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ameshaanza ziara katika Mkoa wa Morogoro, ameshapita kwenye baadhi ya majimbo, nikuhakikishie kwamba atakuja kwenye jimbo lako ili aje aone madhara makubwa ambayo yametokana na mvua nyingi zinazonyesha kwenye miundombinu ya barabara. Kwa hiyo, naomba nikupe hiyo *comfort* Mheshimiwa Waziri atakuja jimbo lako.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba Serikali inafuata Sheria ya Manunuzi, lakini nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, je, ni kwa nini sasa wasifanye manunuzi ya dharura kwenye barabara ambazo zimeharibika na mvua iliyopita katika Mkoa wa Dar es Salaam na majimbo yote ambayo zimepata pesa za *emergence?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kabla hujajibu ujue uchumi unategemea barabara. Mazao yanakwama kwenye mashamba, barabara siyo nzuri. Rais ametoa pesa za kutengeneza barabara, lakini wakurugenzi wanashindwa kwa sababu sheria zinawabana hapa na pale, lakini vipo vipengele vya kisheria vinaweza vikasaidia sheria ifuatwe na huduma za wananchi zipatikane, haya jibu sasa.*(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha na imefanya ongezeko la bajeti, Mheshimiwa Rais amefanya ongezeko la bajeti ya *TARURA* kutoka shilingi bilioni 210 kwenda shilingi bilioni 710. Pia kwenye fedha za dharura Mheshimiwa Rais ameongeza kutoka shilingi bilioni 21 kwenda shilingi bilioni 131, lakini kuna fedha maalumu za bajeti ya nyongeza ya shilingi bilioni 350 ambazo zote hizi zimetoka kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Serikali inaboresha miundombinu ya barabara zetu hizi za wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haitoshi hivyo tu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilishatoa maelekezo kwa halmashauri za majiji ili na zenyewe ziweze kutenga mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara, naweza nikatoa mfano, Jiji la Dar es Salaam tayari lilishapewa hayo maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nichukue nafasi hii kutoa maelekezo kwa halmashauri zote za majiji ambazo zilipewa maelekezo zitenge fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara sasa zichukue hatua za dharura kwa ajili ya kuanza ukarabati wa barabara hizo kwa sababu fedha zipo, zimeshatengwa na utaratibu wa dharura unafahamika, washirikiane na Mameneja wa *TARURA* kuhakikisha kwamba miundombinu hii inajengwa kwa maslahi mapana ya wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Maboto.

Na. 420

**Malipo ya Kifuta Jasho/Machozi Wahanga wa Wanyama Waharibifu**

**MHE. ROBERT C. MABOTO** aliuliza:-

Je, lini Serikali italipa kifuta machozi kwa wahanga wa wanyama waharibifu – Bunda Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa wilaya hii ambao wamekuwa wakipata changamoto ya uharibifu unaofanywa na wanyamapori wakali na waharibifu wamekuwa wakilipwa kifuta jasho/machozi kwa nyakati tofauti tofauti kadiri fedha zinavyopatikana. Mathalani, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 Serikali wamekwishalipa jumla ya shilingi 72,650,000 kwa wahanga 299 kutoka katika takribani mitaa 15 ya Halmashauri ya Mji wa Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii inaendelea kushughulikia madai mengine ya wananchi 1,111 kutoka katika Halmashauri ya Mji wa Bunda ambayo yamekwishawasilishwa Wizarani. Malipo yatafanyika mara tu baada ya taratibu kukamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Robert.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, kwa hiyo shilingi 72,650,000 ambayo imelipwa kwa watu hao 299 nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, bado watu 1,111 ambao hawajalipwa na hawa watu waliobaki ndiyo idadi kubwa kati ya watu waliolipwa? Swali la kwanza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni kwa nini Serikali isitengeneze utaratibu wa hao watu ambao wanapata madhara kulishiwa mazao yao katika halmashauri zao, kwa nini Serikali isipeleke fedha kwenye zile halmashauri husika ili halmshauri iwe inawalipa wale wananchi wake wanaokuwa wamepata matatizo hayo kwenye halmashauri hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye swali la msingi ni kweli tunao watu 1,111 ambao tumepokea madai yao, tupo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha tathmini ili tuwasiliane na wenzetu wa Wizara ya Fedha waweze kulipwa fedha hizi. Naomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa na subira kidogo tunakamilisha jambo hili na wananchi hawa watalipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kupeleka fedha kwenye halmashauri zetu, ni wazo zuri, lakini kama mnavyofahamu taratibu za fedha hasa fedha zinapotoka Wizara ya Fedha kule ni lazima kwanza tathmini iwe imefanyika. Kiwango halisi cha mahitaji ya fedha kijulikane, ndipo ambapo tunaweza kupeleka fedha hizi kwenye halmashauri. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge ucheleweshaji mkubwa wa malipo ya fedha hizi huwa unatokana na maafisa wanyamapori walioko kwenye halmashauri zetu kutokuwasilisha madai ya wananchi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kwa pamoja kuwakumbusha na kuwasukuma wataalamu wetu kule katika halmashauri wawasilishe madai haya kwa wakati ili wananchi waweze kupata stahiki zao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali italipa fidia/kifuta machozi katika Vijiji vya Hunyali, Kihumbu, Maliwanda, Sarakwa, Mugeta, Kyandege na Tingilima kwa sababu madai hayo yamekuwa ya muda mrefu na ziko shilingi milioni 316 mnadai, lini mtawalipa ndugu yangu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema ni miongoni mwa maeneo ambayo tumekamilisha tathmini ambapo takribani shilingi bilioni 2.3 zinahitajika, tumewasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha mara tu baada ya kupata fedha hizi wananchi hawa watapata malipo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amandus.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, katika Jimbo langu la Nachingwea, kifuta jasho kwa mara ya mwisho tumelipwa mpaka Oktoba, 2022. Nini mpango wa Serikali wa kulipa kwa wale ambao wameathirika kuanzia Novemba, 2022 mpaka sasa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema zipo fedha ambazo zinahitajika kulipwa takribani shilingi 1,300,000,000 kwa sasa. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira ili tuweze kukamilisha utaratibu huu na wananchi waweze kulipwa. Vilevile nimwombe kama anazo nyaraka za wananchi wake ambao hawajalipwa kwa kipindi hiki alichosema anisaidie kuzipata ili tuweze kuangalia kule Wizarani, tuweze kujiridhisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha 2022/2023 katika Wilaya ya Karatu, wananchi 111 wameharibiwa mazao yao na wengine kujeruhiwa na kufariki kutokana na wanyama wakali na waharibifu. Je, ni lini na wenyewe watalipwa fidia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hao watalipwa mara baada ya kukamilisha tathmini na upatikanaji wa fedha utakapokuwa umefanyika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Mifugo, Mheshimiwa Maige.

Na. 421

**Mafunzo ya Ufugaji wa Kisasa Ngazi ya Kata**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza: -

Je ni lini Serikali itaanzisha mafunzo ya ufugaji wa kisasa kwa wafugaji ngazi ya kata ili kuwa na ufugaji wenye tija?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikitoa mafunzo rejea kwa maafisa ugani na wafugaji ambao wanatoka katika kata na vijiji kutoka maeneo mbalimbali hapa nchini. Aidha, katika mwaka 2023/2024 jumla ya maafisa ugani 1,058 walipatiwa mafunzo rejea ukilinganisha na maafisa ugani 515 waliopatiwa mafunzo mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi imetoa mafunzo ya ufugaji bora kwa wafugaji 250,000 kutoka mikoa 12 nchini. Mafunzo hayo, yamelenga kuwajengea uwezo maafisa ugani na wafugaji ili kuongeza tija, uzalishaji na kuwa na ufugaji wa kibiashara unaolenga mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025 Wizara itaanza utekelezaji wa mradi wa miaka mitano wa mageuzi katika tasnia ya maziwa kwa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi. Kupitia mradi huu, mafunzo ya ufugaji wa kisasa unaozingatia mabadiliko ya tabianchi yatatolewa kwa wanufaika wapatao 600,000 katika mikoa mbalimbali nchini. Mradi huu utaongeza tija katika ufugaji hususani katika tasnia ya maziwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali ilijikita katika kufundisha maafisa ugani wake tu, je, Serikali itaanzisha lini mafunzo kwa ajili ya wananchi wafugaji vijijini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, vituo vilivyoitwa vya kufundisha wanyama kazi vilikuwa na manufaa sana kwa wakulima na wafugaji kupeleka wanyama kwenda kufundishia pale, lakini bahati mbaya vikatelekezwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua tena vituo hivi kama kile kilichopo Upuge, jimboni kwangu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba Serikali imeendelea kutoa mafunzo na mafunzo haya imekuwa ikiyatoa kwa maafisa ugani na wafugaji pia. Maafisa ugani wanapewa mafunzo ili wakawafundishe wafugaji wetu, lakini pia imekuwa

ikiwafundisha na wafugaji katika maeneo mbalimbali ya nchi kama nilivyosema katika jibu la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukitoa wito kwa wafugaji wote ambao wanahitaji mafunzo na Mheshimiwa Mbunge kama jimboni kwako kuna wafugaji ambao wanahitaji mafunzo, Serikali iko tayari kuja kuwafundisha wafugaji hao ili waweze kufanya ufugaji wenye tija katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili la vituo ambavyo vimetelekezwa, ni kweli kulikuwa na vituo ambavyo vilikuwa vikifundisha wafugaji namna ya kukaa na wanyama wetu na namna ya kuwafundisha wanyama wetu kwa ajili ya kufanya kazi. Vituo hivi vingi vimekufa na huo ni ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa tutatuma wataalamu katika jimbo lake ili kuainisha vituo vyote ambavyo vimekufa na vimetelekezwa kwa ajili ya kuvifufua ili viweze kutoa huduma ambayo Mheshimiwa Mbunge anahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko tayari kufanya hiyo kazi na vituo hivi ni vingi. Tukishapata idadi yake tuko tayari kuweka nguvu kurudisha huduma iliyokuwa ikitolewa katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamguna.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na wimbi kubwa la wafugaji katika Mkoa wa Morogoro, Serikali imejipangaje kutoa mafunzo katika ngazi za kata katika mkoa huo ili kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, ni kweli tumeshaanza kutoa mafunzo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Katika hali ya kupunguza migogogro ya wakulima na wafugaji tunaendelea kuhamasisha Serikali za Mitaa kupitia vijiji na halmashauri za wilaya kupanga matumzi bora ya ardhi ili kuondoa migogoro hiyo ya wakulima na wafugaji kwa sababu watu wamekuwa wakiishi bila ya kujua wapi anatakiwa kulima, wapi anatakiwa kuishi na wapi anatakiwa kufuga mifugo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mipango bora ya matumizi ya ardhi itatusaidia sana watu wetu kujua na kuainisha maeneo haya yanatakiwa yakae katika mpango gani ili kupunguza migogoro hiyo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi Wizara ya Mifugo kama wanufaika namba moja wa masuala ya mifugo tuko tayari kutoa ushirikiano kwa Serikali za Mitaa ili kuweza kupanga matumizi ya mipango bora ya ardhi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Furaha Matondo.

Na. 422

***Mafunzo kwa Beach Management Unit (BMU)***

**MHE. FURAHA N. MATONDO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itavipatia mafunzo vikundi vya *Beach Management Unit* ili kukabiliana na uvuvi haramu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeendelea kutoa mafunzo kwa Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi yaani *BMUs* kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha ambapo katika mwaka 2023/2024 Wizara kwa kushirikiana na shirika lisilokuwa la kiserikali la *Tanzania Nature Conservancy* yaani *TNC* imetoa mafunzo juu ya usimamizi wa rasilimali na athari za uvuvi haramu kwa wanachama 558 wa *BMUs* kutoka katika Vijiji vya Karungu watu 62, Mandakerenge watu 62, Mtakuja watu 62, Manda Uhuru watu 62, Mkinga watu 62, Tanganyika watu 62, Isasa watu 62, Kichangani watu 62 na Kipili watu 62 katika Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kutoa mafunzo juu ya athari za uvuvi haramu kwa viongozi 144 wa *BMUs* nane za Dunda (18), Kaole (18) Mlingotini (18), Kitame (18), Changuahela (18), Pande (18), Kisutu (18) na Kondo (18) katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo; Viongozi 108 wa *BMU* sita za Maloo (18), Mchinga I (18) Mchinga II (18), Kijiweni (18), Mvuleni Mashariki (18) na Ruvu (18) katika Halmashauri ya Mji wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatoa wito kwa wananchi na wavuvi wote hapa nchini kupiga vita uvuvi haramu ili rasilimali za uvuvi ziweze kuwa endelevu kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Furaha.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa hatua ilizochukua ila kwa Ziwa Victoria bado hatua hazijachukuliwa. Ziwa Victoria limekuwa na changamoto kubwa sana ya uvuvi haramu na hii inapelekea Serikali kukosa mapato na samaki kupungua. Viwanda vingi sasa vinafungwa kwa sababu uzalishaji umekuwa ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini kauli ya Serikali kuona sasa *BMUs* zinakwenda kuundwa na kupewa mafunzo ili ziweze kwenda kufanya kazi ya kuondokana na uvuvi haramu na Serikali

iweze kupata mapato, lakini changamoto ya uvuvi haramu iweze kuisha katika Ziwa Victoria. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kweli *BMUs* hizi zimekuwa zikifanya kazi nzuri sana katika maeneo mbalimbali hapa nchini hasa kwenye ushiriki wake kwenye kudhibiti uvuvi haramu. Ukweli ni kwamba katika Ziwa Victoria, *BMUs* hizi zimekuwa zina mchango mdogo kwa sababu ni chache na nyingi zimekufa, hazifanyi kazi nzuri katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya hapa tutatuma wataalamu kwenda Ziwa Victoria kwa ajili ya kwenda kuainisha maeneo ambayo *BMUs* hizi zitakwenda kuanzishwa ili ziweze kuanzishwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Furaha Matondo kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika maeneo hayo hasa kwenye kutetea *professionalism* yake ya uvuvi. Kwa kweli amekuwa na msaada mkubwa sana katika Wizara ya Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, swali la Mheshimiwa Ndingo linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Suma.

Na. 423

**Ujenzi wa Barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO K.n.y. MHE. BAHATI K. NDINGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga yenye urefu wa kilometa 151?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 151.1 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya meta 850 zimejengwa na katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya meta 470 zinaendelea kujengwa kwa sehemu ya Madibira - Rujewa ambapo ujenzi umefikia 10% na unategemewa kukamilika mwezi Agosti, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa meta 830 kwa sehemu ya Igoma hadi Kinyanambo A, kilometa 55.2 zinaendelea ambapo mkataba unatarajiwa kusainiwa mwishoni mwa mwezi Juni, 2024. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imekuwa ni ya muda mrefu sana kweye ilani za chaguzi, je, viongozi hamuoni haja sasa ya kutekeleza ahadi hiyo ili wananchi wa Mbarali waweze kufurahia barabara yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, barabara hiyo ni barabara ya mapato mengi sana kiuchumi, je, Serikali hamuoni kwamba kwa kuikosa barabara hiyo wananchi wa Mbarali, inapoteza mapato mengi katika Taifa hili la Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Jimbo la Mbarali, kwa Mkoa wa Mbeya na kwa Taifa zima na ndiyo maana barabara hii yote tayari imeshafanyiwa usanifu kwa maana dhamira ya Serikali ni kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami na ndiyo maana imesanifiwa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali inatafuta fedha imeona ni busara ianze kujenga kwa hatua hasa yale maeneo muhimu ambayo tunaona yana changamoto na ni kwenye sehemu za miji. Dhamira ya Serikali ni kuijenga yote kwa kiwango cha lami na kuhakikisha kwamba uchumi wa maeneo hayo na wananchi wanapata huduma bora ya usafiri na usafirishaji, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, tuna dakika kumi sasa. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Gallos.

Na. 424

**Kushughulikia Mashauri ya Ndoa kwa Wakati**

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kushughulikia kwa haraka mashauri ya migogoro ya ndoa ili kuepuka utelekezaji wa familia na vitendo vya ukatili na unyanyasaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeandaa Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji, Usimamizi na Uratibu wa Mabaraza ya Usuluhishi wa Migogoro ya Ndoa wa mwezi Mei, 2023 ambao umebainisha afua za kuwajengea uwezo Wajumbe wa Mabaraza juu ya namna bora ya kufanya usuluhishi wa migogoro kwa lengo la kuepusha athari zinazoweza kuwapata watoto kutokana na vitendo vya ukatili na unyanyasaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, migogoro ya ndoa hushughulikiwa pia na taasisi za dini zilizosajiliwa kisheria pamoja na maafisa ustawi wa jamii walio katika halmashauri zote hapa nchini, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gallos.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri natoa ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini kuna maswali mawili madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa matatizo makubwa ni migogoro ambayo inasababishwa na ndoa inayopelekea watoto wadogo wengi wa Tanzania kuelekea kwenye kubakwa pamoja na kupata mimba. Je, ni upi mkakati wa Serikali kunusuru watoto kwenye matatizo haya yanayosababishwa na ndoa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, takwimu zinaonesha watoto wengi wanaofeli shuleni, matatizo yao makubwa yanasababishwa na migogoro inayosababishwa na ndoa. Serikali ina mikakati gani ya kuweza kuwasaidia watoto hawa ili kuwanusuru na matatizo yanayosababishwa na migogoro ya ndoa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tauhida, kwanza nimpongeze sana, amekuwa mfuatiliaji sana na amekuwa anakerwa na masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na wakati wote amekuwa akifanya ufuatiliaji mkubwa na kuhakikisha kwamba Taifa hili linakua kwa misingi na maadili ambayo yanatakiwa, kwa hiyo, nampongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake ni kweli kwamba Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeliona hilo na ikachukua hatua mbili mahususi kwa sababu Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amekuwa anakerwa sana na masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na akaunda Wizara maalumu ambayo inaweza ikashughulikia masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya hatua ambazo imezichukua ni pamoja na kuandaa mwongozo maalumu uliohusisha taasisi za dini za kiislamu na kikristo. Mwongozo huu unaojulikana kwa jina la Wazazi Wangu, Kesho Yangu una lengo la kuwahamasisha wazazi waweze kuwalea watoto wao kwa kuzingatia maadili mema na pia kuwa karibu zaidi na watoto ili wasiweze kuharibikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu hilo linaenda pia katika maeneo ya taasisi za elimu ili kuweza kuhakikisha kwamba watoto wetu wanakua katika misingi ya maadili na kuwaepusha na matendo ya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, kama nimempata vizuri amesema kwamba ni kweli shuleni kumekuwa na changamoto ya watoto kufeli kutokana na migogoro ya ndoa. Katika hilo, kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 kwenye kifungu 102 kinampa mamlaka Waziri wa Katiba na Sheria kutunga au kuandaa mabaraza ambayo anayarasimisha katika ngazi za kata yaweze kufanya kazi ya usuluhishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, inapotokea migogoro ya ndoa ni muhimu sana na nitoe nasaha kwa wazazi, nawasihi wazazi na walezi kuzingatia sana kushirikiana kuweza kutoa mafunzo na malezi bora kwa ajili ya watoto ili kuondoa tofauti ambazo zinatokana na wao zinazoenda kupelekea kupoteza maslahi mapana ya watoto, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Sanga.

Na. 425

**Hatua za Maandalizi ya *AFCON***

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza: -

Je, Serikali imefikia wapi katika maandalizi ya *AFCON 2027* kwenye ujenzi wa viwanja na hoteli nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imepata fursa ya kuwa mwenyeji wa Fainali za Mpira wa Miguu Barani Afrika *(AFCON 2027)* kwa kushirikiana na Kenya na Uganda baada ya kushinda zabuni ya kuwa wenyeji iliyofanyika mwezi Septemba, 2023 Jijini Cairo nchini Misri. Uratibu wa maandalizi ya mashindano hayo unaendelea kwa kufanyika vikao vya pamoja na kila nchi inakarabati na kujenga miundombinu yenye kukidhi viwango na vigezo vya *CAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tanzania maandalizi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu hususani

viwanja unaendelea ambapo Serikali imeanza ujenzi wa Uwanja wa Mpira katika Jiji la Arusha ambao utakuwa na uwezo wa kubeba watazamaji 30,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali inakarabati Uwanja wa Uhuru na Benjamin Mkapa, Jijini Dar es Salaam na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imefanya ukarabati mkubwa wa Uwanja wa Amaan. Sambamba na ujenzi na ukarabati wa viwanja unaoendelea, Serikali ina mpango wa kujenga viwanja katika Jiji la Dodoma na Fumba, Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa hoteli, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wadau pamoja na wamiliki wa hoteli kubwa ili kufanya na kuboresha hoteli hizo ili ziweze kukidhi viwango na hatimaye kuhudumia ugeni wa *AFCON 2027*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri na yenye matumaini kwa Watanzania, ninaomba kuuliza maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Serikali imezungumzia suala la ujenzi wa viwanja vya michezo *(playing grounds)* hizi ambazo ni Arusha, Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar, lakini kwenye maandalizi ya *AFCON* viwanja vingi vinavyotakiwa pia kujengwa ni viwanja vya *training grounds* kwa ajili ya kufanyia mazoezi kwa hizo timu kwa sababu timu zitakuwa ni nyingi, kwa hiyo viwanja vingi vinahitajika.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga viwanja vingi vya mazoezi kwa ajili ya ku-*facilitate* hiyo *AFCON* kuliko kujikita kwenye kuwaza tu hizo *grounds* kubwa ambazo ni za mechi?

Mheshimiwa Naibu Spika, cha pili kwenye *issue* ya hoteli, kilio cha Mheshimiwa Rais hadi leo kwenye sekta ya utalii ni uhaba wa hoteli nchini. Ukifanya *research* jinsi ambavyo *AFCON* imefanyika Ivory Coast, zaidi ya watu 500,000 wameingia pale. Sisi kwenye

Taifa letu tuna uhaba wa hoteli. Uki-*mention* Dar es Salaam hoteli tano ambazo zinaweza zikahudumia kwa *five stars* hazifiki, uki-*mention* Zanzibar, uki-*mention* Arusha.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa *incentives* kwa ajili ya kui-*support* sekta binafsi ili iweze kujenga hoteli nyingi za kisasa zitakazoweza ku-*facilitate AFCON?* Tena nikishauri kwamba kwa kuwa Serikali imehamia Dodoma na kuna majengo mengi ya Serikali yapo kwenye *potential areas* Dar es Salaam, upi mkakati wa Serikali ku-*support* wananchi na wa sekta binafsi iweze kujenga hoteli za kisasa ili tuweze kufanya *AFCON*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sanga, ni kwamba pamoja na kujenga viwanja ambavyo vitakuwa vinatumika kwa ajili ya mashindano katika Majiji ya Dar es Salaam, Zanzibar na Arusha, pia miji hii yote mitatu itakuwa na viwanja vitano kwa ajili ya mazoezi; vinne ni kwa ajili ya timu ambazo zitakuwa zinashiriki, kwa sababu kila kituo kitakuwa na timu nne, na kimoja kitakuwa ni kwa ajili ya waamuzi kwa sababu na wao wanatakiwa kufanya mazoezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili la viwanja vya mazoezi, tunalifahamu na hatujaliacha nyuma kusema ukweli, usiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na la pili ambalo ni wazo Mheshimiwa Sanga amelitoa kwa namna ya swali, kwanza Serikali inalichukua wazo lake kuhusiana na kutumia majengo ya Serikali ambayo ofisi zake zimehamia Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Mchezo na Kituo cha Uwekezaji imekuwa ikiendelea kufanya vikao na mikutano na wawekezaji mbalimbali wenye maslahi katika sekta ya hoteli ili kuwaelezea kuhusiana na vivutio mbalimbali hasa vya kikodi ambavyo Serikali imevitoa kwa ajili ya kuhakikisha majengo ya

hoteli na vyumba vinaongezeka ili kuwa na uwezo wa kumudu ugeni ambao tutaupata mwaka 2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika Wizara ya Utamaduni, Sanaa na michezo kwa sasa inajiandaa kuanza kutengeneza kanzidata ambayo itakuwa na taarifa za majengo yote yanayoweza kutumika na ugeni huo zikiwemo *apartments* na *Air Bed and Breakfast* kote nchini. Kwa hiyo, ni rai yangu kwa Watanzania kuichangamkia fursa hii kwa sababu itakuwa na faida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo hatutegemei kupata mkwamo ni eneo hili la malazi kwa sababu timu ambayo tuliituma Ivory Coast, moja ya maeneo ambayo wametilia mkazo sana kwenye taarifa yao ni hili. Utayari wa Serikali na wadau ambao wana maslahi kwenye sekta ya hoteli ni mkubwa, kwa hiyo, hatutegemei kupata mkwamo wa aina yeyote, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali yetu yamekwisha. Sasa ni matangazo ya wageni.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wageni wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ndugu Gerson Msigwa – Katibu Mkuu, Profesa Saudin Mwakaje – Mwenyekiti wa Bodi Baraza la Sanaa Tanzania, Ndugu George Yambesi – Mwenyekiti wa Bodi Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo na Ndugu Victor Tesha – Mwenyekiti wa Bodi Taasisi ya Hakimiliki Tanzania. *(Makofi)*

Pia wapo Ndugu Leah Kihimbi – Mwakilishi wa Mwenyekiti Bodi ya Filamu na Ndugu Antonia Tonisiza Sangalali – Mwenyekiti wa Umoja wa Machifu Tanzania. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Odo Klian Mwisho – Mwenyekiti CCM Mkoa wa Ruvuma, Ndugu Mohamed Khalfan – Katibu CCM Mkoa wa Ruvuma, Ndugu Mwinyi Abdalah Msolomi – Mwenyekiti wa CCM Wilaya Songea Mjini, Ndugu James Dani Mgego – Katibu wa

CCM Wilaya ya Songea Mjini na Ndugu Omary Msigwa maarufu kama *Super Feo* – Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Wengine ni Profesa Shadrack Mwakalila – Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere, Mzee Galus Abeid – Msaidizi Maalumu wa Mkurugenzi Mtendaji – Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Ndugu Isack Joseph Mwalituke – Rais wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo, Ndugu Dennis Simba – Mwakilishi wa Mwenyekiti Baraza la Michezo Tanzania (BMT) na Ndugu Hassan Njama – Mwakilishi wa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)*. *(Makofi)*

Wengine ni Naibu Kamishna Kennedy Komba – Makamu Mwenyekiti Baraza la Michezo la Majeshi Tanzania na Kanali Martin Msumari – Katibu Mkuu Baraza la Michezo la Majeshi Tanzania. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Florah Ndumbaro ambaye ni mke wa Mheshimiwa Waziri, ahsanteni. *(Makofi/Vigelegele)*

Wapo pia Ndugu Raphael Damas Ndumbaro – mtoto wa Mheshimiwa Waziri na Ndugu Barnaba Elias – msanii wa *Bongo Flavour. (Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 50 wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni walimu na wanafunzi wa *Lucas Maliaa Girls High School* kutoka Wilaya ya Ruangwa, Mkoa wa Lindi, karibuni. *(Makofi)*

Wageni kumi wa Mheshimiwa Daniel Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Cosato Chumi, mwandishi na mtangazaji wa habari za michezo kutoka *EATV* na *East Africa Radio*. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, Msemaji wa Tawi la *Simba VIP* kutoka Dar es Salaam, nilikuwa sijakuona, karibu. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Esther Matiko, mwandishi wa habari wa *PMTV* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Hawa Mchafu, Kada wa CCM kutoka Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Masache Kasaka ambaye ni mpiga kura wake kutoka Chunya, Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ramadhan Ighondo ambaye ni mpiga kura wake kutoka Singida Kaskazini. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wawili wa Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Zanzibar. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula, rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambao ni makada wa CCM kutoka Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Boniphace Getere ambao ni wafugaji kutoka Bunda, Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma ambao ni marafiki zake kutoka Hanang, Mkoa wa Manyara na Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 75 na walimu nane kutoka Shule ya Awali na Msingi Lusasaro ya Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi 100 na walimu kumi wa Shule ya Msingi *Green Bird* kutoka Wilaya ya Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, iliyochambua bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Bunge lako Tukufu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo - Fungu 96 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba hotuba yangu yote iingizwe katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuendelea kutujalia afya njema na ulinzi na hatimaye kutuwezesha kukutana tena leo katika Bunge lako Tukufu ili kuendelea kujadiliana na kupanga maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza kwa kuniamini kuendelea kuwapo katika nafasi ya Uwaziri katika Serikali yake hususan Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na

pili, kwa utekelezaji thabiti wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 iliyosababisha leo hii kuja kifua mbele katika Bunge lako Tukufu kuyasema mafanikio makubwa ya Serikali na kuendelea kuomba fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mipango mikubwa zaidi ya maendeleo kwa Taifa letu katika kila chombo na wimbile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili husema, chanda chema huvikwa pete. Kama Taifa tunayo kila sababu kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mafanikio makubwa, yasiyo kifani na ya kihistoria katika sekta ya utamaduni, sanaa na michezo katika kipindi kifupi cha miaka mitatu ya uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya ya kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais. Aidha, nisiwe mnyimi wa fadhila, niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuongoza vyema, kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar pamoja na kuudumisha na kuuenzi Muungano wetu, kwa hakika ya kale ni dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fauka ya hayo, naomba niwapongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko - Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu makubwa ya kutumikia Watanzania na kuwaletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nampongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza kwa busara na hekima kubwa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile nakupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika Mussa Azzan Zungu, kwa kumsaidia Mheshimiwa Spika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza sana Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika - Mbunge wa Njombe Mjini na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama - Mbunge wa Madaba kwa kusimamia vyema mijadala hususani ya kibajeti katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimsifia mwenye mwendo, mpongeze zaidi anayemkimbiza. Nyuma ya mafanikio haya makubwa, naomba niishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima - Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote wa Kamati kwa kusimamia vyema Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo na ushauri wao kwa Wizara umezingatiwa na ndiyo msingi mkuu wa mafanikio tunayoyaona leo hii. Wizara inaahidi kuendelea kuzingatia maelekezo ya Kamati katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa mustakabali wa sekta za utamaduni, sanaa na michezo, na kwa hapa tunasema Kazi Iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wasemavyo wahenga, kidole kimoja hakivunji chawa, ninasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu ya Bajeti nikiwa na timu ya ushindi nyuma yangu iliyofanikisha haya yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma almaarufu Mwana-FA, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kunisaidia vyema kusimamia majukumu ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nampongeza Ndugu Gerson Partinus Msigwa, Katibu Mkuu, Dkt. Suleiman Hassan Serera, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, watumishi na wadau wote kwa kutimiza vyema majukumu yao na hatimaye kuiletea Wizara hii sifa katika utekelezaji wa majukumu yake. Bila

ninyi hatuna Wizara. Tuendelee kuchapa kazi kwa bidii katika nafasi hizi tulizokasimiwa kuwaletea Watanzania maendeleo. Hawa ndio msingi wa mageuzi makubwa yanayofanywa katika sekta zetu hususani kuzifanya za kiuchumi zaidi, kuzalisha ajira, mapato na hatimaye kupunguza umaskini. Tunasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwapo kwangu katika Bunge lako Tukufu kuna deni kubwa la shukurani na kuwatumikia vyema wapiga kura wangu wa Jimbo la Songea Mjini. Ninawashukuru sana kwa kuniamini na kunipa nafasi ya kuwatumikia. Ninawaahidi sitowaangusha, tupo pamoja, iwe mvua liwe jua, Songea iende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilikadiria kukusanya shilingi 1,000,000,000. Hadi kufika mwezi Aprili, 2024 shilingi 683,000,502,708 sawa na 68.3% ya lengo la mwaka zilikuwa zimekusanywa. Kwa upande wa taasisi zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni shilingi 5,970,428,000. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 shilingi 5,632,107,874.95, sawa na 94% ya lengo zilikuwa zimekusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara iliidhinishiwa bajeti yenye jumla ya shilingi 35,445,041,000. Kati ya fedha hiyo, mishahara ni shilingi 9,651,285,000, matumizi mengine ni shilingi 13,962,596,000, na miradi ya maendeleo ni shilingi 11,831,160,000 na hadi kufikia Aprili, 2024 Wizara imepokea jumla ya shilingi 40,487,566,685.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizotekelezwa; katika kuhakikisha kwamba tunalinda, kudumisha na kuendeleza maadili ya Mtanzania yanayozingatia mila, desturi na miiko ya Taifa letu yaani ustaarabu tulioupokea kutoka kwa waasisi wa Taifa na mababu zetu, Wizara imeendelea kuhamasisha na kutoa elimu ya maadili mema kwa umma kupitia vipindi vya redio, televisheni, matamasha na midahalo mbalimbali katika kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini. Vipindi vya elimu ya maadili vilitolewa katika televisheni na redio mbalimbali zikiwamo *TBC, Azam TV*, *ITV, Radio One, Clouds FM* na Wapo Redio katika Mkoa

wa Dar es Salaam; *AFm Radio* katika Mkoa wa Dodoma; *ICE FM, Kings FM* na *Uplands FM* katika Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia BAKITA iliandaa maadhimisho ya pili ya Siku ya Kiswahili duniani yaliyofanyika duniani kote tarehe 7 Julai, 2023. BAKITA imeendeleza kongoo za Kiswahili kuongeza maneno milioni saba ambapo kwa sasa kongoo hiyo ina jumla ya maneno milioni 34 kati ya lengo la maneno milioni 50 sawa na 68% ya malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno haya yalichukuliwa kutoka kwenye mitandao ya kijamii, tovuti za Serikali na mashirika ya umma na binafsi na kuskani machapisho mbalimbali yaliyoandikwa kwa Kiswahili. Kongoo hii inalenga kuhakikisha Kiswahili kinasheheni katika uwanja wa teknolojia na hususanI akili mnemba. Aidha, wataalamu na watu mbalimbali watakuwa na uwezo wa kuitumia kongoo hii kwa shughuli za uandishi wa kamusi, ujifunzaji wa Kiswahili, uandishi wa vitabu na tafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kwa sasa ina vituo 44 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni ambapo kati ya hivyo vituo 16 viko ndani ya nchi na vituo 28 viko nje ya nchi. Fauka ya hayo, BAKITA imefanya utafiti na kubaini jumla ya vituo na vyuo zaidi ya 150 vinafundisha Kiswahili nje ya nchi na Watanzania zaidi ya 113 wanafanya kazi kupitia Kiswahili na taaluma zake husianifu huko ughaibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi kubwa iliyofanywa kwenye eneo hili la lugha adhimu na aushi ya Kiswahili, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi sasa Kiswahili ni miongoni mwa lugha saba kubwa zenye wazungumzaji wengi Duniani ambapo Kiswahili kina wazungumzaji takribani milioni 500. Kwa msingi huu tuna kila sababu ya kujivunia na kutembea kifua mbele kutokana na mafanikio tuliyoyapata ya lugha ya Kiswahili na hivyo tusikubali mtu yeyote aipuuze au kuibeza lugha yetu kwani hivi sasa imetupa utambulisho pekee duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nia ya dhati napenda kutoa shukrani za pekee kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha zaidi ya bilioni moja kwa ajili ya ukarabati wa maeneo ya Urithi wa Ukombozi Barani Afrika. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kimefanya ukarabati mkubwa wa jengo la kihistoria na yaliyokuwa Makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika ambapo mipango na mikakati yote ya kulikomboa Bara la Afrika lilifanyika hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika kimefanya ukarabati wa handaki la kihistoria lililopo katika Wilaya ya Kongwa, Dodoma ambapo lilijengwa na kutumiwa na Rais wa kwanza wa nchi ya Msumbiji Hayati Samora Machel wakati akiratibu mafunzo ya kijeshi kwa wapigania uhuru wa nchi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya utamaduni, kutokana na umuhimu wa uzingatiaji wa maendeleo ya utamaduni na sanaa, Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichukua jitihada za makusudi za kuhuwisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Desemba, 2022 kwa lengo la kukuza na kuendeleza sekta hii kupitia utoaji wa mitaji yenye masharti nafuu na mafunzo ili kuziwezesha kazi za wadau wa utamaduni na sanaa kukidhi vigezo vya ushindani wa masoko hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2024 Mfuko wa Utamaduni na Sanaa umewezesha utoaji wa mikopo ya shilingi bilioni 4.2 kwa miradi 216 ya utamaduni na sanaa iliyopo katika mikoa 16. Sekta zilizonufaika na mikopo hiyo ni pamoja na muziki, filamu, sanaa za maonesho na miradi ya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kunakuwa na ubunifu na utengenezaji wa sanaa bora kwa wasanii, Baraza limeendelea kurasimisha wasanii kwa njia ya kisasa ya kidijiti kupitia mfumo wa Usajili wa Wadau wa Sanaa *(Artist*

*Management Information System (AMIS))*. Mfumo wa *AMIS* umerahisisha utoaji wa huduma kwa wasanii na wadau wa sanaa kwa vile huduma za maombi na utoaji wa vibali na malipo ya ada hukamilika kwa njia ya mtandao, hivyo wasanii na wadau hawalazimiki kusafiri mahali walipo kwenda Dar es Salaam katika Ofisi za BASATA ili kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza limerejesha Tuzo ya Muziki wa Tanzania *(Tanzania Music Award)* ambazo zilikoma mwaka 2014. Tuzo hizo zimefanyika kwa mara nyingine tena mwaka 2021/2022 na kwa mwaka huu zitafanyika Juni, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto ya mmomonyoko wa maadili kwa wasanii wa Kitanzania, Baraza limeandaa mwongozo wa uzingatiaji maadili katika kazi za sanaa ambapo ulizinduliwa rasmi tarehe 3 Novemba, 2023 na kupata idhini ya matumizi. Mwongozo huo umesambazwa kwa viongozi wa sanaa, wasanii na wadau wa sanaa. Aidha, umewekwa kwenye tovuti ya Baraza yenye kiungo cha *www.basata.go.tz.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa wasanii na waandishi wananufaika kwa kupata kipato kutokana na ubunifu wao, Ofisi ya Hakimiliki kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi 639,096,726.40 kupitia chanzo kipya cha mapato cha Tozo ya Hatimiliki *(Copyright levy)* kupitia Kanuni za Tozo ya Hakilimiki *(The Copyright and Neighbouring Rights (Copyright levy on blank devices)) Regulations* ya mwaka 2023).

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya jukumu la Ofisi ya Hakimiliki Tanzania ni kutatua migogoro baina ya wabunifu. Katika kipindi hiki Ofisi ya Hakimiliki Tanzania ilipokea jumla ya migogoro 19 kati ya hiyo migogoro 12 imesuluhishwa na migogoro saba inaendelea na usuluhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza utamaduni na sanaa, Serikali imeweka nguvu kubwa katika utaalamu, utafiti na ushauri ambapo chuo chetu cha *TaSUBa* ni taasisi inayotoa

mafunzo ya aina mbalimbali hususani katika masuala ya sanaa na utamaduni ya hapa nchini. Mwaka 2012 chuo hiki kiliteuliwa kuwa Kituo cha Jumuiya ya Afrika Mashariki chenye ubora uliotukuka katika ufundishaji wa fani za utamaduni na sanaa hivyo ni chuo chenye hadhi ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa mwaka 1957 kwa Mashindano ya Mpira wa Miguu Afrika yajulikanayo kwa jina la *AFCON* yataweza kufanyika hapa Tanzania kwa kushirikiana na majirani zetu wa Kenya na Uganda. Nchi hizi za Afrika Mashariki zimeshinda zabuni ya kuandaa mashindano haya iliyofanyika mwezi Septemba, 2023 kule nchini Cairo. Nchi hizi tatu imeyapa jina mashindano haya na kuyaita *Pamoja AFCON* 2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza katika historia katika hatua ya kufuzu *AFCON* ya mwaka 2023 tumefanikiwa kuwatumia wachezaji wa Kitanzania wanaoishi nchi nyingine na wana asili ya Tanzania *(diaspora)*. Hiki kimekuwa kilio na maombi ya Watanzania kwa muda mrefu sana, wachezaji hao hakika wameleta tija na hamasa katika timu yetu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ujenzi wa Kiwanja cha Michezo Dodoma, pia Serikali imeanza kujenga kiwanja chenye uwezo wa kuchukua watazamaji 30,000 wakiwa wameketi katika Jiji la Arusha kiwanja ambacho kimepewa jina kinaitwa *Samia Suluhu Hassan Stadium*. Kiwanja hiki kinajengwa kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya michezo ya *AFCON* yanayotarajiwa kufanyika mwaka 2027. Mkandarasi amepatikana na kazi ya ujenzi imeanza, kiwanja hiki kinatarajiwa kuwa kimekamilika ifikapo Desemba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali imeanza kutekeleza mradi wa ukarabati wa kiwanja cha Benjamin Mkapa, tunatarajia ukarabati huo utakuwa umekamilika ifikapo mwezi Agosti, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Baraza la Michezo la Taifa limeendelea kuwezesha na kugharamia timu za Taifa zinazoshiriki katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Serikali kupitia BMT imewezesha jumla ya timu 15 kushiriki katika mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia BMT imeendelea kugharamia timu ya Taifa ya mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu *(Tembo Warriors)*. Timu hiyo imefanya kambi ya maandalizi ya muda mrefu ili kushiriki mashindano ya mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu wa nchi za Afrika yanayofanyika nchini Misri hivi sasa kuanzia tarehe 18 mpaka 29 Mei na tayari timu hiyo imefuzu kuingia robo fainali ya mashindano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni matunda ya uwekezaji wa Mama Dkt. Samia kwa vijana hawa wenye ulemavu. Mashindano haya yatatumika kufuzu kushiriki mashindano ya dunia ambapo timu nne zitakazofuzu zitawakilisha Bara la Afrika katika mashindano ya dunia. Mchezo huu ni muhimu kwa watu wenye mahitaji maalumu, kwani umeendelea kutoa fursa za ajira nje ya nchi ambapo wachezaji wa Kitanzania Shedrack, Hebron Sembele na Ramadhani Ally Chomelo wanacheza soka la kulipwa nchini Uturuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika mchezo wa mpira wa miguu. Miongoni mwa timu zilizofanya vizuri ni pamoja na timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wanawake *(Twiga Stars)* iliyofuzu kucheza mashindano ya *WAFCON* yanayotarajiwa kufanyika mwezi Juni, 2024 nchini Morocco. Pia Klabu ya Mpira wa Miguu ya Wanawake *(JKT Queens)* iliyofuzu kushiriki mashindano ya Klabu Bingwa ya Afrika Mashariki na Kati ikiwa ni mwakilishi pekee katika ukanda wa *CECAFA,* timu ya *Taifa Stars* katika mashindano ya *AFCON,* 2023 ambapo ilikuwa ni timu pekee kutoka kwenye ukanda wa *CECAFA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, fauka ya hayo, Klabu za Simba na Yanga zimeweza kufika katika hatua ya robo fainali kwa pamoja

katika michezo ya Klabu Bingwa Barani Afrika ambapo Tanzania kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi hii imefanikiwa kuwa timu mbili katika hatua za makundi na timu mbili katika hatua za robo fainali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruska yako tunaomba kuipongeza sana timu ya Simba kwa kuwa timu ya saba kwa ubora Barani Afrika na hivyo kuwa kati ya timu kumi bora Barani Afrika. Tunaziomba na timu zingine zijitahidi kuingia kwenye kumi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio haya yamechochewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alizihamasisha timu hizo kwa kununua magoli yaliyofungwa. Aidha, kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Michezo pamoja na kushiriki katika harambee ya kuzichangia timu za Taifa ni kichocheo kingine cha kufikia hatua hiyo ya mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza kwa kushirikiana na Taasisi ya Ushirikiano wa Kimataifa wa Japani *(JICA)* waliandaa Awamu ya Tano ya Mashindano ya Riadha kwa Wanawake ya Juma Ikangaa *(5th Juma Ikangaa Ladies First)* ambapo yalifanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 24 mpaka 26 Novemba, 2023. Lengo la mashindano hayo ni kuendelea kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika michezo. Kutokana na matamasha na mashindano hayo kumeshuhudiwa kuhamasika kwa hali ya juu kwa wanawake kushiriki katika michezo mbalimbali ambapo jumla ya wanawake wanamichezo 186 walishiriki kutoka mikoa yote 31 ya Tanzania. Katika kilele cha tamasha hilo kwa awamu zijazo litatambulika rasmi kama *Juma Ikangaa Ladies First. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na utoaji wa mafunzo kwa wanachuo wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya, chuo hicho kimeendelea kuboresha miundombinu ya kufundisha na kujifunzia kwa kuendelea na ujenzi wa hosteli za wanachuo. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 shughuli mbalimbali zimefanyika kwa upande wa ujenzi wa hosteli za

wanafunzi. Kwa sasa kazi zinazoendelea ni kuezeka, kujenga kuta za sakafu ya nne na kumalizia jengo *(finishing)* ikiwemo kupiga plasta jengo lote na kuweka vigae *(tiles)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha michezo inaendeshwa kisasa zaidi Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea na ujenzi wa kituo cha kitaifa cha kuendeleza vipaji katika Chuo cha Maandeleo cha Malya. Kituo hiki ni sehemu ya maandalizi ya *AFCON 2027* na ushiriki wa Kombe la Dunia mwaka 2030 ambapo kitatumika kuibua na kuendeleza vipaji kwa ajili ya michezo hiyo. Mkandarasi ambaye ni Kampuni ya *CRJE* ya China yupo eneo la ujenzi na mpaka kufikia mwezi Aprili, 2024 tayari alishakamilisha kuchimba msingi ya majengo matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa bajeti kwa mwaka 2024, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara na taasisi zake kwa kushirikiana na wadau itatekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025, maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021 pamoja na maelekezo na mwongozo uliotolewa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati anatoa mwongozo katika Bunge lako Tukufu tarehe 3 Aprili, 2024 pamoja na miongozo mingine mbalimbali ya kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2024/2025 majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na kufanya maadhimisho ya tatu ya Siku ya Kiswahili Duniani, kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili wa mwaka 2022/2032, kufungua vituo 100 vya kufundisha Kiswahili nje ya nchi kwa kushirikiana na *diaspora,* kuandaa kongamano la Kiswahili nje ya nchi mwezi Novemba, 2024, kuchapisha vitabu viwili vya kufundishia Kiswahili, kuimarisha Kiswahili nchini na kukitangaza kimataifa na kutoa elimu ya matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika katika mwaka wa fedha 2024/2025 kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Kituo Kikuu cha Uhifadhi wa Urithi wa Ukombozi wa Afrika kitakachojengwa Bagamoyo mkoani Pwani;

(ii) Kukamilisha ukarabati wa Jengo la Kamati ya Ukombozi lililoko Jijini Dar es Salaam; na

(iii) Kukarabati mahandaki na makaburi katika maeneo mbalimbali yaliyoko katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu zaidi kituo kimekuja na wazo jipya la kuhakikisha kinaanzisha mashindano ya mpira wa miguu kwa vijana chini ya miaka 20 kwa nchi za Afrika yatakayojulikana kama *Mwalimu Nyerere Liberation Cup,* lengo likiwa ni kuhakikisha tunafikisha elimu ya ukombozi wa Bara la Afrika kwa vijana wengi zaidi wa Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania; mfuko umepanga kutekeleza majukumu mbalimbali katika mwaka wa fedha 2024/2025 ikiwemo ni pamoja na kuendesha programu ya mafunzo na kutoa mikopo kwa miradi 475 ikiwa ni wastani wa miradi 18 kwa kila mkoa ili kuhakikisha kila msanii mwenye sifa na haki anapata mkopo huu kama ambavyo Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 malengo yaliyopangwa katika sekta ya sanaa ni kuandaa mpango wa maendeleo ya sekta ya sanaa, kufanya na kutathmini utekelezaji wa majukumu ya sekta ya sanaa katika mikoa na wilaya za Tanzania Bara, kufanya utafiti na kubaini michango ya sekta ya katika ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa kushirikiana na taasisi za utafiti na kusimamia maandalizi ya ujenzi wa vituo vya sanaa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa BASATA majukumu yatakayotekelezwa kwa mwaka 2024/2025 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuimarisha utawala bora katika kutekeleza shughuli za Baraza na uendeshaji wa sekta ya sanaa;

(ii) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Baraza;

(iii) Kukarabati na kujenga vituo vya sanaa na ofisi za Baraza;

(iv) Kusimamia maslahi ya wasanii yasiyo ya hakimiliki au hakishiriki;

(v) Kuhamasisha elimu na shughuli za sanaa katika shule za msingi na sekondari;

(vi) Kusimamia matumizi ya sanaa za jadi, kuimarisha ushiriki wa jamii katika shughuli za sanaa ikiwemo utekelezaji wa mradi wa *BASATA Vibes* na Programu za Sanaa Mtaa kwa Mtaa; na

(vii) Kuratibu ujenzi wa ukumbi wa sanaa kwa wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *COSOTA* katika mwaka 2024/2025 imepanga kutekeleza Kampeni maalumu ya elimu inayofahamika kama "Hakimiliki yako Hailiki, Kamata Fursa Twenzetu," kukusanya na kugawa mirabaha katika madaraja ya kazi ambazo hazisimamiwi na kampuni za ukusanyaji na ugawaji mirabaha *(CMOs),* kusimamia kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha ambazo zimeshaanzishwa, kusajili wasanii, waandishi na wabunifu wa masuala ya hakimiliki 1,150 na kazi 2,850 na kufanya *operation* za kupambana na uharamia wa kazi za ubunifu

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *TaSUBa* katika mwaka 2024/2025 imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kudahili wanachuo wa kozi ndefu wapatao 800 na kozi fupi 280;

(ii) Kuendesha mafunzo maalumu ya sanaa na utamaduni kwa kushirikiana na wadau katika mikoa mitatu (Kigoma, Mtwara na Ruvuma);

(iii) Kufanya tafiti kwenye eneo la utamaduni;

(iv) Kutafuta eneo la kuanzisha kampasi mpya jijini Dodoma; na

(v) Kuanzisha Kituo cha Mafunzo ya Sanaa na Utamaduni jijini Dar es Salaam na Mjini Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maendeleo ya michezo, katika mwaka wa fedha 2024/2025 malengo yaliyopangwa ni kuratibu kikao cha Kanda ya Tano Afrika kuhusu Mapambano ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni, kuratibu Mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuratibu kikao kazi cha wadau cha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo, kuratibu Mkutano wa Mwaka wa Maafisa Michezo Tanzania Bara, kuratibu matukio ya Michezo ya Kitaifa na shughuli nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Baraza la Michezo, katika mwaka wa fedha 2024/2025 majukumu yatakayotekelezwa ni pamoja na kuendelea kuwezesha na kuzigharamia Timu za Taifa kushiriki mashindano mbalimbali ya Kimataifa, kuendelea kusajili vyama na mashirikisho na vilabu vya michezo, kuanzisha safari ya Kombe la Dunia mwaka 2030, kwa sababu tumeamua kama Tanzania kwa mwongozo wa Mheshimiwa Rais, tunataka tukacheze Kombe la Dunia mwaka 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutekeleza mkakati maalumu wa kulea timu za vijana kuwa na timu ya vijana chini ya miaka 17 ambayo itatokana na mashindano ya UMITASHUMTA, chini ya miaka 20 ambayo itatokana na mashindano ya UMISSETA na timu

ya chini ya miaka 23 ambayo itatokana na wachezaji wanaocheza ligi, wasio kwenye ligi na *diaspora* walioko nje ya nchi. Pia kuratibu matamasha mawili ya Michezo ya Wanawake ya *Tanzanite,* kuendelea kuhamasisha utawala bora katika vyama na mashirikisho ya michezo, kuidhinisha vibali vya matukio mbalimbali ya michezo na majukumu mengine ni kutoa tuzo kwa wanamichezo bora ambapo katika mwaka huu tumetoa tuzo tarehe 9 Juni, jijini Dar es Salaam. Pia ujenzi wa maeneo mbalimbali ya michezo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuratibu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli za ofisi ikiwemo matengenezo na mafuta ya magari, huduma za usafi na ulinzi, umeme pamoja na ununuzi wa vitendea kazi mbalimbali na samani za ofisi. Aidha, itaendelea kuwezesha upatikanaji wa stahili mbalimbali za wafanyakazi ikiwemo uhamisho, likizo na safari za kikazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile itaendelea kuratibu mafunzo, ajira na upandishwaji wa vyeo kwa watumishi, kuendesha vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi, kuandaa Mpango Mkakati wa Urithishwaji Madaraka, na kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo na mpango wa rasilimaliwatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio ya bajeti kwa mwaka 2024/2025; Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 1,000,000,000 kupitia vyanzo ambavyo ni viingilio katika matukio ya michezo yatakayofanyika katika viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru. Aidha, mapato mengine yanatokana na huduma za kukodisha kumbi na *gym* zilizopo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na ada za mafunzo na mitihani katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa taasisi sita zilizo chini ya Wizara zinatarajia kukusanya shilingi 7,001,600,000 kama ambavyo imeonesha katika Kiambatanisho 1(a) na (b) kilichopo katika hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imetengewa bajeti ya shilingi 285,318,387,000; kati ya bajeti hiyo shilingi 11,280,116,000 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 15,847,483,000 ni matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo ni shilingi 258,190,788,000. Kiambatanisho Namba 2(a), (b) na (c) kinaonesha mgawanyo wa bajeti ya Wizara katika Idara, Vitengo, Taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2024; ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2024/2025 naomba sasa niliombe Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yenye jumla ya shilingi 285,318,387,000, kati ya bajeti hiyo shilingi 11,280,116,000 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 15,847,483,000 ni matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo ni shilingi 258,190,788,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu naomba nikushukuru wewe kwa kupata fursa hii ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha hotuba ya bajeti. Pia nawashukuru wadau wote wa sekta za utamaduni, sanaa na michezo waliofanikisha kwa ushirikiano mkubwa mafanikio yaliyopatikana katika Wizara mwaka 2023/2024. Kwa makundi yao nawashukuru washirika wa maendeleo, taasisi za umma na binafsi za ndani na nje ya nchi, taasisi za dini, vyama, mashirikisho, vilabu na wanatasnia za utamaduni, sanaa na michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo rahisi kuwataja wadau wote kwa majina, lakini naomba niwatambue wachache ambao ni Kampuni za Azam *Media,* Shirika la Ushirikiano la Kimataifa la Japan – *JICA*, Ubalozi wa Ufaransa, Kituo cha Utamaduni cha Ufaransa, Ubalozi wa Korea Kusini, Ubalozi wa Urusi, Kituo cha Utamaduni cha Urusi, *Bagamoyo Friendship Society* - Ujerumani, *Musicians for a Better Life* - Ujerumani, Jamhuri ya Watu wa China, Umoja wa Ulaya, Baraza la Michezo Zanzibar, Baraza la Kiswahili Zanzibar, Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu Zanzibar, Ofisi ya Hakimiliki Zanzibar, Benki ya Biashara ya Taifa *(NBC),* Benki ya *CRDB* na Benki ya *NMB.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau wengine ni pamoja na Shirika la Hakimiliki Ubunifu Duniani, Shirika la Miliki Ubunifu Afrika, Shirika la Jumuiya za Waandishi Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Chama cha Lugha na Fasihi za Kiswahili Tanzania, Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani, Shirikisho la Muziki Tanzania, Shirikisho la Sanaa za Maonesho Tanzania, Shirikisho la Filamu Tanzania, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar, Shirikisho la Sanaa za Ufundi Tanzania, *Peramiho Events and Designing, Airtel Tanzania,* Kampuni ya *Startimes,* Azam pamoja na *Multichoice*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwashukuru wadau ambao wameungana na sisi leo na kwa namna ya kipekee naomba nitambue uwepo wa Harmonize, Ali Kiba, Mwijaku, Baba Levo, lakini pia kwa namna ya kipekee uwepo wa Miso Misondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia hotuba yangu kwa kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maelekezo na miongozo yake madhubuti katika utekelezaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko - Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais na kwa miongozo na maelekezo wanayotupatia kufanikisha utekelezaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Husna Sekiboko, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Sima na Wajumbe wote wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu naomba nimshukuru mke wangu mpendwa Bi. Flora Ndumbaro

na familia yangu kwa kuniunga mkono katika wakati wote ninapotimiza majukumu ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kukushukuru wewe binafsi, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni *www.michezo.go.tz.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (MB.), WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Bunge lako Tukufu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuendelea kutujalia afya njema na ulinzi na hatimaye kutuwezesha kukutana tena leo katika Bunge lako Tukufu kuendelea kujadiliana na kupanga maendeleo ya Taifa letu. Aidha, Taifa letu limeshuhudia kuendelea kubarikiwa kwa kuwapo kwa Amani, utulivu, mshikamano na umoja wa kitaifa. Wananchi wameendelea kujihusisha na shughuli zao za kiuchumi kwa utulivu mkubwa na tumejaliwa baraka tele hususan hali nzuri ya hewa iliyowezesha wananchi kuvuna chakula cha kutosha na kuwa na akiba. *Hakika Mungu si athumani na jitihada haiondoi kudra.*

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **kwanza** kwa kuniamini kuendelea kuwapo katika nafasi ya Waziri katika Serikali yake hususan Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, na **pili,** kwa utekelezaji thabiti wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 iliyosababisha leo hii kuja kifua mbele kwenye Bunge lako Tukufu kuyasema mafanikio makubwa ya Serikali na kuendelea kuomba fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mipango mikubwa zaidi ya maendeleo kwa Taifa letu *kwa hakika kila chombo na wimbile*.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ninatambua dhamana kubwa aliyoiweka Mheshimiwa Rais kwangu ya kusimamia Wizara hii inayojulikana kama Nguvu Shawishi (soft power) ya Taifa letu. Sekta hizi ndizo zinazojumuisha makundi makubwa ya Watanzania kwa umoja wao kuenzi mila, tamaduni, sanaa na michezo mbalimbali. Wizara hii inahudumia Watanzania wote wa marika mbalimbali, wengi wao wakiwa vijana, hivyo ni sehemu kubwa ya kutengeneza ajira, uchumi na mapato kwa Watanzania walio wengi. Kwa mustakabali wa Amani na mshikamano wa Taifa letu, Wizara hii na taasisi zake ni wadau wakubwa wa kuimarisha umoja wa Kitaifa, na hivyo, tutaendelea kuzingatia falsafa hii. Tutaendelea kufanyia kazi Maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kujenga uchumi kupitia sekta za Wizara hii na kubadili mtazamo wa sekta za kutoa burudani na kujenga afya pekee *na kwa hakika yaliyopita si ndwele tugange yajayo na sasa tumedhamiria kuleta mabadiliko.*

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** *chanda chema huvikwa pete!* Kama Taifa tunayo kila sababu kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mafanikio makubwa, yasiyo kifani na ya kihistoria katika sekta za utamaduni, sanaa na michezo katika kipindi kifupi cha miaka mitatu (3) ya uongozi wake. Niruhusu nitaje mafanikio machache yanayoonekana katika sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo:

(i) Amehamasisha na kufufua utamaduni wa mtanzania, hivi sasa, matamasha na makongamano ya utamaduni na sanaa yameanzishwa na hivyo, kuimarisha utamaduni, kujenga ajira zikiwamo za utalii wa kiutamaduni na kuimarisha mshikamano wa kitaifa. Matamasha kama vile: tamasha la utamaduni la jamii za Mkoa wa Kilimanjaro, tamasha la BULABO la jamii ya watu wa Mwanza, Maasai Festival la jamii ya Wamaasai, tamasha la Majimaji Selebuka la jamii ya watu Songea; tamasha la Utamaduni la Tulia jijini Mbeya; tamasha la Cigogo la jamii ya watu wa Dodoma, Tamasha la Yamnyausi la jamii ya watu wa Dodoma, Tamasha la kumbukizi ya Vita vya Majimaji na mengineyo, yamefufuliwa;

(ii) Hivi sasa, Kiswahili lugha yetu adhimu na aushi kimetangazwa kama lugha rasmi na ya kazi ya Umoja wa Afrika, uamuzi uliopitishwa katika mkutano wa wakuu wa nchi na serikali za umoja huo, tarehe 6 Februari, 2022 Jijini Addis Ababa, Ethiopia;

(iii) Kiswahili, lugha inayozunguzwa na watu zaidi ya milioni 500 duniani imekuwa bidhaa na kupitia Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili imezalisha ajira nyingi kwa wataalamu wakiwamo walimu, wafasiri, wakalimani, waandishi wa habari na wa vitabu na Watanzania kwa ujumla wao hususan walio katika mzunguko wa lugha hii;

(iv) Kwa kufanya uamuzi mgumu, Mheshimiwa Rais ameufufua Mfuko wa Utamaduni na Sanaa uliokuwa umekufa tangu mwaka 2002 na hadi sasa Mfuko umetoa mikopo yenye jumla ya Shilingi bilioni 4.2 kwa miradi 216 katika mikoa 16 ya Tanzania Bara na kuzalisha jumla ya ajira 14,902 zilizowanufaisha wananchi 447,060. Aidha, kupitia shughuli za Mfuko, hatua za uhakika za urasmishaji wa Sekta zimeanza kuchukuliwa. Sasa Wasanii wanatambulika kwenye uongozi wa Serikali za maeneo yao ya kazi, wamefungua Namba za Utambulisho wa mlipakodi (TIN), wanapitisha malipo yao Benki, wanajisajili katika Vyama, Mashirikisho na Taasisi zinazowasimamia na wameanza

kujikita zaidi katika kuendesha shughuli zao kibiashara badala ya kuiona sekta kama burudani tu;

(v) Kuwaunganisha Wasanii wa Tanzania na soko la kimataifa kupitia mikutano na matamasha mbalimbali ikiwamo Mkutano wa ACCES uliowakusanya Jijini Dar es Salaam wazalishaji, wasambazaji na watumiaji wa muziki wa Tanzania kutoka kote duniani ambapo Wasanii walipata fursa ya kukutana nao na kujenga uhusiano wa moja kwa moja. Aidha, Tamasha la *World Happy Deaf Family Festival* liliwaunganisha jamii ya wasanii viziwi hapa Tanzania na wenzao kutoka kote duniani na kuwapa fursa ya kushindana katika urembo, utanashati, mitindo, ngoma na futuhi huku wakijenga ushirikiano. Kupitia mashindano hayo, Tanzania ilijitangaza kama nchi yenye fursa kwa wote bila kujali changamoto walizonazo wanadamu. Matamasha na maonesho mengine ya kimataifa ni pamoja na Surajkund Crafts Mela iliyofanyika India, *Salon International du Textil Africain* nchini Sierra Leone na *Venice Art Biennale* ya nchini Italia;

(vi) Kubadili mfumo wa usimamizi wa hakimiliki na hakishiriki kwa kuongeza ushiriki wa moja kwa moja wa wadau. Kwa sasa kampuni binafsi za wasanii wanakusanya na kujigawia mirabaha wenyewe chini ya usimamizi wa COSOTA ambayo inasimamia zaidi masuala ya utoaji elimu na kupambana na uharamia. Aidha, ada ya *Blank Tape Levy* iliyoanzishwa kwenye vifaa vinavyozalisha, kusambaza, kuhifadhi au kudurufu kazi za ubunifu kwa lengo la kuwanufaisha wenye haki yameanza na hadi sasa tayari imevunja rekodi ya makusanyo ya mirabaha yaliyowahi kukusanywa huko nyuma;

(vii) Kubadili mfumo wa uendeshaji wa Taasisi za Sekta ya Sanaa kwa kuhama kutoka kuwa wadhibiti na kwenda kuwa wawezeshaji bila kuathiri masuala ya maadili katika uendeshaji wa kazi za Sanaa;

(viii) Kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwake mwaka 1957, Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Mataifa ya Afrika (AFCON 2027) yatafanyika Tanzania kwa ushirikiano na nchi za Kenya na Uganda. Pia tumepata fursa ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya CHAN yatakayofanyika nchini Tanzania mwezi Septemba 2024. Haya ni maono na maelekezo binafsi ya Mheshimiwa Rais. Mashindano haya ya AFCON yatachagiza kuwapo kwa fursa lukuki za ujenzi wa miundombinu, kujenga uchumi, kuvutia utalii, ajira na kuitangaza Tanzania kimataifa. Ni matunda ya uwekezaji mkubwa katika michezo uliofanywa na Mheshimiwa Rais;

(ix) Serikali imeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Michezo *(Sports Development Fund)* kwa ajili ya uwezeshaji wa timu za Taifa kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kimataifa, uibuaji wa vipaji vya wanamichezo, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo, kulipa mshahara wa kocha wa timu ya Taifa ya mpira wa miguu (Taifa Stars), pamoja na kuwajengea uwezo wa utawala bora viongozi wa vyama na mashirikisho ya michezo nchini. Mfuko huu unategemea chanzo kikuu cha michezo ya kubashiri matokeo ya michezo, ambapo Serikali ilipitisha sheria kuwa asilimia 5 ya makusanyo ya michezo ya kubashiri *(Sports Betting)* ielekezwe kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Michezo. Kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2021/2022, Serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni tisa milioni sita hamsini na mbili elfu mia nane thelathini na mbili (9,006,052,832), hakika fedha hizo zimeleta mafanikio makubwa katika sekta ya michezo nchini. Nani kama Mheshimiwa Rais. Michezo imeimarika zaidi kupitia Mfuko huu;

(x) Kwa kipindi cha zaidi ya miaka 40 tangu Baraza la Michezo la Taifa lianzishwe Tanzania hazikutolewa tuzo kwa wanamichezo bora waliofanya vizuri, kwa mara ya kwanza tuzo zimeanzishwa na kutolewa mwaka 2022/23 na mwaka 2023/24 zinatarajiwa kutolewa mwezi Juni 2024 Jijini Dar es Salaam. Kutolewa kwa tuzo imekuwa chachu kwa wanamichezo ili kufanya vizuri nchini katika aina zote za michezo. Hakika, sisi wadau wa michezo tunamshukuru

sana Mheshimiwa Rais kwa mchango wake katika sekta ya michezo;

(xi) Ada ya mja kunena, muungwana ni kitendo! Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha timu za michezo mbalimbali za Taifa kushiriki mashindano ya kimataifa. Mafanikio makubwa yamepatikana katika suala hili ikiwamo:

(a) Kwa mara ya kwanza michezo kwa watu wenye ulemavu imezingatiwa ambapo Timu ya Mpira wa Miguu kwa Watu wenye ulemavu Tanzania *(Tembo Warriors)* ilishiriki mashindano ya Dunia yaliyofanyika nchini Uturuki mwezi Desemba, 2022, na kufanikiwa kufikia hatua ya robo fainali. Timu hii ni ya saba (7) kwa ubora duniani. Kwa mwaka 2024 timu hii imeshiriki mashindano ya kufuzu kombe la dunia yanayofanyika nchini Misri kuanzia tarehe 18 hadi 29 Mei, 2024 na tayari imefuzu robo fainali katika mashindano hayo, pamoja na kuwa ilikuwa kundi moja na bingwa wa dunia timu ya Angola. Haya ni matunda ya uwekezaji wa Mama Samia kwa vijana hawa wenye ulemavu;

(b) Kwa upande wa mpira wa wanawake, timu ya Mpira wa Miguu ya wasichana chini ya umri wa miaka 17 *(Serengeti Girls)* ilishiriki katika mashindano ya Dunia yaliyofanyika nchini India mwezi Oktoba, 2022 na kufanikiwa kuingia hatua ya robo fainali;

(c) Tanzania kupata medali tatu za shaba kwenye mchezo wa ngumi katika mashindano ya Afrika yaliyofanyika nchini Ghana mwezi April 2024. Haya ni mafanikio makubwa kwani kwa kipindi cha zaidi ya miaka 10 Tanzania haikuwahi kupata medali yeyote katika mashindano hayo makubwa na yanayoheshimika zaidi barani Afrika;

(d) Timu ya Taifa ya mpira wa miguu “Taifa Stars” ilishiriki mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON)

yaliyofanyika nchini Ivory Coast mwezi Januari 2024 kwa mara ya tatu katika historia ya Taifa letu;

(e) Timu ya Taifa ya wanawake ya Mpira wa miguu "Twiga Stars" imefuzu kucheza mashindao ya WAFCON ambayo yatafanyika mwaka 2024 nchini Morocco. Nani kama Mheshimiwa Rais katika michezo!!!;

(f) Ligi ya mpira wa miguu NBC imekuwa ligi bora ya sita (6) barani Afrika na ya 64 duniani. Mafanikio hayo yametokana na uwekezaji wa Serikali katika sekta ya michezo kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi zikiwamo kampuni mbalimbali kama vile Azam na NBC ambao kwa namna moja au nyingine wameamua kuwekeza katika michezo hususan mpira wa miguu;

(g) Klabu ya Yanga ilifika hatua ya fainali katika kombe la Shirikisho la Afrika (CAF) na kuwa mshindi wa pili kwa msimu wa mwaka 2022/23. Na katika Msimu wa 2023/24, timu za Simba na Yanga zimefikia hatua ya robo fainali katika Mashindano ya Kombe la Klabu Bingwa Barani Afrika jambo hili limewezesha vilabu vyetu kupanda na kushika nafasi ya 13 kwa klabu ya Yanga na nafasi ya saba (7) kwa klabu ya Simba. Mafanikio haya yamechagizwa na jitihada na hamasa ya Mheshimiwa Rais hususan motisha ya kati ya shilingi milioni 5 mpaka 10 kwa kila goli la ushindi kwa timu hizi kwa hatua mbalimbali wanapofika, kupewa usafiri na motisha nyingine kwa timu zetu;

(h) Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) lilichagua Uwanja wa Benjamin Mkapa kutumika kwa ufunguzi wa mashindano makubwa kabisa ya vilabu ya soka bora Barani Afrika (African Football League) yaliyohusisha timu nane bora katika Bara la Afrika ikiwamo Klabu ya Simba;

(i) Tanzania kwa mara ya kwanza tumesaini makubaliano ya ushirikiano na Ivory Coast kupitia sekta ya michezo ambapo tumepanga kuwa na programu mbalimbali za maendeleo ya michezo ikiwamo kuwa na programu ya mafunzo na mechi za kirafiki kwa timu zetu za Taifa za vijana zitakazochezwa Tanzania, Ivory Coast na katika nchi nyingine; na

(j) Tangu nchi yetu ipate uhuru 1961 hatukuweza kuwatumia wanamichezo wa Diaspora kama ambavyo nchi nyingi za Afrika zimekuwa zikinufaika na utaratibu wa kuwatumia wachezaji wa Diaspora. Kwa mara ya kwanza katika historia katika hatua ya kufuzu AFCON ya 2023 tumefanikiwa kuwatumia wachezaji wa Kitanzania wanaoishi nchi nyingine ambao wana asili ya Tanzania (Diaspora). Wachezaji hao hakika wameleta tija na hamasa katika timu yetu ya Taifa Stars. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia kuwatumia vijana hao wa Diaspora katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais. Aidha, nisiwe mnyimi wa fadhila, niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuongoza vyema, kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar pamoja na kuudumisha na kuuenzi Muungano wetu, *kwa hakika ya kale ni dhahabu.* Fauka ya hayo, naomba niwapongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu makubwa ya kuwatumikia Watanzania kuwaletea maendeleo. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania, kwa Hotuba yake ya Bajeti iliyotoa utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2023/2024 na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2024/2025. Wizara inaahidi kuzingatia mwelekeo huo wa Shughuli za Serikali ili kuyafikia malengo makubwa ya Serikali.

**7. *Mheshimiwa Spika*,** kipekee nikupongeze wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza kwa busara na hekima kubwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nikupongeze kwa kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Bara la Afrika na wa tatu duniani kuchaguliwa na kuaminiwa kuwa Rais wa Taasisi nyeti na kubwa ya Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Hakika umeing'arisha Tanzania kimataifa, hongera sana *na Wahenga walisema ukiona zinduna na ambari iko nyuma.* Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukusaidia na kukushauri vyema katika majukumu yako ya kuliongoza Bunge. Nawapongeza sana Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mbunge wa Viti Maalumu), Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mbunge wa Njombe Mjini) na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama (Mbunge wa Madaba) kwa kusimamia vyema mijadala hususan ya kibajeti katika Bunge lako Tukufu.

**8. *Mheshimiwa Spika*,** *ukimsifu mwenye mwendo, mpongeze zaidi anayemkimbiza.* Nyuma ya mafanikio haya makubwa, naomba niishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko (Mbunge wa Viti Maalumu), Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima (Mb.), Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote wa Kamati kwa kuisimamia vyema Wizara. Maelekezo na ushauri wao kwa Wizara umezingatiwa na ndiyo msingi mkuu wa mafanikio tunayoyaona leo hii. Wizara inaahidi kuendelea kuzingatia maelekezo ya Kamati katika mwaka wa fedha 2024/25 kwa mustakabadhi wa Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo, na kwa hapa tunasema Kazi Iendelee.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama wasemavyo wahenga, Kidole kimoja hakivunji chawa, ninasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu ya Bajeti nikiwa na timu ya ushindi nyuma yangu iliyofanikisha haya yote. Kwa dhati kabisa, nitambue mchango na juhudi kubwa zilizofanyika na zinazoendelea kufanywa na Watendaji wote wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hawa ndio msingi wa mageuzi makubwa yanayofanywa katika sekta zetu hususan kuzifanya za kiuchumi zaidi kuzalisha ajira, mapato na hatimaye kupunguza umaskini. **Kwanza** kabisa, ninamshukuru sana Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma (Mb.), almaarufu "Mwana-FA", Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kunisaidia vema kusimamia majukumu ya Wizara hii. **Pili,** nampongeza Ndugu Gerson Partinus Msigwa, Katibu Mkuu; Dkt. Suleiman Hassan Serera, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kutimiza vyema majukumu yao na hatimaye kuiletea Wizara hii sifa katika utekelezaji wa majukumu yake. Bila ninyi hakuna Wizara, tuendelee kuchapa kazi kwa bidii katika nafasi hizi tulizokasimiwa kuwaletea Watanzania maendeleo. Asanteni sana.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake, Vyama, Mashirikisho, Vilabu na wadau wote walio chini ya sekta za Wizara kwa kuendelea kutekeleza kwa weledi majukumu yao. Kadhalika, ninawashukuru Washirika wa Maendeleo tuliofanya kazi kwa pamoja katika kutekeleza malengo ya sekta za utamaduni, sanaa na michezo.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuwapo kwangu katika Bunge lako Tukufu kuna deni kubwa la shukurani na kuwatumikia vyema wapiga kura wangu wa Jimbo la Songea Mjini. Ninawashukuru sana kwa kuniamini na kunipa nafasi ya kuwatumikia. Ninawaahidi sitowaangusha. Tupo pamoja, iwe mvua liwe jua, Songea iende mbele. Vilevile, nikishukuru sana Chama cha Mapinduzi chini ya Uongozi mahiri wa Mwenyekiti wake Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kunipa dhamana ya kupeperusha bendera ya Chama Songea Mjini na kuendelea

kuniamini hata katika nafasi ya Uwaziri katika Serikali yake. Ninatambua ni heshima kubwa na ninaahidi kutumikia kwa moyo wangu wote. Kwa kuzingatia Miongozo na Maelekezo ya Mheshimiwa Rais na Chama cha Mapinduzi tunaiona Tanzania mpya yenye neema na ustawi wa maisha kwa Watanzania wote. Tunasema kwa Mama Samia, Mitano tena!!
Kazi Iendelee!!

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Hussein Alli Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Alli Hassan Mwinyi pamoja na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa niaba ya Wizara na wadau wetu wote, naomba nitoe pole kwako Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, familia ya marehemu, ndugu, jamaa na marafiki na wananchi wote wa majimbo ya Mbarali na Kwahani na Tanzania kwa ujumla wake kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa jimbo la Mbarali na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Kwahani, Zanzibar. Tunaendelea kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awajalie pumziko jema peponi. Amina.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** Penye urembo pana ulimbo, nchi yetu imepitia kipindi chenye changamoto mbalimbali ikiwamo athari za mvua kubwa zilizonyesha katika maeneo mbalimbali na kuleta athari za mafuriko, kuharibu mashamba, mali na hata kuchukua uhai wa Watanzania wenzetu. Aidha, kwa sababu mbalimbali tasnia ya wanautamaduni, wasanii na wanamichezo imepoteza watu nguli katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Mei, 2024. Niungane na Viongozi wakuu wa Kitaifa kuendelea kutoa pole kwa wote waliokumbana na majanga hayo, na kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu kuwapa

subra na uvumilivu katika kipindi hiki, kwani subira yavuta heri. "Tunaziombea kwa Mwenyezi Mungu roho za marehemu wote azipokee na kuzilaza mahali pema peponi". Amina.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba yangu imezingatia Maelekezo na Mwogozo uliotolewa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2023/24 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2024/25 aliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 3 Aprili, 2024. Aidha, kwa kuwa mtoto akibebwa hutazama kisogo cha mamaye, hotuba hii imezingatia Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipolihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa Kipindi cha Mwaka 2020 – 2025; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Mpango Mkakati wa Wizara (2021/22 - 2025/26); na Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali ya Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; na maelekezo mbalimbali ya viongozi wakuu wa Serikali.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba yangu imegawanyika katika sehemu nane: Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Dira, Dhima, Majukumu, Misingi ya Mwelekeo, na Vipaumbele vya Wizara; Sehemu ya Tatu inaelezea Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka 2023/24 na Sehemu ya Nne inabainisha changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Sehemu ya Tano ni Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2024/25; Sehemu ya Sita ni Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2024/25; Sehemu ya Saba ni Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Mwaka 2024/25; na mwisho, Sehemu ya Nane ni shukurani kwa wadau mbalimbali wa Wizara.

## 2.0 MISINGI YA MWELEKEO, VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia Dira ya Wizara, majukumu mbalimbali lazima yatekelezwe na Wizara. Majukumu ya Wizara ni pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mipango, Miradi na Programu mbalimbali katika Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuendeleza shughuli za Utamaduni, Sanaa na Michezo na kusimamia shughuli za filamu na michezo ya kuigiza. Majukumu mengine ni kuimarisha utendaji na Rasilimali Watu Wizarani na kusimamia utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania (TFB), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), na Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Vilevile, Wizara inaratibu na kusimamia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza na kuimarisha utendaji kazi, Wizara inaongozwa na misingi saba ya kimkakati na kimageuzi ambayo ni kuwafikia wadau *(Outreach Programmes)*; mageuzi ya taasisi *(Institutional Reforms)*; utawala bora *(Good Governance)*; ujenzi wa miundombinu *(Infrastructure Construction)*; Kutafuta rasilimali pamoja na matumizi stahiki ya rasilimali; kuongeza ajira; na kubainisha, kukuza na kuongeza mchango wa sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Pato la Taifa.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** chini ya misingi hiyo, katika mwaka 2024/25 Wizara imejipanga kutekeleza maeneo ya kipaumbele kama ifuatavyo:

(i) Kufanya tamasha la utamaduni la kitaifa kuwa kubwa zaidi kwa kufanyika mikoa yote kwa kushirikiana na sekta binafsi, kwa ushindani, ambapo mkoa mshindi hufanya tamasha kwa mwaka unaofuata. Hii itaibua chachu ya kukuza na kulinda tamaduni zetu;

(ii) Kufungua vituo 100 vya ufundishaji Kiswahili kote Duniani kwa kushirikiana na Diaspora, lengo ni kukuza, kueneza na kubidhaisha zaidi Kiswahili;

(iii) Kukuza sanaa mtaa kwa mtaa kupitia programu ya BASATA Vibes ili kufikia kila mtaa nchini kuibua, kuilea na kuipatia jukwaa la kutangaza na kuuza sanaa yetu;

(iv) Kuipeleka sanaa yetu kimataifa zaidi kwa kuwaunganisha wasanii na masoko makubwa ya kimataifa ya sanaa;

(v) Kuimarisha utoaji wa mikopo na ruzuku kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania;

(vi) Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya utamaduni, sanaa na michezo kwa kuboresha miundombinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia;

(vii) Kufanya tafiti za kutambua mchango wa sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo katika uchumi;

(viii) Kuianza safari ya mafanikio ya AFCON 2027 kwa kuandaa Kombe la Mataifa ya Afrika – CHAN 2024 yatakayofanyika Septemba 2024; kujenga miundombinu na timu imara ya Taifa kwa ajili ya AFCON 2027; Katika hili, timu imara ya Taifa itaandaliwa kwa kuwa na timu tatu za vijana chini ya miaka 17 (itakayotokana na UMISSETA na UMITASHUMTA); chini ya miaka 20 na chini ya miaka 23, makocha wazoefu wataajiriwa na huduma za timu hizi zitasimamiwa kama programu maalumu ya Serikali kuifikia AFCON 2027;

(ix) Kuanza safari ya Kombe la Dunia 2030;

(x) Ujenzi wa miundombinu ya michezo itakayotumika kwa mechi na mazoezi kwa timu zitakazoshiriki mashindano ya AFCON 2027;

(xi) Kuendelea kuwatumia wachezaji vijana wenye asili ya Tanzania kutoka katika kundi la Diaspora wanaocheza katika ligi mbalimbali Duniani katika mashindano ya kimataifa;

(xii) Ujenzi wa akademia 10 za kulea vipaji katika shule maalumu za michezo;

(xiii) Kuendesha kibiashara ligi kuu ya Tanzania na hususan michezo ya Dabi 'Derby' za watani wa Jadi, Simba na Yanga ili kuhakikisha ligi yetu inakuwa na thamani kubwa, timu zinatengeneza uchumi na zinafanikiwa kufika zaidi ya robo fainali katika mashindano ya kimataifa;

(xiv) Kuondoa migogoro kwa wadau wa utamaduni, sanaa na michezo kwa kuwa na katiba mfano kwa vyama na mashirikisho yote itakayotumiwa na vyama na mashirikisho yote ili kuboresha usimamizi katika utekelezaji wa majukumu kwa vyama na mashirikisho ya utamaduni, sanaa na michezo nchini;

(xv) Kutunga kanuni za uwazi za fedha kwa vyama na mashirikisho ya michezo; na

(xvi) Kutunga na kuhuisha Sera, mikakati, sheria, miongozo na kanuni za usimamizi wa sekta za utamaduni, sanaa na michezo ili kuzifanya zijiendeshe kibiashara zaidi, kuzalisha ajira na kujenga uchumi.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2023/24

### 3.1 MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA

#### 3.1.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Wizara ilikadiria kukusanya Shilingi Bilioni Moja (Shilingi 1,000,000,000) kutoka kwenye vyanzo viwili ambavyo ni mapato yatokanayo na viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru pamoja na Ada za mafunzo na mitihani kutoka Chuo cha Maendeleo ya

Michezo Malya. Vyanzo vyote vinatoka Idara ya Maendeleo ya Michezo. Hadi kufika mwezi Aprili, 2024 Shilingi Milioni Mia Sita Themanini na Tatu, Mia Tano na Mbili Elfu, Mia Saba na Nane (Shilingi 683,502,708), sawa na asilimia 68.3 ya lengo la mwaka zilikuwa zimekusanywa. Miongoni mwa sababu za kutofikia lengo ni pamoja na kusimama kwa matukio ya michezo ya Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza kutokana na kuwapo kwa Ukarabati mkubwa wa viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru vilivyosababisha kufungwa kwa viwanja vinavyohusika. Pamoja na makusanyo hayo, viwanja hivi hulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa viingilio vya milangoni na timu za mataifa na vilabu vya kimataifa vinavyotumia kiwanja huchangia mapato yasiyo ya moja kwa moja kutokana na kuishi nchini na kutumia huduma za hoteli, usafiri, bima, fedha, utalii, n.k.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza makusanyo ya mapato ikiwamo kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu katika viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru, ili kuwezesha kuvutia mashabiki wengi zaidi; kuongeza hamasa katika michezo ikiwamo zawadi mbalimbali kwa washindi ili kuhamasisha matokeo mazuri yatakayochochea ushabiki na hatimaye mapato; na ufuatiliaji wa karibu wa madai ya pango kwa mujibu wa mikataba ya upangaji.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tisa Sabini, Mia Nne Ishirini na Nane Elfu (Shilingi 5,970,428,000). Hadi kufikia mwezi Aprili 2024, Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Sita Thelathini na Mbili, Mia Moja na Saba Elfu, Mia Nane Sabini na Nne na senti tisini na tano (Shilingi 5,632,107,874.95) sawa na asilimia 94 ya lengo zilikuwa zimekusanywa. Sababu kuu ya kuimarika kwa makusanyo ya jumla ya taasisi za Wizara ni utekelezaji wa mikakati bunifu ya kuifanya sekta kujiendesha kiuchumi zaidi kupitia ushirikiano na sekta binafsi na wadau wa maendeleo. Taasisi ziliendesha changizo na harambee mbalimbali kwa wadau. Katika kuunga mkono hatua hizi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alichangia Shilingi milioni

500 kwa ajili ya timu zetu za Taifa. Mchango huu binafsi wa Mheshimiwa Rais ndio ulioipeleka timu yetu ya Mpira wa miguu katika mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika – AFCON nchini Ivory Coast mwezi Januari na Februari 2024. Tunathamini mchango huu mkubwa na Wizara inaahidi kusimamia vyema taasisi hizi kujiendesha kibiashara ili zitengeneze ajira na uchumi zaidi.

**3.1.2 Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha**

**23.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara iliidhinishiwa bajeti yenye jumla ya Shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Nne Arobaini na Tano, na Arobaini na Moja Elfu (Shilingi 35,445,041,000). Kati ya fedha hiyo, Mishahara ni Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Sita Hamsini na Moja, Mia Mbili Themanini na Tano Elfu (Shilingi 9,651,285,000), Matumizi Mengineyo ni Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Tisa Sitini na Mbili, Mia Tano Tisini na Sita Elfu (Shilingi 13,962,596,000) na Miradi ya Maendeleo ni Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nane Thelathini na Moja, Mia Moja Sitini Elfu (Shilingi 11,831,160,000).

**24.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na majukumu mengi na makubwa ambayo Wizara inatakiwa kuyatekeleza hasa ukizingatia mwaka 2027 nchi za Tanzania, Kenya na Uganda zitakuwa wenyeji wa mashindano ya AFCON, Serikali ilitakiwa kuanza maandalizi mwaka 2023. Kutokana na bajeti ndogo iliyokuwa imetengewa, imeilazimu Serikali kuiongezea Wizara bajeti ili kuweza kutekeleza majukumu ambayo yanatakiwa kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2023/24. Majukumu makubwa yaliyoongezewa bajeti yalikuwa: Ukarabati wa uwanja wa Benjamin Mkapa; Ujenzi wa Akademia ya Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya; na ushiriki wa timu ya Taifa ya mpira wa miguu (Taifa Stars) katika mashindano ya kombe la mataifa ya Afrika – AFCON yaliyofanyika nchini Ivory Coast, Januari 2024.

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa muktadha huo, hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 bajeti ya mwaka 2023/24 imeongezeka na kufikia Shilingi Bilioni Arobaini na Nane, Milioni Mia Tatu Arobaini na

Nane, Mia Nane Ishirini na Saba Elfu, Mia Nane Tisini na Tano (Shilingi 48,348,827,895) ikiwa ni ongezeko la Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Tisa na Tatu, Mia Saba Themanini na Sita Elfu, Mia Nane Tisini na Tano (Shilingi 12,903,786,895). Hadi Aprili, 2024 Wizara imepokea jumla ya Shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Nne Themanini na Saba, Mia Tano Sitini na Sita Elfu, Mia Sita Themanini na Tano (Shilingi 40,487,566,685), sawa na asilimia 83.7 ya bajeti yote iliyotengwa mwaka wa fedha 2023/24. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Sita Hamsini na Nne, Mia Nane Themanini na Tisa Elfu, Mia Saba Sitini na Nane (Shilingi 7,654,889,768) ni Mishahara, sawa na asilimia 79 ya bajeti ya mishahara; Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Mbili Themanini na Nne, Mia Tatu na Mbili Elfu, na Kumi (Shilingi 19,284,302,010) ni Matumizi Mengineyo, sawa na asilimia 90 ya bajeti ya Matumizi Mengineyo; na Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Tano Arobaini na Nane, Mia Tatu Sabini na Nne Elfu, Mia Tisa na Saba (Shilingi 13,548,374,907) ni Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia 78 ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo.

## 3.2 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24

### 3.2.1 SEKTA YA UTAMADUNI

#### 3.2.1.1 IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya utamaduni imekasimiwa majukumu ya kulinda, kuhifadhi na kuendeleza urithi wa utamaduni wa Taifa ikiwamo lugha, mila, desturi, historia na maadili ya Taifa; kudumisha na kuendeleza utambulisho wa Taifa; kuhimiza na kukuza thamani ya utaifa kwa wananchi wote hususan vijana na watoto ambao ndiyo Taifa la leo na kesho; kuratibu na kusimamia maendeleo ya lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi; kuratibu na kufanya tafiti katika uga wa sekta ya utamaduni hususan lugha za kijamii ambazo ni kibebeo kikuu cha urithi wa utamaduni wa Taifa letu. Aidha, Sekta hii ya Utamaduni ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2023

hadi Aprili, 2024, Sekta hii imetekeleza majukumu mbalimbali kama ifuatavyo:

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa wananchi wa Tanzania wanaendelea kuenzi, kujivunia, kuthamini na kunufaika na urithi wa utamaduni wao, Wizara iliratibu Tamasha kubwa la Pili la Kitaifa la Utamaduni lililofanyika kuanzia tarehe 25 hadi 27 Agosti, 2023 Mkoani Njombe ambalo lilihusisha washiriki zaidi ya 2,000. Tamasha hilo lililenga kutoa fursa kwa Wananachi na wageni kutoka nje ya nchi kutambua, kujivunia na kujionea tamaduni, mila na desturi mbalimbali za Kitanzania kwa kufanya matembezi ya kiutamaduni, mashindano ya ngoma za asili na vyakula vya asili, maonesho ya kazi za mikono za kiutamaduni, sanaa na ubunifu pamoja na kuuza kazi hizo. Katika Tamasha hilo, jumla ya vikundi 18 vya ngoma za kitamaduni kutoka mikoa 17 ya Tanzania Bara na kikundi kimoja (1) kutoka Zanzibar vilishiriki katika Tamasha hilo ambapo kila Kikundi kilikuwa na washiriki 13 chini ya uongozi wa Afisa Utamaduni kutoka Mkoa husika. Aidha, Tamasha hilo lilihudhuriwa na Machifu na Viongozi wa Kimila; Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa Tanzania ikiwamo India na Malawi; Mashirika ya Kimataifa kama vile UNESCO; Taasisi zote za Wizara; Maafisa Utamaduni; wajasiriamali; na wananchi wa Mikoa jirani ya Iringa, Ruvuma, Mbeya na Songwe. Aidha, Tamasha hilo lilipambwa na shughuli nyingine zikiwamo bonanza la Michezo; utoaji wa elimu ya ujasiriamali kwa wananchi; huduma za mikopo inayotolewa na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa; uibuaji wa vipaji vya Sanaa kupitia programu ya Sanaa mtaa kwa mtaa; semina ya matumizi sanifu na fasaha ya Kiswahili kwa waandishi wa habari; elimu ya mchango wa Tanzania katika harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika na utoaji wa huduma za afya bure kwa wananchi na washiriki wote.

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, miongoni mwa manufaa yaliyopatikana katika Tamasha hilo ni pamoja na: kuchochewa kwa ari ya kuuishi, kuuenzi na kuuthamini urithi wa utamaduni wa Mtanzania uliojengwa kwenye misingi ya umoja, upendo, mshikamano, amani na utulivu; kurithishwa kwa urithi wa utamaduni kwa vijana na watoto ambao walishirikishwa katika

shughuli za ngoma za kiutamaduni na maonesho ya kazi za utamaduni na ubunifu; kuibuliwa kwa vipaji vya muziki na uchoraji; kutangazwa kwa uanuai wa urithi wa utamaduni kwa wageni kutoka mataifa ya nje; na kuongeza kipato kwa washiriki na kukuzwa kwa uchumi wa wananchi wa Mkoa wa Njombe kupitia uuzaji wa vyakula, nyumba za kulala wageni na uuzaji wa bidhaa mbalimbali zikiwamo za kiutamaduni.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo; Wizara iliendelea kuratibu na kushiriki katika matamasha, makongamano na Maadhimisho mbalimbali yakiwamo yaliyoandaliwa na Wadau wa Utamaduni kama vile Tamasha la Majimaji Selebuka lililofanyika kuanzia tarehe 22-29 Julai, 2023 Mkoani Ruvuma; Tamasha la 13 la Muziki wa Cigogo lililofanyika tarehe 22 - 23 Julai, 2023 Wilaya ya Chamwino, Mkoani Dodoma chini ya usimamizi wa Kituo cha Sanaa cha Chamwino yaani "Chamwino Arts Center (CAC)" ambapo wadau wa Utamaduni na Sanaa zaidi ya 700 walishiriki katika Tamasha hilo; Tamasha la Ngoma la Asili Yetu lililofanyika tarehe 07-08 Novemba, 2023 Jijini Dodoma chini ya usimamizi wa Taasisi ya Sanaa na Michezo ya Yamnyausi (Yamnyausi Organization for Arts and Sports) ambapo zaidi ya wadau wa Utamaduni 800 walishiriki katika Tamasha hilo; na Tamasha la Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Mashujaa wa Vita vya Majimaji lililofanyika tarehe 24-27 Februari, 2024 katika Viwanja vya Mashujaa wa Vita vya Majimaji Songea, Mkoani Ruvuma na kuvutia washiriki zaidi ya 1,000. Kwa ujumla wake, matamasha haya hutoa fursa na nafasi kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini kusherekea na kudumisha urithi wa utamaduni wa Taifa na kuonesha kwa vitendo kuwa Taifa bado ni hai na lina sifa ya kuendelea kuitwa Taifa.

**30.** ***Mheshimiwa Spika***, mojawapo ya mambo ya kujivunia kama Taifa ni kupanuka kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Afrika sambamba na kutambuliwa kwa lugha hii na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa kama lugha rasmi ya mawasiliano na hivyo kuifanya lugha hii kuwa bidhaa yenye thamani kubwa mbele ya uso wa dunia. Kitendo cha lugha ya Kiswahili kutambuliwa kuwa Lugha rasmi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

(SADC), na Umoja wa Afrika (AU), kimeiongezea hadhi, nafasi na thamani ya lugha hii na hivyo kuifanya kuwa fursa ya kukuza diplomasia ya uchumi na utangamano miongoni mwa watumiaji. Jambo la kufurahisha zaidi ni kuwapo kwa Tamko la Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwamba tarehe 7 Julai ya kila mwaka ni Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani. Siku hii imeendelea kusherehekewa katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa. Mathalani, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) pamoja na Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) kwa mwaka 2023 ziliadhimisha kwa kundaa Mbio za Masafa ya Kiswahili yaani Kiswahili Marathoni ambazo zilifanyika Arusha tarehe 01 Julai, 2023. Maadhimisho hayo yaliendelea Visiwani Zanzibar katika ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil tarehe 04 na 05 Julai, 2023 na hatimaye Ukumbi wa Chuo cha Polisi Ziwani tarehe 06 hadi 07 Julai, 2023. Aidha, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika maadhimisho ya Pili ya Kikanda ya Siku ya Kiswahili Duniani kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika kuanzia tarehe 05 hadi 07 Julai, 2023 katika Jiji la Kampala nchini Uganda ambapo mada mbalimbali kuhusu maendeleo ya Kiswahili na fursa za kiuchumi zinazotokana na lugha ya Kiswahili zilijadiliwa. Vilevile, Wizara iliratibu Kongamano la Nne (4) la Kimataifa la Idhaa za Kiswahili Duniani lililofanyika tarehe 18 hadi 22 Machi, 2024 Jijini Mbeya na kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya 900 kutoka ndani na nje ya nchi.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** Fauka ya hayo, kumekuwa na mwitikio chanya kwa vyama vya Kiswahili na wadau katika kuchagiza matumizi na maendeleo ya Kiswahili ambapo Wizara iliratibu Kongamano la Sita la Chama cha Lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania (CHALUFAKITA) lililofanyika Mkoani Mwanza tarehe 09-10 Agosti, 2023. Lengo la Kongamano hilo lilikuwa ni kujadili mustakabali wa lugha ya Kiswahili na maendeleo yake ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara iliratibu Tamasha la Tatu (3) la Washairi Tanzania lililoandaliwa na Chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA) kwa kushirikiana na Chama cha Kukuza na Kuendeleza Washairi Zanzibar (CHAKUWAZA) tarehe 11-12 Agosti, 2023 kwa lengo la kuhimiza matumizi sanifu na fasaha ya Kiswahili; na Kongamano la nane (8) la Chama

cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani (CHAUKIDU) lililofanyika 14-16 Desemba, 2023 Jijini Arusha kwa lengo la kujadili maendeleo ya lugha ya Kiswahili duniani na kuweka mikakati ya kukikuza zaidi. Vilevile, katika kuchangamkia fursa za lugha ya Kiswahili, Wizara iliratibu maandalizi ya Andiko la Mpango Kazi wa utekelezaji wa Mkakati wa Kubidhaisha Kiswahili ambapo Kikao cha Kamati ya watalaamu kilifanyika tarehe 12-13 Septemba, 2023 mkoani Morogoro na kufuatiwa na Kikao kingine tarehe 05 Oktoba, 2023 kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kupokea maoni ya uboreshaji wa rasimu ya andiko hilo.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa tunaongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu ya kutoa huduma bora kwa wananchi wa Tanzania kupitia Sekta ya Utamaduni, Wizara ilifanya Kikao Kazi cha Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo nchini kilichofanyika tarehe 28-29 Agosti, 2023 katika Ukumbi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Mkoani Njombe. Jumla ya Maafisa Utamaduni na Michezo 250 kutoka katika Halmashauri, Wilaya na Mikoa walishiriki katika Kikao Kazi hicho. Kikao hicho kilijikita katika kujadili masuala muhimu ya ukuaji wa Sekta ya Utamaduni na Michezo ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Utamaduni ya mwaka 1997 katika ngazi za Serikali za Mitaa; kuchagiza fursa zinazotokana na sekta hii na namna ya kuzichangamkia; kubaini changamoto na kupendekeza njia za kuzitatua; na kutoa miongozo mbalimbali ya namna ya kutekeleza Shughuli za Wizara katika maeneo yao.

**33.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa tunalinda, kudumisha na kuendeleza maadili ya Mtanzania yanayozingatia mila, desturi na miiko ya Taifa letu yaani ustaarabu tulioupokea kutoka kwa waasisi wa Taifa na mababu zetu, Wizara imeendelea kuhamasisha na kutoa elimu ya maadili mema kwa umma kupitia vipindi vya redio na televisheni, matamasha na midahalo mbalimbali katika kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini. Vipindi vya elimu ya maadili vilitolewa katika televisheni na redio mbalimbali zikiwamo TBC, Azam TV, ITV, Radio One, Clouds FM, na Wapo Redio katika Mkoa wa Dar es Salaam; AFm Radio katika Mkoa wa Dodoma; ICE FM, Kings FM na Uplands FM katika Mkoa wa Njombe. Pia, Wizara iliendesha

mdahalo maalumu wa Maadili wakati wa Tamasha la Pili la Kitaifa la Utamaduni lililofanyika tarehe 25-27 Agosti, 2023 Mkoani Njombe ambapo mdahalo huo ulifanyika tarehe 26 Agosti, 2023. Mdahalo huo uliwakutanisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, Maafisa Utamaduni, Maafisa Ustawi wa Jamii, Lishe na Waratibu wa Vituo vya Mama na Mtoto, lengo likiwa kupokea maoni na mapendekezo ya namna ya kukabiliana na mmomonyoko wa Maadili katika Taifa letu.

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na jitihada za Serikali za kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kulinda maadili ya Mtanzania kwa kukemea vitendo viovu vinavyokiuka maadili yetu kama vile ubakaji, ulawiti, mahusiano ya jinsia moja, ubadhilifu wa mali za umma, rushwa, n.k, naomba nitumie fursa hii kuliomba Bunge lako na Watanzania wote wanaonisikiliza, kuwa suala la kukabiliana na mmomonyoko wa maadili ni jukumu la kila Mtanzania. Ni lazima tuwalinde watoto na vijana wetu na vitendo viovu kama vile matumizi ya dawa za kulevya na mahusiano ya jinsia moja. Vitendo hivi vinaonekana kuchagizwa na mageuzi makubwa ya teknolojia na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii ambako vijana wetu wanapenda kutumia muda mwingi kuangalia na kusoma vitu visivyofaa. Nazisihi Taasisi zote kuanzia ngazi ya familia kulipa kipaumbele suala la kupinga mmomonyoko wa maadili kwani tusiposimama pamoja kuwalinda watoto wetu, tutakuwa tumeliangamiza Taifa la kesho kwa mikono yetu wenyewe.

**35.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kutekeleza Mikataba ya Kimataifa kuhusu kulindwa kwa urithi wa utamaduni usioshikika, katika Kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili 2024, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliandaa Taarifa ya miaka minne (4) kuanzia mwaka 2020 hadi 2024. Taarifa iliyoandaliwa ni ya utekelezaji wa Mkataba wa UNESCO wa mwaka 2003 kuhusu kulinda Urithi wa Utamaduni usioshikika. Taarifa hiyo ilijumuisha masuala mbalimbali yakiwamo ushirikishwaji wa jamii katika kutambua na kuorodhesha vipengele vya urithi wa utamaduni usioshikika; changamoto zinazokwamisha uorodheshaji na uhifadhi wa urithi wa utamaduni usioshikika; wajibu wa Asasi zisizo za Kiserikali na sekta binafsi katika kuhifadhi na kulinda urithi

wa utamaduni usioshikika; sera, sheria na miongozo inavyolinda na kuhamasisha ushirikishwaji wa jamii katika kulinda urithi wa utamaduni usioshikika. Masuala mengine ni urithi wa utamaduni kufungamanishwa na maendeleo endelevu, utunzaji wa mazingira, kuhamasisha amani na umoja miongoni mwa wanajamii na ubunifu wa kazi na bidhaa mbalimbali za utamaduni na ubunifu; jamii kuishi pamoja kwa kuvumiliana na kustahimiliana licha ya kuwapo tofauti za mila, desturi, historia, lugha miongoni mwa jamii hizo; umuhimu wa kuzingatia urithi wa utamaduni katika programu na mipango ya maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa; na utumiaji wa vyombo vya habari na teknolojia ya habari na mawasiliano katika kutangaza, kulinda na kuendeleza urithi wa utamaduni usioshikika kwa manufaa ya kiuchumi. Matokeo ya taarifa hiyo ni pamoja na kupanua wigo wa uelewa wa jamii kuhusu masuala ya urithi wa utamaduni usioshikika na kuutumia kama fursa ya kukuza uchumi wao.

### 3.2.1.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) liliundwa kwa sheria ya Bunge Na. 27 ya mwaka 1967 na marekebisho ya mwaka 1983 na mwaka 2016. Kutokana na sheria hii Baraza ndilo Wakala wa Serikali mwenye mamlaka ya kusimamia maendeleo ya lugha ya Kiswahili nchini pamoja na kutoa ithibati ya matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili. Aidha, BAKITA ina jukumu la kuratibu vyama, Asasi na wadau wote wanaojishughulisha na ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufuatilia maendeleo yake nje ya nchi. Majukumu mengine ni pamoja na kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za Serikali na umma. Katika kipindi hiki mafanikio lufufu yamepatikana kama ifuatavyo:

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BAKITA, iliandaa maadhimisho ya pili ya Siku ya Kiswahili duniani (MASIKIDU) yaliyofanyika duniani kote tarehe 07 Julai, 2023. Kwa hapa Tanzania maadhimisho yalifanyika Zanzibar. MASIKIDU ya mwaka 2023 yalifana, ambapo yalianza kwa Mbio za Masafa za Kimataifa za Kiswahili zilizofanyika Jijini Arusha tarehe 01 Julai,

2023 na kuwahusisha jumla ya wakimbiaji 323. Malengo ya mbio hizo yalikuwa kuleta ari na mwamko kwa Tanzania, Afrika na Duniani kote ili kuyapa hadhi Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani, kuchochea na kuendeleza juhudi za kutangaza utalii wa Tanzania ambazo zilianzishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kupitia filamu aliyoianzisha ya *Royal Tour*.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuelekea kilele cha MASIKIDU 2023 kulikuwa na Mkutano wa Wahariri wakuu wa redio na televisheni ambao ulifanyika tarehe 4 Julai, 2023. Mkutano huo ulihudhuriwa na jumla ya wahariri 137. Aidha, tarehe 5 Julai, 2023 kulikuwa na mjadala mpana wa wazi kuhusu nafasi ya Kiswahili duniani kwa sasa, na wachokoza mada wakuu walikuwa Prof. Patrice Loch Otieno Lumumba wa Kenya na Prof. Amani Lusekelo Mwamakombe wa Tanzania. Mjadala huu ulikuwa na tija kubwa kwa washiriki kupata wasaa wa kushirikishana uzoefu kupitia mjadala huo na pia kutathmini kwa kina namna nchi za Afrika Mashariki zilivyojipanga kunufaika kupitia nafasi ya Kiswahili hivi sasa na nini malengo ya baadaye. Tarehe 6 Julai, 2023 ilikuwa siku ya wanafunzi ambapo washindi wa uandishi wa insha kwa Tanzania Bara na Zanzibar walitunukiwa tuzo pamoja na shule zao kupata zawadi. Lengo la tukio hili ni kujenga kizazi kitakachoendelea kuenzi maadhimisho haya na kuwajengea ari ya kukipenda Kiswahili.

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na hayo siku ya kilele cha Maadhimisho ya MASIKIDU yalifanyika Ukumbi wa Chuo cha Polisi, Bomani Zanzibar tarehe 07 Julai, 2023. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi alikuwa mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho. Maadhimisho haya yalihudhuriwa na washiriki takribani 2,601 wakiwamo wa nje ya nchi ambao ni Urusi, Uingereza, China, Ghana na Zimbabwe. Pia, Mabalozi mbalimbali na wakurugenzi wa mashirika ya kimataifa akiwamo Mkurugenzi wa UNESCO nchini Tanzania, walishiriki. Kupitia maadhimisho haya BAKITA na BAKIZA zimefanikiwa kuanzisha ushirikiano kati yake na Chuo kikuu cha Taifa cha *Institute of Asian and African studies of M.V.*

*Lovonosov Moscow* ambapo tayari Hati ya ushirikiano imesainiwa.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** mojawapo ya majukumu ya BAKITA ni kukiimarisha Kiswahili ndani na nje ya nchi. Katika kipindi hicho, BAKITA iliendesha Mtihani wa Kupima Umahiri wa Lugha kwa wageni 49 walioingia nchini kwa malengo mbalimbali ikiwamo kufanya kazi, biashara na shughuli za kidiplomasia. Miongoni mwa wageni waliofanya mitihani hiyo ni madaktari 23 kutoka nchi za Afrika Kusini; Angola; Comoro; Ghana; Nigeria; Uganda na Zimbabwe. Aidha, mabalozi, maafisa wa ubalozini na raia wengine 10 wa nchi za Denmark, Italia, Jamhuri ya Cheki; Polandi, Uingereza, na Uswisi walifanya mtihani huo. Jukumu hilo lilitekelezwa kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia kikao chake na Mabalozi kilichofanyika Zanzibar mwezi Novemba, 2022. Vilevile, BAKITA iliendesha Mafunzo ya Kiswahili kwa wageni 20 wakiwamo mabalozi wa nchi za Uturuki, Misri na Zambia hapa nchini. Aidha, wageni wengine waliohudhuria mafunzo hayo nje ya mabalozi ni raia kutoka nchi za Angola, Algeria, Marekani, Uingereza, Scotland, Denmark, Zimbabwe, na Komoro. Mafunzo hayo yalitolewa katika ofisi yalipo Makao Makuu ya BAKITA. Pia, BAKITA iliendelea kuimarisha na Kusimamia Mfumo wa *SwahiliPrime* wa kufundisha Kiswahili kwa Wageni kwa njia ya mtandao ambapo hadi Aprili, 2024 wanafunzi 100,000 waliingia kwenye mfumo wa kujifunza Kiswahili. Wanafunzi walioingia katika mfumo walitoka nchi mbalimbali ambapo miongoni mwa nchi hizo ni Marekani, Tanzania, Kenya, Uganda, Uingereza, Ujerumani, Vietnamu, Afrika Kusini, Ugiriki, Kanada, India na Zambia.

**41. *Mheshimiwa Spika***, Sambamba na hayo BAKITA ilitoa afunzo ya mbinu za kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni kwa diaspora na wenyeji wa nchi zinazohusika ambapo BAKITA kwa kushirikiana na Balozi za Tanzania ilitoa mafunzo kwa diaspora na wenyeji 111 katika nchi za Ufaransa (38), Uswisi (29), Uturuki (17) na Komoro (27). Aidha, BAKITA iliwezesha kutoa mafunzo kwa walimu watakaofundisha, kutoa ushauri wa kitaalamu wa namna ya kufundisha na kutoa vitabu 242 vya kufundishia na

kujifunzia kwenye Balozi hizo. Aidha, kupitia mafunzo haya BAKITA imepata fursa ya kuanzisha ushirikiano na taasisi za nje ikiwa ni pamoja na Assalam Foundation – Uturuki, Chuo Kikuu cha *Institut National des Language et Civilisations Orientales* (INALCO) - Ufaransa, *Universite de Sciences* - Ufaransa na shule za Kimataifa za *Junior School* ya nchini Zimbabwe, na *Maputo International School* ya Msumbiji ambayo tayari imeanza kufundisha Kiswahili kwa kutumia mwalimu Mtanzania.

Aidha, Ubalozi wa Tanzania mjini Moscow nchini Urusi uliratibu Kongamano la Utamaduni na lugha ya Kiswahili lililofanyika tarehe 4 Aprili, 2024 katika Chuo Kikuu cha Patrice Lumumba (RUDN) nchini humo. Kongamano hilo liliambatana na uzinduzi rasmi wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika chuo hicho.

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, BAKITA imeendeleza kongoo ya Kiswahili kwa kuongeza maneno milioni 7 ambapo kwa sasa kongoo hiyo ina jumla ya maneno milioni thelathini na nne (34,000,000) kati ya maneno milioni hamsini (50,000,000) sawa na lengo la asilimia 68. Maneno haya yalichukuliwa kutoka kwenye mitandao ya kijamii, tovuti za Serikali na mashirika ya umma na binafsi na kuskani machapisho mbalimbali yaliyoandikwa kwa Kiswahili. Kongoo hii inalenga kuhakikisha Kiswahili kinasheheni katika uwanja wa kiteknolojia na hususan Akili Mnemba. Aidha, wataalamu na watu mbalimbali watakuwa na uwezo wa kuitumia kongoo hili kwa shughuli za uandishi wa kamusi, ujifunzaji wa Kiswahili, uandishi wa vitabu na tafiti mbalimbali.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Halikadhalika BAKITA imeendelea kuuelimisha umma kuhusu kuzingatia matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, BAKITA iliandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 884 kupitia redio na televisheni za Redio One, TBC- Taifa, TBC1, Clouds Fm, Kiss FM, U-FM, WAPO Redio, MVIWATA FM, Redio Maria, Redio Idea, Redio Shine na Idhaa ya Kiswahili ya Redio ya Umoja wa Mataifa. Aidha, BAKITA iliandaa jumla ya makala 42 zilizochapishwa katika gazeti la Habari Leo toleo la kila siku ya Ijumaa. Vilevile, BAKITA ilitoa jarida la mtandaoni linalojulikana kama Lugha ya Taifa mara 10. Fauka ya hayo, BAKITA ilirusha maudhui

mbalimbali yanayohusu sarufi na fasihi ya Kiswahili kupitia akaunti zake za mitandao ya kijamii ikiwamo X (zamani Twitter), Facebook, Instagram na chaneli ya Youtube. (Facebookbakitatz, Instagram - bakita_tz na X– bakita_tz, Youtube – Kiswahili TV) na Kirungu cha BAKITA kimebuniwa kwa lengo la kuelekeza matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili. Maudhui haya yamefanya BAKITA iwe na takribani wafuasi 69,925 wa akaunti zake kwa ajili ya kujifunza lugha na kujenga ulumbi wa lugha.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili kwa wageni ni sehemu ya utekelezaji wa *Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili*. Katika kipindi hiki, BAKITA lilitoa mafunzo ndani ya nchi kwa walimu 258 sawa na asilimia 103.2 ya lengo la kufundisha walimu 250 wa kufundisha wageni. Mafunzo hayo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni yamefanyika katika mikoa mitatu ya Tanzania Bara ambayo ni Iringa (24), Dar es Salaam (97) na Mwanza (137). Manufaa ya mafunzo haya ni kujenga uwezo wa nchi wa kuteka soko la Kiswahili ndani na nje ya nchi na kuwabaini wahitimu wa Kiswahili kwa kila mwaka kupitia vyuo vikuu nchini.



*Mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa wahitimu wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) Mwanza, yaliyofanyika mwezi Julai, 2023.*

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** BAKITA katika kutoa huduma ya tafsiri kwa nyaraka mbalimbali, lilitafsiri jumla ya kazi kubwa na ndogo

990 sawa na asilimia 141 ya lengo la tafsiri ya nyaraka 700 ambazo zilitafsiriwa kutoka na kwenda Kiswahili kwa lugha za Kichina, Kiingereza, Kiarabu, Kihindi, Kigujarati, Kijerumani, Kifaransa, Kireno, Kihispaniola, Kiitaliano, Kifarsi (Kiajemi) na Kikorea. Aidha, hadi Aprili 2024 Baraza lilithibitisha nyaraka kubwa na ndogo 2,819 sawa na asilimia 94 ya lengo la nyaraka 3,000.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufanikisha jitihada za Serikali za kuongeza idadi ya wakalimani, BAKITA iliendesha mafunzo ya kuimarisha stadi za ukalimani kwa wakalimani 32 sawa na asilimia 106 ya lengo la wakalimani 30 wa lugha za Kiarabu, Kifaransa, Kijerumani, Kirusi, Kireno na Kiingereza, na kufanya Tanzania kuwa na jumla ya wakalimani 150. Lengo la programu hiyo ni kuhakikisha Taifa linapata wataalamu wa kutosha na wenye weledi katika kutoa huduma ya ukalimani, kwenye mikutano ya kitaifa na kimataifa.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** fauka ya hayo, jumla ya mikutano 16 ilipatiwa huduma ya ukalimani. Mikutano hiyo ni pamoja na Mkutano wa 23 wa Mwaka wa Mapitio ya Kitaalamu ya Sekta ya Afya uliondaliwa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dodoma; Mkutano wa Kawaida wa 77 wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu (ACHPR) uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha nchini Tanzania; Mkutano wa 24 wa Tume ya Misitu na Wanyamapori ya Afrika uliofanyika katika Hoteli ya Gran Melia Jijini Arusha; Mkutano Kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi – Tukio la ziada katika Mkutano wa 77 wa Kawaida wa ACHPR - uliofanyika kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa jijini Arusha; Mkutano wa Kukabiliana na Hotuba zinazopinga Haki za Binadamu katika Utetezi wa Haki za Binadamu barani Afrika ulioandaliwa kwa Ushirikiano wa Asasi za Kiraia za Afrika (ACSE) uliofanyika katika hoteli ya Mount Meru, Arusha; Mkutano wa Tathmini na Mipango wa Kikosi Kazi cha hafla ya ECOSOC katika Mkutano wa 77 wa Kawaida wa ACHPR - uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC); na Mkutano wa Mradi wa Lishe uliodhaminiwa na USAID mjini Kigoma. Huduma hii ya ukalimani

katika mikutano hii inatokana na kukubalika kwa Kiswahili kama lugha rasmi katika jumuiya za kitaifa, kikanda na kimataifa. Aidha, idadi inatarajiwa kuongezeka sana kutokana na mvuto wa lugha ya Kiswahili kwa mataifa na jumuiya mbalimbali.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza kasi ya kufundisha lugha ya Kiswahali kama lugha ya Kigeni, BAKITA ilitambua Vituo kumi na kimoja (11) vya kufundisha Kiswahili kwa wageni, ambapo vituo viwili (2) viko nje ya Tanzania katika nchi za Ufaransa na Uturuki na vituo tisa (9) viko hapa nchini katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Arusha. Hivyo, Tanzania kwa sasa ina vituo 44 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni ambapo miongoni mwao 16 viko nje ya nchi na 28 viko nchini. Utekelezaji huu unafanyika ili kukidhi matakwa ya Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili wa miaka kumi kuanzia mwaka 2022 hadi mwaka 2032. Fauka ya hayo, BAKITA imefanya utafiti na kubaini jumla ya vituo na vyuo zaidi ya 150 vinafundisha Kiswahili nje ya nchi na Watanzania zaidi ya 113 wanafanya kazi kupitia Kiswahili na taaluma zake husianifu huko ughaibuni.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BAKITA katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 imesajili Wataalamu wa Kiswahili 328 katika Kanzidata sawa na asilimia 82 ya lengo la kusajili watalaamu 400, ambapo hadi sasa kanzidata ina jumla ya wataalamu 1,820 ambapo miongoni mwao wanawake ni 989 na wanaume ni 831. Kwa mujibu wa kanzidata hiyo mgawanyo wa wataalamu kwa kigezo cha elimu ni kama ifuatavyo: shahada ya kwanza 1,606, Shahada ya uzamili (umahiri) 189 na shahada ya uzamivu 25. Lengo la kuwasajili wataalamu hawa ni kuwaandaa kuchangamkia fursa zinazotokana na kupanuka kwa mahitaji ya lugha ya Kiswahili duniani.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jukumu la kutoa ithibati ya matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu, BAKITA kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 imetoa ithibati kwa miswada ya vitabu 60 vya kiada na ziada sawa na asilimia 70.5 ya lengo la miswada 85. Vitabu hivi viliwasilishwa na Taasisi ya Elimu Tanzania, Room to Read, Mkuki na Nyota, E&D Vision, KIUTA, Aznas Printing na waandishi binafsi. Aidha, katika

kusimamia matumizi Bora ya Kiswahili kwa Waandishi na Watangazaji kutoka vyombo vya habari nchini, BAKITA iliendesha mafunzo kwa waandishi na watangazaji 166 ambapo waandishi na watangazaji 137 walipatiwa mafunzo Zanzibar na waandishi 29 walipatiwa mafunzo mkoani Njombe. Vilevile, BAKITA iliendesha kongamano la idhaa za Kiswahili za ndani na nje ya Tanzania tarehe 18 - 22 Machi 2024 jijini Mbeya ambapo mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.). Kongamano hili lilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 900. Miongoni mwa idhaa za nje zilizoshiriki ni Deutsche Welle – DW ya Ujerumani, Redio ya Kimataifa China - CGTN, Radio France International, Redio ya Taifa ya Malawi - MBC, Redio Burundi, Redio Kwanza ya Kenya na Redio Sauti ya Injili Goma – Kongo.

**51.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na kazi kubwa iliyofanywa kwenye eneo hili la lugha adhimu na aushi ya Kiswahili, ninapenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi sasa Lugha hii ni miongoni mwa lugha saba (7) kubwa zenye wazungumzaji wengi Duniani ambapo Kiswahili kina wazungumzaji takribani Milioni Mia Tano (500). Kwa msingi huo tuna kila sababu ya kujivunia na kutembea kifua mbele kutokana na mafanikio tuliyoyapata ya Lugha ya Kiswahili na hivyo tusikubali mtu yeyote aipuuze au kuibeza lugha yetu kwani kwa hivi sasa imetupa utambulisho wa pekee duniani.

**3.2.1.3 KITUO CHA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa masuala muhimu kwa Taifa lolote ni kuenzi na kuendeleza historia na urithi wa Taifa hilo kwa manufaa ya kizazi kilichopo na kijacho. Aidha, changamoto za kufundisha na kujifunza historia, hususan katika muktadha wa itikadi ya Umajumui wa Afrika, ni uhaba na kutokufahamika kwa vyanzo vyenye taarifa zinazofaa kwa kazi hiyo. Hata hivyo Tanzania ni miongoni mwa nchi katika Bara la Afrika yenye hazina kubwa ya hifadhi ya maeneo, vifaa, nyaraka na machapisho yanayoeleza historia ya ukombozi wa Bara la Afrika yaliyo chini ya Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika kinachosimamiwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na

Michezo. Hiki sio Kituo cha Kitaifa tu, bali ni Kituo cha Kimataifa cha Bara la Afrika kilichoanzishwa kwa Azimio Maalumu la Umoja wa Afrika (African Union (AU) mwaka 2011 na kuipa heshima Tanzania kuratibu uanzishwaji wa Makao Makuu yake.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa nia ya dhati napenda kutoa shukurani za pekee kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha zaidi ya bilioni moja kwa ajili ya ukarabati wa maeneo ya urithi wa ukombozi wa Afrika. Aidha, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kimetekeleza majukumu yafuatayo: Kufanya ukarabati mkubwa wa jengo la kihistoria la yaliyokuwa Makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) ambapo mipango na mikakati yote ya kuzikomboa nchi za Afrika ilifanyika hususan za Kusini mwa Afrika. Ukarabati wa jengo umefikia asilimia 99 ambapo gharama zilizotumika ni Shilingi Bilioni Moja, Milioni Themanini na mbili, Mia Tisa Kumi na Saba Elfu, Mia Nne Sabini na Tisa na Senti Themanini na Nane (Shilingi 1,082,917,479.88). Kukamilika kwa ukarabati huo kutawezesha eneo la kituo kuwa muhimu na kutembelewa na nchi zilizotumia eneo hilo wakati wa ukombozi pia pamoja na nchi nyinginezo ambazo hazikulitumia.



*Jengo lililotumiwa na Kamati ya Ukombozi ya OAU likiwa limekarabatiwa*

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika kimefanya ukarabati wa kiuhifadhi wa handaki la kihistoria lililopo Wilaya ya Kongwa, Dodoma ambalo lilijengwa na kutumiwa na Rais wa Kwanza wa nchi ya Msumbiji Hayati Samora Machel wakati akiratibu mafunzo ya kijeshi kwa wapigania uhuru wa nchi yake. Gharama za ukarabati wa handaki hilo ni Shilingi Milioni Tisa, Mia Nane Hamsini na Mbili Elfu (9,852,000). Handaki hilo ni kivutio kikuu cha utalii wa kiukombozi katika eneo hilo la kihistoria la Kongwa ambapo viongozi, wanafunzi na watafiti wa ndani na nje ya nchi hufika kutembelea eneo hilo. Kwa kuwa eneo hilo lipo hapahapa Dodoma, naomba nitumie fursa hii kukualika wewe Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge mliopo hapa kutembelea eneo hilo lililosheheni kumbukumbu za historia ya ukombozi wa Afrika ili muweze kujionea ninyi wenyewe utajiri wa historia hiyo.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa jamii inafahamu na kupata sura halisi ya historia hii na mchango wa Tanzania katika ukombozi wa Afrika, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kimeendelea kutoa elimu kupitia

vipindi vya redio, Televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii. Aidha, Kituo kimeingia makubaliano maalumu na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) kwa kuanzisha vipindi maalumu vya kurusha maudhui ya elimu kwa jamii kuhusu historia ya ukombozi wa Afrika na mashujaa wake kama vile Hayati Mwl. Nyerere, Samora Machel, Brg. Gen. Hashim Mbita, n.k. Vipindi hivyo ni kipindi cha **"Ng'ariza Afrika"** na kipindi cha **"Miviga".** Nitoe wito kwa Watanzania wote kuvifuatilia vipindi hivi ambavyo hurushwa kila Siku ya Jumamosi saa moja usiku na Jumanne saa nane mchana.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo kimeendelea kufanya mahojiano na Wazee walioshiriki na kushuhudia harakati za ukombozi wa Afrika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Njombe, Songea na Kagera kwa ajili ya kuhifadhi taarifa zao. Kwa kipindi hiki jumla ya watu 81 walioshiriki katika mapambano ya ukombozi wamehojiwa na hivyo kufanya jumla ya watu waliohojiwa kufikia 281. Mahojiano hayo hutumiwa kuandalia vipindi vya Televisheni, redio na makala fupi ambazo hurushwa kwenye mitandao ya kijamii kwa ajili ya kutoa elimu kwa Watanzania.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sambamba na hayo, Kituo kimekusanya Hotuba za sauti za viongozi mbalimbali wa Afrika waliokuwa mstari wa mbele katika ukombozi wa Bara la Afrika. Hotuba zaidi ya 920 zikiwamo za Baba wa Taifa, Hayati Mwl. Julius K. Nyerere zinazohusu harakati za ukombozi wa Afrika pamoja na nyimbo 27 zenye maudhui ya ukombozi wa Afrika zikiwamo nyimbo zilizoandaliwa na kuimbwa na wapigania uhuru wa vyama vya ukombozi zimekusanywa. Vyama vilivyohusika na zoezi hilo ni vya Kusini mwa Afrika kama vile ANC-Afrika Kusini, FRELIMOMsumbiji, ZANU PF- Zimbabwe, MPLA-Angola na SWAPO - Namibia. Hotuba na nyimbo hizo zote zimehifadhiwa vizuri kwenye Kituo hiki na kutumika kutolea elimu kwa jamii.

Fauka ya hayo, katika kuhakikisha kuwa maudhui ya ukombozi yaliyopo kwenye mifumo ya kizamani ya analojia yanahamishiwa kwenye mifumo ya Kisasa ya kidijiti. Kituo

kimefanya uchambuzi wa tepu za kanda za zamani 1,250 zenye kumbukumbu ya historia ya ukombozi wa Afrika zilizopo katika Maktaba za Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kwa lengo la kuhifadhi katika mfumo wa kidijiti. Mikanda iliyochambuliwa ni ya REEL TO REEL, DVCAM, MIN DV na VHS ambayo kwa sasa haiwezi kutumika kwenye vifaa vya kisasa.



*Baadhi ya mikanda ya zamani yenye maudhui ya historia ya ukombozi iliyochambuliwa kwa ajili ya kuhifadhiwa kidijitali katika maktaba ya TBC*

**58. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha historia ya Ukombozi wa Afrika inafundishwa kikamilifu katika ngazi za elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na vyuo vya Ualimu, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika kimeingia Makubaliano maalumu na Taasisi ya Elimu Tanzania. Lengo la makubaliano hayo ni kushirikiana katika uibuaji wa mada zenye maudhui ya historia ya ukombozi wa Bara la Afrika. Mada zitakazoibuliwa zitaingizwa katika vitabu vya kufundishia somo la historia ya Tanzania. Hii itawajengea uwezo wanafunzi kutambua na kuenzi umoja na mshikamano ulioasisiwa na waasisi wa nchi yetu. Kituo kimeandaa rasimu za vitabu vya baadhi ya mashujaa wa Tanzania ambao ni R.M. Kawawa, S.A. Salim, J.S. Warioba, na Br. Gen. H. Mbita ambapo vitabu hivyo vitatumika kama vitabu vya kiada katika kufundishia somo la Historia ya Tanzania na Maadili.

**59. *Mheshimiwa Spika,*** nitoe pongezi nyingi kwa wadau wa Kituo hiki wakiwamo Waheshimiwa Wabunge, ambao

wanaunga mkono juhudi za kuhifadhi historia ya ukombozi wa Bara la Afrika katika maeneo yaliyotumiwa na Wapigania Uhuru kutoka nchi za Kusini mwa Afrika. Nianze na Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kufanikiwa kuyatangaza maeneo 9 yenye urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kwenye Gazeti la Serikali kuwa Urithi wa Taifa tarehe 15 Machi, 2024 na hivyo kuyafanya kuwa Urithi wa Taifa kwa mujibu wa Sheria ya Malikale ya mwaka 2022. Maeneo yaliyotangazwa ni Minara Mitatu Tabora, Jengo la Redio Tanzania Idhaa ya Nje (RTD) Dar es Salaam, Nyumba ya Kumbukizi ya Hayati Mwl. Julius K. Nyerere Magomeni Dar es Salaam, Mnara wa Kumbukumbu wa Mashujaa wa Vita vya Majimaji Nandete Lindi, Kambi ya Wapigania Uhuru wa Msumbiji Likuyu Sekamaganga Ruvuma, Makumbusho ya Mtwa Mkwawa Iringa, Mapango ya Nang'oma Lindi, Mapango ya Namaingo Lindi, na Kambi ya Wapigania Uhuru Kongwa Dodoma. Aidha, maeneo hayo kupewa hadhi ya kuwa urithi wa Taifa kunayafanya yalindwe Kisheria na kuwezesha kuanza mchakato wa kuyawasilisha UNESCO ili yafanywe kuwa Urithi wa dunia.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** fauka ya hayo, nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika na Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa kuridhia eneo la Shule ya Sekondari ya Samora Machel lililokuwa likitumiwa kwa mafunzo ya kijeshi na Chama cha FRELIMO kutoka Msumbiji kuwa miongoni mwa maeneo mengine yenye urithi wa ukombozi. Eneo hilo litakuwa miongoni mwa maeneo yatakayotangazwa kuwa Urithi wa Taifa, ambapo mchakato upo katika hatua za mwisho.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika, naipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kwa kuanzisha Kongwa Liberation Marathon. Mbio hizi zilifanyika kwa mara ya kwanza tarehe 25 Novemba, 2023 kwa lengo la kutangaza na kutoa elimu kwa jamii kuhusu urithi wa Ukombozi unaopatikana Wilaya ya Kongwa na kuhamasisha utalii wa kiukombozi. Mbio hizo zilihudhuriwa na washiriki takribani 600 na kurushwa mubashara na kituo cha Televisheni cha AZAM.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, natoa pongezi kwa Mkoa wa Njombe kwa uhifadhi wa kumbukumbu za historia ya

Ukombozi wa Bara la Afrika. Kwa nafasi ya pekee nimpongeze Baba Paroko wa Parokia ya Ihalula Jimbo Katoliki la Njombe kwa jitihada zake binafsi za kuandaa miradi ya utafiti na uhifadhi wa urithi wa ukombozi. Baba Paroko ameandaa utafiti wa Utamaduni unaopatikana katika Mkoa wa Njombe na yupo katika hatua za ujenzi wa Makumbusho maalumu kwenye pango la Kihistoria na kiutamaduni la Lyangolufinye kwa lengo la kuhifadhi historia ya eneo hilo. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine ambao wana maeneo yaliyotumiwa na Wapigania Uhuru, waendelee kushirikiana na Serikali kuyaendeleza na kuyahifadhi maeneo hayo kwa ajili ya kukuza utalii wa kiukombozi na wa kiutamaduni.

### 3.2.1.4 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**63.** ***Mheshimiwa Spika***, maendeleo ya Utamaduni na Sanaa ni hali ya kuwapo kwa ongezeko la ushiriki wa watu katika shughuli za Utamaduni na Sanaa pamoja na kuimarika kwa ubora wa kazi za sekta hizo. Manufaa yatokanayo na shughuli hizo ni pamoja na kukua kwa uchumi wa wadau wa utamaduni na sanaa na Taifa kwa ujumla sambamba na kuimarika kwa maadili ya jamii. Aidha, maendeleo hayo yanajipambanua kupitia kuwawezesha wadau hao kimitaji kutimiza malengo na ndoto walizonazo katika kutekeleza shughuli za Utamaduni na Sanaa kwa kuzingatia mahitaji yao kufikia viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa katika fani husianifu.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu wa uzingatiaji wa maendeleo ya Utamaduni na Sanaa, Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichukua jitihada za makusudi za kuhuisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Desemba 2022 kwa lengo la kukuza na kuendeleza Sekta hii kupitia utoaji wa mitaji yenye masharti nafuu na mafunzo ili kuziwezesha kazi za wadau zikidhi vigezo vya ushindani katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Mfuko huu unatoa huduma katika maeneo ya sekta za Muziki, Filamu, Sanaa za Ufundi, Maonesho, Lugha na Fasihi, Urithi wa Utamaduni na miradi mingine ya kukuza Utamaduni, Sanaa na Maadili. Aidha, walengwa wa Mfuko ni

watu binafsi, vikundi, vyama, mashirikisho, vituo vya elimu na mafunzo, asasi za kiraia na taasisi zinazojishughulisha na kazi za kukuza na kuendeleza kazi za Utamaduni na Sanaa.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Utamaduni na Sanaa unawezesha upatikanaji wa mikopo kwa wasanii kwa kushirikiana na Taasisi za Fedha ambazo ni Benki ya CRDB na NBC kupitia Hati ya Makubaliano iliyoingiwa tarehe 08 Julai, 2023. Serikali kupitia Mfuko huu iliamua kuzishirikisha taasisi za fedha katika utoaji wa huduma hii ili kufikisha huduma kwa wasanii wa mikoani na walio pembezoni mwa miji kwa kutumia miundombinu ya Ofisi za matawi ya Benki iliyotapakaa nchi nzima. Lengo likiwa ni kupunguza gharama za uendeshaji ambapo ili kuwafikia wasanii wengi Mfuko ungelazimika kuwa na Ofisi hadi katika ngazi ya Wilaya, kuwa na watumishi wengi na vitendea kazi vya kutosha kama vile magari, kompyuta, viti, meza, n.k. Kutumia wataalamu wa benki walio na uzoefu katika ukaguzi wa miradi, utoaji wa mikopo, ufuatiliaji wa marejesho na usimamizi wa mikopo kwa ujumla pamoja na kuulinda mtaji ili ukue, uwe endelevu na hatimaye uweze kuwafikia wasanii wengi zaidi ilikuwa ni lazima Mfuko uingie makubaliano na benki.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi kufikia Aprili 2024, Mfuko umewezesha utoaji wa mikopo ya Shilingi Bilioni 4.2 kwa miradi 216 ya Utamaduni na Sanaa iliyo katika mikoa 16 ya Tanzania Bara. Aidha, mikoa hiyo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Geita, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Njombe, Pwani, Shinyanga na Tabora. Sekta zilizonufaika na mikopo hiyo ni Muziki (miradi 68) iliyowezeshwa Shilingi Bilioni Moja Milioni Mia Tatu Sabini na Saba, Mia Moja Hamsini na Saba Mia tano (1,377,157,500); Filamu (miradi 70) iliyowezeshwa Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia tano Arobaini na Tatu, Mia Tatu na Saba Elfu, Mia Tano (1,543,307,500); Sanaa za Maonesho (miradi 30) iliyowezeshwa Shilingi Milioni Mia Tano Ishirini na Moja, Mia Mbili Tisini na Saba Elfu, Mia Tano (521,297,500); Sanaa za Ufundi (miradi 46) iliyowezeshwa Shilingi Milioni Mia Saba Thelathini na Sita, Mia Sita Tisini na Sita elfu Mia Nne Tisini na Tisa (736,696,499); na Lugha na

fasihi – (mikopo 2) iliyowezeshwa Shilingi Milioni Thelathini (30,000,000).

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia miradi 216 iliyowezeshwa, miradi 68 inamilikiwa na wanawake ambayo iliwezeshwa Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Ishirini na Nne, Mia Nane Themanini na Tano elfu, Mia Mbili Arubaini (1,324,885,240), miradi 107 inamilikiwa na wanaume na iliwezeshwa Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Themanini na Nne, Mia Saba Arobaini na Tano elfu Mia Nane Tisini na Tatu (2,084,745,893), miradi 14 inamilikiwa na vikundi na iliwezeshwa Shilingi Milioni Mia MbiliSabini na Mbili, Mia Saba Sabini elfu Mia Nne Tisini na Moja (272,770,491) na miradi 27 inamilikiwa na kampuni na iliwezeshwa Shilingi Milioni Mia Tano Ishirini na Sita, Hamsini na Saba elfu, Mia Tatu Sabini na Tano (526,057,375).

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Mfuko umewezesha mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Moja Thelathini na Moja, Milioni Mia Nne hamsini na Nane elfu, Mia Tisa Tisini na Tisa (3,131,458,999) kwa miradi 171 ya Utamaduni na Sanaa katika mikoa 16 ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Geita, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Njombe, Pwani, Shinyanga na Tabora. Katika miradi hiyo, miradi inayomilikiwa na wanawake ni 56 ambayo ni sawa na asilimia 33 na iliwezeshwa kiasi cha Shilingi Bilioni Moja, Milioni Ishirini na Tano, Mia Tano na Saba elfu, na Arobaini na Moja (1,025,507,041); miradi inayomilikiwa na wanaume ni 78 sawa na asilimia 46 iliwezeshwa Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Ishirini na Nane, Mia tatu Themanini na Nne elfu, Mia Nane na Saba (1,428,384,807); miradi ya vikundi ni 13 sawa na asilimia 8 na iliwezeshwa Shilingi Milioni Mia Mbili Thelathini na Nane, Sitini na Nne elfu, Mia Moja Thelathini na Nne (238,064,134) na kampuni ni miradi 24 sawa na asilimia 14 iliyowezeshwa Shilingi Milioni Mia Nne Thelathini na Tisa, Mia Tano na Tatu elfu na Kumi na Saba (439,503,017).

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha uzalishaji wa kazi za kiutamaduni na sanaa ili ziwe na ubora wa hali ya juu kwa lengo

la kukuza Sekta za Utamaduni na Sanaa nchini, Mfuko umewezesha upatikanaji wa vitendea kazi vya kuzalishia kazi za kiutamaduni na Sanaa kwa miradi 98 yenye thamani ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Saba Tisini na Nne, Mia Sita Thelathini na Saba elfu, Mia Tatu Ishirini na Moja (1,794,637,321) kwa ajili ya kununua vitendea kazi. Miongoni mwa miradi hiyo ni kuwezesha Studio 53 kuwa na vifaa vya kisasa ambapo hali hii inapunguza adha kwa wasanii wetu kwenda nje ya nchi kwa ajili ya kuzalisha kazi zao, Bendi 12 zinazotumbuiza mubashara, Vikundi vinne (4) vya kutumbuiza nyimbo za Injili na Kwaya 14 zinazomilikiwa na makanisa na Miradi 15 ya mapambo na upishi.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza na kuwezesha shughuli za kibiashara za Utamaduni na Sanaa zilizoanzishwa na kuendeshwa na wadau; Mfuko umewezesha shughuli za kibiashara za Utamaduni na Sanaa kwa miradi 73 yenye thamani ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Thelathini na Sita, Mia Nane Ishirini na Moja elfu, Mia Sita Sabini na Nane (1,336,821,678). Miradi iliyowezeshwa ni pamoja na: Utengenezaji na uzalishaji wa tamthilia 13 ambapo tamthilia tano (5) zinarushwa katika vituo vya habari vya Azam na DSTV, Tamthilia tatu (3) zimezinduliwa, Tamthilia tano (5) zimekamilika na zinasubiria kuingia sokoni; Uzalishaji wa filamu 36 zinazorushwa katika Vipindi vya Azam; Uzalishaji wa albamu nane (8) zenye jumla ya nyimbo 79 ambapo miongoni mwa nyimbo hizo, nyimbo zilizochukuliwa video ni arobaini na tatu (43); na kuwezesha uzalishaji wa kazi za Sanaa kwa miradi 15 katika Mkoa wa Arusha kupitia Soko la Masai (Masai Market) ambapo Soko hili ni kitovu cha Utalii mkoani Arusha.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo ni miongoni mwa huduma kuu inayotolewa na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa, huduma hii ni muhimu kwa msanii kwani inamwezesha Msanii kutengeneza kazi zenye ubora unaotakiwa katika soko la ndani na nje ya nchi. Mafunzo yanamsaidia msanii kupata ujuzi wa kuendesha biashara yake kwa mafanikio, kutoa huduma nzuri kwa wateja wake; kumsaidia kuwa na mtandao mkubwa wa kibiashara wenye tija pamoja na kumkutanisha Msanii na wasanii wengine ili kubadilishana mawazo; kupata uzoefu wa biashara; na

kupata maarifa ya kumsaidia Msanii kujua mahitaji ya wateja wake.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua hilo, Mfuko kwa kushirikiana na wadau umeendesha mafunzo katika mikoa 13 ya Tanzania Bara, ambayo ni Dar es Salaam, Tanga, Dodoma, Arusha, Morogoro, Lindi, Njombe, Mtwara, Pwani, Mbeya, Tabora, Shinyanga na Iringa. Mafunzo yamewafikia wasanii 9,267 ambapo kati ya hao wanaume 3,394 sawa na asilimia 37 na wanawake 5,873 sawa na asilimia 63. Wadau walioshiriki katika utoaji wa mafunzo haya ni Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Maafisa Utamaduni, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Benki ya CRDB, na Vyama vya Utamaduni na Sanaa. Aidha, mada zilizofundishwa ni namna ya kubadili uendeshaji wa Sanaa kutoka burudani mpaka kuwa biashara; elimu ya fedha iliyohusisha umuhimu wa uwekaji wa akiba na utunzaji wa kumbukumbu; umuhimu wa afya njema kama mtaji wa shughuli za sanaa; umuhimu wa urasimishaji wa kazi za sanaa katika mamlaka zinazohusika; uandaaji wa maandiko ya miradi; na uwekezaji wa mapato yatokanayo na kazi za Sanaa.



*Wasanii wakipatiwa mafunzo mbalimbali ikiwamo namna ya kutunza kumbukumbu za biashara, umuhimu wa kurasimisha biashara, n.k. yaliyotolewa na Mfuko wa Utamadui na Sanaa tarehe 13 Agosti, 2023 katika Chuo cha Kreluu mkoani Iringa.*

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania unatambua umuhimu na faida za urasimishaji wa kazi za Utamaduni na Sanaa kwa wasanii. Miongoni mwa faida hizo ni biashara za wasanii kutambuliwa na Serikali, wateja na jamii kwa ujumla; kuongezeka kwa fursa za kupata huduma za Serikali; kurahisisha upatikanaji wa mitaji kutoka serikalini na taasisi za kifedha kama vile benki na taasisi zinazotoa mikopo. Manufaa mengine ni kupata huduma mbalimbali za Serikali kama vile, mafunzo, msaada wa kitaalamu na kiteknolojia; kuiwezesha Serikali na wadau wengine kuboresha mipango yake ya kuwahudumia wasanii kwa kuwa itakuwa na uelewa wa idadi kamili ya wasanii waliopo; wasanii kusaidia kikamilifu katika ujenzi wa ukuaji wa uchumi wa nchi na kuwa walipa kodi wazuri na washiriki wenza wa Serikali katika kutoa huduma kwa jamii; na kuongezeka kwa uaminifu kwa wateja kutokana na kutambulika na Serikali hivyo wasanii kuwa katika nafasi nzuri ya kuingia mikataba ya kibiashara ama ubia na wadau wengine pamoja na kampuni za ndani na nje ya nchi sambamba na kurahisisha upatikanaji wa dhamana kutoka serikalini au taasisi binafsi.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu huu, Mfuko umechochea na kuhamisha urasimishaji wa kazi za utamaduni na sanaa ambapo wasanii 1,963 walifungua akaunti za Benki katika Benki za CRDB na NBC, Wasanii 117 walijisajili katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kupata namba za Walipa Kodi (TIN), wasanii 84 wamejisajili BRELA na kupata majina ya biashara, makampuni 28 yamefunguliwa, wasanii 235 wamesajaliwa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) ili kupata vyeti vya usajili, wasanii 283 walihuisha vibali vya kazi za sanaa, na wasanii 458 walitambuliwa na Bodi ya Filamu Tanzania kama wasanii wanaotekeleza kazi mbalimbali katika Sekta ya Filamu.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili wasanii waendelee kuona umuhimu wa kurasimisha sanaa na kuiendesha kibiashara, Mfuko umefanikiwa kufanya mkutano wa mwaka wa wadau tarehe 29 Februari, 2024 katika ukumbi wa mikutano wa hoteli ya Johari, Rotana, Jijini - Dar Es Salaam. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kuwakutanisha wasanii na wadau mbalimbali wa uwezeshaji ili waweze kufahamiana na kubadilishana uzoefu, kujenga mtandao

wa kufahamiana, kutoa elimu ya uwezeshaji iliyojikita katika maeneo ambayo ni korofi na yanayowazuia wasanii mbalimbali washindwe kupata fursa za mikopo kwa Mfuko na Taasisi mbalimbali za kifedha. Aidha, mkutano huo uliobebwa na kauli Mbiu '***RASIMIKA UNUFAIKE'***. Mkutano huo ulihudhuriwa na wadau 1,178 kati ya hao wanawake walikuwa ni 567 sawa na asilimia 48.1 na wanaume 611 sawa na asilimia 51.9. Mgeni Rasmi ambaye alikuwa ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati alitoa zawadi kwa wanufaika wa mikopo 15 wanaofanya vizuri katika usimamizi wa miradi yao pamoja na kupokea zawadi kwa niaba ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mchango wake wa kukuza Sekta ya Utamaduni na Sanaa kupitia uanzishwaji wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa. Zawadi hiyo ilitolewa na Wasanii wa Mkoa wa Dar es Salaam wakiwakilisha wasanii wote nchini.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Utamaduni na Sanaa unajukumu kubwa la kufanya ufuatiliaji na tathmini juu ya miradi iliyowezeshwa kupitia rasilimali zake ili kuona mwenendo wa hali halisi ya miradi na matokeo ya matumizi ya rasilimali fedha. Mfuko ulifanya tathmini na ufuatiliaji kwa miradi 67 iliyowezeshwa kwa lengo la kuona matokeo ya uwezeshaji kiuchumi kwa mnufaika mwenyewe, jamii na nchi kwa ujumla wake. Matokeo ya ziara yalibainisha kuwa wanufaika wanamudu kuhudumia kaya zao katika maeneo ya elimu kwa watoto, matibabu, kutoa ajira, pamoja na kulipa kodi mbalimbali. Aidha, ilibainika kuwa kuna mahitaji makubwa ya mitaji kwa wasanii ukilinganisha na kiwango cha mikopo kinachotolewa na Mfuko.

**77.** ***Mheshimiwa Spika***, dhamira kuu ya Serikali kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania ni kukuza na kuendeleza Sekta ya Sanaa ili iweze kuzalisha ajira nchini pamoja na kuchangia katika pato la Taifa. Aidha, katika eneo hili, hadi kufikia mwezi Apili, 2024, Mfuko umezalisha jumla ya ajira Kumi na Nne Elfu Mia Tisa na Mbili (14,902) zilizowanufaisha wananchi Laki Nne Arobaini na Saba Elfu na Sitini (447,060) nchini.

**SEKTA YA SANAA**
**3.2.1.5 IDARA YA MAENDELEO YA SANAA**

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Maendeleo ya Sekta ya Sanaa nchini yanasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Sanaa na Taasisi zilizo chini yake ambapo masuala ya Filamu yanasimamiwa na Bodi ya Filamu Tanzania (TFB) kwa Sheria ya Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya mwaka 1976; masuala ya Hakimiliki yanasimamiwa na Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) kwa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999; Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) linasimamia, Tasnia nyingine za Sanaa kama vile Muziki, Sanaa za Maonesho na Sanaa za Ufundi kwa Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Na. 23 ya mwaka 1984 ikisomwa na marekebisho yake ya mwaka 2019. Aidha, Idara pia inasimamia Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) ambayo imeanzishwa kwa Sheria Na. 30 ya mwaka 1997, ambapo jukumu lake kubwa ni kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri kwa wadau wa Sanaa na Utamaduni.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kuhakikisha kunakuwapo na ustawi katika utendaji wa Taasisi zake, imeratibu kuandaliwa kwa mapendekezo ya maboresho ya Sheria na Kanuni za Taasisi zake zikiwamo sheria ya Bodi ya Filamu, Kanuni za Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) ambazo zimeshatangazwa kwenye gazeti la Serikali (Kanuni za Ada ya Hakimiliki kwa vibebeo vya kazi za ubunifu, 2023, Kanuni za usimamizi wa kampuni za ukusanyaji na ugawaji mirabaha (Collective Management Organizations – CMOs), 2023 na Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa za mwaka 2018 ambapo Baraza bado linaendelea na ukusanyaji wa maoni ya wadau.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara imehakikisha viongozi wa Taifa wanaenziwa kutokana na Mchango wao kwa Taifa, ambapo Wizara ilisimamia Mradi wa Ujenzi wa Sanamu ya Mwl. Julius K. Nyerere ikiwa ni sehemu ya kuuenzi mchango wake wa kulikomboa Bara la Afrika, hususan nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Wazo hili liliazimiwa katika Kikao cha 35 cha mwezi Agosti, 2015 cha Wakuu wa Nchi na Serikali za SADC

ambapo Sanamu hiyo tayari imesimikwa katika viwanja vya Jengo la Mwl. Julius K. Nyerere Peace and Security lililopo Makao Makuu ya Umoja wa Afrika Jijini Addis Ababa, Ethiopia. Mradi wa Ujenzi wa Sanamu ya Mwl. Nyerere uliolenga kumwonesha mhusika katika umri wa miaka ya 1960 – 1980 alipokuwa katika harakati za ukombozi wa bara la Afrika, uligharamiwa na nchi Wanachama wa SADC kupitia Sekretarieti ya SADC na umesimamiwa na Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005. Sanamu hiyo ilizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika tarehe 18 Februari, 2024.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wasanii wa Tanzania wanatangazwa Kimataifa na kuwajengea uwezo katika masuala mbalimbali ya Sanaa na Ubunifu, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na Asasi ya Music in Africa Foundation iliratibu mkutano wa *The Music in Africa Conference for Collaboration, Exchange and Showcase (ACCES)*. Lengo lilikuwa ni kuwakutanisha wadau wa muziki nchini Tanzania na watumiaji wa muziki wa Afrika kutoka Duniani kote. Tukio hilo lilihudhuriwa na wadau mbalimbali wa muziki wakiwamo Manjumuziki (MaDJ), Waandaaji wa Matamasha, Mapromota, Mawakala wa Muziki, Mameneja wa Wasanii, Lebo za Kurekodi Muziki, Watangazaji, Waandishi wa Habari za Muziki, wahandisi wa sauti *(sound engineers)*, Wenye Shule za Kufundisha Muziki, Wafanyabishara wa kazi za muziki na wadau wa muziki. Mkutano ulifanyika kwa mafanikio makubwa na ulihudhuriwa na jumla ya washiriki 5,015 wa muziki wa Afrika kutoka duniani kote. Kati ya hao washiriki 504 walitoka nje ya Tanzania na 4,511 walitoka ndani ya nchi. Katika Mkutano huo ziliendeshwa warsha mbalimbali za Muziki na Burudani kuanzia tarehe 9 - 11 Novemba 2023. Aidha, Mkutano huo uliwapa fursa Wasanii wa Tanzania kutumbuiza sambamba na wenzao kutoka maeneo mbalimbali ya Afrika. Wasanii wa Tanzania waliotumbuiza ni Marioo, Leo Mkanyia, Balaa Mc, Kadilida, Christian Bella, Damian Soul, Siti Muharam na The Unguja All Stars. Aidha, kulikuwa na wasanii mbalimbali wa Kimataifa kama

vile Zolani Mahola and Feminine Force (Afrika Kusini), Ngwaka Son Systeme (DRC), Sho Madjozi, Feli Nandi (Zimbabwe), Madalittso Band (Malawi), Kasiva Mutua (Kenya) na Alostmen (Ghana). Itakumbukwa kuwa hii ilikuwa ni mara ya pili Mkutano huu kufanyika hapa Tanzania baada ya ule wa mwaka 2022 kufanyika kwa mafanikio makubwa ambapo Wadau wa muziki hapa Tanzania waliunganishwa na soko la kimataifa.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na jitihada za kukuza Tasnia ya Urembo na Utanashati nchini hasa kwa makundi maalumu, ambapo kwa kushirikiana na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na Kituo cha Sanaa na Utamaduni kwa Viziwi Tanzania (KISUVITA) iliandaa Tamasha la "World Happy Deaf Family Festival" (WHDFF), Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 15 – 30 Novemba, 2023 ambalo lilihudhuriwa na washiriki wa moja kwa moja 169 kutoka nchi 43 duniani kote. Nchi hizo ni pamoja na Afrika Kusini, Australia, Austria, Belarus, Burundi, Brazili, Ethiopia, Falme za Kiarabu, Guyana, Haiti, India, Iran, Italia, Kenya, Kongo DRC, Malaysia, Macedonia, Marekani, Mexico, Misri, Morocco, Msumbiji, Nigeria, Pakistani, Poland, Romania, Rwanda, Senegal, Sierra Leone, Sudani, Sudani Kusini, Thailand, Tunisia, Scheck, Ufaransa, Uganda, Uhispania, Ujerumani Ukraine, Ureno, Urusi, Zambia, Zimbabwe na mwenyeji Tanzania.




*Kushoto: Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb.), Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mgeni Rasmi wa Tamasha la WHDFF akifuatilia mashindano ya Urembo, Utanashati na mitindo. Kulia: Mshindi wa dunia wa shindano la urembo kwa viziwi Bi. Nashua Patience kutoka Uganda akivalishwa taji na Mhe. Patrobus Katambi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu tarehe 25 Novemba, 2023 katika ukumbi wa The Super Dome Masaki Jijini Dar es Salaam.*

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Tamasha hilo, jamii ya viziwi kutoka kote duniani ilionesha vipaji vyao kwa kushindana kupata washindi katika urembo, utanashati, mitindo, ngoma, uchoraji na futuhi. Kupitia Tamasha hilo, Tanzania ilijitangaza kimataifa kama nchi ya fursa kwa wote bila kujali tofauti za kimaumbile pamoja na kutumika kutangaza utalii wa Tanzania kwa kuwapeleka washiriki wote kutalii katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi na kuwapatia chakula, vinywaji na burudani yenye asili ya Tanzania katika fukwe za Bahari ya Hindi (Swahili Experience – Coco Beach). Itakumbukwa hii ilikuwa ni mara ya pili mashindano haya yanafanyika hapa nchini baada ya yale ya Oktoba, 2022 kufanyika kwa ufanisi mkubwa ambapo washiriki pia walitembelea Hifadhi ya Ngorongoro.



*Washiriki wa Tamasha la World Happy Deaf Family Festival wakiwa katika ziara ya kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Mikumi tarehe 27 Novemba, 2023.*

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaratibu Tamasha la *Serengeti Arts Festival* kila mwaka. Mwaka 2023 Tamasha hili lilifanyika Kimataifa kupitia majukwaa mbalimbali ya Sanaa yalioandaliwa Kimataifa. Wizara ilishiriki kwenye maonesho ya Sanaa ya mavazi *(Salon International du Textil Africain, SITA)* ambayo ni maonesho yanayotokana na vitambaa vilivyotengenezwa Afrika. Maonesho hayo kwa mwaka 2023 yalikuwa ya msimu wa tisa (9), yalifanyika kuanzia tarehe 6 hadi 11 Novemba, 2023 katika

viwanja vya *Esplanade du palais du people* nchini Guinea. Maonesho hayo, hufanyika kila mwaka katika nchi tofauti za Afrika ambapo nchi inayohitaji kuwa mwenyeji huomba nafasi kwa uongozi wa *Salon International du Textil Africain*. Gharama za uendeshaji hugharamiwa na SITA kwa kushirikiana na nchi mwenyeji. Lengo la maonesho ya *Salon International du Textil Africain* ni kulinda wabunifu wa mavazi ya Kiafrika dhidi ya uharamia; kusherehekea na kuonyesha utajiri wa Sanaa na Utamaduni uliopo Afrika; kuonesha vipaji vya wabunifu wa mavazi kutoka Afrika; pamoja na kuhamasisha utumiaji wa vitambaa kutoka Afrika kupitia zao la pamba.




*Washiriki kutoka Tanzania katika maonesho ya Salon nternational du Textil Africain (SITA) wakionesha mavazi yenye asili ya Tanzania wakiwa Conakry nchini Sierra Leone tarehe 6 – 11 Novemba, 2023.*

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** nchi 42 kutoka Afrika zilishiriki maonesho hayo ambapo Tanzania ilishiriki kwa mara ya kwanza. Wanamitindo, wabunifu wa mavazi, wajasiriamali wa sanaa na utamaduni, walipata nafasi ya kuonyesha vipaji vyao pamoja na kuuza kazi zao za sanaa na utamaduni. Vilevile, Wizara ilishiriki kwenye Tamasha la Kimataifa la Sanaa za Ufundi lijulikanalo kama Suraj Kund Mela lililofanyika kuanzia tarehe 2 - 18 Februari,

2024 katika mji wa Hariana nchini India. Tamasha hili lilishirikisha nchi zaidi ya 52 kutoka duniani kote. Mwaka 2024 Tanzania ilishiriki kama nchi mshirika "Partner State" nafasi hiyo ilipatikana baada ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya ziara nchini India. Lengo la kushiriki Tamasha hilo ni kuonesha Sanaa mbalimbali za Mtanzania na kuuza bidhaa mbalimbali za Sanaa za Ufundi. Tanzania iliwakilishwa na jumla ya washiriki 22 ambao walishiriki kwenye maeneo matatu ambayo ni Sanaa za Ufundi, muziki wa Bongo Fleva na Wapishi. Katika Tamasha hilo, Tanzania ilifanikiwa kuongeza wadau wa Kimataifa ambao wamevutiwa na kazi za Sanaa za Ufundi za hapa nchini ambao wameahidi kushirikiana na wadau wa Tanzania. Katika Tamasha hilo, Tanzania ilishinda Tuzo ya banda bora kwa mwaka 2024 na ilishinda Tuzo bora ya ubunifu wa mitindo *(Fashion and Design)*.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Sanaa hapa nchini, walishirikiana kuratibu Matamasha mbalimbali ikiwemo Tamasha la Sauti za Busara, ambalo limekua likifanyika tangu mwaka 2003 Ngome Kongwe, Zanzibar. Kwa mwaka 2023, Tamasha hili lilishirikisha jumla ya vikundi 25, vikiwemo 18 kutoka nchi mbalimbali za Afrika na nje ya Afrika; vikundi vinne (4) kutoka Zanzibar na vikundi vitatu (3) kutoka Tanzania Bara vilivyokonga nyoyo za wapenzi wa Tamasha hilo lililokuwa limesheheni wageni mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi. Tamasha hilo kwa mwaka 2023, lilifanikiwa kwa kiwango kikubwa kwa kuzingatia ongezeko la idadi ya washiriki waliohudhuria.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuelekea Siku ya Maadhimisho ya Kiswahili Duniani Wizara iliandaa Tamasha la Kimataifa la Muziki wa Taarabu lililofanyika tarehe 06 Julai, 2023 Zanzibar. Tamasha hili lilijumuisha vikundi vya muziki kutoka nchi za Burundi, Kenya na Visiwa vya Komoro na mwenyeji Tanzania. Lengo la Tamasha hili ilikuwa ni kubainisha mchango wa Muziki wa Taarabu kwenye kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili duniani.

Aidha, Tanzania imeshiriki maonesho ya Sanaa za Ufundi ya *Venice Art Biannale* nchini Italia, ambapo Wizara ilipeleka Wasanii wanne (4) kushiriki maonesho hayo. Wasanii hao ni Lutengano Anganile Mwakisopile, Haji Musa Chilonga, Happy Frank Robert na Yahya Mzee Mwinyikombo, wakiongozwa na Kamishna Bi. Leah Kihimbi kutoka Idara ya Maendeleo ya Sanaa. Ingawa Wasanii na Kamishna walirejea nchini tarehe 24/04/2024, maonesho ya kazi zao yanaendelea hadi Novemba, 2024. Katika maonesho hayo, Wasanii wetu waliweza kuuza baadhi ya kazi zao mapema, kujipatia kipato na kujitangaza kimataifa.

### 3.2.1.6 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

**88.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha Baraza linakuwa msimamizi mahiri wa kuchochea maendeleo ya sanaa nchini, Baraza linatekeleza majukumu yake mbalimbali yakiwamo; kurasimisha sekta ya Sanaa kupitia usajili wa wasanii, vikundi, wadau wa sanaa, vyama na Mashirikisho ya Sanaa yanayosimamiwa na Baraza ambayo ni Shirikisho la Sanaa za Maonesho, Ufundi na Muziki. Vilevile Baraza linasimamia uendeshaji wa matukio ya sanaa nchini, kufufua na kukuza Sanaa kupitia programu mbalimbali za sanaa, kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wasanii na wadau wa sanaa kuhusu uanzishwaji na uendelezwaji wa sanaa, kuandaa miongozo mbalimbali ya kusimamia uendeshaji wa Sekta ya Sanaa nchini. Katika kipindi cha mwaka 2023/24 majukumu yaliyotekelezwa na BASATA ni kama ifuatavyo:

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BASATA imeendelea kukuza ubunifu na utengenezaji wa sanaa bora kwa wasanii kwa lengo la kuwawezesha wasanii kuwa wabunifu na kubuni kazi za sanaa zilizo bora. Ubunifu na kazi bora za Sanaa zitasaidia wasanii kushindanisha kazi zao na wasanii wengine walio nje ya nchi na hatimaye kupata masoko ya bidhaa Kimataifa. Masoko ya Kimataifa yatawezesha wasanii kuongeza kipato cha mtu binafsi na kuongeza pato la Taifa.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kunakuwa na ubunifu na utengenezaji wa Sanaa Bora kwa wasanii, Baraza limeendelea kurasimisha wasanii kwa njia ya kisasa ya kidijiti kupitia mfumo wa Usajili wa Wadau wa Sanaa (Artist Management Information SystemAMIS). Mfumo wa AMIS umerahisisha utoaji wa huduma kwa wasanii na wadau wa sanaa kwa vile huduma za maombi na utoaji wa vibali na malipo ya ada hukamilika kwa njia ya mtandao, hivyo wasanii na wadau hawalazimiki kusafiri kutoka mahali walipo kuja ofisi za BASATA Jijini Dar es Salaam ili kupata huduma. Katika kuthibitisha ubora wa mfumo wa AMIS; kwa kipindi kuanzia Julai 2023 hadi Aprili 2024, Baraza limefanya usajili na kutoa vibali vya kuendesha shughuli za Sanaa nchini kupitia mfumo wa AMIS kwa mafanikio makubwa ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/24 limesajili Wasanii binafsi 749, sawa na asilimia 94 ya lengo la mwaka. Aidha, Baraza lilitoa Vibali vya wasanii kwenda nje ya nchi 204 na kuwaingizia kipato cha fedha zaidi ya shilingi bilioni 7. Kwa upande wa matukio ya sanaa, Baraza lilitoa vibali 37, sawa na asilimia 154 ya lengo na kuzalisha ajira za muda mfupi zaidi ya 200,000.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limetoa ushauri wa kitaalamu kwa wasanii na wadau wa Sanaa wapatao Elfu Mbili Mia Nne Thelathini na Wawili (2,432) kutoka maeneo mbalimbali nchini. Ushauri huu ulitolewa katika maeneo ya masoko ya kazi za sanaa, uendeshaji wa matukio, utafutaji fedha kwa vikundi na taasisi, usajili na vibali pamoja na masuala ya kisheria na utatuzi wa migogoro mbalimbali katika sekta ya sanaa. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Baraza lilipokea migogoro 22 ya wasanii na wadau wa sanaa. Migogoro 16 kati ya hiyo imepata utatuzi baada ya kupata msaada wa kisheria na migogoro sita (6) ipo katika hatua mbalimbali za utatuzi.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limerejesha Tuzo za Muziki Tanzania (Tanzania Music Award-TMA) ambazo zilikoma mwaka 2014. Tuzo hizi zimefanyika kwa mara nyingine tena mwaka 2021 na 2022. Katika kuboresha Tuzo hizo na kuhakikisha zinakuwa bora zaidi na kupunguza malalamiko, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo aliteua Kamati Maalumu yenye wajumbe sita (6) wenye ubobezi katika tasnia ya muziki na wazoefu katika

masuala ya tuzo za Kitaifa na Kimataifa ambao wanashirikiana na BASATA kuandaa tuzo bora za mwaka 2023 zinazotarajiwa kutolewa mwezi Juni, 2024. Kamati hiyo ilizinduliwa tarehe 03 Novemba, 2023 katika Ukumbi wa Hoteli ya Peacock Jijini Dar es Salaam. Kamati ilikabidhiwa Hadidu za rejea zitakazofanikisha Tuzo za Muziki kuwa za Kimataifa na kuitangaza nchi Kimataifa. Hadi kufika Aprili, 2024 wadau wanane (8) kutoka Tanzania na mdau mmoja (1) kutoka nchini Nigeria wamejitokeza na kuonesha nia ya kufadhili shughuli mbalimbali za Tuzo hizo. Aidha, Tuzo za mwaka 2022 zilifanyika kwa mafanikio makubwa, kwa sababu kulikuwa na ushindani mkubwa na kazi zilizofanyika kwa ubora wa hali ya juu.




*Bw. Gerson Msigwa Katibu Mkuu, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo (wa tatu kutoka kushoto) akimkabidhi Mwongozo wa Tuzo za Muziki Tanzania (Tanzania Music Award – TMA) Bi. Christine Mosha (Seven) Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya kuratibu Tuzo za Muziki katika hafla iliyofanyika katika Ukumbi wa Peacock Hotel Jijini Dar es Salaam tarehe 03 Novemba 2023.*

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** tatizo la mmomonyoko wa maadili hususan katika sanaa limekua kwa kasi. Hii inatokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Baadhi ya wasanii huiga

tamaduni kutoka nje ambazo zipo kinyume na Mila na Desturi za Kitanzania. Baadhi ya mambo yanayofanywa na baadhi ya wasanii hufanya hivyo kutafuta umaarufu (kick) ili kupata mashabiki wengi. Hali hii husababisha ukiukwaji wa maadili katika uendeshaji wa shughuli za sanaa unaofanywa na wasanii na wadau wa sanaa kwa kukiuka Sheria na Kanuni zinazosimamia tasnia ya sanaa.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutatua changamoto hiyo, Baraza limeandaa Mwongozo wa Uzingatiaji Maadili katika kazi za Sanaa ambao ulizinduliwa rasmi tarehe 3 Novemba, 2023 na kupata idhini ya matumizi. Mwongozo huo umesambazwa kwa viongozi wa sanaa, wasanii na wadau wa sanaa. Aidha, umewekwa kwenye tovuti ya Baraza yenye kiungo cha www.basata.go.tz. Mwongozo huu umefikishwa kwa wasanii zaidi ya 179 kwa nyakati tofauti, vyombo vya habari, taasisi na kampuni mbalimbali zinazojihusisha na shughuli za sanaa na burudani. Wahusika wa utekelezaji wa Mwongozo huu ni wasanii, wabunifu na watunzi wa kazi za sanaa, wasimamizi/menejimenti ya wasanii na kazi zao, wasambazaji au wazalishaji wa kazi za sanaa, vyombo vya habari, mitandao ya kidijiti na akaunti za mitandao ya kijamii. Watekelezaji wengine ni vyombo vya usafiri, washereheshaji/ manjumuziki (MaDJ) na jamii yote kwa ujumla.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** wote waliotajwa katika mwongozo huo wanajukumu la kulinda maadili katika sanaa. Elimu inaendelea kutolewa ili wazingatie Kanuni za Baraza na kuweza kujiendesha kiuchumi. Hadi kufikia mwezi Aprili 2024, mwongozo umesambazwa kwa viongozi wa sanaa na wasanii zaidi ya 179; Mashirikisho ya Muziki matatu (3); Vyama vya Sanaa za Maonesho na Ufundi 24; wadau mbalimbali wakiwamo watoa huduma za mabasi ya mikoani 10; vyombo vya habari 26; Vyuo Vikuu vinne (4) na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, mwongozo huu uligawiwa kwa wajumbe wote Kamati ya Kitaifa ya Maadili iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na Wajumbe Kamati ya Kudumu ya Bunge Elimu, Utamaduni na Michezo.

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 imeeleza bayana dhima ya Utamaduni, kulitambulisha Taifa. Baraza limeendelea kuweka mipango ya utekelezaji wa programu ya mdundo wa Taifa kwa kuhamasisha watozi (producers) kutumia kivunge cha mtozi (producers kit) kilichotengenezwa na wabobezi wa muziki. Baraza kwa kushirikiana na Chama cha Watayarishaji na Wazalishaji wa Muziki Tanzania lipo katika hatua za mwisho za kuzindua kampeni kwa watozi (producers), kuzalisha kazi bora za muziki kwa kutumia vionjo vya Kitanzania. Kampeni hii itazinduliwa kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2023/24.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** miundombinu ya sanaa ni suala muhimu katika kukuza na kuendeleza sanaa hapa nchini. Kwa sasa, sekta ya sanaa inakua kwa kasi na vipaji vinaongezeka. Vipaji vya wasanii vimeleta chachu katika maendeleo ya sanaa na nchi kwa ujumla. Ili vipaji viweze kufanya vizuri zaidi vinahitaji miundombinu ambayo itatumika katika kuboresha kazi zao hatimaye kuzalisha kazi bora na zenye ubunifu mkubwa. Vilevile miundombinu hiyo itatumika kama eneo la burudani kwa wananchi kupunguza msongo wa mawazo. Katika kuhakikisha suala hilo linatekelezeka, Baraza linatekeleza Mradi wa ujenzi wa Kituo Jumuishi cha Ukuzaji Sanaa kwa kuliendeleza upya eneo la Baraza la Sharif Shamba kwa kuzingatia mahitaji ya sasa ya wasanii na wadau wa sekta ya sanaa. Lengo la mradi ni kuwa na Kituo Kimoja cha Huduma za Sanaa (National Arts Promotion Hub) chenye miundombinu muhimu ya uzalishaji wa kazi za sanaa na burudani kwa ajili ya kujenga weledi wa wasanii wa Tanzania na kukidhi mahitaji ya wateja na wadau wa sanaa na burudani nchini. Kazi ambazo zimeanza na zinaendelea ni maandalizi ya Mpango wa Uendelezaji (Master Plan) wa eneo hilo; michoro ya miundombinu mbalimbali ya sanaa; na Andiko Mradi kwa ajili ya kuutangaza mradi kwa lengo la kupata wabia kutoka sekta binafsi ili ujenzi uanze kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP).

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** BASATA inajivunia kuimarisha utoaji wa habari kwa umma, mawasiliano na ushawishi ili wasanii na wadau waweze kufahamu kwa kina kinachofanywa na BASATA

na kupata elimu. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2023 hadi Aprili 2024 kwenye mitandao ya kijamii ya *Instagram,* wafuatiliaji wameongezeka kutoka 69,000 hadi 83,300 na Facebook, wafuatiliaji wameongezeka kutoka 1,000 hadi 1,300. Elimu kwa umma imetolewa kwa njia ya kutembelea vyombo vya habari (*Media Tour)* ambapo kuanzia Mwezi Julai 2023 hadi Aprili, 2024 Baraza limetembelea jumla ya vyombo vya habari 21, ambapo redio tisa (9) na runinga 12 na kufanya mahojiano maalumu katika redio tatu (3) na runinga mbili (2). Pia, Baraza liliandaa taarifa kwa Vyombo vya Habari (Press Release) 14, pamoja na Mikutano na Vyombo vya Habari (Press Conference) zipatazo 11. Aidha, Baraza limechapisha matoleo manne (4) ya *Jarida la Msanii* ambalo limesheheni taarifa na matukio mbalimbali ya utekelezaji wa programu za Baraza na wadau wa Sekta ya Sanaa nchini. Vilevile jumla ya vyombo vya habari 16 na mitandao ya kijamii hamsini na miwili (52) vilitangaza habari za Baraza.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha shughuli za Sanaa zinaendelea, utoaji wa elimu katika ngazi ya shule za Msingi na Sekondari, Baraza limetekeleza Programu ya Sanaa kwa Watoto kwa shule za Msingi na Sekondari tarehe 01 - 02 Desemba, 2023 ambapo mafunzo yalitolewa katika shule tano (5), zikiwamo Shule za Msingi tatu (3) na Sekondari mbili (2) zilizopo katika Mkoa wa Arusha. Jumla ya wanafunzi mia nane hamsini na watatu (853) na walimu wanane (8) walishiriki na kupewa elimu sahihi kuhusu uimbaji sahihi wa nyimbo za Uzalendo ikiwamo Wimbo wa Taifa, Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania Nakupenda na Tazama Ramani. Hii inasaidia kulinda hadhi ya utambulisho wa Taifa letu na kupanda mbegu ya uzalendo kwa kizazi cha sasa na cha baadaye kupitia nyimbo za uzalendo.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza matakwa ya sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya Mwaka 1999, Baraza limeandaa marekebisho ya Kanuni zake za mwaka 2018 kwa kuingiza Sehemu ya 14 ambayo ni mahsusi kwa ajili ya kuweka utaratibu wa ulinzi wa kazi za sanaa za jadi. Vilevile, Baraza linaendelea

na kazi ya kuandaa Mwongozo wa Ulinzi wa Sanaa za Jadi kwa ajili ya kulinda na kusimamia matumizi ya Sanaa za Jadi.

Aidha, Baraza limeendelea kushirikisha jamii kushiriki katika masuala ya shughuli za sanaa kwa njia mbalimbali, ikiwamo Programu ya Sanaa Mtaa kwa Mtaa. Kupitia programu hii katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024, BASATA iliendesha programu hii katika mikoa mitatu ambayo ni Njombe, Tanga na Arusha. Jumla ya vipaji 70 viliibuliwa ambapo Mkoa wa Njombe vipaji kumi na vitano (15), Tanga Arobaini na viwili (42) na Arusha kumi na vitatu (13).

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza linatekeleza Mradi wa BASATA Vibes, unaofadhiliwa na Serikali ya Ufaransa kupitia Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufaransa chini ya Kituo cha Utamaduni cha Ufaransa (Alliance Française). Mradi huu ulizinduliwa tarehe 14 Septemba 2023 na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mradi umepata ufadhili wa fedha Euro laki moja (€100,000). Lengo la mradi huu ni kutoa fursa kwa wasanii na wadau wa sanaa kuonesha na kuuza kazi zao kwenye majukwaa mbalimbali Tanzania Bara na Zanzibar. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024, Mradi umetekeleza yafuatayo: uliwezesha Maofisa Utamaduni na wadau wa sanaa kupata mafunzo kuhusu uandaaji bora wa matukio ya sanaa nchini; wajumbe wa Tanzania walienda nchini Ufaransa kuhudhuria jukwaa la sanaa na ubunifu wa Kiikolojia baina ya nchi za Afrika na Ufaransa (Euro Africa-Bienalle); na kuandaa na kufanya matukio 6 kati ya kumi na mawili (12) ya sanaa na burudani kwenye mikoa 6 kati ya minane (8) ambayo mradi utatekelezwa.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** matukio yote haya yanajulikana kwa jina la "**BASATA VIBES".** Hadi Mei 2024 mradi umetekelezwa katika mikoa saba (7) ambayo ni Dar es Salaam, Tanga, Arusha, Dodoma, Morogoro, Iringa na Ruvuma. Kwa ujumla BASATA *Vibes* imeonesha mchango mkubwa katika maendeleo ya tasnia ya Sanaa ikiwamo kuibuliwa kwa vipaji, kutoa ajira na kuongeza kipato kwa wadau katika maeneo ya mradi ulikotekelezwa. Katika mikoa saba (7) BASATA *Vibes* ilitoa fursa za ajira za muda mfupi 624 na kuwapatia wasanii zaidi ya shilingi

milioni mia moja sitini na nne, mia tatu thelathini na tano elfu (164,335,000) kupitia ajira.




*Mheshimiwa Dkt. Damas D. Ndumbaro (Mb.), Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo (kushoto) akiwa na Axel-David Guillon, Balozi Msaidizi wa Ubalozi wa Ufaransa Tanzania (kulia) katika hafla ya kusaini Hati ya Makubaliano ya Mradi wa BASATA Vibes iliyofanyika katika Ukumbi wa Kituo cha Utamaduni cha Ufaransa (Alliance Française) jijini Dar es Salaam tarehe 14 Septemba 2023.*

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza katika utekelezaji wa jukumu lake la kusimamia na kuratibu matukio ya sanaa, limeendelea kushirikiana na jamii katika shughuli mbalimbali za utamaduni na sanaa kama vile Matamasha, Mashindano, Maonesho, Warsha na Makongamano. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, Baraza liliratibu matukio ya wadau kwa kutoa vibali vya matukio na kufuatilia mwenendo wa matukio kama ifuatavyo; Tamasha la Muziki wa Cigogo linaloandaliwa na Kituo cha Sanaa na Utamaduni cha Chamwino, Tamasha la Majimaji Selebuka, Tamasha la Utamaduni la Tulia *(Tulia Traditional Dances Festival),* Tamasha la Fiesta, Tamasha la Muziki Mnene, Tamasha la Wasafi, Tamasha la Nandy, Tamasha la Swahili Fashion, Shindano la Miss Tanzania, Bongo Star Search (BSS), Tamasha la

Hip Hop Asili, na Tamasha la Sanaa Blast la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).



*Mhe. Hamis Mwinjuma (Mb.), Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo (wa kwanza kushoto mbele) akishuhudia kukabidhiwa zawadi kwa mshindi wa kwanza wa Shindano la Bongo Star Search ndugu Razack Adam (wa kwanza kulia mbele) katika hafla iliyofanyika katika Ukumbi wa Ware House Masaki jijini Dar es Salaam tarehe 29 Januari 2024.*

**104. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha Utawala Bora katika kutekeleza Shughuli za Baraza na Uendeshaji wa Sekta ya Sanaa, Baraza linaendelea na mchakato wa Marekebisho ya Kanuni za Baraza za mwaka 2018 ambapo maoni yamepokelewa kutoka kwa wadau mbalimbali. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 maoni yalipokelewa kutoka kwa; Viongozi Wakuu 4 wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo wakiwa sehemu ya wadau wa Sanaa; watumishi na menejimenti ya Baraza la Sanaa la Taifa 53; maofisa utamaduni wa halmashauri 187; Marais wa mashirikisho ya muziki, sanaa za maonesho na sanaa za ufundi 3; na baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ikiwamo COSOTA na Bodi ya Filamu. Aidha, wadau wengine waliohusika kutoa maoni ni Taasisi ya TARO (Tanzania Artists Rights Organization), Taasisi ya CINT (Creative Industry Network of Tanzania),

CHIMABA Sanaa Group, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

**105. *Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuimarisha utawala Bora kazini, Baraza kwa kushirikiana na Kituo cha Utamaduni cha Ufaransa Jijini Dar es Salaam lilifanya mafunzo kwa washiriki 50, wakiwamo Maofisa Utamaduni ishirini na wawili (22), viongozi wanane (8) wa vyama na mashirikisho ya Sanaa na wadau wa sanaa 20. Mafunzo hayo yalihusu kuwajengea uwezo wa uandaaji bora wa matukio ya sanaa nchini, utendaji kazi wa Baraza, na kupokea maoni ya maboresho ya Kanuni zinazoboreshwa za mwaka 2018. Mafunzo hayo yalifanyika tarehe 22 - 26 Septemba 2023.

**3.2.1.7 BODI YA FILAMU TANZANIA (TFB)**

**106. *Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ni pamoja na kusimamia na kuratibu kazi za filamu zikiwamo kuhakiki na kuzipanga katika madaraja; kutoa vibali vya usambazaji, maonesho ya filamu, michezo ya kuigiza, kampuni za usambazaji wa filamu, kumbi za maonesho ya filamu, maktaba za picha za filamu, studio za uandaaji wa filamu; pamoja na kujenga uwezo wa wadau waliojiajiri au kuajiriwa katika tasnia ya filamu.

**107. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Bodi ya Filamu kwa mwaka 2023 ilifanya Tamasha la Tuzo za Filamu tarehe 16 Desemba 2023 jijini Dar es Salaam ambapo washiriki 1,000 walihudhuria. Jumla ya tuzo 41 zilitolewa kwa wasanii, ikiwa tuzo 34 ni za ushindi, tuzo 2 za mafanikio ya muda mrefu (Life Time Achievement) na tuzo 5 za kutambua mchango wao katika kukuza na kuendeleza Tasnia ya Filamu nchini. Tuzo zinazotolewa kwa wasanii zimekuwa motisha kubwa na kuongeza hamasa katika kutengeneza filamu bora zenye viwango vya kimataifa.




*Waanzilishi na Waratibu wa Tuzo za Kimataifa za Hollywood and African Prestigious (HAPAwards) Bi. Tina Weisinger na Bi. Amberr Washington kutoka Marekani wakimkabidhi Tuzo ya Makala Bora Mwandaaji wa Filamu kutoka Zanzibar Bi. Salma Adim katika Tuzo za Filamu Tanzania 2023 zilizofanyika tarehe 16 Desemba 2023 katika Ukumbi wa The Super Dome, Masaki jijini Dar es Salaam.*

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imeendelea kuratibu suala la kuwajengea uwezo wadau wake kwa lengo la kuimarisha ujuzi na weledi katika utayarishaji wa filamu ili kukuza na kuendeleza Tasnia ya Filamu nchini. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 programu zifuatazo ziliratibiwa na kuwezeshwa:

(i) Kushirikiana na Taasisi za kimataifa kwa lengo la kuendeleza jitihada za ukuzaji na uendelezaji wa Tasnia ya Filamu. Mathalani, Shirika la Maendeleo nchini Korea (KOICA) na Taasisi ya Kimataifa ya Mafunzo nchini Korea (KOICS) iliendesha mafunzo ya namna bora ya kusimamia Tasnia ya Filamu kwa Maofisa Filamu kumi na watano (15) na wadau wa Filamu 10, ambapo mafunzo hayo yalitolewa kwa siku nane (8) kuanzia tarehe 25 Oktoba hadi 01 Novemba 2023 jijini Dar es Salaam;

(ii) Kushirikiana na Chama cha Waigizaji katika ngazi za mikoa ya Njombe na Mara, mafunzo yalifanyika, ambayo yalitolewa kwa wasanii 136, ikiwa ni wasanii 30 Mkoa wa Njombe na wasanii 106 Mkoa wa Mara. Mafunzo hayo yalitolewa katika fani za uandaaji wa filamu ikiwamo uigizaji, uongozaji, upigaji picha, ufundi wa mwanga na uhariri;

(iii) Kupitia Programu ya kuwaendeleza wasanii chipukizi ijulikanayo kama ***The Coming Film Stars*** iliwajengea uwezo wasanii chipukizi 50 katika masuala ya weledi, fedha na uwajibikaji;

(iv) Katika mwendelezo wa programu ya mafunzo yanayotolewa kwa mtindo wa uchambuzi wa filamu ***(Film Screening and Reviewing)***, wasanii 100 wamenufaika kupitia uchambuzi wa filamu 10. Baadhi ya filamu zilizochambuliwa kupitia programu hiyo ni; Dar, Kilio chetu, Melisa, Sauti, Dosari na Ndonga; na

(v) Programu maalumu ya kutetea haki za wasanii inayotekelezwa kupitia Kamati ya Haki za Wasanii chini ya uratibu wa Bodi ya Filamu imeendelea kuchukua hatua stahiki za kuhakikisha wasanii wanapata haki zao ambapo katika kipindi husika, Kamati ilipokea na kushughulikia jumla ya malalamiko matatu (3). Aidha, kwa ulinganifu wa vipindi hivyo, idadi ya malalamiko imepungua kutoka malalamiko kumi na manne (14) mwaka 2022/23 hadi kufikia malalamiko matatu (3) mwaka 2023/24, sawa na upungufu wa asilimia 78.5 hali inayoonesha kuimarika kwa elimu na uelewa wa masuala ya kimikataba miongoni mwa wasanii nchini.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imetoa leseni 129 za uendeshaji wa shughuli na biashara za Filamu na Michezo ya Kuigiza, ambayo ni sawa na asilimia 49.6 ya lengo la mwaka la kutoa leseni 260. Leseni hizo zilitolewa ikiwa ni hatua za urasimishaji wa shughuli na biashara ya filamu nchini. Aidha, katika jitihada za kuendelea kuwatambua wasanii wanaojihusisha na shughuli za Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini ili kurahisha utoaji wa huduma miongoni mwao, Bodi imetoa Vitambulisho mia moja

sitini na kimoja (161) ambayo ni sawa na asilimia 16.1 ya lengo la mwaka la kutoa vitambulisho 1,000. Kutokana na mwitikio huo Serikali inaangalia namna ya kuiwezesha Bodi ya Filamu ili kufikia maeneo mengi zaidi ya nchi tofauti na ilivyo sasa ambapo imejikita zaidi Mkoa wa Dar es Salaam.

**110. *Mheshimiwa Spika,*** wasanii wa filamu wameendelea kuhamasishwa na kuelimishwa kutumia huduma za kidijiti za Bodi ya Filamu kupitia mfumo wa Utambuzi wa Wasanii *(Artists Management Information System - AMIS)* unaotoa fursa kwa wasanii kupata huduma bila kulazimika kufika ofisi za Bodi. Jumla ya wasanii mia tano na watano (505) wamesajiliwa na kupatiwa huduma. Huduma hizo ni pamoja na vibali vya utayarishaji wa filamu vimetolewa kwa wasanii mia moja ishirini na watatu (123), vibali vya uhakiki wa filamu vimetolewa kwa wasanii sitini na wanane (68), na vitambulisho vya wasanii wa filamu mia tatu kumi na vinne (314) vimetolewa.

**111. *Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni mwendelezo wa jitihada za kuweka mazingira ya wadau wa filamu kujadili masuala muhimu yanayohusu maendeleo ya Tasnia ya Filamu, Bodi ilifanya kongamano (Symposium) la wadau wa filamu lililofanyika mwezi Desemba 2023 jijini Dar es salaam. Kongamano hilo lilihudhuriwa na wadau wa filamu takribani 206 na lilihusisha mijadala ya masuala mbalimbali ya tasnia ikiwamo fedha, mitaji na weledi katika uandaaji wa filamu. Aidha, vikao viwili (2) vilivyoshirikisha viongozi wa Shirikisho la Filamu Tanzania (TAFF) vilifanyika, ambapo masuala mbalimbali yanayohusu uongozi na mipango ya kuendeleza Tasnia ya Filamu kupitia vyama vinavyounda Shirikisho hilo yalijadiliwa.

**112. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Bodi iliwezesha kufanyika kwa matamasha matano ya wadau ya Tuzo zilizohusisha Filamu ambapo jumla ya Tuzo 67 zilitolewa kwa washindi kwenye vipengele mbalimbali. Matamasha hayo ni UNI Awards lililofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 5 Agosti 2023 kwa kutoa tuzo 4 na kuhudhuriwa na wadau 1,200; Tamasha la Kigamboni lilifanyika tarehe 05 Agosti, 2023 na kuhudhuriwa na wadau 650 na kutoa tuzo 22; Tamasha la Filamu Morogoro tarehe 10

Septemba 2023 lilihudhuriwa na wadau 500 na kutoa tuzo 17; Tamasha la Tuzo Iringa tarehe 29 Septemba 2023 lilihudhuriwa na wadau 600 na kutoa tuzo 12; na Tamasha la Filamu Mbeya tarehe 23 Februari 2024 lilihudhuriwa na wadau 1,500 na kutoa Tuzo 12. Kufanyika kwa matamasha kumechochewa na ukuaji wa tasnia ya filamu na kuongezeka kwa ushindani na utayarishaji wa filamu bora.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ilipokea na kushughulikia miswada ya vibali vya kutayarisha filamu 163 ikiwa ni asilimia 13 ya lengo la vibali 1,300 kwa mwaka. Kati ya vibali vilivyoombwa, maombi 115 yalikuwa ya Watanzania na 48 yalikuwa ni ya kutoka nje ya nchi. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 maombi yote yalipatiwa vibali.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** sababu za kutokufikiwa kwa lengo ni kutokana na waombaji kutokudaiwa vibali kwa kuwa kazi zao zinasambazwa kwenye Youtube, ambapo Bodi ya Filamu haina mamlaka ya kuzuia kazi hizo kusambazwa kwenye mtandao huo. Sababu nyingine ni mabadiliko ya aina za filamu zinazozalishwa. Kwa sasa wasanii wengi wanatengeneza tamthilia ambazo zinachukuwa muda mrefu tofauti na filamu (feature films) zilizokuwa zikizalishwa kwa wingi hapo awali.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na changamoto hizo, Bodi ya Filamu imeendelea kudhibiti maudhui ya filamu ambapo kutokana na udhibiti huo, ilipokea na kuhakiki jumla ya filamu 318 zinazojumuisha tamthiliya 40 zenye jumla ya Sehemu (episodes) 1,624. Kati ya filamu hizo, filamu 232 zilikuwa za Kitanzania na filamu 86 zilikuwa za kutoka nje ya nchi.

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kupitia programu ya Sanaa ya Mtaa kwa Mtaa katika Tasnia ya Filamu, Bodi iliandaa mikutano na mafunzo kwa vitendo yaliyotolewa kwa wadau wa filamu na michezo ya kuigiza ambapo jumla ya wadau 453 waliweza kufikiwa na kupewa elimu kuhusu masuala yanayohusu filamu na michezo ya kuigiza katika mikoa 25 ya Tanzania Bara.

### 3.2.1.8 OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hakimiliki ni moja ya mwavuli wa miliki bunifu (Intelletual Property) ambapo lengo hususan la miliki bunifu ni kulinda ubunifu na uvumbuzi (creativity and innovation) mbalimbali kwa lengo la kuwawezesha wabunifu kunufaika kwa kujipatia kipato katika kazi zao za ubunifu. COSOTA inasimamia masuala ya Sanaa na uandishi ambapo majukumu ya Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) ni pamoja na kukuza na kulinda maslahi ya watunzi, waandishi, wasanii, wafasiri, watayarishaji wa kurekodi sauti, watangazaji, na wachapishaji kwa kulinda haki zao zilizofafanuliwa katika Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya Mwaka 1999; kusajili kazi za Sanaa (artistic works) na kazi za uandishi (literary works); kubainisha masuala ya umiliki inapotokea kuna migogoro ya hakimiliki baina ya pande mbili; kusimamia uanzishwaji na utendaji wa kampuni za wasanii wenyewe kwa ajili ya kukusanya na kugawa mirabaha; kutoa ushahidi wa umiliki wa hakimiliki; kutoa elimu katika masuala ya hakimiliki; kusimamia ukusanyaji wa mapato katika tozo za hakimiliki na kushirikiana na Taasisi kama COSOTA katika nchi nyingine na ushirikiano baina ya Tanzania na Ofisi za Kanda na zile za Kimataifa zinazoshughulikia masuala ya hakimiliki.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuhakikisha kuwa wasanii na waandishi wananufaika kwa kupata kipato kutokana na ubunifu wao, Ofisi ya Hakimiliki kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Aprili 2024 imefanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi 636,096,726.40 kupitia chanzo kipya cha mapato cha Tozo ya Hakimiliki (Copyright levy) kupitia Kanuni ya Tozo ya Hakimiliki (The Copyright and Neighbouring Rights (Copyright levy on blank devices)) Regulations, 2023.

Aidha, kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji, Sekta ya Sanaa imeendelea na utekelezaji wa mpango huo ambapo kupitia Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7/1999 marekebisho ya mwaka 2022 na 2023, kumekuwa na mgawanyo wa majukumu ya Ofisi ya Hakimiliki na kutoa nafasi kwa sekta binafsi kupitia kampuni za wasanii wenyewe za

kukusanya na kugawa mirabaha. Kupitia mabadiliko haya COSOTA imetoa leseni moja kwa Kampuni ya kukusanya na kugawa mirabaha katika daraja la muziki (Collective Management Organizations – CMOs) ya Tanzania Music Rights Society (TAMRISO) na tayari imeanza zoezi la kukusanya mirabaha.



*Mhe. Hamis Mwinjuma (Mb.), Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo (wa tatu mbele kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi na wanachama waanzilishi wa Kampuni ya kukusanya na kugawa mirabaha kwa kazi za Muziki ijulikanayo kama Tanzania Music Rights Society (TAMRISO), iliyofanyika katika Ukumbi wa Hoteli ya Hyatt Jijini Dar es Salaam tarehe 21 Julai 2023. Wa kwanza kulia ni Bi. Doreen Anthony Sinare Afisa Mtendaji Mkuu wa COSOTA.*

**119. *Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa wabunifu kutakiwa kupata kipato kutokana na matumizi ya kazi zao, COSOTA ilikusanya mapato kwenye maeneo mbalimbali yanayotumia muziki katika biashara kama vile hoteli, baa, disko, redio na televisheni ambapo tarehe 21 Julai 2023 COSOTA ilifanya mgao wa 24 wa mirabaha wa jumla ya kiasi cha Shilingi 396,947,743 kwa wanufaika 8,018 nyimbo 35,543. Mgao huo ulikuwa ni wa mwisho kwa COSOTA kuufanya kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na 7/1999 yaliyofanyika mwaka 2022 kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka

2022. Marekebisho hayo yamezipa mamlaka Kampuni binafsi za wasanii kufanya kazi ya kukusanya na kugawa mirabaha kwa wadau wanaohusika.

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji, COSOTA imetengewa jumla ya Shilingi 319,527,000 ambapo inategemewa kufanyia kazi masuala ya maboresho ya kanuni kuhusu hakimiliki; elimu kwa umma kuhusu hakimiliki na uharamia, kuweka mazingira bora ya uwezeshaji wa wasanii, waandishi na watumiaji wa kazi za Sanaa wanaopewa leseni ambapo itafanyika kupitia ushirikiano wa COSOTA, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania (TFB) na ulinzi wa kazi za hakimiliki kupitia mfumo jumuishi ambapo mfumo huu utakapokamilika utanufaisha taasisi husika na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa pamoja na wadau wengine kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ili kuwezesha urasimishaji na utekelezaji wa taasisi mbalimbali zenye uhitaji wa taarifa za wasanii, waandishi na wabunifu wengine pamoja na kazi zao.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Hakimiliki Tanzania imeendelea na usajili wa kazi za wasanii, waandishi na wabunifu wanaomiliki kazi za ubunifu. Jumla ya wabunifu 172 pamoja na kazi zao za kibunifu 566 zilisajiliwa. Aidha, COSOTA ilitoa idadi ya vyeti vya uthibitisho wa umiliki, (Copyright Clearance Certificate) 637 kwa kazi zilizosajiliwa katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** mojawapo ya jukumu la Ofisi ya Hakimiliki Tanzania ni kutatua migogoro baina ya wabunifu. Kumekuwapo na migogoro katika masuala ya hakimiliki ili kuhakikisha kuwa wenye hakimiliki wanapata haki zao na kupata mapato stahiki, COSOTA inatekeleza jukumu hili na pale pande mbili wanaposhindwa kuelewana mgogoro husika unafikishwa katika Mahakama. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Ofisi ya Hakimiliki (COSOTA) ilipokea jumla ya migogoro 19 na kufanikiwa kufanyia kazi migogoro 12 na

migogoro saba (7) iliyobaki inaendelea na usuluhishi. Aidha, COSOTA imeshiriki kutoa ushahidi wa kitaalamu katika kesi nne (4) za masuala ya hakimiliki zilizokuwa katika Mahakama za Arusha na Dar es Salaam zilizopokelewa katika kipindi cha mwaka 2023/24. Ofisi ya Hakimiliki itaendelea kutatua migogoro kadiri itakavyokuwa ikipokea.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa lengo la kuufahamisha umma kuhusu haki zao, Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) imeendelea na zoezi la kutoa elimu kupitia njia mbalimbali. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 elimu imetolewa kwa wabunifu wa Mkoa wa Pwani, Dar es Salaam na Tanga. Pia, kwa kutumia vipindi katika vyombo vya habari ikiwamo Kituo cha TBC 1, TBC Taifa, Uhai Tv, Clouds Fm, Wasafi Fm, Wasafi Tv, Channel Ten, EATV, Sinema Zetu na UFM elimu imeendelea kutolewa kwa wadau. Aidha, elimu imetolewa kwa njia ya mitandao ya kijamii kupitia *WhatsApp, Zoom, Instagram, Facebook, Thread* na *XSpace* ambapo watumiaji wa mitandao 435,000 wamefikiwa.

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kufuatia Sheria ya Hakimiliki NA. 7/1999 marekebisho ya mwaka 2022 na 2023, kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2022 na Sheria ya Fedha ya mwaka 2023, Wizara kwa kushirikiana na COSOTA imekamilisha na kuboresha Kanuni ya kutoza ada kwa vibebeo vya kazi za wasanii, waandishi na wabunifu wengine yaani tozo ya hakimiliki (copyright levy) inayofahamika kama Kanuni ya Tozo ya Hakimiliki (Copyright Levy), 2023 ya tarehe 1 Septemba 2023. Utekelezaji wa ukusanyaji wa mapato umeanza kwa COSOTA kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Aidha, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo imejadili maboresho kuhusu Kanuni za kuanzisha kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha yaani Kanuni za Hakimiliki na Hakishiriki (Kampuni za Ukusanyaji na Ugawaji Mirabaha), Serikali ilifanya marekebisho katika kanuni na zipo kwenye hatua za mwisho za kukamilika.

COSOTA pia imeandaa rasimu za kanuni mbalimbali zinazohusu usajili, kanuni kwa ajili ya kundi maalumu la wasioona na kanuni kuhusu utatuzi wa migogoro ambazo zitasaidia kuboresha utendaji kazi na ufanisi wa Ofisi katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Namba 7 ya Mwaka 1999. Hadi Aprili, 2024, COSOTA ipo kwenye hatua ya kupokea maoni ya wadau ili kukamilisha kanuni zinazohusika.

### 3.2.1.9 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

**125. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza utamaduni na sanaa, Serikali imewekeza nguvu kubwa katika utaalamu, utafiti na ushauri ambapo TaSUBa ni Taasisi inayotoa mafunzo ya aina mbalimbali kuhusiana na masuala ya sanaa na utamaduni nchini. Mwaka 2012 Taasisi hii iliteuliwa kuwa Kituo cha Jumuiya ya Afrika Mashariki chenye Ubora Uliotukuka katika Ufundishaji wa Fani za Utamaduni na Sanaa hivyo ni Chuo chenye hadhi ya Kimataifa.

**126. *Mheshimiwa Spika***, mafunzo yanayotolewa na Taasisi hii, yanafundishwa kwa vitendo asilimia 70 na nadharia asilimia 30 katika kozi za Filamu na Uzalishaji wa Vipindi vya Televisheni (Film and TV Production); Uzalishaji wa Muziki na Sauti (Music and Sound Production); na Sanaa za Maonesho na Ufundi (Performing and Visual Arts). Hii inaonesha ni kwa jinsi gani wanachuo wanapohitimu mafunzo yao ni rahisi kuingia kwenye soko la ajira kwa kuajiriwa au kujiajiri wenyewe katika tasnia ya sanaa na utamaduni ndani na nje ya nchi.

**127. *Mheshimiwa Spika***, katika kupanua wigo wa mafunzo na kuongeza udahili kwa kutoa nafasi zaidi kwa vijana wa Kitanzania kujiunga na sekta ya ubunifu, Taasisi inatarajia kuanza kutoa mafunzo ya kozi mpya ambazo ni Usimamizi wa Sanaa na Masoko katika Sanaa *(Arts Management and Marketing)*. Kozi hii inatarajia kuwa na lengo la kumwandaa Ofisa Masoko kutafuta masoko kwa msanii na kazi yake, ndani na nje ya nchi; kozi ya pili ni Urithi wa Utamaduni na Utalii *(Cultural Heritage and Tourism)*; Kozi hii itamwezesha mhitimu kuingia kwenye soko la Utalii wa Kiutamaduni ambao kwa sasa unakua kwa kasi kubwa

sana duniani, na ya tatu ni Kozi ya Muziki (Music). Mafunzo ya kozi hizi yataanza mara tu baada ya kukamilika kwa mitaala ambayo imeshawasilishwa NACTVET ili kupata ithibati.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** juhudi kubwa zilizofanywa na Wizara kushirikiana na TaSUBa kwa kuweka mikakati mbalimbali zimeweza kuongeza udahili ambapo hadi mwezi Aprili, 2024 imedahili jumla ya wanachuo 798 wa kozi ndefu, sawa na asilimia 106 ya lengo la kudahili wanachuo 750. Sambamba na hilo, ili kuwafikia vijana wengi zaidi ambao wana vipaji, TaSUBa imewekeza katika utoaji wa mafunzo ya kozi fupi ambapo katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 washiriki 289 wamepatiwa mafunzo, sawa na asilimia 116 ya lengo la washiriki 250.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa taarifa na ushawishi kwa umma pamoja na kujitangaza, TaSUBa imekamilisha Mpango Mkakati wa Kutangaza Taasisi (Communication Strategy) ambapo hadi kufikia Aprili, 2024 imefanya ziara 14 katika Vituo vya Habari pamoja na kufanya vikao 15 na waandishi wa Habari. Vilevile, TaSUBa imeendelea kutumia kurasa zake za mtandaoni za *Instagram* (Tasuba. Bagamoyo), *facebook* (Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo), *Youtube* (TaSUBa TV) na *Twitter* (TAASISISANAA) kutoa elimu na taarifa mbalimbali kwa jamii kuhusiana na masuala ya utamaduni na sanaa. Aidha, TaSUBa imeweza kutumia blogu mbalimbali katika kufikisha taarifa kwa jamii hali iliyosababisha kuongezeka kwa udahili.

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** TaSUBa imeendelea kuwawezesha kitaaluma wadau wa utamaduni na sanaa kwa kuendesha mafunzo maalumu kwa Vyama, Mashirikisho, Asasi zisizo za Kiserikali, na Taasisi Binafsi. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo katika utekelezaji wa shughuli za utamaduni na sanaa na kuwa mahiri katika tasnia zao, hatimaye waweze kujiajiri na kukuza pato binafsi na Taifa kwa ujumla. TaSUBa imetoa mafunzo ya sanaa kwa bendi ya Maofisa wa Jeshi la Uhamiaji ambapo jumla ya wahitimu 25 walitunukiwa vyeti katika mafunzo yaliyofanyika mwezi Oktoba 2023. Aidha, TaSUBa kwa kushirikiana na Chuo cha Taaluma cha Ukerebishaji

Tanzania (TCTA) imeweza kuendesha mafunzo kwa maafisa 60 wa Jeshi la Magereza. TaSUBa kwa ushirikiano na asasi ya "Musicians for a Better Life" kutoka nchini Ujerumani waliendesha mafunzo ya muziki wa kuimba na ala kwa wanachuo na wadau kutoka mikoa mbalimbali wapatao 60. Pia, TaSUBa kwa kushirikiana na wanachuo kutoka Chuo cha "Filmakademie" cha nchini Ujerumani waliendesha mafunzo ya utengenezaji na uandaaji wa filamu fupi za mtindo wa makala (Documentary) ambapo wanachuo 47 walinufaika. Pia, TaSUBa imeendesha mafunzo ya uimbaji na upigaji wa ala za muziki kwa waumini wa kanisa la Waadventista wa Sabato wapatao 58.



*Mhe. Hamis Mwinjuma (Mb.), Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo (wa pili kutoka kushoto) akimtunuku cheti Msanii wa Bongo Fleva Bw. Farid Kubanda (FidQ) (wa kwanza kulia) ambaye pia ni Katibu wa Shirikisho la Muziki Tanzania kwenye mahafali ya 34 yaliyofanyika TaSUBa tarehe 8 Disemba, 2023.*

**131. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TaSUBa imekuwa ikiimarisha shughuli za Utamaduni na Sanaa kupitia Taasisi mbalimbali za elimu ikiwemo Shule za Msingi na Sekondari. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 TaSUBa kwa kushirikiana na Taasisi ya *Bagamoyo Friendship Society* ya nchini Ujerumani ilitoa mafunzo ya Utamaduni na Sanaa kwa watoto 78 kutoka shule 8 za Msingi na 5 za Sekondari za Mkoa wa Pwani. Aidha, kupitia mashindano ya UMISSETA na UMITASHUMTA 2023, TaSUBa imetoa mafunzo ya Utamaduni na Sanaa kwa wanafunzi. Mafunzo hayo yalijikita katika kufundisha namna bora ya kuendesha Sanaa za Maonesho hususan katika

maeneo ya fani za maigizo, muziki na ngoma za asili. Jumla ya walimu 8 wa shule za Msingi, 6 wa Shule za Sekondari na wanafunzi 134 walipatiwa mafunzo hayo. Vilevile, mradi wa TaSUBa Kids unaofadhiliwa na Taasisi ya Bagamoyo *Friendship Society* ya nchini Ujerumani umetoa mafunzo kwa wanafunzi 30 wa shule tatu (3) za Sekondari za Wilaya ya Bagamoyo.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** TaSUBa imetoa ushauri kwa wadau wa Utamaduni na Sanaa wapatao 259 kutoka maeneo mbalimbali nchini na nje ya nchi. Mmoja ya wadau waliopatiwa ushauri ni pamoja na asasi ya ''*Good Neighbors*'' Tanzania kwa kuandaa makala fupi ya filamu inayohusu namna ya kuwasaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu katika kijiji cha Suli kilichopo Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma. Aidha, ushauri huo ulitolewa kupitia vikao vya wadau, mawasiliano ya simu, na mazungumzo ya wadau wanaotembelea TaSUBa.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** TaSUBa inafanya tafiti mbalimbali na hadi kufikia Aprili, 2024 Taasisi imesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na asasi ya NAWEZA iliyopo Tanzania na asasi ya "*Media for Development International*" (MFDI) ya nchini Marekani. Lengo la MoU hiyo ni kuandaa mradi wa kutoa elimu ya afya ya hedhi salama kwa kutumia sanaa pamoja na utafiti wa tamaduni za makabila mbalimbali ya Tanzania. Aidha, Taasisi ipo katika hatua za mwisho za majadiliano ya kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shiriki Muhimbili (MUHAS) na Chuo Kikuu cha Bergen (UiB) cha nchini Norway, kufanya utafiti ili kuona uwezekano wa muziki kuwa sehemu ya tiba ya afya ya akili (*music therapy*).

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na ongezeko kubwa la vijana wanaodahiliwa kila mwaka, TaSUBa imeendelea na ukarabati wa miundombinu ambapo hadi kufikia Aprili, 2024 madarasa, ukumbi mkuu wa maonesho, ukumbi wa "flexible", Jukwaa la Mwembeni, pamoja na ofisi vimefanyiwa ukarabati na miundombinu ya TEHAMA imeimarishwa. Aidha, vifaa vya kufundishia na kujifunzia vimenunuliwa pamoja na jukwaa la kuendeshea Tamasha la Kimataifa la Utamaduni na Sanaa Bagamoyo. TaSUBa pia imekamilisha ukarabati wa

miundombinu ya studio za redio na televisheni ambapo kinachosubiriwa ni ununuzi na kusimika mitambo ya kurushia matangazo.




*Jukwaa lililonunuliwa na Serikali kwa ajili ya kutumika kwenye matamasha mbalimbali kama linavyoonekana kwenye picha lilipotumika wakati wa Tamasha la 42 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo tarehe 26 – 28 Oktoba, 2023.*

**135. *Mheshimiwa Spika***, Taasisi iliendesha Tamasha la 42 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo lililofanyika tarehe 26 – 28 Oktoba, 2023 ambapo Mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati. Tamasha lilihusisha maonesho ya sanaa za jukwaani, filamu, sanaa za ufundi, huduma za biashara, kongamano na mafunzo. Aidha, liliambatana na kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo Bagamoyo. Tamasha lilihusisha watazamaji wa ndani na nje wanaokadiriwa kufikia 50,815. Fauka ya hayo, vikundi mbalimbali vya sanaa kutoka ndani na nje ya nchi vipatavyo 46 vilishiriki. Kati ya hivyo, vikundi vya ndani vilikuwa 39 na vya nje 4 ambavyo vilitoka katika nchi za Zambia, Canada, Kenya na Uganda.



*Kikundi cha ngoma almaarufu Makirikiri wa Bongo kikitoa burudani katika Jukwaa la Tamasha la 42 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo lililofanyika katika viwanja vya Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) tarehe 26 – 28 Oktoba, 2023.*

**136.** ***Mheshimiwa Spika***, TaSUBa imeendelea kuimarisha mtandao (Networks) kati ya Taasisi na wadau wa sanaa nje na ndani ya nchi. Makubaliano ya ushirikiano (MoU) yamesainiwa na wadau wa ndani. Wadau hao ni pamoja na *Good Neighbours Tanzania;* Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji Tanzania *(Tanzania Correction Training Academy - TCTA); Tanzania House of Talent (THT);* na *Naweza Foundation*. Wadau wa nje ambao Taasisi inashirikiana nao na makubaliano ya ushirikiano (MoU) yamesainiwa ni pamoja na *Bagamoyo Friendship Society* (Ujerumani); *Musicians for a Better Life* (Ujerumani); *Volkshochschule Ahlen* (VHS Ahlen - Ujerumani), *Pedagogical Studies & Arts Teacher's Pedagogical Studies - University of the Arts Helsinki* Finland; *Teaching Artist Institute - TAI* (Marekani); na *Media for Development International Inc*. (Marekani).

**3.2.2 SEKTA YA MICHEZO**
**3.2.2.1 IDARA YA MAENDELEO YA MICHEZO**

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Maendeleo ya Michezo hapa nchini ina jukumu la kuhakikisha inaweka mazingira bora na wezeshi kwa Maendeleo ya Michezo hususan kuzalisha ajira, kuimarisha afya za wananchi pamoja na kuwaletea furaha Watanzania. Lakini pia kupitia sekta ya michezo nchi yetu inaendeleza ushirikiano na mataifa mbalimbali kupitia diplomasia ya michezo. Sekta hii kwa sasa inatekeleza majukumu yake kwa kufuata Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 ambayo imetengenezewa mkakati wa Utekelezaji wa mwaka 2022. Sekta hii ni miongoni mwa mihimili inayotoa ajira na kuchangia katika uchumi wa mtu mmojammoja na kwa Taifa kwa ujumla. Aidha, sekta hii inahusisha Idara ya Maendeleo ya Michezo, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Katika kutekeleza majukumu yake Wizara kupitia Sekta hii imetekeleza majukumu yafuatayo:

**138.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa mwaka 1957, Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Mataifa ya Afrika (AFCON 2027) yatafanyika Tanzania kwa ushirikiano na nchi za Kenya na Uganda. Nchi hizi za Afrika Mashariki zimeshinda zabuni ya kuandaa mashindano hayo iliyofanyika mwezi Septemba, 2023 Cairo, Misri. Uratibu wa maandalizi ya mashindano hayo unaendelea kwa kufanyika vikao vya pamoja. Ili kufanikisha kufanyika kwa mashindano hayo, kila nchi inakarabati na kujenga miundombinu yenye kukidhi viwango na vigezo vya Kimataifa. Tanzania kupitia uwenyeji wa mashindano ya AFCON, 2027 itapata fursa ya kuwa na miundombinu bora ya michezo ambayo itakidhi vigezo vya Kimataifa. Aidha, mashindano hayo yataimarisha na kuendeleza ushirikiano na ujirani mwema na nchi ya Kenya na Uganda. Mashindano haya pia yatafungua fursa mbalimbali za biashara na kuitangaza Tanzania na vivutio vyake Kimataifa pamoja na kuongeza pato la Taifa kupitia michezo.

**139.** ***Mheshimiwa Spika***, Tanzania imepata fursa ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya CHAN yatakayofanyika nchini

Tanzania mwezi Septemba 2024. Mashindano haya ni ya maandalizi ya AFCON 2027. Mashindano haya ya AFCON yatachagiza kuwapo kwa fursa lukuki za ujenzi wa miundombinu, kujenga uchumi, kuvutia utalii, ajira na kuitangaza Tanzania kimataifa. Ni matunda ya uwekezaji mkubwa katika michezo uliofanywa na Mheshimiwa Rais na yanatokana na maono na maelekezo binafsi ya Mheshimiwa Rais.

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, tangu nchi yetu ipate uhuru 1961 hatukuweza kuwatumia wanamichezo wa Diaspora kama ambavyo nchi yingi za Afrika zimekuwa zikinufaika na utaratibu wa kuwatumia wachezaji wa Diaspora. Kwa mara ya kwanza katika historia katika hatua ya kufuzu AFCON ya 2023 tumefanikiwa kuwatumia wachezaji wa Kitanzania wanaoishi nchi nyingine ambao wana asili ya Tanzania (Diaspora). Wachezaji hao hakika wameleta tija na hamasa katika timu yetu ya Taifa Stars. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia kuwatumia vijana hao wa Diaspora katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa.

**141.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia mafanikio ya kuwa wenyeji wa CHAN 2024 na AFCON 2027 tumeianza safari ya mafanikio ya kushiriki Kombe la Dunia 2030 kwa kuanza kujenga miundombinu na timu imara ya Taifa. Katika hili, timu imara ya Taifa itaandaliwa kwa kuwa na timu tatu za vijana chini ya miaka 17 (itakayotokana na UMISETA na UMITASHUMTA); chini ya miaka 20 na chini ya miaka 23, makocha wazoefu wataajiriwa na huduma za timu hizi zitasimamiwa kama programu maalumu ya Serikali.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Serikali kupitia Wizara imetekeleza majukumu mbalimbali. Miongoni mwa majukumu hayo ni; kuratibu na kusimamia ushiriki wa Tanzania katika mashindano ya *African Games* (AG) yanayoshirikisha nchi 54 za Bara la Afrika yaliyofanyika tarehe 8 hadi 23 Machi, 2024 katika Jiji la *Accra* Nchini *Ghana*. Katika mashindano hayo, Tanzania iliwakilishwa na Timu saba (7)

zikiwamo Timu za michezo ya mpira wa miguu kwa wanawake chini ya miaka 20, Kriketi wanawake, Kuogelea, Baiskeli, Riadha, Ngumi na Judo. Jumla ya wanamichezo na viongozi 109 kutoka Tanzania wameshiriki mashindano hayo. Hii ni idadi kubwa ya washiriki kwa mara ya kwanza tangu nchi yetu ilipoanza kushiriki mashindano hayo mwaka 1963.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu mashindano ya Kombe la Taifa (Taifa Cup), Mtaa kwa Mtaa. Kutokana na mpango huo, Serikali imefanikiwa kupata vifaa vya michezo vinavyotumika katika maandalizi na mashindano hayo kutoka kwa wafadhili wa Jamhuri ya Serikali ya Watu wa China. Vifaa vilivyopokelewa ni pamoja na: Jezi na Mipira ambapo mipira 54 imekwishagawiwa kwa kila Mkoa, ambapo kila Mkoa ulipata mipira 18 ya mchezo wa soka, mipira 18 ya mchezo wa kikapu na mipira 18 ya mchezo wa mpira wa wavu. Hii ni katika hatua ya kuwezesha mashindano hayo kuwa na hamasa na ufanisi katika ngazi zote.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** mashindano ya Michezo ya Shule za Sekondari za Afrika Mashariki (FEASSA) kwa mwaka 2023/24 yalifanyika kuanzia tarehe 17 hadi 28 Agosti, 2023 Kigali nchini Rwanda. Jumla ya washiriki 440 kutoka Tanzania walishiriki michezo hiyo ambapo wanafunzi walikuwa 365, na walimu na viongozi 75. Mashindano haya kwa ujumla yamekuwa na manufaa makubwa katika upatikanaji wa vipaji vya michezo mbalimbali hapa nchini.

**145.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha utendaji na usimamizi wa shughuli za michezo katika ngazi zote, Wizara iliandaa kikao kazi kilichohusisha Maofisa Michezo wote Tanzania Bara kilichofanyika Tarehe 28 - 29 Agosti, 2023 Mkoani Njombe. Kikao hiki kililenga kuwajengea uwezo Maofisa Michezo walio katika Idara, Taasisi, mikoa na Halmashauri katika utekelezaji wa majukumu yao ya uendeshaji wa shughuli za michezo katika maeneo yao. Kupitia kikao hiki washiriki walijadili na kupokea maelekezo ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya michezo zinazoratibiwa katika ngazi zote. Kikao hicho kilihudhuriwa na jumla ya washiriki 250.



*Washiriki wa Kikao Kazi cha Maofisa Michezo wote nchini, kilichofanyika Mkoani Njombe katika Ukumbi wa Halmashauri Mji tarehe 28 – 29 Agosti, 2023.*

**146.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Serikali imeweza kuratibu na kushiriki Kikao cha Kanda V Afrika kuhusu Mapambano ya Kuzuia Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni *(Anti doping)*. Kikao hicho kilifanyika tarehe 21 – 22 Septemba, 2023 Cairo Misri ambapo katika mkutano huo iliazimiwa nchi zote kutimiza masharti ya RADO na WADA ikiwemo kulipa ada, kuhudhuria mikutano ya Kanda na kujibu dodoso ya upimaji wa utekelezaji wa matakwa ya WADA; nchi kutenga bajeti na kusisitiza Vyama/Mashirikisho, mashirika au waandaaji wa mashindano kutenga bajeti ya uchukuaji sambuli kwa ajili ya upimaji wa kuwapo kwa vimelea vya dawa zinazokatazwa michezoni. Mkutano ujao utafanyika nchini Tanzania mwezi Septemba 2024.




*Washiriki wa Kikao cha Kanda V Afrika kuhusu Mapambano ya Kuzuia Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni (Anti doping) uliofanyika Cairo, Misri, tarehe 21 – 22 Septemba, 2023*

**147. *Mheshimiwa Spika***, Serikali imeweza kutoa mafunzo kwa wachezaji 120 kwa Timu za Tanzania zilizoshiriki mashindano ya *African Games* (AG) na kufanikiwa kupima sampuli za wachezaji 15 wa Timu ya Tembo Warriors, 2 Judo, 4 Riadha Kilimanjaro Marathon na 8 Soka wakati wa *African football League* (AFL) na Klabu Bingwa Africa. Matokeo ya vipimo hivyo ni kwamba wachezaji waliochukuliwa sampuli hawakukutwa na vimelea vyovyote vinavyohusiana na dawa za kuongeza nguvu michezoni.

**148. *Mheshimiwa Spika***, Fauka ya hayo, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa Mawaziri wa Afrika kuhusu mwenyeji wa mashindano ya Afrika (*African Games)* pamoja na kujadili mwenendo wa *Anti-doping* ulifanyika nchini Ghana tarehe 6 hadi 9 Machi, 2024. Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi chache za AU ambazo zimeweza kuzingatia kwa ufasaha Sheria ya *Anti-doping* kwa kutoa mafunzo kikamilifu kwa wanamichezo wote walioshiriki mashindano hayo.

**149. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu matunzo na matumizi ya viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru ambapo mwezi Oktoba, 2023 Ligi ya Mpira wa Miguu Barani Afrika (AFL) ilifanyika katika uwanja huo, pamoja na michezo ya Ligi Kuu ya

Mpira wa Miguu. Ili kuhakikisha matunzo ya viwanja yanafanyika kwa weledi, Wizara imewajengea uwezo watumishi watatu (3) kwa kushiriki mafunzo ya Utunzaji wa Miundombinu ya Michezo yaliyofanyika mwezi Agosti, 2023 nchini China.

**150.** ***Mheshimiwa Spika***, katika juhudi za kuhakikisha kuwa wachezaji wetu wanapata huduma ya Kinga na Tiba michezoni, Wizara imeendelea kuhudumia wanamichezo walioshiriki katika matukio mbalimbali ambapo jumla ya wanamichezo 112 walipatiwa huduma za kinga na tiba kupitia kitengo cha Kinga na Tiba kilichopo katika Kiwanja cha Benjamin Mkapa. Huduma hiyo ilifanyika kwa kushirikiana na Chama cha Madaktari wa Tiba kwa Wanamichezo (TASMA).

### 3.2.2.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kusimamia aina zote za michezo ya ridhaa na ya kulipwa kwa kushirikiana na Vyama na Mashirikisho ya Michezo; kusajili Vyama vya Michezo; kutoa Tuzo kwa Wanamichezo wanaofanya vizuri katika mashindano ya Kitaifa na Kimataifa; na kuamsha ari ya wananchi kupenda aina zote za michezo.

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Baraza la Michezo la Taifa imeendelea kuwezesha na kugharimia Timu za Taifa zinazoshiriki katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, Serikali kupitia BMT, imewezesha jumla ya timu 15 kushiriki katika mashindano ya Kimataifa. Timu hizo ni pamoja na; Timu ya Taifa ya Mpira wa wavu kushiriki mashindano ya Afrika nchini Misri Mwezi Julai, 2023; Timu ya Taifa ya Karate iliwezeshwa kwenda nchini Kongo kushiriki mashindano ya Nchi za Maziwa Makuu mwezi Agosti, 2023; Timu ya Taifa ya Ngumi za Wazi iliwezeshwa kushiriki mashindano ya Afrika nchini Senegal mwezi Septemba, 2023; Timu ya Taifa ya Gofu ya Wanawake iliwezeshwa kushiriki mashindano ya Gofu ya Afrika Mashariki na Kati ambayo yalifanyika nchini Rwanda mwezi Novemba 2023. Timu ya Taifa ya mpira wa Miguu "Taifa Stars" ambayo imeshiriki mashindano

ya Afrika AFCON, (2023) nchini Ivory Coast mwezi Februari, 2024; na Timu ya Taifa ya Wanawake ya Mpira wa Miguu "Twiga Stars" iliwezeshwa kufuzu kucheza mashindano ya WAFCON yanayotarajiwa kufanyika mwezi Juni, 2024 nchini Morocco. Timu ya Taifa ya Netiboli imewezesha kushiriki mashindano ya kufuzu kombe la Dunia yaliyofanyika nchini Afrika kusini mwezi machi 2024. Timu ya Taifa ya Baseball iliwezeshwa kushiriki mashindano ya kufuzu kombe la Dunia yaliyofanyika nchini Malaysia mwezi Machi 2024 na Timu saba za Tanzania ikiwamo mpira wa Miguu kwa wanawake chini ya miaka 17, Ngumi, Baiskeli, Kuogelea, Riadha, Kriketi, na Judo ziliwezeshwa kujiandaa na kushiriki mashindano ya Afrika (All African Games) yaliyofanyika nchini Ghana mwezi April 2024. katika mashindano hayo Tanzania ilipata medali tatu (3) za shaba baada ya ukame wa miaka zaidi ya kumi.

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Baraza la Michezo la Taifa inaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa Wataalamu wa michezo waliopo katika sekta mbalimbali za usimamizi wa michezo. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi kufikia Aprili 2024 zaidi ya walimu wa shule za Msingi na Sekondari 192 sawa asilimia 107 ya lengo la wataalamu 180 kutoka Halmashauri wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya ukocha na ufundishaji wa michezo. Halmashauri zilizonufaika na mafunzo hayo ni Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Jiji la Arusha na Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

Mafunzo kama haya yametolewa pia kwa viongozi wa Vyama/Mashirikisho ya Michezo ya Tanzania Bara. Mafunzo haya yalifanyika tarehe 20 Julai, 2023 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere – JNICC jijini Dar es Salaam yakiwa na lengo la kuwajengea uwezo viongozi wa Vyama/Mashirikisho ya michezo kutekeleza majukumu yao kwa kufuata utawala bora pamoja na kufanikisha utekelezaji wa mipango iliyowekwa ya kuendeleza michezo nchini.

***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa imeendelea kuigharamia Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa Watu Wenye Ulemavu (*Tembo Warriors)*. Timu hiyo imefanya

kambi ya maandalizi ya muda mrefu ili kushiriki mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Watu Wenye Ulemavu kwa nchi za Afrika yanayofanyika nchini Misri kuanzia tarehe 18 hadi 29 Mei, 2024. Mashindano hayo yatatumika kufuzu kushiriki Mashindano ya Dunia ambapo timu nne (4) zitakazofuzu zitaliwakilisha Bara la Afrika katika mashindano hayo ya Dunia. Tayari timu imefuzu robo fainali katika mashindano hayo, pamoja na kuwa ilikuwa kundi moja na bingwa wa dunia timu ya Angola. Mchezo huu ni muhimu kwa watu wenye mahitaji maalumu, kwani umeendelea kutoa fursa za ajira nje ya nchi, ambapo wachezaji wa Tanzania wanaendelea kucheza katika klabu za Uturuki. Wachezaji hao ni pamoja na Shedrack, Hebron, Ramadhan na Chomelo.



*Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa Watu wenye Ulemavu Tembo Warriors wakiwa katika Kambi ya ndani iliyofanyika Karatu katika maandalizi ya mwisho kuelekea Mashindano ya African Amputee Football Cup of Nations (AAFCON 2024), yatakayofanyika jijini Cairo Misri.*

**155. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya ngumi ya Kimataifa ambapo mafanikio hayo ni ya mchezaji mmojammoja na ya timu. Wachezaji hao ni pamoja na Grace Joseph Mwakamela mchezaji wa Ngumi za Ridhaa alishinda medali ya Fedha katika pambano la Ubingwa wa Afrika kwa Wanawake lililofanyika mwezi Agosti, 2023 Yaounde, Cameroon.

Grace alimtwanga Ndiaye Ndye Seynabou Dieng wa Senegal; Yusuph Lucas Changarawe mchezaji wa ngumi za ridhaa pia alishinda medali ya Shaba katika pambano la Ubigwa wa Afrika lililofanyika mwezi Agosti, 2023 Yaounde, Cameroon ambapo alimtandika mwanamasumbwi Landu Mbeli Nathani wa Ivory Coast. Changarawe pia alipata medali ya Fedha katika pambano la kufuzu Olimpiki, 2024 lililofanyika mwezi Septemba, 2023 Dakar, Senegali kwa kumcharanga bondia Younes Nemouchi wa Algeria. Aidha, Changarawe alipata ushindi mwingine wa KO baada ya kumcharaza Pireira Diego wa Venezuela katika pambano la kwanza la Dunia la kufuzu Olimpiki ya Paris, 2024. Fadhili Majiha mchezaji wa ngumi za kulipwa alishinda Ubingwa wa WBC Africa katika pambano lililofanyika mwezi Oktoba, 2023 Jijini Dar es Salaam. Majiha alipata ushindi huo baada ya kumdunda bondia Bongani Mahlangu wa Afrika Kusini. Bondia mwingine aliyepata ushindi ni Hassan Mwakinyo mchezaji wa ngumu za kulipwa ambaye alishinda Ubingwa wa WBO Africa. Katika pambano lililofanyika Januari, 2024 visiwani Zanzibar baada ya kumchakaza bondia Elvis Ahogah wa Ghana. Vilevile, Josephat Joshua Gisemo mchezaji wa riadha alishinda nafasi ya kwanza katika mbio za km 10 zilizofanyika mwezi Januari, 2024 nchini Brazil.

**156.** ***Mheshimiwa Spika***, Madina Hussein mchezaji wa mchezo wa Gofu alikuwa mshindi wa kwanza kwenye *Ghana Ladies Open* katika *Gross Champion Category* iliyofanyika mwezi Agosti, 2023 Ghana, alishinda nafasi ya pili katika mashindano ya "Uganda open ",na alishinda pia nafasi ya pili katika Mashindano ya Gofu Wanawake Afrika Mashariki na Kati yaliyofanyika Kigali, Rwanda. Mchezaji mwingine Neema Olomi mchezaji wa Gofu alishinda nafasi ya kwanza kwenye mashindano ya Mombasa Coastal Open Leasure na nafasi ya tatu kwenye mashindano ya Mombasa Coastal Open yaliyofanyika Mombasa, Kenya. Aidha, Timu ya Taifa ya Golf ilikuwa mshindi wa kwanza katika Mashindano ya Gofu ya Afrika Mashariki na Kati.

**157.** ***Mheshimiwa Spika***, Wanariadha wa Kitanzania wameendelea kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa

ambapo mwanariadha Magdalena Shauri aling'ara katika mbio za kimataifa za "Berlin Marathon" ambapo alishika nafasi ya tatu (03), Alphonce Simbu alishika nafasi ya pili katika mbio ya kimataifa ya Shanghai International Marathoni pamoja na kushinda nafasi ya pili katika michezo ya dunia ya majeshi katika mashindano ya mbio ya "International Military Half Marathoni (CISM) yaliyofanyika tarehe 27 Oktoba, 2023 nchini Uswisi. Mwanariadha Jackline Sakilu alishinda medali ya shaba katika michezo ya dunia ya majeshi katika mbio za "International Military Half Marathoni (CISM).

**158.** ***Mheshimiwa Spika***, Timu ya Taifa ya mchezo wa Kuogelea ilishinda nafasi ya pili kati ya nchi 13 katika mashindano ya Aquatics Zone 3 Championship yaliyofanyika mwezi Novemba, 2023 Kigali, Rwanda. Aidha, Timu ya Taifa ya kuogelea ya Vijana ilishinda na kufika hatua ya fainali katika mashindano ya Vijana ya Afrika (Africa Aquatics Junior Championships) yaliyofanyika mwezi Desemba, 2023 nchini Mauritius. Timu nyingine ni Timu ya Taifa ya Karate iliyoshinda nafasi ya tatu na kunyakua jumla ya medali 45 zikiwamo medali mbili (2) za dhahabu, medali saba (7) za Fedha na Medali 36 za Shaba katika mashindano ya Karate ya Nchi za Maziwa Makuu yaliyofanyika mwezi Julai, 2023 nchini Congo.




*Baadhi ya wachezaji na viongozi wa Timu ya Taifa ya Karate walioshiriki katika mashindano ya Karate yaliyofanyika nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Julai 2023 na kujipatia medali 45.*

**159. *Mheshimiwa Spika***, Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika mchezo wa Mpira wa Miguu. Miongoni mwa Timu zilizofanya vizuri ni pamoja na Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wanawake Twiga Stars iliyofuzu kucheza mashindano ya WAFCON yanayotarajiwa kufanyika mwezi Juni, 2024 nchini Morocco; Klabu ya Mpira wa Miguu ya Wanawake ya JKT Queens iliyofuzu kushiriki mashindano ya Klabu Bigwa ya Afrika Mashariki na Kati, ikiwa ni mwakilishi pekee katika ukanda wa CECAFA. Timu ya Taifa Stars katika mashindano ya AFCON, 2023 ilicheza na kuishangaza dunia baada ya kupata sare ya 1:1 dhidi ya Zambia na suluhu ya bila kufungana dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Taifa Stars ilikuwa timu pekee kutoka Ukanda wa CECAFA. Fauka ya hayo, Klabu za Simba na Yanga zimeweza kufika katika hatua ya robo fainali kwa pamoja katika michezo ya Klabu Bingwa Barani Afrika ambapo, Tanzania kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi imeweza kufanikiwa kuingiza timu mbili (2) katika hatua ya robo fainali katika mashindano hayo.

**160.** ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio hayo yamechochewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye alizihamasisha timu hizo kwa kununua magoli yaliyofungwa. Aidha, kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Michezo pamoja na kushiriki katika harambee ya kuzichangia Timu za Taifa ni kichocheo kingine cha kufikia hatua iliyofikiwa.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, Baraza limesajili jumla ya Vyama vya Michezo 154 sawa na asilimia 77 ya lengo lililopangwa kusajiliwa. Usajili huu umefanyika kwa njia ya mfumo wa kielektroniki (SARS), Vyama vya Kitaifa 14, Vilabu 80, Akademia za michezo kumi (10), Vituo vya Michezo kumi (10), wakuzaji 38 na Wakala wawili (2). Vilevile, yalifanyika mabadiliko ya Katiba za Vilabu viwili (2) vya Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo Kitayose ya Tabora imebadilishwa jina kuwa *Tabora United Football Club* na Singida United ya Singida kuwa Singida *Fountain Gate Football Club.*

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Michezo la Taifa (BMT) limeendelea kusimamia utawala bora kwenye vyama vya michezo kwa kuhakikisha vyama vyote vinafanya uchaguzi wa viongozi wao kwa mujibu wa Katiba zao. Katika kipindi cha mwezi Julai 2023 hadi Aprili 2024, Baraza limeratibu na kusimamia chaguzi mbalimbali ikiwemo; Uchaguzi Mkuu wa Shirikisho la Michezo la Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania (SHIMIVUTA) ambao ulifanyika tarehe 27 Oktoba, 2023 jijini Tanga; Uchaguzi wa Chama cha Kriketi Tanzania (TCA) ambao ulifanyika tarehe 27 Desemba, 2023 jijini Dar es Salaam; Uchaguzi wa Shirikisho la Michezo Serikali za Mitaa Tanzania (SHIMISEMITA) ambao ulifanyika tarehe 29 Julai, 2023 Jijini Dodoma, Uchaguzi wa Chama cha CHESS Tanzania ambao ulifanyika tarehe 25 Februari, 2024 jijini Dar es salaam na Chama cha makocha wa riadha Tanzania (TACA) uliofanyika tarehe 24 Machi, 2024 jijini Dodoma.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Michezo la Taifa (BMT) lilifuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Kamati za Michezo za Mikoa katika mikoa mitatu (3) ikiwemo

Mkoa wa Pwani, Lindi na Mtwara. Ufuatiliaji huu umelenga kufanya tathmini shughuli za uendeshaji wa michezo katika ngazi za mikoa. Maeneo yaliyozingatiwa ni pamoja na kuona uhai wa Kamati, utekelezaji wa shughuli za michezo, taarifa za mashindano katika ngazi za mikoa pamoja na utatuzi wa migogoro katika ngazi za mikoa. Tathmini hii ilifanyika kuanzia tarehe 18 Januari hadi 02 Februari, 2024. Katika vikao hivyo ilisisitizwa kuendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa shughuli za michezo katika ngazi za mikoa ikiwemo kuhamasisha ushiriki wa jamii katika michezo, kusimamia uendelezaji wa viwanja na miundombinu ya michezo, kuibua vipaji, na kusimamia Vyama na Vilabu vya Michezo katika ngazi za mikoa na Wilaya.




*Kamati ya Michezo ya Mkoa wa Lindi pamoja na Maafisa wa Ufuatiliaji kutoka BMT wakiwa katika picha ya pamoja walipotembelea Mkoa huo tarehe 29 Januari, 2024.*

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika Michezo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, Baraza liliratibu Tamasha la Kimataifa la Michezo la Wanawake *(Tanzanite International Women Sports Festival)* ambapo kwa mwaka huu liliadhimishwa kwa kufanya Kongamano ambalo lililenga kuwajengea uwezo wanawake katika uendeshaji wa shughuli za michezo. Kongamano hili lilifanyika tarehe 21 0ktoba, 2023 likiwakutanisha viongozi wanawake wa Michezo, Maafisa Michezo wanawake wa Wilaya na mikoa, Watumishi wanawake wa Wizara na Baraza

pamoja na wadau wengine wa michezo. Manufaa yaliyopatikana kutokana na Tamasha hilo ni pamoja na kujenga uelewa mpana kuhusu masuala mbalimbali ya michezo na uongozi pamoja na kubadilishana uzoefu baina ya wanawake wa kada mbalimbali. Wanawake wapatao 200 walishiriki Kongamano hilo.

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na Tamasha hilo Baraza kwa kushirikiana na Taasisi ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Japani (JICA) waliandaa Awamu ya Tano ya Mashindano ya Riadha kwa Wanawake ya Juma Ikangaa "*5th Juma Ikangaa Ladies First*" ambayo yalifanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 24 hadi 26 Novemba, 2023. Lengo la mashindano hayo ni kuendelea kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika michezo. Kutokana na matamasha na mashindano hayo kumeshuhudiwa kuhamasika kwa hali ya juu kwa wanawake kushiriki katika michezo mbalimbali ambapo jumla ya wanawake wanamichezo 186 walishiriki kutoka mikoa yote 31 ya Tanzania. Katika kilele cha tamasha hilo kwa awamu zijazo litatambulika rasmi kama ***Juma Ikangaa Ladies First.***




*Maandamano ya Ufunguzi wa Awamu ya 5 ya Tamasha la Ladies First lililofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 24 – 26 Novemba, 2023.*



*Michuano ya riadha ya Awamu ya Tano (5) ya Tamasha la Ladies First, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 24 – 26 Novemba, 2023.*

**166. *Mheshimiwa Spika,*** kwa lengo la kuendelea kutambua vipaji vya wanamichezo na vilabu mahiri na wanaofanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) liliratibu utoaji Tuzo kwa wanamichezo waliofanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa. Tukio la utoaji wa tuzo lilifanyika tarehe 17 Machi, 2023 katika ukumbi wa Mlimani City, jijini Dar es Salaam ambapo tuzo hizo hazikutolewa zaidi ya miaka 40 tangu Baraza la Michezo la Taifa lianzishwe. Aidha, kwa mwaka 2023/24 hafla ya utoaji wa Tuzo inatarajiwa kufanyika mwezi Juni, 2024 Jijini Dar es Salaam.

**167. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika juhudi za kuhakikisha kunakuwa na miundombinu ya kutosha, kupitia Baraza la Michezo la Taifa litajenga viwanja vya mazoezi ya michezo katika Mkoa wa Manyara ambavyo vitahusisha kiwanja cha mpira wa miguu, pete, kikapu, wavu, mpira wa mikono na riadha. Viwanja hivi vitasaidia uibuaji na ukuzaji wa vipaji katika michezo. Mradi huu unatarajiwa kuanza utekelezaji katika mwaka wa fedha 2024/25. Aidha, Baraza linatarajia kujenga

viwanja vingine vya michezo katika mkoa wa Ruvuma (Songea) na Njombe.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya mapendekezo ya mabadiliko madogo ya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa ya mwaka 1967 (Sura ya 49) ya Sheria za Tanzania na Kanuni za Matumizi ya Mfuko wa Maendeleo ya Michezo kwa lengo la kuboresha ili sheria hiyo iweze kuendana na wakati wa sasa pamoja na kuongeza ufanisi katika usimamizi wa rasilimali fedha katika Mfuko huo. Aidha, Serikali imeanza hatua za kutunga Kanuni za Uwazi wa Matumizi ya Fedha katika Michezo.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Michezo la Taifa limeendelea kutoa vibali na idhini kwa timu na wachezaji kushiriki katika matukio mbalimbali ya michezo ya Kimataifa ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 jumla ya vibali 194 sawa na asilimia 107.7 ya lengo lililopangwa la vibali 180 vimetolewa. Vibali hivyo vimetolewa kwa matukio ya mbio za Marathoni, Mapambano ya Ngumi za Kulipwa, na matukio mengine ya michezo pamoja na vibali vya kazi kwa wachezaji na wataalamu wa michezo wa kigeni yaliyowasilishwa kuombewa vibali na vyama vya michezo inayohusika kwa niaba ya Vilabu na Taasisi zinazoshiriki mashindano hayo.

### 3.2.2.3 CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ni chuo pekee kinachotoa mafunzo ya michezo kwa wataalamu wa michezo nchini. Chuo hiki kipo mkoani Mwanza katika Wilaya ya Kwimba. Jukumu kuu la chuo hiki ni kufundisha taaluma ya michezo, kufanya utafiti na kutoa ushauri kuhusu masuala ya maendeleo ya michezo.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya imeendelea kudahili wanachuo katika masomo ya Michezo. Katika juhudi hizo, Chuo kimefanikiwa kuongeza idadi ya wanachuo ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 Chuo kilifanya usajili wa wanachuo 196 wa mwaka wa kwanza ambapo Wanaume ni 139 na Wanawake ni

57 ukilinganisha na usajili wa wanachuo 154 katika mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 27. Kwa upande wa mwaka wa pili Chuo kina wanachuo 90, Wanaume 61 na Wanawake 29. Hivyo jumla ya wanachuo wote kwa mwaka 2023/24 ni 286 ikilinganishwa na jumla ya wanachuo 261 mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 9.6.

**172. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2023/24 Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimetoa mafunzo ya muda mfupi katika kituo chake cha Dar es Salaam, Makao Makuu ya Chuo Malya na mkoani Morogoro. Aina ya mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na; Lishe katika michezo, Tiba na Kinga katika michezo, uandaaji na uratibu wa matukio mbalimbali ya michezo *(sports event management)*, Usimamizi wa viwanja *(Stadia management),* Uandishi wa Habari za Michezo *(Sports journalism)*, Ufundishaji wa Mpira wa Miguu, Mikono, Wavu, Netiboli na Kikapu. Mafunzo hayo yalifanyika kwa kushirikiana na Vyama/Mashirikisho ya Michezo nchini. Jumla ya washiriki 450 walishiriki mafunzo hayo na kupatiwa vyeti vya ushiriki. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 50 ya lengo la washiriki 300 lililowekwa.



*Washiriki wa mafunzo ya ufundishaji wa michezo mbalimbali walio pata mafunzo mkoani Morogoro yaliyofanyika katika shule ya Sekondari Morogoro kuanzia tarehe 27 Februari hadi 03 Machi, 2024.*

**173. *Mheshimiwa Spika,*** sambamba na utoaji wa mafunzo kwa wanachuo, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya

kimeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kuendelea na ujenzi wa hosteli za wanachuo. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, shughuli mbalimbali zimefanyika kwa upande wa ujenzi wa hosteli za wanafunzi. Shughuli hizo ni pamoja na; Usukaji wa nondo kwa ajili ya nguzo (column) za sakafu ya nne (4); Ujenzi wa nguzo mlalo (*beam)*; kujenga tofali; Ujenzi wa kuta kuanzia slabu ya kwanza, ya pili, ya tatu pamoja na ujenzi wa nguzo na uwekaji wa mfumo wa maji na umeme.



*Mwonekano wa Ujenzi wa Hosteli za Wanafunzi unaoendelea katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Hosteli hiyo itakuwa na jumla ya sakafu nne (4) itakapokamilika na itakuwa na uwezo wa kuchukuwa wanachuo 192.*

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha michezo inaendeshwa kisasa zaidi Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea na ujenzi wa kituo cha kitaifa cha kuendeleza vipaji *(National Sports Academy)* katika Chuo cha Maandeleo ya Michezo Malya. Mkandarasi ambaye ni kampuni ya CRJE ya China yupo eneo la ujenzi. Mpaka kufikia mwezi Aprili 2024 tayari alishakamilisha kuchimba misingi ya majengo matatu (jengo la darasa, jengo la utawala na jengo la kulia chakula) ujenzi unaendelea. Kukamilika kwa ujenzi wa kituo hiki utakifanya kuwa kituo pekee cha uibuaji na ukuzaji wa vipaji katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kituo kuchukua vijana walio katika mfumo rasmi wa elimu, kituo pia kitasaidia kutoa mafunzo kwa vijana wetu walioko katika mfumo usio rasmi wanaopaswa kuendelezwa katika michezo. Kituo kitakuwa sehemu ya mafunzo kwa vitendo kwa wanachuo wanaosomea michezo pia kitatumika kama kambi ya maandalizi kwa timu zitakazokuwa zinashiriki michezo ya Kitaifa na Kimataifa. Mradi huu utakapokamilika unakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 33 za Kitanzania.

**MIRADI YA MAENDELEO**

**A. Ujenzi wa Viwanja vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi *(Recreational and Sports Centres*) ya Dar es Salaam**

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na ujenzi wa viwanja vya mazoezi na kupumzika wananchi kwa lengo la kuongeza miundombinu bora ya michezo nchini. Katika mwaka 2023/24 Serikali imeendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi *(Recreational and Sports Centres*) vya Dar es salaam na Dodoma ambapo kwa Dar es Salaam mradi unatarajiwa kugharimu kiasi cha Shilingi 21,797,261,042.22. Hadi kufikia Aprili 2024 shughuli mbalimbali za ujenzi wa mradi huo zimefanyika ikijumuisha; maeneo ya kubadilisha nguo wachezaji; jengo la utawala; uwanja wa ndani *(Indoor stadium)*; Uzio (Fence); viwanja vya mpira wa mkono; na viwanja vya mpira wa Miguu. Mradi huu kwa ujumla umefikia asilimia 45 za utekelezaji.

**B. Ujenzi wa Viwanja vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi *(Recreational and Sports Centres)* ya Dodoma**

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatekeleza mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi *(Recreational and Sports Centres*) katika Jiji la Dodoma ambao utagharimu kiasi cha Shilingi 32,959,346,497. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi kufikia Aprili 2024, kiasi cha Shilingi 808,028,675 kimelipwa kwa Mkandarasi wa mradi huu. Fedha hizi zimetumika katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa mradi huo ambazo zimejumuisha; Maeneo ya maandalizi ya mwanzo; Jengo la utawala; Jengo la

kubadilishia nguo wachezaji; Majengo mawili ya vyoo; Viwanja viwili vya mpira wa miguu *(natural and artificial grass football pitch*); Viwanja vya mpira wa wavu, kikapu, pete na tenesi; jengo la jiko; kaunta na vibanda vya vinywaji (*counter and huts);* majengo ya vyumba vya kubadilisha nguo kwa ajili ya mabwawa ya kuogelea *(swimming pools changing rooms);* bwawa la kuogelea la wakubwa na la watoto *(adult and children swimming pools);* mazingira ya nje *(paved areas and landscaping)*. Mradi huu kwa ujumla uko katika asilimia 41 za utekelezaji.

**C. Ujenzi wa Kiwanja cha Michezo katika Mkoa wa Arusha**

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na ujenzi wa Kiwanja cha Michezo Dodoma, pia Serikali imeanza kujenga Kiwanja chenye uwezo wa kuchukuwa watazamaji 30,000 wakiwa wamekaa katika Jiji la Arusha. Kiwanja hiki kinajengwa kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya Michezo ya AFCON yanayotarajiwa kufanyika mwaka 2027. Mkandarasi amepatikana na kazi ya ujenzi imeanza. Kiwanja hiki kinatarajiwa kuwa kimekamilika ifikapo Desemba 2025.

**D. Ujenzi wa Kiwanja cha Michezo katika Mkoa wa Dodoma**

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatarajia kuanza kujenga kiwanja cha michezo katika Mkoa wa Dodoma mwaka 2024/25 ambapo bajeti ya kuanza ujenzi huo jumla ya Shilingi 55,500,000,000 imetengwa. Kiwanja hiki kikikamilika kitakuwa na uwezo wa kuchukuwa watazamaji 30,000 wakiwa wamekaa.

**E. Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam (Ukarabati Kiwanja cha Benjamin Mkapa)**

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Serikali inatekeleza mradi wa ukarabati wa kiwanja cha Benjamin Mkapa ambao kwa awamu ya kwanza kinatarajiwa kugharimu kiasi cha Shilingi 31,329,180,963.16. Hadi kufikia Aprili 2024 kiasi cha Shilingi 7,449,955,077 kimelipwa kwa Mkandarasi wa mradi huu. Fedha hizi zimetumika katika shughuli mbalimbali za ukarabati ambazo zimejumuisha maeneo ya; vyumba vya

wachezaji *(Dressing room);* maeneo ya waandishi wa habari *(Media tribune and Press conference);* sehemu ya watu mashuhuri (VVIP); eneo la kuchezea mpira *(pitch);* taa za eneo la kuchezea *(pitch light);* na kuweka mfumo wa matangazo ya kidigiti. Awamu ya kwanza ya ukarabati imekamilika kwa asilimia 98, ambapo: vyumba vya wachezaji, ukarabati umefikia asilimia 80; chumba cha mkutano wa waandishi wa habari, ukarabati umefikia asilimia 60; eneo la watu mashuhuri, ukarabati umefikia asilimia 80; kutengeneza eneo la waandishi wa habari *(media tribune),* ukarabati umefikia asilimia 85; kupaka rangi maeneo mbalimbali ya kiwanja, ukarabati umefikia asilimia 52; kusafisha maeneo machafu *(fungus),* ukarabati umefikia asilimia 50; na kuziba nyufa sehemu mbalimbali za ukuta, ukarabati umekamilika kwa asilimia 100.

**F. Mradi Na. 6398 – Mfuko wa Maendeleo ya Michezo**

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Michezo la Taifa (BMT) linatekeleza mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Michezo ambapo majukumu yaliyotekelezwa na mradi huu ni pamoja na: kujenga kituo cha mafunzo ya michezo katika Mkoa wa Manyara; kuziwezesha Timu za Taifa kushiriki katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa; Kuratibu matukio ya michezo ya Kimataifa yakiwemo mashindano ya Kimataifa ikiwemo CHAN, Mashindano ya Afrika *(All African Games)* na Matamasha ya *(Tanzanite Women Festival na Juma Ikangaa Ladies First);* kutoa mafunzo ya michezo kwa wataalamu na viongozi nchini; kununua vifaa vya michezo; na kuratibu utoaji wa tuzo na motisha kwa wanamichezo bora katika michezo ya vipaumbele, kujengea uwezo (capacity building) kwa wataalamu wa michezo hususan makocha, kuibua na kuendeleza vipaji pamoja na kuimarisha ushiriki wa michezo kwa wanawake. Aidha, Mfuko huu utawezesha kufanya marekebisho ya sheria za Baraza la Michezo pamoja na kuandaa Kanuni za Uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya michezo.

### 3.2.3 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALI WATU

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 Wizara iliratibu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli mbalimbali za ofisi ikiwamo matengenezo ya magari, ununuzi wa mafuta ya magari, huduma za usafi na ulinzi, kulipa pango la ofisi, umeme na simu pamoja na ununuzi wa vitendea kazi mbalimbali na samani za ofisi. Pia Wizara imeendelea kusimamia na kuwezesha upatikanaji wa stahili mbalimbali za watumishi ikiwamo malipo ya nauli za likizo, safari za kikazi na uhamisho.

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na uratibu wa masuala mbalimbali ya watumishi. Katika kuimarisha ushiriki wa watumishi katika kupanga na kutekeleza majukumu ya Wizara mikutano miwili ya Baraza la Wafanyakazi imefanyika; Wizara imeendelea kushiriki katika Sherehe za Siku ya Wanawake Duniani zilizofanyika kimkoa katika Wilaya ya Chamwino na Michezo ya SHIMIWI iliyofanyika Mkoani Iringa. Aidha, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 Wizara imeajiri watumishi kumi na sita (16) wa Kada mbalimbali wakiwemo Maafisa Utamaduni tisa (9), Afisa Michezo mmoja (1), Mhasibu mmoja (1), Mtakwimu mmoja (1), Mchumi mmoja (1), Dereva mmoja (1) na Maafisa Ugavi wawili (2), na watumishi watatu (3) walipandishwa vyeo pia Wizara imewezesha watumishi 32 kushiriki mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

## 4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NAZO

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2023/24, changamoto katika utekelezaji wa majukumu hazikosekani. Changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa na Serikali kukabiliana nazo ni kama ifuatavyo:

(i) Mahitaji makubwa ya fedha hususan kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikilinganishwa na ukomo mdogo wa bajeti ya Wizara. Aidha, Wizara inatekeleza shughuli za kuitangaza Tanzania kimataifa zenye mahitaji makubwa ya fedha.

Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara iliwasilisha Wizara ya Fedha mahitaji yaliyokuwa nje ya bajeti ya utekelezaji wa mwaka 2023/24. Aidha, Wizara ilitumia njia mbadala kupata rasilimali fedha ikiwemo Harambee na michango ya wadau. Wizara inaendelea kujadiliana na Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kufadhili utekelezaji wa shughuli za Wizara.

(ii) Uelewa mdogo wa jamii hususan vijana kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kuenzi Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na nafasi ya Tanzania kama kitovu cha harakati za ukombozi wa Bara la Afrika.

Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara kupitia Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, imeendelea kutoa elimu kupitia makongamano, mitandao ya kijamii na kuweka maonesho mbalimbali ya kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kulinda urithi wa ukombozi wa Bara la
Afrika.

(iii) Jamii kutokuthamini umuhimu wa michezo na vijana kuiga tamaduni za nje na kuacha tamaduni za Kitanzania. Katika jamii ya Kitanzania bado haiamini kama michezo ni uchumi na ajira. Hivyo, wazazi wengi bado hawawaruhusu watoto wao kujihusisha na michezo kwa sababu ya imani kuwa watoto kujihusisha na michezo ni kupoteza muda. Aidha, kutokana na maendeleo ya teknolojia, kumekuwa na mwingiliano mkubwa wa jamii za kigeni na jamii zetu. Kutokana na hilo mambo mengi yamekuwa yakifanywa na vijana wetu ambayo siyo desturi wala maadili ya nchi yetu.

Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inaendelea na utoaji wa elimu kwa njia ya vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, mikutano mbalimbali, makongamano n.k. kwa lengo la kuielimisha jamii umuhimu wa michezo na madhara ya kuiga tamaduni za kigeni.

(iv) Uvamizi wa maeneo ya viwanja vya michezo nchini. Kutozingatiwa kwa mipango miji na mabadiliko ya matumizi ya maeneo ya wazi imepelekea kuvamiwa kwa maeneo ya wazi

ya michezo katika jamii na hivyo kuathiri uendeshaji wa shughuli za uibuaji na uendelezaji wa vipaji vya michezo.

Katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali imeandaa mwongozo madhubuti wa usimamizi wa viwanja na maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za michezo; kuhamasisha wataalamu wa michezo kuwa na kanzidata ya maeneo yote yaliyotengwa kwa shughuli za michezo ili kuyabaini na kuyalinda na uvamizi; na kuandaa muundo au mfumo madhubuti wa ufuatiliaji wa mara kwa mara wa maeneo yote yaliyotengwa kwa shughuli za michezo ili kuyatunza.

## 5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2024/25 Wizara na Taasisi zake kwa kushirikiana na wadau itatekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 2025; Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021; Ahadi na Maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Dira ya Taifa ya Maendeleo; na Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2021/22 - 2025/26. Aidha, utekelezaji wa majukumu utazingatia pia malengo ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030 katika maeneo yanayohitaji kuchukuliwa hatua na Wizara, pia utazingatia Mwongozo wa Bajeti wa mwaka 2024/25. Majukumu yatakayotekelezwa yanaainishwa kama ifuatavyo kwa kila Sekta.

## 5.1 SEKTA YA UTAMADUNI

### 5.1.1 IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**186.** ***Mheshimiwa Spika***, malengo yaliyopangwa kutekelezwa ni kuandaa Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Utamaduni ya mwaka 1997; kufanya Tamasha la tatu la Kitaifa la

Utamaduni pamoja na kuratibu Matamasha ya Kiutamaduni yanayoandaliwa na wadau mbalimbali; na Kuratibu Maadhimisho ya tatu ya Kitaifa na Kikanda ya Siku ya Kiswahili Duniani. Majukumu mengine ni pamoja na kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kulinda Utamaduni na Maadili ya Mtanzania; kufanya Kikao Kazi cha Maafisa Utamaduni nchini; kuratibu na kushiriki katika mikutano, makongamano, maadhimisho na matamasha ya kiutamaduni ya kitaifa, kikanda, na kimataifa; kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika; na kuratibu shughuli za Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

### 5.1.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25 majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na kufanya maadhimisho ya tatu ya Siku ya Kiswahili Duniani ambapo kutatolewa tuzo maalumu ya Mwalimu Nyerere katika Kiswahili itakayotolewa nchini Ufaransa; kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili wa mwaka 2022 – 2032 kwa kutoa mafunzo ya stadi za kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni kwa diaspora 150; kufungua vituo 100 vya kufundisha Kiswahili nje ya nchi kwa kushirikiana na Diaspora; kuandaa kongamano la Kiswahili nje ya nchi mwezi Novemba 2024 litakalofanyika Havana nchini Cuba; kuchapisha vitabu 2 vya kufundishia na kujifunzia Kiswahili; kuimarisha Kiswahili nchini na kukitangaza kimataifa; na kutoa elimu ya matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili kwa kuandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 750 kupitia redio na televisheni. Majukumu mengine yatakayo tekelezwa ni kuchapisha makala 35 katika magazeti na maudhui mbalimbali kuhusu Kiswahili yatakayotolewa kupitia mitandao ya kijamii ambayo ni YouTube, Facebook na Twitter; kutoa mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa wataalamu 441 kutoka katika mikoa mbalimbali ya Tanzania; na kutoa semina kuhusu matumizi bora ya Kiswahili kwa waandishi na watangazaji kutoka vyombo vya habari duniani; na kutoa ithibati.

### 5.1.3 KITUO CHA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika katika mwaka wa fedha 2024/25 kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: kufanya upembuzi yakinifu wa Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Uhifadhi wa Urithi wa ukombozi wa Afrika kitakachojengwa Bagamoyo mkoani Pwani; Kukamilisha ukarabati wa Jengo la Kamati ya Ukombozi ya O.A.U na kukarabati mahandaki na makaburi yenye masalia ya wapigania uhuru wa nchi za Afrika. Shughuli nyingine zilizopangwa ni kufanya utafiti wa kubainisha kumbukumbu za ukombozi na kuandaa taarifa za Maeneo yenye Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika katika mikoa ya Mwanza, Tabora, Tanga, Njombe, Pwani, Ruvuma na Kagera; Kukuza utalii wa historia ya ukombozi; Kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika Machi 23 na siku ya Afrika 25 Mei; Kufanya ziara kwenye nchi za Kusini mwa Afrika kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi wa Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na kubadilishana uzoefu; Kuanzisha Maktaba na Makumbusho ya kidijitali ya Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika; Kuanzisha programu za elimu ya historia ya ukombozi wa Afrika kwa vijana kwa ajili ya kukuza uzalendo; na kuanzisha mashindano ya mchezo wa mpira wa miguu kwa vijana chini ya miaka 20 kwa nchi za Afrika yatakayojulikana kama *Mwlalimu Nyerere Liberation Cup* kwa ajili ya kukuza utalii wa historia ya ukombozi.

### 5.1.4 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo yaliyopangwa kutekelezwa na Mfuko kwa mwaka 2024/25 ni kama ifuatavyo: Kufanya mageuzi katika Sekta ya Utamaduni na Sanaa ili ijiendeshe kibiashara, izalishe ajira kwa wingi, iwe chanzo cha mapato ya fedha za kigeni pamoja na kuwa kinara cha uchangiaji wa pato la taifa nchini. Aidha, Katika eneo hili Mfuko utaendesha programu ya mafunzo ya urasimishaji wa kazi za Utamaduni na Sanaa nchi nzima na walengwa wakiwa ni wasanii wachanga na chipukizi. Programu hii itakuwa na hatua kuu nne; **Moja** wasanii watapata mafunzo ya mada mbalimbali zitakazowasaidia kuendesha

Sanaa kibiashara, **Pili**, wasanii waliofuzu katika awamu/hatua ya kwanza wataunganishwa na Taasisi/wadau wa sanaa kwa ajili ya kufanya mazoezi ya vitendo, **Tatu**, wasanii waliofuzu katika awamu ya pili wataunganishwa na wasanii waliofanikiwa katika maeneo hisika kwa ajili ya kulelewa na kujifunza mbinu mbalimbali za kibiashara na **Nne na mwisho**, wataunganishwa katika fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupata mikopo kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Utamaduni pia utatoa mikopo kwa miradi 475 ikiwa ni wastani wa miradi 18 kwa kila mkoa na miradi hii inategemewa kuzalisha jumla ya ajira zisizopungua 71,250 na zitakazowanufaisha wananchi 926,250. Aidha, Mfuko kwa kushirikiana na maafisa Utamaduni katika ngazi ya mikoa na Wilaya, Vyama vya Sanaa na matawi ya benki washirika (NBC na CRDB) utaendelea kutangaza huduma zake kupitia njia mbalimbali hasa katika maeneo ya pembezoni mwa miji ili ziweze kufahamika kwa wadau. Kupitia Ushirikiano huo elimu hii inategemewa kuwafikia wananchi takribani milioni tano (5,000,000).

### 5.2 SEKTA YA SANAA

#### 5.2.1 IDARA YA MAENDELEO YA SANAA

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali kupitia Wizara itaendelea na Kuratibu maandalizi ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 kwa kuzingatia masuala ya sekta ya Sanaa; kuratibu Matamasha manne (4) ya Kitaifa na Kimataifa ambayo ni Tamasha la Sanaa la Serengeti *(Serengeti Arts Festival)*, World Happy Deaf Family Festival, Usiku wa Taarabu na Sauti za Busara; kuratibu shughuli za Burudani katika maadhimisho ya Sherehe za Uhuru na Muungano na hafla nyingine za kitaifa; kufanya mkutano wa mwaka wa wadau wa Sekta ya Sanaa na Burudani; kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Sanaa; kufanya na kutathmini utekelezaji wa Majukumu ya Sekta ya Sanaa katika mikoa na Wilaya za Tanzania Bara; kufanya utafiti kubaini Mchango wa Sekta ya Sanaa katika

ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa kushirikiana na taasisi ya utafiti; na kusimamia maandalizi ya ujenzi wa vituo vya Sanaa nchini.

### 5.2.2 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa kwa mwaka 2024/25 ni kama ifuatavyo, kuimarisha ubunifu na utengenezaji wa sanaa bora; kuratibu Tuzo za Muziki Tanzania (Tanzania Music Awards - TMA 2024); kuandaa Tuzo za Sanaa za Ufundi za mwaka 2024; kuratibu Shindano la Kimataifa la Utanashati na Ulimbwende kwa Viziwi (Mr. And Miss Deaf International – 2024); kuandaa Tamasha la Muziki la Serengeti (Serengeti Music Festival 2024); kuimarisha mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI; kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa mahala pa kazi; kuimarisha Utawala bora katika kutekeleza shughuli za Baraza na uendeshaji wa Sekta ya Sanaa; kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Baraza; kukarabati na kujenga vituo vya sanaa na Ofisi za Baraza; kuimarisha utoaji habari, mawasiliano ya umma na ushawishi; kusimamia maslahi ya wasanii yasiyo ya hakimiliki au hakishiriki; kuhamasisha elimu na shughuli za sanaa katika shule za Msingi na Sekondari; kusimamia matumizi ya sanaa za jadi; na kuimarisha ushiriki wa jamii katika shughuli za sanaa ikiwemo utekelezaji wa mradi wa Basata Vibes na Programu ya Sanaa Mtaa kwa Mtaa.

### 5.2.3 BODI YA FILAMU TANZANIA

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa ni kusimamia maudhui ya filamu nchini kwa kuhakiki na kupanga katika madaraja filamu 1,000; kurasimisha shughuli/biashara za filamu na kutoa leseni 250 za uendeshaji wa shughuli/biashara hizo; kushughulikia maombi na kutoa vibali 1,200 vya uandaaji wa filamu nchini; kuwatambua wadau wa filamu na Michezo ya Kuigiza kwa kutoa vitambulisho 300 kwa wadau; kuendesha Tamasha la Kitaifa la utoaji wa Tuzo za Filamu; kuendesha mafunzo kwa lengo la kuwajengea uwezo wadau wa filamu; kuendelea na mkakati wa kuyabaini na kuyatangaza maeneo ya upigaji picha za filamu nchini; na kuendelea kuwawezesha wadau kutumia huduma za Bodi kupitia mfumo wa Utambuzi wa

wadau (Arts Management Information System-AMIS) pamoja na kuwasajili.

### 5.2.4 OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** COSOTA katika mwaka 2024/25 imepanga kutekeleza Kampeni maalumu ya elimu inayofahamika kama "Hakimiliki yako Hailiki, Kamata Fursa Twenzetu" kwa kushirikiana na Ruge Mutahaba Foundation inayolenga kutoa elimu kwa wabunifu na wadau wa kazi za hakimiliki milioni moja (1,000,000) ili kuongeza ulinzi wa kazi za wabunifu; kukusanya na kugawa mirabaha katika madaraja ya kazi ambazo hazisimamiwi na kampuni za ukusanyaji na ugawaji mirabaha (Collective Management Organizations – CMOs); kusimamia Kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha ambazo zimeshaanzishwa, kusajili wasanii, waandishi na wabunifu wa masuala ya hakimiliki 1,150 na kazi 2,850 kwa ajili ya kulinda hakimiliki, kufanya Operesheni tano (5) za Kupambana na Uharamia wa kazi za ubunifu; na kuandaa Kanuni za usimamizi wa kampuni za ukusanyaji na ugawaji mirabaha (Collective Management Organizations – CMOs) kwa madaraja ya kazi za Sanaa za Ufundi, Sanaa za Maonesho, Filamu na Kazi za Maandishi, katika madaraja ambayo kampuni zake hazijaanzishwa na Kuandaa Kanuni za uendeshaji wa migogoro ya hakimiliki ili kushughulikia migogoro ya hakimiliki ya wadau kupitia utaratibu maalumu wa usuluhishi wa migogoro inayoletwa COSOTA pamoja na kukuza ushirikiano wa masuala ya hakimiliki baina ya Tanzania na nchi mbalimbali kwa upande mmoja na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa kwa upande mwingine.

### 5.2.5 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** TaSUBa katika mwaka 2024/25 imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo; kudahili wanachuo wa kozi ndefu za Astashahada na Stashahada wapatao 800 na kozi fupi 280; kuendesha mafunzo maalumu ya sanaa na utamaduni kwa kushirikiana na wadau katika mikoa mitatu ya Kigoma, Mtwara na Ruvuma; kufanya tafiti moja (1) kwenye

eneo la utamaduni; kukamilisha ithibati ya mitaala minne ambayo ni Usimamizi wa Sanaa na Masoko (Art Management and Marketing), Urithi wa Utamaduni na Utalii (Cultural Heritage and Tourism) na Muziki (Music), na Ualimu wa Sanaa (Arts with Education); kutafuta eneo la kuanzisha kampasi mpya jijini Dodoma; kuanzisha kituo cha mafunzo ya sanaa na utamaduni jijini Dar es Salaam na Songea Mjini; kuendesha Tamasha la 43 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo; na kutangaza Taasisi na Mazao yake katika vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii. Aidha, wanachuo zaidi ya 700 wanategemewa kuhitimu mafunzo ya kozi ndefu na fupi ambao watajiajiri na kutoa ajira kwa wengine kwa kutumia ujuzi waliopata na kutumia fursa zilizopo kwenye uchumi unaotokana na sekta za utamaduni na sanaa ili kuinua pato la Taifa na uchumi wa mtu mmojammoja.

## 5.3 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

### 5.3.1 IDARA YA MICHEZO

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali kupitia Wizara itatekeleza majukumu mbalimbali. Miongoni mwa majukumu hayo ni pamoja na: kuratibu kikao cha Kanda ya Tano Afrika kuhusu Mapambano ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni; kuratibu Mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI; kuratibu kikao kazi cha wadau cha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo; kuwezesha ushiriki wa nchi katika Mikutano ya Michezo ya Kimataifa; kuratibu Mkutano wa Mwaka wa Maafisa Michezo Tanzania Bara; kuratibu matukio ya Michezo ya Kitaifa na Kimataifa ikiwamo michezo ya Olimpiki; kuratibu miradi ya ujenzi wa miundombinu ya michezo nchini, ikiwemo ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu Dodoma, Ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu Arusha, Ujenzi wa Viwanja vya Mazoezi na Kupumzikia Wananchi Dar es Salaam na Dodoma, Ujenzi wa Arena ya Michezo na Sanaa Dar es Salaam, Ujenzi wa Akademia ya Michezo Malya, Ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa na Uhuru n.k; kuendelea kuimarisha ushiriki wa timu za Taifa katika mashindano ya kimataifa kwa kuwatumia

Diaspora; ujenzi na ufufuaji wa viwanja vya wazi vya michezo katika ngazi ya jamii; kuboresha sheria mbalimbali zinazosimamia michezo nchini; kutoa ushauri na kuandaa viwango vya miundombinu ya michezo nchini; kuendesha kampeni ya utunzaji wa miundombinu ya michezo nchini; kuendelea kuratibu maandalizi ya kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu ya Kombe la Mataifa ya Afrika - AFCON 2027; kuratibu Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika – CHAN 2024; kuratibu shughuli za Sekretarieti ya Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV; kutoa mafunzo kwa kozi za muda mrefu kwa washiriki wapatao 310 na mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki wapatao 300 katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya; kusimamia ujenzi wa miundombinu ya michezo ikiwemo Akademia ya Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya; na kuendelea kukamilisha hatua za kukifanya chuo kuwa taasisi ya elimu ya michezo.

**5.3.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)**

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, majukumu yatakayotekelezwa ni pamoja na: kuendelea kuwezesha na kuzigharamia Timu 10 za Taifa kushiriki mashindano mbalimbali ya Kimataifa; kuendelea kutoa mafunzo ya utaalamu wa michezo na usimamizi kwa wataalamu 300 ili kupata wataalamu wa michezo nchini; kuendelea kusajili Vyama/ Mashirikisho na vilabu vya michezo vipatavyo 120; kuanza safari ya kombe la dunia mwaka 2030 kwa kuandaa timu bora za vijana, mafunzo na kugharamia makocha bora; kutekeleza mkakati maalumu wa kulea timu za vijana kwa kuwa na timu ya vijana chini ya miaka 17 (inayotokana na UMISETA na UMITASHUMTA), chini ya miaka 20 na chini ya miaka 23 zitakazokuwa na mafunzo maalumu, kambi na makocha wenye weledi wa hali ya juu; kuratibu matamasha mawili (2) ya Michezo ya Wanawake (*Tanzanite*); kuendelea kuhamasisha Utawala Bora katika vyama na mashirikisho ya michezo 45; kuidhinisha vibali 200 vya matukio mbalimbali ya michezo; kuendelea kutoa tuzo kwa wanamichezo bora kwa michezo yote inayochezwa Tanzania; kuendelea kutoa elimu kwa umma na wadau 250 kushiriki katika

michezo kupitia vyombo vya habari; kujenga viwanja vya mazoezi vya michezo katika Jiji la Dodoma, Mkoa wa Manyara, Ruvuma na Njombe; kuwajengea uwezo wataalam wa Michezo hususan makocha; kuibua na kuendeleza vipaji; na kuwekeza katiba programu za kuinua na kuongeza ushiriki wa wanawake katika michezo; na Kufanya marekebisho ya sheria ya Baraza la Michezo la Taifa.

## 5.4 MIRADI YA MAENDELEO

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu wa Arusha umetengewa Shilingi 125,290,774,000. Uwanja huu utakuwa na uwezo wa kuchukua watu 30,000 unaojumuisha miundombinu ya eneo la kukimbilia riadha, uwanja wa ndani (Indoor stadium), viwanja vya mpira wa mikono, pete na netiboli. Haya ni Maandalizi ya Tanzania kuwa mwenyeji wa AFCON 2027 kama uwanja wa mashindano.

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma, katika mwaka wa fedha 2024/25 umetengewa Shilingi 55,500,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni Kuanza ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu wenye uwezo wa kuchukua watu 30,000. Uwanja utajumuisha miundombinu ya uwanja wa ndani *(Indoor stadium),* viwanja vya mpira wa mikono, pete, na netiboli. Huu ni utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Mwaka 2020 hadi 2025.

**200.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, katika mwaka wa fedha 2024/25 imetengewa jumla ya Shilingi 2,000,788,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali ambazo ni kufanya utafiti wa kubainisha kumbukumbu za ukombozi na kuandaa taarifa za maeneo yenye Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika katika mikoa ya Mwanza, Tabora, Tanga, Pwani, Kagera na Ruvuma; kuanzisha kombe la ukombozi la Mwl. Julius Nyerere *(Mwl. Julius Nyerere Liberation Cup)*; kuhamasisha utalii wa historia ya ukombozi; kutoa elimu ya historia ya ukombozi kwa vijana; ukamilisha ukarabati wa Jengo la Kamati ya Ukombozi ya O.A.U na kukarabati mahandaki na makaburi yenye masalia ya wapigania uhuru wa nchi za Afrika;

kuanza upembuzi yakinifu wa Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Uhifadhi wa Urithi wa ukombozi wa Afrika, Bagamoyo mkoani Pwani; kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika Machi 23 na siku ya Afrika Mei 25; kufanya ziara kwenye nchi za Kusini mwa Afrika kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi wa Urithi wa Ukombozi wa Afrika na kubadilishana uzoefu; na kuanzisha Maktaba na Makumbusho ya kidijitali ya Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika.

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania, katika mwaka wa fedha 2024/25 umepangiwa jumla ya Shilingi 3,000,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau kwa ajili ya kuongeza mtaji ili wasanii wengi waweze kunufaika; kuendelea kutoa ruzuku na mikopo kwa wasanii nchini; na kuwajengea uwezo wasanii ili kurasimisha kazi zao pamoja na kuziendesha kibiashara.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kupitia Mradi wa Kuimarisha BAKITA na kukibidhaisha Kiswahili umetengewa jumla ya Shilingi 500,000,000 kwa ajili ya kuanzisha vituo 100 vya kufundisha Kiswahili kupitia balozi za Tanzania nje ya nchi kwa kushirikiana na Diaspora; kufundisha diáspora na wenyeji stadi za kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni katika nchi sita (6); kuongeza samani za darasa la Kiswahili kwa wageni na kununua vifaa vya kielektroniki vya kuwezesha ufundishaji kwa njia ya masafa; kuandika na kuchapisha vitabu vya kufundishia na kujifunzia Kiswahili kwa wageni. Vitabu hivyo ni Furahia Kiswahili hatua mbili (2), kitabu cha misemo ya kila siku cha Kiswahili - Kiingereza na Kihispaniola, na Mwongozo wa kutahini umahiri wa lugha ya Kiswahili; kuimarisha mfumo wa *Swahiliprime*; na kuendesha mafunzo ya msasa ya ufananivu wa lugha ya alama ya Tanzania na alama za kimataifa kwa wakalimani 200 wa lugha ya alama.

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na mradi wa ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, katika mwaka 2024/25

umetengewa jumla ya Shilingi 1,500,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea kuimarisha ujenzi wa chuo kwa kufanya ukarabati wa miundombinu mbalimbali ikiwemo madarasa mawili (2) na ukarabati wa uwanja wa ndani; na ununuzi wa samani za Chuo katika hosteli mpya iliyojengwa ikiwemo vitanda, magodoro na kabati, kununua samani za madarasa zikiwemo viti na meza pamoja na vitendea kazi vya Chuo vinavyohusisha kompyuta na vifaa vya michezo.

**204. *Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa Akademia ya Michezo Malya kwa mwaka 2024/25 umetengewa jumla ya Shilingi 10,020,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya akademia ikiwemo viwanja vya mpira wa miguu, netiboli, kikapu, mikono, madarasa, bwalo, jengo la utawala na hosteli.

**205. *Mheshimiwa Spika,*** kuhusiana na Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi (Recreational Centre) katika mwaka 2024/25 umetengewa Shilingi 12,000,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi kwa Dar es Salaam na Dodoma inayojumuisha miundombinu ya majengo ya utawala, viwanja vya mpira wa miguu, netiboli, pete, wavu, tenisi, vyumba vya kubadilishia nguo na eneo la mapumziko *(recreation)*; na kuanza ujenzi wa awamu ya pili kwa Dar es Salaam na Dodoma inayohusisha jiko, bwawa la kuogelea lenye hadhi ya Olimpiki, uzio na eneo la mapumziko.

**206. *Mheshimiwa Spika***, mradi wa Ujenzi wa *Sports and Arts Arena* katika mwaka 2024/25 umetengewa jumla ya Shilingi 150,000,000 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kutafuta Mshauri Elekezi, kufanya upembuzi yakinifu wa mradi.

**207. *Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Maendeleo ya Michezo ni mradi ambao utatekelezwa katika mwaka 2024/25 na umetengewa jumla ya Shilingi 8,000,000,000. Majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni kujenga kituo cha mafunzo ya michezo katika Mkoa wa Manyara, Dodoma na Ruvuma; kulipa mishahara ya makocha wa timu za Taifa; kuziwezesha Timu za Taifa kushiriki katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa;

kuratibu matukio ya michezo ya Kimataifa yakiwemo mashindano ya Kimataifa ikiwemo CHAN na Matamasha ya Tanzanite Women Festival na Juma Ikangaa Ladies First; kutoa mafunzo ya michezo kwa wataalamu na viongozi wa nchini; kununua vifaa vya Michezo; kuratibu utoaji wa Tuzo na Motisha kwa wanamichezo bora katika michezo ya vipaumbele; na kufanya marekebisho ya sheria za Baraza la Michezo pamoja na kuandaa Kanuni za uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya michezo.

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam katika mwaka 2024/25 umepangiwa jumla ya Shilingi 26,629,226,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ukarabati mkubwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa unaojumuisha ubadilishaji wa viti vyote vya uwanja, ubadilishaji wa eneo la kukimbilia riadha, mfumo wa taa, TEHAMA, mfumo wa maji, na upakaji rangi; na kuendelea na ukarabati mkubwa katika Uwanja wa Uhuru katika eneo la kuchezea (pitch), kuweka viti, mfumo wa maji, mfumo wa umeme, TEHAMA na upakaji rangi.

Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na wadau wamiliki wa viwanja itakamilisha taratibu na kuanza ukarabati mkubwa wa viwanja vya CCM Kirumba (Mwanza), Jamhuri (Morogoro), CCM Mkwakwani (Tanga), Sokoine (Mbeya) na Majimaji (Ruvuma). Msingi wa ukarabati huu ni kuongeza miundombinu ya michezo nchini, kuimarisha vituo vya mazoezi, ubora wa ligi na hatimaye timu zetu za Taifa.

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika Shule Maalumu za Michezo kwa mwaka 2024/25 umepangiwa Shilingi 11,500,000,000 na shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuanza kwa ukarabati wa miundombinu ya shule maalumu kumi (10) za michezo ambazo ni Shule ya Sekondari Dodoma, Shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora, Shule ya Sekondari Kicheba, Shule ya Sekondari ya Kanono, Shule ya Sekondari ya Ufundi Tanga, Shule ya Sekondari Mpya Ikungi, Shule ya Sekondari ya Ikwiriri, Shule ya Sekondari Dkt. Damas Ndumbaro, Shule ya

Sekondari ya Ufundi Mtwara na Shule ya Sekondari Babati; pamoja na ununuzi wa vifaa vya michezo katika shule hizo.

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** ukarabati wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), katika mwaka 2024/25 umetengewa Shilingi 1,500,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kuanza ujenzi wa uzio kuzunguka Taasisi; kununua vifaa vya kujifunzia na kufundishia; kuendelea na ukarabati wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia; kuimarisha TEHAMA na Mifumo ya Mawasiliano; kukarabati mifumo ya maji taka na safi; kununua vifaa na kukamilisha miundombinu ya TV na Redio; na kukamilisha ununuzi wa vifaa na miundombinu ya Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo.

**211.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Jumba Changamani la Filamu ni mradi utakaotekelezwa katika mwaka 2024/25 ambapo umetengewa Shilingi 300,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha upembuzi yakinifu na kuanza ujenzi wa mradi.

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Sanaa katika mwaka 2024/25 umepangiwa Shilingi 300,000,000 na shughuli zitakazotekelezwa ni kuandaa andiko kwa ajili ya kuutangaza mradi ili kupata mbia wa kuendeleza eneo la Ilala Sharif Shamba kwa njia ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP); kuandaa kongamano la wawekezaji kwenye Sekta ya Sanaa *(Investors Forum)* kwa ajili ya kuwahamasisha kushiriki kwenye mradi uliokusudiwa; na kuanza uwekezaji wa mradi.

### 5.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALI WATU

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu na kuwezesha uendeshaji wa shughuli za ofisi ikiwemo matengenezo na mafuta ya magari, huduma za usafi na ulinzi, kulipa pango la ofisi, umeme na simu pamoja na ununuzi wa vitendea kazi mbalimbali na samani za ofisi, kuwezesha upatikanaji wa stahili mbalimbali za wafanyakazi ikiwemo

uhamisho, likizo na safari za kikazi n.k. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu mafunzo, ajira na upandishwaji vyeo kwa watumishi; kuendesha vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi; kuandaa Mpango Mkakati wa Urithishanaji Madaraka, Mpango wa Mafunzo na Mpango wa
Rasilimaliwatu

**6.0 MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA 2024/25**

**6.1 MAPATO**

***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2024/25 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni Moja (Shilingi 1,000,000,000) kupitia vyanzo ambavyo ni viingilio katika matukio ya michezo yanayofanyika katika viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru, upangishaji wa maeneo, huduma za kukodisha kumbi na *gym* zilizopo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na ada za mafunzo na mitihani ya Kitaifa kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Taasisi sita (6) zilizo chini ya Wizara zinatarajia kukusanya Shilingi Bilioni Saba, Milioni Moja, Mia Sita Elfu (Shilingi **7,001,600,000**). ***Kiambatisho Na. 1*** kinaonesha mchanganuo wa mapato yanayotarajiwa kukusanywa na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2024/25.

**6.2 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO**

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2024/25 Wizara imetengewa bajeti ya **Shilingi Bilioni Mia Mbili Themanini na Tano, Milioni Mia Tatu Kumi na Nane, Mia Tatu Themanini na Saba Elfu (Shilingi 285,318,387,000)** Kati ya bajeti hiyo **Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Mbili Themanini, Mia Moja Kumi na Sita Elfu** (**Shilingi 11,280,116,000)** ni kwa ajili ya Mishahara; **Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Nane Arobaini na Saba, Mia Nne Themanini na Tatu Elfu (Shilingi 15,847,483,000)** ni Matumizi Mengineyo; na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Bilioni Mia Mbili Hamsini na Nane, Milioni Mia Moja Tisini, Mia Saba Themanini na Nane Elfu** (**Shilingi 258,190,788,000). *Kiambatisho Na. 2*** kinaonesha mgawanyo wa Bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo, Taasisi zilizo chini ya Wizara na Miradi ya Maendeleo.

## 7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO NA BAJETI WA MWAKA 2024/25

**217. *Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2024/25 naomba sasa niliombe Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2024/25 yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Mbili Themanini na Tano, Milioni Mia Tatu Kumi na Nane, Mia Tatu Themanini na Saba Elfu (Shilingi 285,318,387,000).** Kati ya bajeti hiyo **Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Mbili Themanini, Mia Moja Kumi na Sita Elfu** (**Shilingi 11,280,116,000)** ni kwa ajili ya Mishahara; **Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Nane Arobaini na Saba, Mia Nne Themanini na Tatu Elfu (Shilingi 15,847,483,000)** ni Matumizi Mengineyo; na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Bilioni Mia Mbili Hamsini na Nane, Milioni Mia Moja Tisini, Mia Saba Themanini na Nane Elfu** (**Shilingi 258,190,788,000).**

## 8.0 MWISHO NA SHUKURANI

**218. *Mheshimiwa Spika*,** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kupata fursa hii ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu ya Bajeti. Pia, niwashukuru wadau wote wa sekta za utamaduni, sanaa na michezo waliofanikisha kwa ushirikiano mkubwa, mafanikio yaliyopatikana katika Wizara kwa mwaka 2023/24. Kwa makundi yao nawashukuru Washirika wa Maendeleo, Taasisi za umma na binafsi za ndani na nje ya nchi, taasisi za dini, vyama, mashirikisho, vilabu na wanatasnia za utamaduni, sanaa na michezo. Nafasi ya kipekee kwao wananchi wote waliotikia wito wa utekelezaji wa mipango ya sekta zetu na hatimaye kupata mafanikio makubwa haya.

**219. *Mheshimiwa Spika,*** siyo rahisi kuwataja wadau wote kwa majina, lakini naomba niwatambue wachache, ambao ni Kampuni za Azam Media; Shirika la Ushirikiano la Kimataifa la Japan – JICA; Ubalozi wa Ufaransa; Kituo cha Utamaduni cha Ufaransa (Alliance Française); Ubalozi wa Korea Kusini; Ubalozi wa Urusi; Kituo cha Utamaduni cha Urusi; Bagamoyo Friendship Society (Ujerumani); Musicians for a Better Life (Ujerumani); Jamhuri ya Watu wa China; Umoja wa Ulaya; Baraza la Michezo Zanzibar; Baraza la Kiswahili Zanzibar; Baraza la Sanaa na Sensa

ya Filamu Zanzibar; Ofisi ya Hakimiliki Zanzibar; Benki ya Biashara ya Taifa (NBC); Benki ya CRDB; na Benki ya NMB.

**220. *Mheshimiwa Spika*,** wadau wengine ni pamoja na: Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (World Intellectual Property Organization - WIPO); Shirika la Miliki Ubunifu Africa (African Regional Intellectual Property Office-ARIPO); Shirikisho la Jumuiya za Waandishi (Confédération of Authors Societies - CISAC); *International Federation of Phonograms Industries (IFPI);* Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS); Chama cha Lugha na Fasihi za Kiswahili Tanzania (CHALUFAKITA); Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani (CHAUKIDU); Shirikisho la Muziki Tanzania; Shirikisho la Sanaa za Maonesho Tanzania; Shirikisho la Filamu Tanzania; Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania – TFF; Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar – ZFF; Shirikisho la Sanaa za Ufundi Tanzania (TAFCA); Peramiho Events and Designing; Airtel Tanzania; Kampuni ya Startimes; Azam Media; Multichoice Tanzania; Kituo cha Televisheni cha DSTV; Shirika la Utangazaji la Taifa – TBC; na Vituo vya Redio vya CLOUDS Media group, Uhai, EFM na Wasafi.

**221. *Mheshimiwa Spika*,** naomba kumalizia hotuba yangu kwa kumshukuru tena Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na miongozo yake madhubuti katika utekelezaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Ilani ya CCM kwa kipindi cha miaka mitatu (3) ya Serikali ya awamu ya Sita. Pia, nawashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuendelea kumsaidia vema Mheshimiwa Rais na kwa miongozo na maelekezo yao kwa Wizara yaliyofanikisha kufikiwa kwa mafanikio makubwa niliyoyataja.

**222. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mara nyingine tena naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma (Mb.), Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa

kunisaidia vyema utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Bw. Gerson Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Suleiman Serera, Wakuu wa Idara na Vitengo vya Wizara, Wakuu wa Taasisi pamoja na wadau wote wa wizara tulioshirikiana. Kipekee kabisa niishukuru familia yangu, hususan mke wangu kipenzi na watoto wangu. Natambua nimekuwa adimu sana katika familia kutokana na majukumu, lakini nawashukuru zaidi kwa kunielewa, kunifariji na kuwa sababu ya furaha katika kufanikisha majukumu yangu.

**223.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kukushukuru wewe binafsi, Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni *www.michezo.go.tz.*

**224.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

## VIAMBATISHO

***Kiambatisho Na. 1***

## MADUHULI YANAYOTARAJIWA KUKUSANYWA NA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA 2024/25

### (a) Maduhuli Yatakayokusanywa na Wizara kwa Mwaka 2024/25

**Idara ya Maendeleo ya Michezo**

| Kijifungu | Maelezo | Makadirio ya Mapato | |
|---|---|---|---|
| | | Mwaka 2023/24 (Shilingi) | Mwaka 2024/25 (Shilingi) |
| 14220133 | Mapato ya Viwanja vya Michezo (Uhuru na Benjamin Mkapa) | 907,696,000 | 907,696,000 |
| 14220143 | Ada za Mafunzo | 92,302,000 | 92,302,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 14220161 | Mapato kutoka vyanzo mbalimbali | 1,000 | 1,000 |
| 14220211 | Marejesho ya fedha za Umma | 1,000 | 1,000 |
| **Jumla Ndogo** | | **1,000,000,000** | **1,000,000,000** |
| **JUMLA KUU** | | **1,000,000,000** | **1,000,000,000** |

**(b) Mapato Yatakayokusanywa na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara kwa Mwaka 2024/25**

| Na | Jina la Taasisi | Makadirio ya Mapato 2023/24 (Shilingi) | Makadirio ya Mapato 2024/25 (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) | 480,228,000 | 581,700,000 |
| 2. | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) | 800,000,000 | 885,000,000 |
| 3. | Bodi ya Filamu Tanzania | 1,460,000,000 | 1,460,000,000 |
| 4. | Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) | 950,200,000 | 1,514,900,000 |
| 5. | Baraza la Michezo la Taifa (BMT) | 920,000,000 | 1,200,000,000 |
| 6. | Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) | 1,360,000,000 | 1,360,000,000 |
| **JUMLA** | | **5,970,428,000** | **7,001,600,000** |

*Kiambatisho Na. 2*

**MGAWANYO WA BAJETI YA WIZARA KWA IDARA NA VITENGO, TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2024/25**

**(a) Mgawanyo wa Bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo kwa Mwaka 2024/25**

| Kifungu | Idara/Kitengo | Makisio ya Bajeti Mwaka 2024/25 | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Mishahara (PE) (Shilingi) | Matumizi Mengineyo (OC) (Shilingi) | Jumla |
| 1001 | Utawala na Rasilimali Watu | 872,368,000 | 6,533,111,000 | **7,405,479,000** |
| 1002 | Fedha na Uhasibu | 379,572,000 | 218,874,000 | **598,446,000** |
| 1003 | Sera na Mipango | 259,680,000 | 430,271,000 | **689,951,000** |
| 1004 | Mawasiliano Serikalini | 109,116,000 | 154,583,000 | **263,699,000** |
| 1005 | Ununuzi na Ugavi | 137,244,000 | 194,842,000 | **332,086,000** |
| 1006 | Ukaguzi wa Ndani | 111,588,000 | 162,163,000 | **273,751,000** |
| 1007 | TEHAMA | 148,812,000 | 229,024,000 | **377,836,000** |
| 1008 | Huduma za Sheria | 134,425,000 | 126,260,000 | **260,685,000** |
| 1009 | Ufuatiliaji na Tathmini | 139,749,000 | 178,379,000 | **318,128,000** |
| 6001 | Maendeleo ya Utamaduni | 522,578,000 | 748,731,000 | **1,271,309,000** |
| 6004 | Maendeleo ya Michezo | 914,019,000 | 1,455,264,000 | **2,369,283,000** |
| 6005 | Maendeleo ya | 260,772,000 | 832,314,000 | **1,093,086,000** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Sanaa | | | |
| **Jumla Ndogo** | | **3,989,923,000** | **11,263,816,000** | **15,253,739,000** |

**(b) Mgawanyo wa Bajeti kwa Taasisi Zilizo Chini ya Wizara kwa Mwaka 2024/25**

| **Jina la Taasisi** | **Makisio ya Bajeti Mwaka 2024/25** | | |
|---|---|---|---|
| | **Mishahara (PE) (Shilingi)** | **Matumizi Mengineyo (OC) (Shilingi)** | **Jumla (Shilingi)** |
| **6001-26311266** Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) | 1,040,666,000 | 304,404,000 | **1,345,070,000** |
| **6001-26311231** Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania | - | 91,660,000 | **91,660,000** |
| **6005-26311352** Bodi ya Filamu Tanzania (TFB) | 1,081,242,000 | 1,288,800,000 | **2,370,042,000** |
| **6005-26311267** Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) | 2,063,603,000 | 295,700,000 | **2,359,303,000** |
| **6005-26311234** Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) | 801,378,000 | 1,575,000,000 | **2,376,378,000** |
| **6005 - 26311130** Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) | 1,472,724,000 | 264,200,000 | **1,736,924,000** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **6004 – 26311273** Baraza la Michezo la Taifa (BMT) | 830,580,000 | 443,403,000 | **1,273,983,000** |
| **6004 – 26311346** Chuo cha Maendeleo ya Michezo-Malya | - | 320,500,000 | **320,500,000** |
| **Jumla Ndogo** | **7,290,193,000** | **4,583,667,000** | **11,873,860,000** |
| **JUMLA KUU (W+T)** | **11,280,116,00 0** | **15,847,483,000** | **27,127,599,000** |

**(c) Mgawanyo wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

| Na. | Jina la Mradi | Bajeti 2024/25 (Shilingi) |
|---|---|---|
| **Idara ya Maendeleo ya Utamaduni** | | |
| 1. | 6293 - Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika | 2,000,788,000 |
| 2. | 6502 – Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania | 3,000,000,000 |
| 3. | 6521 - Kuimarisha BAKITA na Kukiuza Kiswahili Kikanda na Kimataifa | 500,000,000 |
| **Jumla Ndogo** | | **5,500,778,000** |
| **Idara ya Maendeleo ya Michezo** | | |
| 4. | 6385 – Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya | 1,500,000,000 |
| 5. | 6395 - Ujenzi wa Akademia ya Michezo Malya | 10,020,000,000 |
| 6. | 6397 - Ujenzi wa Arena ya Michezo na Sanaa | 150,000,000 |
| 7. | 6398 – Mfuko wa Maendeleo ya Michezo | 8,000,000,000 |
| 8. | 6503 - Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma | 55,500,000,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | 6504 - Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi Dar es Salaam na Dodoma | 12,000,000,000 |
| 10. | 6523 - Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam | 26,629,226,000 |
| 11. | 6527- Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika Shule za Michezo | 11,500,000,000 |
| 12. | 6586 - Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Arusha | 125,290,774,000 |
| **Jumla Ndogo** | | **250,590,000,000** |
| **Idara ya Maendeleo ya Sanaa** | | |
| 13. | 4353 – Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo | 1,500,000,000 |
| 14. | 6355 – Ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Sanaa | 300,000,000 |
| 15. | 6396 – Ujenzi wa Jumba Changamani la Filamu | 300,000,000 |
| **Jumla Ndogo** | | **2,100,000,000** |
| **JUMLA KUU (DEV)** | | **258,190,788,000** |
| **JUMLA KUU YA FUNGU 96 (PE+OC+DEV)** | | **285,318,387,000** |

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, hoja imeungwa mkono.

Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na kabla sijasoma Taarifa ya Kamati naomba taarifa yote kama ilivyoandikwa iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na kwa niaba ya Mwenyekiti naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo - Fungu 96 kwa mwaka wa fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali ili hatimaye liidhinishe bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa taarifa hii unatokana na masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kanuni ya 6(1)(a) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambayo inaipa Kamati jukumu ka kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti na makadirio ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi masharti ya kanuni niliyoitaja, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 22 Machi, 2024, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na matokeo yake ni taarifa hii yenye maoni na ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa taarifa hii umezingatia Masharti ya Kanuni ya 142 kuhusu Muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, taarifa ninayowasilisha imegawanyika katika sehumu kuu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza, inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi, Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(ii) Sehemu ya Pili, inabainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha

2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Sehemu ya Tatu, inabainisha Maoni na Ushauri wa Kamati na kumalizia kwa hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muundo huo, Bunge linaweza kuwa kwenye nafasi nzuri ya kuitumia taarifa hii wakati wa majadiliano. Mtiririko wa maudhui umewekwa kwa namna rahisi ya rejea na matumizi ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi; sehemu hii inafanunua matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi. Katika uchambuzi huo, ufafanuzi unabainishwa kuhusu hali ya uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuhusu uwiano katika makadirio ya matumizi ya maendeleo na matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Sehemu hii inaripoti matokeo ya shughuli kuu tano zilizotekelezwa na Kamati kama ifuatavyo: -

(i) Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(ii) Hali ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iii) Hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa maduhuli kwa kipindi cha Julai 2023, hadi Februari 2024.

(iv) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; na

(v) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa urahisi wa ufuatiliaji na uamuzi wa Kibunge, naomba kubainisha matokeo ya uchambuzi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024; Kamati ilitembelea na kukagua jumla ya miradi ya maendeleo mitatu iliyopo chini ya Wizara hii ambayo inatekelezwa katika Mkoa wa Dar es Salaam kuanzia tarehe 18 hadi 19 Machi, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 11.8 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, sawa na 33.4%. Ufafanuzi zaidi kuhusu miradi unaambatishwa pamoja na taarifa hii kwenye Kiambatisho Na.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaonesha mambo yafuatayo: -

(i) Upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa bajeti nzima ya Wizara haulingani na uwiano wa kiasi cha fedha za miradi ya maendeleo kilichopokelewa. Kiasi hiki cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kilikuwa 33.4% ya bajeti yote na kiasi kilichopokelewa kilikuwa 66% ya fedha zote zilizopatikana;

(ii) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo hauendani na kipindi cha utekelezaji. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 fedha zilizopokelewa ni 66% ya bajeti ya maendeleo katika kipindi cha utekelezaji. Mtiririko huo unaonekana katika Jedwali Na. 1; na

(iii) Makadirio ya baadhi ya gharama kwa miradi inayotekelezwa na Wizara hii hayatolewi kama

ilivyokusudiwa kutekelezwa. Kwa mfano, Mradi Namba 6504 unaohusu Ujenzi wa Kituo cha Mazoezi na Kupumzikia Wananchi unatekelezwa kwa msingi wa makadirio ya mwaka wa fedha 2023/2024. Hadi Kamati inakwenda kukagua mradi huu, hakukuwa na kiasi cha chochote fedha kilichotolewa kutoka Hazina. Mwenendo wa upatikanaji wa fedha usioridhisha unakwamisha utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, suala la ufinyu wa bajeti kwa miradi iliyopangwa kutekelezwa linahitaji kuangaliwa kwa kina kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uzingatiaji wa ushauri wa Kamati; katika kikao cha Kamati na Wizara kilichofanyika tarehe 6 Juni, 2023 wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilitoa ushauri wa masuala mbalimbali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Jumla ya mapendekezo 14 yalitolewa na Kamati. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba sehemu ya ushauri imefanyiwa kazi na sehemu nyingine utekelezaji wake unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utekelezaji mzuri wa ushauri wa Kamati, upo ushauri ambao unahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali, mathalani Serikali kuhakikisha fedha zinatolewa kutokana na michezo ya kubashiri matokeo ya michezo *(sports betting)* zinatolewa kwa kadiri zinavyokusanywa katika kipindi husika ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na maelezo yaliyotolewa na Serikali na hivyo kusisitiza Serikali iendelee kufanyia kazi ushauri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa maduhuli; katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo – Fungu 96 ilikadiria kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 6.9. Hadi kufikia Februari, 2024 Idara na taasisi zilizo chini ya Wizara zilikusanya shilingi bilioni 4.9, sawa na 71.42% tu ya lengo la makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida; taswira halisi ya mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaoneshwa katika Kielelezo Namba 3. Uchambuzi unaonesha kuwa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ulikuwa wa kuridhisha, kwa kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2023 kiasi cha fedha kilichopatikana kilifikia 71% ya kiasi kilichoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 utekelezaji wa mipango na majukumu uliendana na fedha zilizotengwa. Kwa ujumla utekelezaji unaendelea vizuri na ufanisi wake unaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii ulifanyika kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha husika. Uzingatiaji zaidi uliwekwa katika maeneo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli;

(ii) Makadirio ya matumizi kwa ajili ya gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na

(iii) Makadirio ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyofanyiwa uchambuzi yalizingatia majukumu ya msingi ya Wizara pamoja na mwelekeo wa jumla wa Taifa. Aidha, utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake utakuwa na tija endapo Serikali itatenga fedha za kutosha na kuzitoa kwa wakati kadiri zitakavyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa kuzingatia mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya maduhuli; kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo inakadiriwa kukusanya shilingi bilioni nane. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yameongezeka kwa 17.2%,

ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa bajeti ya matumizi ya Wizara imeongezeka kwa 13% katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokwisha, ukusanyaji wa maduhuli hauna dalili ya kufikia lengo, kwani hadi Kamati inachambua bajeti hii Wizara ilikuwa imekusanya 57% tu. Kamati inasisitiza kuwa Wizara iongeze kasi ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya matumizi ya kawaida; mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo inakadiriwa kutumia shilingi bilioni 285.3. Kati ya fedha hizo, misharaha ni shilingi bilioni 11.2 sawa na asilimia nne. Matumizi mengineyo yanaombewa jumla ya shilingi bilioni 15.8, sawa na asilimia sita na miradi ya maendeleo zinaombwa jumla ya shilingi bilioni 258.1 sawa na 90%.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa bajeti ya Fungu 96 imeongezeka kwa 705% kutoka shilingi bilioni 35.4 mwaka 2023/2024 hadi kufikia shilingi bilioni 285.3 mwaka 2024/2025. Aidha, ongezeko zaidi linaonekana katika fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ambazo zimeongezeka kwa 2,082% kutoka shilingi bilioni 11.8 hadi shilingi bilioni 258.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 makadirio ya mishahara yameongezeka kwa 17%. Vilevile bajeti ya matumizi mengineyo imeongezeka kwa 13%.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya matumizi ya miradi ya maendeleo; Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya shilingi bilioni 258.1 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo inayopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, 70% ya ongezeko la fedha za miradi ya maendeleo imechangiwa na bajeti ya ujenzi wa viwanja vya Arusha na Dodoma. Kamati inaipongeza Serikali kwa

kuona umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa viwanja hivyo ambapo kwa kiasi kikubwa vitasaidia kuwa na miundombinu ya michezo na kuwezesha Tanzania kuwa mwenyeji wa fainali za mpira wa miguu za Kombe la Mataifa ya Afrika *(AFCON 2027)*. Aidha, ujenzi huu ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020/2025 Aya ya 243(a). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa bajeti ya Wizara na ulinganisho wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa; Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti ya Wizara dhidi ya bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/2025 kuona ni kwa kiasi gani unaathiri bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kielelezo Na. 7 kinaonesha ulinganisho wa bajeti hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa:-

(i) Wakati bajeti ya matumizi mengineyo ya Taifa ikiwa inaongezeka kwa 25%, bajeti ya matumizi mengineyo ya Wizara hii imeongezeka kwa asilimia sita tu;

(ii) Wakati bajeti ya maendeleo ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa 25%, bajeti ya maendeleo ya Wizara hii imeongezeka kwa 90%; na

(iii) Wakati bajeti ya mishahara ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa 24%, bajeti ya mishahara ya Wizara imeongezeka kwa asilimia nne tu; na

(iv) Kwa ujumla wakati bajeti ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa 11.2% kutoka shilingi trilioni 44 mwaka 2023/2024 hadi shilingi trilioni 49 mwaka 2024/2025, bajeti ya Wizara imeongezeka kwa 705% kutoka shilingi bilioni 35.4 mwaka 2023/2024 hadi shilingi bilioni 285.3 mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hizi mbili zinatupa tafsiri kuwa pamoja na kuwa kuna ongezeko la bajeti ya Taifa, bajeti ya

Wizara imepewa kipaumbele zaidi hasa katika miradi ya maendeleo. Kamati inashauri kuwa fedha hizo zitoke kwa wakati kama zitakavyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati inatoa ushauri, maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

(i) Upatikanaji wa fedha za maendeleo; pamoja na Serikali kuongeza bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, bado Kamati inasisitiza kuwa fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 zitoke kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kabla ya mwaka wa fedha kumalizika; *(Makofi)*

(ii) Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA); itakumbukwa kuwa lugha ya Kiswahili imechaguliwa kuwa ni mojawapo ya lugha za mawasiliano katika nchi za Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara *(SADC)* na nchi mbalimbali kama vile Afrika Kusini zimeanza kutumia lugha hii. Baraza la Kiswahili Tanzania ndiyo nyenzo muhimu katika kubidhaisha lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi. Kamati inaamini kuwa ni lazima kama Taifa tuwe na dhamira ya dhati ya kuwekeza na kutoa kipaumbele katika kukibidhaisha Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa lugha hii, Kamati inashauri ifuatavyo: -

(i) BAKITA iweke mikakati ya makusudi ya kubidhaisha lugha ya Kiswahili kwa kuzalisha wakalimani wengi zaidi ambao watakuwa na uwezo wa kufahamu lugha zaidi ya moja kwa ufasaha ikiwa ni pamoja na kuongeza nyenzo muhimu za kufundishia;

(ii) Ili kufanikisha kubidhaisha Kiswahili, Serikali ianzishe Dawati la Kiswahili katika kila Ubalozi kama wenzetu China wanavyofanya. Aidha, katika kuimarisha matumizi ya Kiswahili Fasaha na Sanifu kwa waandishi wa Kiswahili Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, Kamati inasisitiza kuwa Wizara itumie Balozi zetu kujenga ushawishi wa vyuo vikuu vya nje ya nchi pamoja na taasisi zingine kufundisha Kiswahili kama somo katika vyuo na taasisi hizo; na

(iii) Serikali iongeze bajeti ya BAKITA ili kuongeza kasi ya kubidhaisha Kiswahili ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uwanja wa Michezo wa Taifa *(Benjamin Mkapa Stadium)*; Kamati inasikitishwa na hali ya Uwanja wa Benjamin Mkapa ambayo inapelekea wasiwasi mkubwa wa kutokamilika kwa wakati kwa kuwa mwenendo wa mkandarasi huyu ni wa kusuasua. Kamati imebaini kuwa upo upungufu wa bajeti ya kutekeleza mradi ambapo kwa mwaka 2023/2024 uwanja ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 1.2 pekee hali inayopelekea kuhitaji fedha nje ya bajeti ili kuendelea na utekelezaji wa mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuchukua hatua mbalimbali katika uwanja huo, bado Kamati inaona kuna uhitaji mkubwa wa matumizi ya Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa ajili ya michezo ya Kimataifa ya timu za Taifa kwa vilabu vyetu. Katika kutatua changamoto hizo, Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

(i) Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya ukarabati wa Uwanja wa Benjamini Mkapa zipatikane kwa wakati; *(Makofi)*

(ii) Serikali iandae mkakati wa kuboresha viwanja vingine vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya Kimataifa ili kupunguza mfululizo wa matumizi ya Uwanja wa Benjamini Mkapa *(Benjamini Mkapa Stadium);*

(iii) Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha inasimamia kwa ukaribu ukarabati wa uwanja na unakamilika kwa muda uliopangwa; na

(iv) Menejimenti ya Uwanja wa Benjamini Mkapa ihakikishe inafanya ukarabati wa uwanja mara kwa mara kadiri inavyohitajika ili kuepuka gharama kubwa zisizo na ulazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uwanja wa Mpira wa Miguu Arusha; Kamati inaishukuru na kuipongeza Serikali kwa kutekeleza azma ya kuboresha michezo nchini pamoja na kujenga viwanja wa kisasa vya michezo. Kwa mfano, ujenzi wa Uwanja wa Arusha utakaokuwa na uwezo wa kuchukua mashabiki 30,000. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali izingatie umuhimu wa kutoa fedha za ujenzi wa uwanja huo kama zitakavyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa michezo ya kubashiri *(sports betting)*; kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2020, Serikali ilipitisha Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Mchezo kupokea asilimia tano ya mapato yatokanayo na kubashiri matokeo ya michezo *(sports betting)* inayosimamiwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imekuwa ikiomba fedha hizo kutoka Hazina lakini hawapatiwi fedha zote asilimia tano kama sheria inavyotaka. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024 Wizara ilipokea shilingi bilioni 3.6 pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokupokelewa kwa fedha hizi kwa wakati kumeathiri kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii ikiwemo kushindwa kutekeleza jukumu lake kuu la kugharamia timu za Taifa, ikiwemo timu ya mpira wa miguu kwa wanaume ambayo ina gharama kubwa za uendeshaji. Kamati inapendekeza maoni mahususi katika eneo hili kama ifuatavyo: -

(i) Serikali itoe fedha hizo kwa wakati kama ilivyoelezwa na sheria iliyopitishwa na Bunge; na

(ii) Kwa kuwa mapato yatokanayo na michezo ya kubashiri yametajwa katika Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2021, Kamati inaishauri Wizara kupitia BMT ifanye mchakato wa utungaji wa kanuni kwa ajili ya kusimamia Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Michezo pamoja na mapato yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu programu ya mtaa kwa mtaa; pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo katika kukuza na kuendeleza michezo nchini, lakini bado kuna changamoto ya ukosefu wa fedha za kuendesha programu ya mtaa kwa mtaa ambayo ni suluhisho la uibuaji wa vipaji. Kamati inashauri Serikali ifanye yafuatayo: -

(i) Kwanza izitake halmashauri zitenge fedha za kutosha za kuwezesha mashindano haya kufanyika katika ngazi husika; na

(ii) Iweke utaratibu kutafuta wafadhili watakaosaidi programu hii kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfuko wa Utamaduni na Sanaa; Kamati inapongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuanzisha na kuupatia fedha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa. Mfuko huu utasaidia kuinua ubora wa kazi za utamaduni na sanaa ili ziweze kujiendesha kibiashara, kutengeneza ajira pamoja na kuchangia Pato la Taifa na Kamati inaishauri Serikali ihakikishe inasimamia vizuri matumizi ya fedha hizo ili ziweze kuleta tija ya kweli kama ilivyokusudiwa na Mheshimiwa Rais katika azma yake ya kuendeleza wasanii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali iandae na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa na wenye maudhui ya kulinda Mfuko wa Sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Michezo; kutokana na umuhimu wa Mfuko wa Maendeleo ya Michezo katika sekta ya michezo nchini Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Serikali iendelee kutenga bajeti ya mfuko ili kuimarisha michezo, kufadhili timu nyingi zaidi na masuala yote yanayohusu michezo ya kitaifa; na

(ii) Baraza la Michezo la Taifa liweke mikakati itakayowezesha kuongeza mapato ya mfuko kutokana na fursa zilizopo ili kusaidia shughuli za maendeleo ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambao maoni yao, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilisha kwa taarifa hii, naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo - Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro na Naibu wake Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Katibu Mkuu wa Wizara - Ndugu Gerson Msigwa, Naibu Katibu Mkuu - Dkt. Suleiman Hassan pamoja na watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc,* kwa

kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema wakati wote ilipokutana na hata wakati wa utaarishaji wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii, liijadili na likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**

**1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuikubali ili hatimaye liidhinishe Bajeti ya Wizara hii.

**1.2 Msingi wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Taarifa hii unatokana na masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kanuni ya

6 (1) (a) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7 (1) (a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inaipa Kamati jukumu ka kufanya uchambuzi wa utekeleaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti ya Kanuni niliyoitaja, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, tarehe 22 Machi, 2024, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na matokeo yake ni taarifa hii yenye maoni na ushauri.

### 1.3 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Muundo wa Taarifa hii umezingatia Masharti ya Kanuni ya 142 kuhusu Muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifaninayowasilisha imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya **Kwanza,** inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi, Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(ii) Sehemu ya **Pili,** inabainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(iii) Sehemu ya **Tatu,** inabainisha Maoni na Ushauri wa Kamati na kumalizia kwa hitimisho.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muundo huo, Bunge linaweza kuwa kwenye nafasi nzuri ya kuitumia Taarifa hii wakati wa majadiliano. Mtiririko wa maudhui umewekwa kwa namna rahisi ya rejea na matumizi ya Bunge.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI

### 2.1 Ufafanunuzi wa jumla

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inafanunua matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi. Katika Uchambuzi huo, ufafanuzi unabainishwa kuhusu hali ya uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuhusu uwiano katika makadirio ya matumizi ya maendeleo na matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### 2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inatoa siku zisizozidi tisa (9) kwa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti. Kanuni hiyo inatambua umuhimu wa kufanya ulinganisho kati ya utekelezaji wa Bajeti unaoripotiwa na makadirio ya mapato na mtumizi kwa Mwaka wa Fedha unaofuata. Kwa msingi huo, Sehemu hii inaripoti matokeo ya shughuli kuu tano (5) zilizotekelezwa na Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(ii) Hali ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(iii) Hatua iliyofikiwa katika Ukusanyaji wa Maduhuri kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024;

(iv) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina; na

(v) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa kazi zilizopangwa kufanyika kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, kwa urahisi wa ufatiliaji na uamuzi wa Kibunge, naomba kubainisha matokeo ya uchambuzi kama ifuatavyo:-

### 2.2.1 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha *2023/2024*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea na kukagua jumla ya miradi ya maendeleo mitatu (3) iliyopo chini ya Wizara hii, ambayo inatekelezwa katika Mkoa wa Dar es Salaam kuanzia tarehe 18 hadi 19 Machi, 2024. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ilitengewa jumla ya **Shilingi 11,831,160,000;** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 33.4.** Ufafanuzi zaidi kuhusu Miradi unaambatishwa pamoja na Tarifa hii **(Kiambatisho Na.1**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo unaonesha mambo yafuatayo:

(i) Upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Bajeti nzima ya Wizara haulingani na uwiano wa kiasi cha fedha za miradi ya maendeleo kilichopokelewa. Kiasi hiki cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kilikuwa **asilimia 33.4** ya Bajeti yote na kiasi kilichopokelewa kilikuwa **asilimia 66** ya fedha zote zilizopatikana.

(ii) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo hauendani na kipindi cha utekelezaji. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024, fedha zilizopokelewa ni **asilimia 66** ya Bajeti ya Maendeleo katika kipindi cha utekelezaji. Mtiririko huo unaonekana katika Kielelezo Na. 1.

(iii) Makadirio ya baadhi ya gharama kwa miradi inayotekelezwa na Wizara hii hayatolewi kama ilivyokusudiwa kutekelezwa; kwa mfano, Mradi Na. **6504** unaohusu Ujenzi wa Kituo cha Mazoezi na Kupumzikia Wananchi, unatekelezwa kwa msingi wa makadirio ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. Hadi Kamati

inakwenda kukagua mradi huu, hakukuwa na kiasi cha fedha chochote kilichotolewa kutoka Hazina. Mwenendo wa upatikanaji wa fedha usioridhisha, unakwamisha utekelezaji wa mradi.

(iv) **Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hairidhishi kabisa. Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina na mwenendo wa utolewaji wa fedha usioridhisha unakwamisha utekelezaji wa miradi ambapo ni miongoni mwa changamoto. Hata hivyo, suala la ufinyu wa bajeti kwa miradi iliyopangwa kutekelezwa linahitaji kuangaliwa kwa kina.

**Jedwali Na. 1: Mwendendo wa upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| **Matumizi** | | **Kiasi kilichoidhinishwa** | **Kiasi Iliyoidhinishwa Baada ya Uhamisho Mwaka 2023/24** | **Kiasi kilichopokelewa Hadi Februari, 2024** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|---|---|
| Mishahara ya Watumishi | Wizara | 3,356,416,000 | 3,356,416,000 | 2,247,062,340 | 67 |
| | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 6,294,869,000 | 6,294,869,000 | 3,839,885,784 | 61 |
| **Jumla Ndogo** | | **9,651,285,000** | **9,651,285,000** | **6,086,948,124** | **63** |
| Matumizi Mengineyo (OC) | Wizara | 10,389,429,000 | 11,810,413,945 | 7,624,001,028 | 65 |
| | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 3,356,416,000 | 8,476,591,805 | 8,530,464,193 | 101 |
| **Jumla Ndogo** | | **13,745,845,000** | **20,287,005,751** | **16,154,465,221** | **80** |
| Miradi ya Maendeleo | Wizara | 10,560,000,000 | 14,139,377,144 | 10,117,983,752 | 72 |
| | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 1,271,160,000 | 1,271,160,000 | - | 0 |
| **Jumla Ndogo** | | **11,831,160,000** | **15,410,537,144** | **10,117,983,752** | **66** |
| **JUMLA KUU** | | **35,445,041,000** | **45,348,827,895** | **32,359,397,096** | **71** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025

### 2.2.2 Hali ya Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Katika kikao cha Kamati na Wizara kilichofanyika tarehe 6 Juni, 2023, wakati wa kujadili Makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilitoa ushauri wa masuala mbalimbali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Jumla ya mapendekezo kumi na nne (14) yalitolewa na Kamati. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, sehemu ya ushauri umefanyiwa kazi na sehemu nyingine utekelezaji wake unaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa ushauri uliofanyiwa kazi unahusu Wadau wa Sanaa na Utamaduni nchini kuungana na Serikali katika kukiendeleza, kukuenzi na kukitumia Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) katika kuendeleza Tasnia za Sanaa na Utamaduni. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa, Serikali imeanza kutoa mafunzo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Chuo Kikuu cha Tumaini katika uendeshaji wa warsha, makongamano na semina, kwa lengo la kuwaongezea uwezo wasanii ili kukuza weledi na kuimarisha tasnia ya Sanaa na Utamaduni hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na utekelezaji mzuri wa ushauri wa Kamati, upo ushauri ambao unahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali, Mathalani, Serikali kuhakikisha fedha zinatolewa kutokana na Michezo ya Kubashiri Matokeo ya Michezo (*Sports Betting*) zinatolewa kwa kadri zinavyokusanywa katika kipindi husika ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na maelezo yaliyotolewa na Serikali na hivyo, kusisitiza Serikali iendelee kufanyia kazi ushauri huo.

### 2.2.3 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo - **Fungu 96,** ilikadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 6,970,428,000,** ambapo Wizara yenyewe ilikadiriwa kukusanya **Shilingi 1,000,000,000** na Idara zilizo chini ya

Wizara zilikadiriwa kukusanya **Shilingi 5,970,428,000** kutoka Taasisi zilizokuwa chini ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Wizara, Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara, zilikusanya **Shilingi bilioni 4,978,741,852,** sawa na **asilimia 71.42** tu ya lengo la makusanyo. Makusanyo ya maduhuli kwa Wizara yalikuwa **Shilingi 556,018,433**, sawa na asilimia **57** ya lengo la makusanyo. Wakati huo, Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara zilikusanya **Shilingi bilioni 4,422,633,419,** sawa na asilimia **74** ya lengo la makusanyo, kama inavyooneshwa katika Kielelezo Namba 2.

**Jedwali Na. 2: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 - Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| CHANZO | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| WIZARA | 1,000,000,000 | 556,018,433 | 57 |
| TAASISI | 5,970,428,000 | 4,422,633,419 | 74 |
| JUMLA | **6,970,428,000** | **4,978,741,852** | **71.42** |

**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025

**UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA 2023/2024**




**Chanzo:** Usanifu wa Kamati na Randama ya Wizara ya tamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025

### 2.2.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Bunge kuidhinisha Matumizi ya Kawaida ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, ilibaki kazi ya Kamati kufuatilia utekelezaji uliofanyika. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati iliendelea kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Hata hivyo, tarehe 22 Machi, 2024, Kamati ilipokea maelezo ya Waziri yaliyofafanua upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Taswira halisi ya mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaoneshwa katika Kielelezo Namba 3.

**Jedwali Na. 3: Mwenendo wa upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| Matumizi | | Kiasi Kilichoidhini-shwa | Kiasi kIlichoidhinishwa Baada ya Uhamisho wa fedha Mwaka 2023/2024 | Kiasi kilichopokelewa Hadi Februari, 2024 | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| Mishahara ya Watumishi | Wizara | 3,356,416,000 | 3,356,416,000 | 2,247,062,340 | 67 |
| | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 6,294,869,000 | 6,294,869,000 | 3,839,885,784 | 61 |
| **Jumla Ndogo** | | **9,651,285,000** | **9,651,285,000** | **6,086,948,124** | **63** |
| Matumizi Mengineyo (OC) | Wizara | 10,389,429,000 | 11,810,413,945 | 7,624,001,028 | 65 |
| | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 3,356,416,000 | 8,476,591,805 | 8,530,464,193 | 90 |
| **Jumla Ndogo** | | **13,745,845,000** | **20,287,005,751** | **16,154,465,221** | **80** |
| Miradi ya Maendeleo | Wizara | 10,560,000,000 | 14,139,377,144 | 10,117,983,752 | 72 |
| | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 1,271,160,000 | 1,271,160,000 | - | 0 |
| **Matumizi** | | **Kiasi kilichoidhinishwa** | **Kiasi kIlichoidhinishwa Baada ya Uhamisho wa** | **Kiasi kilichopokelewa Hadi Februari,** | **Asilimia (%)** |

| | | fedha Mwaka 2023/2024 | 2024 | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| Wizara | | | | |
| **Jumla Ndogo** | **11,831,160,000** | **15,410,537,144** | **10,117,983,752** | **66** |
| **JUMLA KUU** | **35,445,041,000** | **45,348,827,895** | **32,359,397,096** | **71** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ulikuwa wa kuridhisha, kwa kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2023 kiasi cha fedha kilichopatikana kilifikia **asilimia 71** ya kiasi kilichoidhinishwa. Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya kawaida ya Wizara hii unaridhisha. Aidha, Kamati imebaini kuwa hakuna tofauti ya uwiano ulioidhinishwa na hali ilivyo katika utekelezaji kama inavyoonekana katika jedwali hapo juu.

**2.2.5 Utekelezaji wa Majukumu na Mipango ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ilikusudiwa kuwezesha utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara hii. Ili kujiridhisha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji, Kamati ilipokea na kuchambua maelezo ya Waziri kuhusu majukumu na mipango inayotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini utekelezaji wa mipango na majukumu uliendana na fedha zilizotengwa. Kwa ujumla, utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 unaendelea vizuri na ufanishi wake unaonekana. Kwa mfano, Wizara ilipanga kutambua na kusajili jumla ya Wataalam 50 katika Kanzidata ya Wataalam wa Kiswahili. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali iliripoti utekelezaji wa Mpango huo. Maelezo ya Waziri yalionesha kuwa, Wataalamu 153 walitambuliwa na kusajiliwa katika mfumo huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilidadisi zaidi kuhusu mpango uliowekwa na Wizara ili kujenga na kukarabati miundombinu ya

michezo. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa, Serikali imeendelea kutekeleza mipango hiyo. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa, utekelezaji huo unakabiliwa na changamoto mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa changamoto hizo ni kuwepo kwa mahitaji ya matumizi mengi ya Uwanja wa Taifa kwa ajili ya michezo ya kimataifa na timu za Taifa. Vilevile, ipo changamoto ya Mkandarasi kutokukamilisha kazi kwa wakati na hivyo, kusababisha kazi ya ukarabati kuchukua muda mrefu. Ni rai ya Kamati kuwa, changamoto hizo zinastahili kuwekewa mikakati mahsusi ya kuzitatua.

### 2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ulifanyika kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha husika. Uzingatiaji zaidi uliwekwa katika maeneo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli;

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na (iii) Makadirio ya Matumizi ya Kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, maeneo yaliyofanyiwa uchambuzi yalizingatia Majukumu ya Msingi ya Wizara pamoja na mwelekeo wa jumla wa Taifa. Aidha, utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake, utakuwa na tija endapo Serikali itatenga fedha za kutosha na kuzitoa kwa wakati kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa kuzingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

#### 2.3.1 Makadirio ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, inakadiriwa kukusanya **Shilingi 8,001,600,000.** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

yameongezeka kwa **asilimia 17.2** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2023/2024. Ingawa Bajeti ya matumizi ya Wizara imeongezeka kwa **asilimia 13** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha unaokwisha, ukusanyaji wa maduhuli hauna dalili ya kufikia lengo, kwani hadi Kamati inachambua bajeti hii, Wizara ilikuwa imekusanya **asilimia 57** tu. Kamati inasisitiza kuwa, Wizara iongeze kasi ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

**Jedwali Na. 4: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara kwa Mwaka 2023/2024 na 2024/2025**

| WIZARA | Makadirio ya Maduhuli 2023/2024 | Makadirio ya Maduhuli 2024/2025 |
|---|---|---|
| Mapato ya Viwanja vya Michezo (Uhuru na Benjamin Mkapa) | 907,696,000 | 907,696,000 |
| Ada za Mafunzo | 92,302,000 | 92,302,000 |
| Mapato kutoka vyanzo mbalimbali | 1,000 | 1,000 |
| Marejesho ya fedha za Umma | 1,000 | 1,000 |
| **Jumla** | **1,000,000,000** | **1,000,000,000** |

**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezokuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025

**Jedwali Na. 5: Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Mapato kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara katika Mwaka 2023/2024 na 2024/2025**

| Na | TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA | Makadirio ya Maduhuli 2023/2024 | Makadirio ya Maduhuli 2024/2025 |
|---|---|---|---|
| 1. | Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) | 480,228,000 | 581,700,000 |
| 2. | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) | 800,000,000 | 885,000,000 |
| 3. | Bodi ya Filamu Tanzania | 1,460,000,000 | 1,460,000,000 |
| 4. | Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) | 950,200,000 | 1,514,900,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5. | Baraza la Michezo la Taifa (BMT) | 920,000,000 | 1,200,000,000 |
| 6. | Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) | 1,360,000,000 | 1,360,000,000 |
| **Jumla** | | **5,970,428,000** | **7,001,600,000** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025

### 2.3.2 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo inakadiriwa kutumia **Shilingi 285,318,387,000;** Kati ya fedha hizo, Misharaha (PE) ni **shilingi 11,280,116,000** sawa na **asilimia 4,** Matumizi Mengineyo (OC) yanaombewa jumla ya **Shilingi 15,847,483,000** sawa na **asilimia 6** na Miradi ya Maendeleo zinaombwa jumla ya **Shilingi 258,190,788,000** sawa na **asilimia 90.**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti ya **Fungu 96** imeongezeka kwa **asilimia 705** kutoka **Shilingi 35,445,041,000** mwaka 2023/2024 hadi kufikia **Shilingi 285,337,887,000** mwaka 2024/2025. Aidha, ongezeko zaidi linaonekana katika fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo, ambazo zimeongezeka kwa **asilimia 2,082** kutoka **shilingi 11,831,160,000** hadi **Shilingi 258,190,160,000**. Hata hivyo, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, makadirio ya mishahara yameongezeka kwa **asilimia 17.** Vilevile Bajeti ya matumizi mengineyo (OC) imeongezeka kwa **asilimia 13.**

### 2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya **Shilingi 258,190,788,000** kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo inayopangwa kutekelezwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Makadirio hayo yameongezeka kwa **asilimia 2,082** kutoka **Shilingi 11,831,160,000** mwaka 2023/2024 hadi **Shilingi 258,190,788,000** mwaka 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** ongezeko la **asilimia 70** ya fedha za miradi ya maendeleo limechangiwa na Bajeti ya ujenzi wa Viwanja vya

Arusha na Dodoma. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa viwanja hivyo, ambapo kwa kiasi kikubwa vitasaidia kuwa na miundombinu ya michezo na kuwezesha Tanzania kuwa mwenyeji wa finali za mpira wa miguu za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027). Aidha, Ujenzi huu ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020/2025 aya 243 (a), inayoelezea azma ya kuboresha michezo nchini, ikiwa ni pamoja na kujenga uwanja wa kisasa wa michezo Makao Makuu ya nchi Jijini Dodoma. Kielelezo Na. 6 linaonesha mchanganuo wa makadirio hayo.

**Jedwali Na. 6: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2023/2024 na Mwaka 2024/2025**

| **Maelezo** | | **Bajeti Iliyoidhinishwa Mwaka 2023/2024 (Shilingi)** | **Bajeti iliyoidhinishwa Mwaka 2024/2025** | **Ongezeko** | **% ya Ongezeko** |
|---|---|---|---|---|---|
| **(1)** | | **(2)** | **(4)** | **(5)** | **(6)=(5)/(4)x100** |
| Mishahara ya Watumishi | Wizara | 3,356,416,000 | 3,989,923,000 | 633,507,000 | 19 |
| | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 6,294,869,000 | 7,290,193,000 | 995,324,000 | 16 |
| **Jumla Ndogo** | | 9,651,285,000 | 11,280,116,000 | 1,628,831,000 | 17 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | Wizara | 10,389,429,000 | 11,263,816,000 | 874,831,000 | 8 |
| | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 3,573,167,000 | 4,583,667,000 | 1,010,500,000 | 28 |
| **Jumla Ndogo** | | 13,962,596,000 | 15,847,483,000 | 1,884,887,000 | **13** |
| Miradi ya Maendeleo | Wizara | 10,560,000,000 | 241,070,788,000 | 230,510,788,000 | 2182 |
| | Taasisi zilizo chini ya | 1,271,160,000 | 17,120,000,000 | 15,848,840,000 | 1246.8 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wizara | | | | |
| **Jumla Ndogo** | | **11,831,160,000** | **258,190,788,000** | **246,359,628,000** | **2082** |
| **JUMLA KUU** | | **35,445,041,000** | **285,318,387,000** | **249,873,346,000** | **705** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025

2.3.4 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara na ulinganisho wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025, kuona ni kwa kiasi gani unaathiri Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kielelezo Na. 7 linaonesha Ulinganisho wa Bajeti hizo.

**Jedwali Na. 7: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

| **BAJETI KUU YA TAIFA 2024/2025** | | | **BAJETI YA WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO (2024/2025)** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Mgawanyo | Bajeti kuu | % ya jumla ya Bajeti kuu | Mgawanyo | Bajeti ya Wizara | % ya Jumla ya Bajeti ya Wizara |
| MISHAHARA | 11,767,987,083,000 | 24 | MISHAHARA | 11,280,116,000 | 4 |
| MATUMIZI MENGINEYO | 21,633,343,682,000 | 44 | MATUMIZI MENGINEYO | 15,847,483,000 | 6 |
| MAENDELEO (ndani) | 12,303,518,651,000 | 25 | MAENDELEO | 258,190,788,000 | 90 |
| MAENDELEO (nje) | 3,640,838,144,000 | 7 | MAENDELEO (nje) | 0 | 0 |
| **Jumla** | **49,345,700,000,000** | 100 | **Jumla** | **285,318,387,000** | 100 |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, Kamati imebaini yafuatayo: -

(i) Wakati bajeti ya matumizi mengineyo (OC) ya Taifa ikiwa inaongezeka kwa **asilimia 25**, bajeti ya matumizi mengineyo ya Wizara hii imeongezeka kwa **asilimia 6;**

(ii) Wakati bajeti ya maendeleo ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 25**, bajeti ya maendeleo ya Wizara hii imeongezeka kwa **asilimia 90**;

(iii) Wakati bajeti ya mishahara ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 24**, bajeti ya mishahara ya Wizara imeongezeka kwa **asilimia 4;** na

(iv) Kwa ujumla wakati Bajeti ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 11.2** kutoka **Shilingi Trilioni 44** mwaka 2023/2024 hadi **Shilingi Trilioni 49** mwaka 2024/2025, Bajeti ya Wizara imeongezeka kwa **asilimia 705** kutoka **Shilingi Bilioni 35.4** mwaka 2023/2024 hadi **Shilingi Bilioni 285.3** mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** bajeti hizi mbili zinatupa tafsiri kuwa, pamoja na kuwa kuna ongezeko la Bajeti ya Taifa, Bajeti ya Wizara imepewa kipaumbele zaidi hasa katika Miradi ya Maendeleo. Kamati inashauri kuwa, fedha hizo zitoke kwa wakati kama zitakavyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati inatoa ushauri, maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

**3.1 Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Serikali kuongeza Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Bado Kamati inasisitiza kuwa, Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 zitoke kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kabla ya mwaka wa fedha kumalizika.

**3.2 Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA)**

**Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kuwa, Lugha ya Kiswahili imechaguliwa kuwa ni mojawapo ya lugha za mawasiliano katika nchi za Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara (*SADC*), na nchi mbalimbali kama vile Afrika Kusini zimeanza kutumia lugha hii. Baraza la Kiswahili Tanzania ndiyo nyenzo muhimu katika kubidhaisha Lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi. Kamati inaamini kuwa ni lazima kama Taifa tuwe na dhamira ya dhati ya kuwekeza na kutoa kipaumbele katika kukibidhaisha Kiswahili. Kutokana na umuhimu wa lugha hii, Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) BAKITA iweke mikakati ya makusudi ya kubidhaisha Lugha ya Kiswahili kwa kuzalisha Wakalimani wengi zaidi ambao wanatakuwa na uwezo wa kufahamu lugha zaidi ya moja kwa ufasaha ikiwa ni pamoja na kuongeza nyenzo muhimu za kufundishia;

(ii) Ili kufanikisha kubidhaisha Kiswahili, Serikali ianzishe Dawati la Kiswahili katika kila Ubalozi kama wenzetu China wanavyofanya. Aidha, katika kuimarisha matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu kwa waandishi wa Kiswahili Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, Kamati inasisitiza kuwa, Wizara itumie Balozi zetu kujenga ushawishi wa Vyuo Vikuu vya nje ya nchi pamoja na taasisi zingine kufundisha Kiswahili kama somo katika vyuo na taasisi hizo; na

(iii) Serikali iongeze Bajeti ya BAKITA ili kuongeza kasi ya kubidhaisha Kiswahili ndani na nje ya nchi.

## 3.3 Uwanja wa Michezo wa Taifa (Benjamin Mkapa Stadium)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasikitishwa na hali ya Uwanja wa Benjamin Mkapa ambayo inapelekea wasiwasi mkubwa wa kutokamilika kwa wakati kwa kuwa mwenendo wa Mkandarasi huyu ni wa kusuasua. Kamati imebaini kuwa, upo upungufu wa bajeti ya kutekeleza mradi, ambapo kwa mwaka 2023/2024 Uwanja ulitengewa jumla ya shilingi 1,120,000,000 pekee, hali inayopelekea kuhitaji fedha nje ya bajeti ili kuendelea na utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Serikali kuchukua hatua mbalimbali katika Uwanja huo, bado Kamati inaona kuna uhitaji mkubwa wa matumizi ya Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa ajili ya michezo ya kimataifa ya timu za Taifa kwa vilabu vyetu. Katika kutatua changamoto hizo, Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

(i) Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya ukarabati wa Uwanja wa Benjamini Mkapa zipatikane kwa wakati;

(ii) Serikali iandae mkakati wa kuboresha viwanja vingine vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya Kimataifa ili kupunguza mfululizo wa matumizi ya Uwanja wa Benjamini Mkapa (*Benjamini Mkapa Stadium*);

(iii) Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha inasimamia kwa karibu ukarabati wa Uwanja na unakamilika kwa muda uliopangwa; na

(iv) Menejimenti ya Uwanja wa Benjamini Mkapa ihakikishe inafanya ukarabati wa uwanja mara kwa mara kadri inavyohitajika ili kuepuka gharama kubwa ambazo zisizo na ulazima.

## 3.4 Uwanja wa Mpira wa Miguu Arusha

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishukuru na kuipongeza Serikali kwa kutekeleza azma ya kuboresha michezo nchini, pamoja na kujenga viwanja wa kisasa vya michezo; kwa mfano, ujenzi wa Uwanja wa Arusha utakaokuwa na uwezo wa kuchukua

mashabiki 30,000. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali izingatie umuhimu wa kutoa fedha za ujenzi wa uwanja huo kama zitakavyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kwa kufanya hivyo, itasaidia kufanikisha na kukamilisha utekelezaji wa mradi huu kama ilivyokusudiwa.

### 3.5 Michezo ya Kubashiri (Sports Betting)

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020, Serikali ilipitisha Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Mchezo kupokea **asilimia 5** ya mapato yatokanayo na kubashiri matokeo ya michezo (Sports Betting) inayosimamiwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imekuwa ikiomba fedha hizo kutoka Hazina lakini hawapatiwi fedha zote (5%) kama Sheria inavyotaka. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024 Wizara ilipokea **shilingi bilioni 3.6** pekee.

**Mheshimiwa Spika,** kutokupokelewa kwa fedha hizi kwa wakati kumeathiri kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii ikiwemo kushindwa kutekeleza jukumu lake kuu la kugharamia timu za Taifa ikiwemo timu ya mpira wa miguu kwa wanaume ambayo ina gharama kubwa za uendeshaji. Kamati inapendekeza maoni mahususi katika eneo hili kama ifuatavyo**:-**

i. Serikali itoe fedha hizo kwa wakati kama ilivyoelezwa na sheria iliyopitishwa na Bunge ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kikamilifu**.**

ii. Kwa kuwa, mapato yatokanayo na Michezo ya Kubashiri yametajwa katika Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT) iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2021, kama mojawapo wa chanzo cha fedha cha kuendesha Mfuko wa Maendeleo ya Michezo; na kwa kuwa, utekelezaji wa Sheria yoyote unahitaji kuwa na Kanuni zake; Kamati inaishauri kuwa, Wizara kupitia BMT ifanye mchakato wa utungaji wa Kanuni kwa ajili ya kusimamia

Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Michezo pamoja na mapato yake.

### 3.6 Programu ya Mtaa kwa Mtaa

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo katika kukuza na kuendeleza michezo nchini, lakini bado kuna changamoto ya ukosefu wa fedha za kuendesha Programu ya Mtaa kwa Mtaa ambayo ni suluhisho la uibuaji wa vipaji. Kamati inaona Programu hii ikiwekewa mazingira wezeshi na misingi bora, itapanua wigo wa kukuza vipaji na ajira. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inashauri kuwa, Serikali ifanye yafuatayo:-

i. Izitake Halmashauri zitenge fedha za kutosha za kuwezesha mashindano haya kufanyika katika ngazi husika; na

ii. Iweke utaratibu wa kutafuta wafadhili watakaosaidia programu hii kufanyika.

### 3.7 Mfuko wa Utamaduni na Sanaa

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuanzisha na kuupatia fedha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa. Mfuko huu utasaidia kuinua ubora wa kazi za Utamaduni na Sanaa ili ziweze kujiendesha kibiashara, kutengeneza ajira pamoja na kuchangia katika Pato la Taifa. Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

(i) Ihakikishe inasimamia vizuri matumizi ya fedha hizo ili ziweze kuleta tija ya kweli kama ilivyokusudiwa na Mheshimiwa Rais katika azma yake ya kuendeleza Wasanii;

(ii) Iweke mikakati ya kuongeza fedha kwa ajili ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ili uweze kuwafikia walengwa wengi zaidi. Hata hivyo, Kamati inasisitiza Wizara ibuni vyanzo vingine vya mapato kwa ajili ya kutunisha Mfuko huo;

(iii) Wizara iimarishe uratibu na usimamizi wa Mfuko katika eneo la ukusanyaji wa fedha za marejesho ya mikopo ili kuwapa fursa wasanii wengine waweze kupata mikopo na kuimarisha ukuaji wa sekta za utamaduni na Sanaa;

(iv) Iandae na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa wenye maudhui ya kulinda Mfuko; na

(v) Itoe mafunzo kwa walengwa kuhusu matumizi ya mikopo au ruzuku zitakazotolewa na Mfuko kwa namna iliyokusudiwa yenye kuleta tija kwao na katika Sekta ya Utamaduni na Sanaa.

**3.8 Mfuko wa Maendeleo ya Michezo**

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Maendeleo ya Michezo ulianzishwa kwa lengo la kusaidia shughuli za maendeleo ya michezo. Hata hivyo, uwekezaji kwenye Mfuko huu bado si wa kuridhisha kwa kuwa unakabiliwa na uhaba wa rasilimali fedha. Kamati ilibaini mara kadhaa kwa baadhi ya Timu za Taifa kushindwa kushiriki katika mashindano ya kimataifa kutoka na upungufu wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** mahitaji ya timu za Tanzania kushiriki katika michezo mbalimbali ya kimtaifa ni makubwa na hivyo kushindwa kushiriki kutoka uhaba wa fedha. Endapo **asilimia 5** ya fedha za michezo ya kubashiri zitaingizwa katika Mfuko kulingana na mapato halisi ya michezo hiyo, zitaweza kusaidia timu nyingi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu wa Mfuko wa Maendeleo ya Michezo katika Sekta ya Michezo nchini, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iendelee kutenga Bajeti ya Mfuko ili kuimarisha michezo, kufadhili timu nyingi zaidi na masuala yote yanayohusu michezo ya kitaifa; na

(ii) Baraza la Michezo la Taifa (BMT) liweke mikakati itakayowezesha kuongeza mapato ya Mfuko kutokana na fursa zilizopo ili kusaidia shughuli za maendeleo ya michezo.

## 3.9 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, Nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

1. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Musa Ramadhani Sima, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Anastazia James Wambura, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Dr. Thea Ntara, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Ester Edwin Maleko, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Hassan Zidadu Kungu, Mb- Mjumbe
9. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Kassim Ali Khamis, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Mwanakhamisi Kassian Said, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Nusrat Shaaban Hanje, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb- Mjumbe
16. Mhe. Rose Syprian Tweve, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Tunza Issa Malapo, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Yahya Ally Hamis, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kumshukuru Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo - Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb), Naibu Waziri - Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara hii - Ndg. Gerson Partinus Msigwa, Naibu Katibu Mkuu - Ndg. Dkt. Suleiman Hassan Serera, pamoja na Watendaji wengine wa Wizara, kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge - Ndg. Nenelwa J. Mwihambi (*ndc*), kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema wakati wote ilipokutana na hata wakati wa utayarishaji wa Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, lipokee Taarifa hii, lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Husna Juma Sekiboko, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO**
23 Mei, 2024

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika, mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaye Mwenyekiti wa Mama Ongea na Mwanao Ndugu Steven Mengele maarufu kwa jina la Steven Nyerere, umesimama au bado umekaa? *(Makofi/Kicheko)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro - Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Maafisa wa Klabu ya Simba kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Hamis Kisiwa - Mkurugenzi wa Wanachama, Ndugu Belinda Paul - Mkurugenzi wa Operesheni na Balozi Christopher Liundi - Katibu Mkuu Mstaafu wa *TANU Youth League*, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, watu maarufu nchini mwetu, *President* wa Klabu ya *Dar Young Africans, Engineer* Hersi. *(Makofi/Vigelegele)*

Ahsanteni, *Engineer* Hersi ukishasimama mara moja unakaa, husimami wakati wote. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, *Engineer* Hersi ameongozana na viongozi wakuu wa klabu hiyo Ndugu Muniri Said, Alex Ngazi, *CEO* wao Andrew Mtine na Kocha Ndugu Gamondi, ahsanteni. *(Makofi)*

Pia wameongozana na wachezaji wa Klabu ya *Young Africans*, ahsanteni na karibuni. Wachezaji kaeni, *Coach Gamondi congratulations. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mgeni mwingine wa Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro ni Mheshimiwa Hamisi Kisiwa, Mkurugenzi wa Wanachama wa Simba, ulishasimama? Simama tena, umependeza na hiyo nguo ya ndani hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro - Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, viongozi na watumishi wa Wizara, wadau wa taasisi zilizo chini ya Wizara, wadau wa sekta ya utamaduni na sanaa, Chama cha Maafisa Utamaduni Tanzania (CHAMUSATA), viongozi wa Klabu ya Pamba kutoka Jijini Mwanza, kikundi cha sanaa cha Miso Misondo na wasanii wa sanaa ya uchekeshaji. *(Makofi)*

Wageni wengine ni Ndugu John Haule - Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Ruvuma, Happiness Mpakate - Mjumbe Baraza Kuu UWT Taifa na Mjumbe wa Kamati ya Siasa Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Eric Shigongo ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na sasa ninamwita Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Kabudi, kuanza mchango wa Wizara hii. Unajua Mheshimiwa Kabudi ukikaa huko sijui kama watu wanakuona maana wewe una mambo makubwa, hebu sogea ndani kidogo huku. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahimu kwa ruzuku ya uhai na afya, pia nikushukuru sana Naibu Spika kwa kunisogeza mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kabisa kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa hotuba nzuri katika bajeti hii na pia Kamati husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo mawili ambayo ningependa kuyachangia, kwanza ni kuhusu ngoma za asili, muziki wa asili na sanaa za asili. Hili ni eneo ambalo sasa dunia ya Magharibi na Marekani wanaichukua na kuhifadhi sanaa za asili, muziki wa asili na ngomza za asili za Afrika. Kama ilivyo katika maarifa mengine ya asili, tusipokuwa waangalifu tutayapoteza na baadaye miaka ijayo watoto wetu, wajukuu wetu, vitukuu vyetu wataenda katika nchi hizo kwenda kuchukua muziki wetu wa asili na tamaduni zetu za asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nichukue nafasi hii kuiomba sana Wizara pamoja na juhudi kubwa zinazofanyika iendelee kuongeza juhudi hizo na sasa iipe Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ambao ni urithi wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, fedha ya kutosha ya kufanya mambo ya kukusanya, kuhifadhi na kutunza ngoma za asili, sanaa za asili na muziki wa asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya eneo ambalo tumepoteza ladha ya asili ya muziki ni muziki wa taarabu kwa kuhamia katika ala za vyombo vya kisasa na kuacha kutumia ala za zamani na ndiyo maana leo hii moja ya taarabu bora kuliko

zote sasa ni taarabu ya eneo la Uarabuni Burundi Bunjumbura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kusikia taarabu nzuri ya asili nenda Bunjumbura eneo la Uarabuni, bado wanatumia ala za asili ambao sisi huku tumezipoteza kwa kuanza kutumia *keyboard*. Katika mnasaba huo huo naomba sasa Wizara ianzishe matamasha ya ngoma na muziki wa asili katika mikoa yote. Katika kufanya hivyo turejeshe tena au tuanzishe mashindano ya ngoma za asili na sanaa za asili katika shule za sekondari za Tanzania na tufanye hivyo kwa kushirikiana na Wizara zote tatu za Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloji na Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujifunze kwa wenzetu Kenya, Kenya sasa matamasha hayo yamerejeshwa na matamasha hayo hayarejeshi ukabila, matamasha hayo ya ngoma za asili na muziki wa asili yanaonesha utajiri mkubwa ambao Taifa linalo na sisi tunao utajiri mkubwa wa jamii zaidi ya 120 ambazo tukizitumia na kuhamasisha vizazi vyetu vya leo, kesho na kesho kutwa vitajitambua kwamba wao ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze hatua inayochukuliwa na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni ya Bagamoyo kufungua *campus* Dodoma, jambo hili zuri sana. Tukumbuke kwamba Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipoanzisha kile chuo aliwachukua wazee watatu ambao hawakuwa na elimu darasani, lakini walikuwa mabingwa, maarufu katika eneo la muziki. Hawa walikuwa ni Dkt. Hukwe Ubi Zawose, Ndugu Chacha Matiaga Werema na Khalfani Omary Matitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Hukwe Ubi Zawose ni mtaalamu wa marimba na zeze ambaye dunia nzima inamkiri na mwaka 1998 Chuo Kikuu cha Helsinki kilimpa Shahada ya Heshima ya Udaktari. Napendekeza *campus* ya Dodoma iitwe *campus* ya Dkt. Hukwe Ubi Zawose, kwa heshima ya huyu mtu ambaye ameukuza muziki huo, lakini Ndugu Chacha Matiaga Werema alikuwa mtaalamu wa litungu na Ndugu Khalfani Omary Matitu alikuwa ni mtaalamu wa marimba ya kizaramo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii miziki yote hii tayari baadhi yake imekwishachukuliwa na Wajapani na wameiingiza katika *keyboard* ya *Yamaha* na *Casio* midundo ya ngoma. Sisi tunapuuza wengine wanaichukua na sasa wanaiuzia dunia nzima, eneo hili tusilipuuze hata kidogo, ikiwa pamoja na sanaa ya uchoraji na ufinyangaji na sanaa nyingine zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, naomba nizungumzie eneo la Kiswahili. Tanzania sisi ndiyo kinara wa Kiswahili, Kiswahili sanifu na Kiswahili fasaha, lakini tusijidanganye kwamba sisi ndiyo pekee wenye Kiswahili sanifu na Kiswahili fasaha. Pwani yote ya Kenya ni wazungumzaji wazuri wa Kiswahili sanifu na fasaha, Congo, Goma, Lubumbashi, Bunjumbura Uarabuni na Kigali kuna wazungumzaji kabisa wa asili wa Kiswahili. Sasa ili tuendelee sisi kubaki kuwa kinara wa Kiswahili tushughulikie vihatarishi vitatu ambavyo vimeanza kujitokeza na visipofanyiwa kazi tutaporomoka katika umaarufu na ukinara wa Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari nchi jirani wameanza kutumia mambo hayo kusema kwamba Tanzania sasa hawazungumzi Kiswahili sanifu na Kiswahili fasaha, kwa hiyo msipeleke wanafunzi wenu wanaofanya mazoezi ya kujifunza Kiswahili cha kusoma na kuandika Tanzania kwa sababu wao wameanza kukiharibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kihatarishi cha kwanza ni kubananga Kiswahili, hii ni pamoja na sisi Wabunge. Imezuka hulka sijui imetoka wapi ya kudondosha "ha" "huyu" amekuwa "uyu," "huyo" amekuwa "uyo," "haya" imekuwa "aya."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mingi tatizo hili lilikuwa ni la kona ya Kaskazini Magharibi ya Tanzania, lakini limehama Kaskazini Magharibi ya Tanzania limetamalaki nchi nzima na sasa linatumiwa na nchi fulani fulani kusema msipeleke watoto wenu wajifunze Kiswahili Tanzania kwa sababu sasa hawajui hata kusema "huyu" wanasema "uyu," hawasemi "hapo" wanasema "apo." Wizara tumieni redio zote za kijamii kusahihisha hilo, tusilidharau hata kidogo. Redio za kijamii, *TBC* na *ITV* zitumike kusahihisha ubanangaji wa Kiswahili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiashiria cha pili cha hatari tumeanza kufubaza Kiswahili. Maneno mengi ya matumizi ya kawaida kwa sababu ya kufikiria ngono, ngono, tumeyapa maana isiyokuwa yenyewe na matokeo yake tumeyaondoa katika matumizi ya kawaida ya Kiswahili. Badala ya matiti tunasema nyonyo, toka lini neno matiti lilikuwa neno baya, lakini kwa sababu sasa tumeanza kufikiri visivyofikirika tunaanza kuondoa maneno ya kawaida ya Kiswahili, tunaanza kufubaza Kiswahili na hapa mimi siingilii tafsida, tafsida ni muhimu lakini sidhani kuita nyonyo ni tafsida, kwa sababu toka asili neno matiti katika utamaduni wetu halikuwa neno lisilokuwa zuri, ni utamaduni wa wazungu kwa sababu wao matiti ndiyo sehemu yenye haiba zaidi, lakini sisi sehemu yenye haiba siyo matiti ni nyingine, hiyo inastahili tafsida. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sikatai kwamba lugha hubadilika na lugha huongezeka na maneno hubadilika hilo silikatai kabisa. Kwa mfano, wengi kabisa hatufahamu kwamba sisi kwa miaka mingi neno “fisadi” na nimekuja na kamusi, zamani neno “fisadi” katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu maana yake ilikuwa ni mtongozaji, mharibifu, mpotevu, muasherati, mbadhilifu, hanithi, lakini leo kwa sababu ya maendeleo ya lugha imekuja maana mpya katika neno “fisadi” yaani mfujaji wa mali, lakini ukienda kwenye kamusi na ndiyo maana sisi wengine na mimi ni mmojawapo nilipata shida sana ya kutumia neno “fisadi” kwa sababu maana ya neno “fisadi” katika Biblia Takatifu ni mtongozaji, msumbufu kwa wanawake wajane na vigoli. Leo tukubali kwamba neno hilo limepata maana mpya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa la tatu kwa maana ya kiashiria cha tatu tumeanza kudumaza lugha ya Kiswahili, tunadumaza lugha ya Kiswahili kwa sababu kubwa mbili; moja uvivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunadhani tunakifahamu sana Kiswahili, kwa hiyo, tumekuwa wavivu wa kutajirisha na kutumia msamiati ambao ni tajiri sana wa Kiswahili na ndiyo maana mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Jesca Msambatavangu alifanya

kwa mara ya kwanza hapa tubishane kuhusu lugha. Jambo lililonifurahisha kuliko yote nilipomwona Mheshimiwa Spika anatumia kamusi, tumeacha matumizi ya kamusi, tuhamasishe matumizi ya kamusi, mimi pamoja na kamusi hiyo iliyopo mezani Kamusi Kuu ya Kiswahili ambayo sina matatizo nayo kabisa ni kamusi nzuri tuongeze hapo kwenye meza yako Kamusi ya Kiswahili Sanifu ya TUKI. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili wana msemo, hakuna ziada mbaya isipokuwa kiboko au kifungo. Kwa hiyo, tuongeze na Kamusi hii. Huku kudumaza Kiswahili kumetufanya tuanze kutumia maneno yale yale katika kila jambo. Kwa hiyo, ushauri wangu mimi kwa Wizara, moja, tuhamasishe tena matumizi ya Kamusi ya Kiswahili zote mbili (Kamusi Kuu na Kamusi Sanifu) katika shule zetu zote za msingi na sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda leo Kenya moja ya vitabu ambavyo ni muhimu kwa mwanafunzi wa Kenya kuwa nacho ni Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Serikali kupitia Wizara yao ya Elimu inatoa fedha kuhakikisha kila mwanafunzi ana kamusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomba Serikali ianze kampeni ya kusambaza kamusi katika shule zote za sekondari na kuhamasisha wanafunzi wetu kutumia kamusi ili baada ya hapo tusitumie na kubananga maneno ya Kiswahili na matokeo yake kukifubaza na kukidumaza Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tumeanza kudumaza Kiswahili kwa kudhani tunafahamu Kiswahili. Kila tunapokuwa na neno jipya ushauri wangu haraka sana twende kwenye Baraza la Kiswahili la Taifa ili litupe neno la Kiswahili lililosanifishwa. Pamekuwa na mjadala mrefu sana kwamba ni neno lipi sahihi la neno *artificial intelligence*. Maana yake sasa *artificial intelligence* ndiyo lugha ya dunia nzima. Watu wanadhani *artificial intelligence* imeanza leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa *artificial intelligence* ulianza mwaka 1956, hapo ndiyo utafiti wa *machine learning* ulianza. Sasa tuharakishe sana kuuliza BAKITA na BAKITA yenyewe

pia iwe na haraka ya kusanifisha maneno hayo, kuyasambaza na kuyatangaza. Tumebishana kwa muda mrefu sana kuhusu nini tafsiri sahihi ya *artificial intelligence*. Kuna waliosema ni akili bandia, lakini kwa Mtanzania wa kawaida neno bandia maana yake *fake* na ile *artificial intelligence* siyo akili *fake,* ni akili nzuri kabisa. Wengine wakaja wakasema akili unde, lakini sasa imekubaliwa kwamba *artificial intelligence* ni akili mnemba. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabudi, malizia.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamalizia, kwa hiyo, mimi ningehamasisha kabisa sisi sote tunapokuwa tuna uhitaji wa neno sahihi la Kiswahili tuitumie BAKITA. BAKITA iwezeshwe kwa haraka sana kila linapotokea jambo jipya basi kutupa tafsiri sahihi ya lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna, ajiandae Mheshimiwa Seif Gulamali, huyu naye mwingine huko huko tena.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kuweza kuchangia mjadala huu muhimu unaohusu uhai wa Taifa letu kwa maana ya utamaduni wetu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa na mimi kusimama mbele yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana tena kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro. Mheshimiwa Waziri amefanya kazi kubwa kwa muda mfupi ambao amehamishiwa kwenye Wizara hii. Kwa kweli sisi

Wanakamati tumeona mambo mengi yanasogea mbele kwa kasi kubwa, tunamshukuru na tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma (Mwana FA). Juhudi zake, maarifa yake na uzoefu wake ambao nao katika Wizara hii kwa kweli inatutia hamasa wadau na tunaona kwamba kesho ya Wizara na sekta hii kwa ujumla ni kubwa na itavutia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa leo nitajikita kwenye Sera ya Maendeleo ya Michezo. Kwa kuanza nitumie fursa hii kumpongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na ninampongeza kwa utayari wake yeye binafsi na utayari wa Serikali yake katika kuwekeza na kuendeleza sekta ya michezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tutakubalina kwamba kwa miaka hii ya karibuni nchi yetu imekuwa na mwamko mkubwa sana kwenye masuala ya michezo. Leo nimejionea hapa pamoja na kwamba Kanuni zetu zinawazuia wageni kupiga makofi, lakini wakati wanatambulishwa Yanga niliona wanafunzi pale wamepiga makofi mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaashiria ni namna gani Serikali imewekeza katika kuendeleza michezo nchini. Hamasa ya wananchi na wadau wa michezo kwa ujumla ni kubwa na hii tumpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Wizara hii mwaka jana ilikuwa shilingi bilioni 35.4. Kwa juhudi za makusudi za Serikali na jitihada zilizofanywa na Kamati hii, bajeti ya mwaka huu imefikia shilingi bilioni 285.3. Hii ni hatua kubwa sana katika kuleta mapinduzi na maendeleo makubwa katika sekta ya michezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapinduzi haya, *willingness* hii inaonekana katika ujenzi wa viwanja vya michezo vyenye hadhi ya Kimataifa. Ukisoma Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka

1995, moja ya jambo ambalo limesisitizwa na sera ilikuwa ni nchi yetu kujenga viwanja vya michezo vitakavyoruhusu kuchezwa michezo ya Kimataifa nchini, viwanja vyenye hadhi ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni katika Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunaenda kushuhudia vinajengwa viwanja vikubwa viwili kwa mpigo. Hii ni hatua kubwa, ni *willingness* kubwa na ni utayari mkubwa wa Serikali yetu katika kuwekeza katika michezo. Nipongeze sana hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali iendelee kuweka jitihada katika mpango huu, viwanja hivi vikamilike kwa muda uliopangwa. Fedha zitoke na utekelezaji ufanyike ili wananchi waweze kunufaika na maono na *willingness* hii ambayo ameionesha kiongozi wetu namba moja Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiisoma sera ya mwaka 1995 inaeleza moja ya jambo ambalo limepewa mkazo ni ujenzi wa vyuo vya michezo kwa lengo la kutengeneza wataalamu (wanataaluma) wa michezo. Hapa wanakusudiwa walimu, makocha, waamuzi na watawala wa sekta ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kwa mara ya kwanza katika nchi yetu tumeona fedha nyingi zimepelekwa katika kujenga na kuimarisha *academia* mbalimbali ikiwemo Chuo cha Michezo cha Malya. Hili ni jambo la makusudi, ni *willingness,* ni utayari wa kisiasa, ni utayari wa Serikali na ni utayari wa nchi katika kuinua jambo hili la sekta ya michezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shauku yetu kama Kamati na shauku yangu mimi kama Mheshimiwa Mbunge, ninatamani kuona utekelezaji unaendana na mipango ambayo imewekwa. Mambo haya ambayo yamewekwa kwenye utaratibu yatekelezwe kwa muda ambao umepangwa ili tija na yale ambayo yanatarajiwa kufanyika yaweze kupatikana ndani ya muda huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe utakuwa ni shahidi. tumeshuhudia waamuzi mbalimbali katika nchi yetu wengi hawapati hadhi ya kwenda kuchezesha michezo ya Kimataifa. Ni kwa sababu gani? Kwa sababu ya kukosa utaalamu katika nafasi hizo. Sasa kama tukiwekeza katika ujenzi wa vyuo vya michezo, taaluma ya michezo ikathaminiwa kama taaluma nyingine tutakuwa tumeimarisha eneo hilo na mwisho wa siku tutakuwa tumeliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limesisitizwa kwenye sera ya mwaka 1995 ni kuwepo kwa viwanda vya kuzalisha vifaa vya michezo nchini ili kupunguza gharama ya kuagiza vifaa hivyo kutoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali za kujenga viwanja na *academia* za michezo, lakini bado tunavyozungumza sasa hakuna kifaa cha michezo kinachotengenezwa nchini. Hili jambo litaturudisha nyuma. Azma ya Serikali ya kukuza michezo nchini itakuwa haina kasi ya kutosha tuweke jitihada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naizungumzia Wizara ya Viwanda na Biashara; katika sera hii ya michezo imezungumza Wizara mbalimbali ambazo zinaguswa moja kwa moja katika utekelezaji wa sera. Wizara ya kwanza, ni Viwanda na Baishara. Wizara hii imetajwa mahususi katika kuanzisha viwanda vitakavyotengeneza malighafi na vifaa mbalimbali vya michezo kwa lengo la kukuza sekta ya michezo nchini. Kwa hiyo, hili liwekwe katika vipaumbele vya Serikali ili kuendeleza kukuza sekta hii ya michezo na iende sambamba Mheshimiwa Waziri pamoja na sheria ile ya mwaka 1962 ambayo imezitaja Wizara mbalimbali ambazo zina-*accompany* utekelezaji wa sera hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutenga fedha katika Wizara ya Afya kwa ajili ya michezo inayosaidia kupunguza magonjwa yasiyoambukiza, Wizara ya TAMISEMI kwa maana ya kuwafundisha watoto waliopo shuleni masuala ya michezo na Wizara ya Vijana, kwa ajili ya kupeleka shughuli za michezo kwenye ngazi hizo pia. Kwa hiyo, Wizara zote ambazo zinahusika

katika utekelezaji wa sera hii ziweze kuamka na kuona tija na haja ya kwenda kuweka fedha za kutosha ili ziweze kutekeleza sera hii kama ambavyo inatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuweka fedha kwa ajili ya kuwakopesha wasanii wetu chini. Kamati yetu ilitembelea wasanii katika maeneo mbalimbali na ilisikia vilio vyao. Fedha ambayo imetengwa imewainua wasanii wengi kutoka hali moja ya uchumi kwenda hali nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali iendelee kutenga na kuongeza fedha hizi. Hizi fedha zinakwenda kupunguza hata ile hali ya watu kutengeneza kiki. Badala ya kwenda kutengeneza kiki ili apate fedha, kwa sababu ana mkopo wa Serikali wa Mama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hasan, anaweza kwenda kufanya kitu ambacho kinaweza kikazalisha na mwisho wa siku akaitengeneza saana yake vizuri. Kuliko kuingia kwenye mambo ambayo pengine yanaweza yakakiuka maadili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme moja kuhusiana na sera. Sera yetu pamoja na mambo mazuri ambayo inayo, haitambui suala la ajira na biashara kama sehemu ya shughuli ambazo zinapaswa kuwepo kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Husna.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nihitimishe kwa kuunga mkono hoja na niiombe Serikali sasa ifanye marekebisho ya sera ili kuingizwa suala la biashara na ajira kuwa sehemu katika shughuli za michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni viongozi wa Umoja wa Machifu Tanzania, wasanii wote walio chini ya Wizara, mtangazaji wa *Wasafi Media Groups TV*, Ndugu Claton Chipando (Baba Levo) na Mtangazaji wa *Clouds Media Groups TV,* Ndugu Mwemba Burton (Mwijaku), karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 112 wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni wanafunzi na walimu kutoka Chuo cha Ufundi *(Dodoma Vocational Training Center),* karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa ninamwita Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali ambaye ni Kiongozi Mkuu wa Klabu ya Yanga ambaye tunaye humu ndani. Mheshimiwa mchango wako ujikite kwenye hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi na mimi kuwa sehemu ya wachangiaji katika hotuba hii ya Wizara ya Michezo na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kutoa shukurani za pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amekuwa mdau namba moja kwenye masuala mazima ya michezo, ameonesha nia ya dhati na hili limeonekana ndani ya muda mfupi tu ambapo tumeweza kupeleka timu yetu ya Taifa *(Taifa Stars)* kwenye Mashindano ya *AFCON* kule Ivory Coast. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, ni mwanamichezo namba moja Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa fedha za hamasa kwenye vilabu vyetu vya Simba na Yanga. Tumeona vilivyofanya vizuri katika mashindano makubwa kabisa Barani Afrika. Tumeshuhudia mwaka jana timu yetu ya *Young Africans*

ikicheza Fainali ya Kombe la *Confederation,* jambo ambalo halikuwahi kutokea katika *records* za Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia mwaka huu kwa *records* za Tanzania tumeingiza timu mbili *quarter final* kwa maana ya Simba na Yanga. Hizi zote ni juhudi za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa fedha nyingi ambazo alikuwa akizitoa kama hamasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ushawishi wake ndani ya Marais wa Afrika na Shirikisho kwa kuweza kupewa kuandaa Mashindano ya Afrika mwaka 2027 yatafanyika Tanzania kwa kushirikiana na chini jirani kwa maana ya Kenya na Uganda kwa mara ya kwanza toka tupate Uhuru. Pongezi nyingi sana kwa Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hakika anaupiga mwingi kwenye upande wa michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona dhamira yake ya dhati kwenye ujenzi wa viwanja vipya vya kisasa. Tunaona kule Arusha, Zanzibar, lakini na uboreshwaji mkubwa ndani ya kiwanja kikubwa cha Dar es Salaam. *(Makofi)*

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE**: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Nani anataka Taarifa? Mheshimiwa Catherine.

## TAARIFA

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpe Taarifa mchangiaji anayechangia sasa hivi. Nimkumbushe kuwa timu ya *Young Africans* imeshashinda mara 30 Tanzania. Pia imeingia fainali ya *FA,* Zanzibar, Jumapili. Kwa hiyo, nimkumbushe Yanga haina mpinzani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Gulamali, ukiipokea hiyo Taarifa unaipokea kwa kigezo kipi?

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipokea Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Haya.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa sababu ametukumbusha kwamba wamechukua ubingwa mara 30, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kwa sababu wewe pia ni Mheshimiwa Mbunge ambako Klabu ya Yanga inatokea, tunakukaribisha siku ya Jumamosi tutakapokuwa tunakabidhiwa Kombe letu la Ligi Kuu ya Tanzania la *NBC,* karibu sana Dar es Salaam Uwanja wa Taifa. Tunategemea uwepo wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo nilitaka nizungumze jambo lingine. Hivi vilabu vikubwa na vidogo bado hatujaviwezesha kwa ajili ya kuweza kuhimili katika kujiendesha vyenyewe. Hili ninapenda…

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. COSATO D. CHUMI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Gulamali kwamba kutokana na ushawishi wa Mheshimiwa Rais kupitia *Sports Diplomacy,* mashindano ya kwanza ya Vilabu Afrika ya *Big Eight* ambayo kwa Tanzania ilishiriki Simba pekee. Uzinduzi wake ulifanyika hapa Tanzania ambapo ulihudhuriwa na Rais wa *FIFA* na viongozi wakubwa wa mpira duniani. *(Makofi/Vigelegele)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima yako Taarifa hiyo ipo nje ya mada hii inayozungumzwa. Hivi vilabu vikubwa vya Simba na Yanga vinajiendesha kwa gharama kubwa sana. Nimwombe sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Damas na Naibu Waziri Mheshimiwa Hamis (Mwana FA) mbebe hii ajenda. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo vinaletewa kodi ya miaka mitano yaani wanafanyiwa *auditing* ya miaka mitano. Ukikuta kwenye gharama ambazo wanaletewa leo, hivi vilabu vinadaiwa kodi kubwa sana. Simba wanaweza kuwa wanadaiwa labda shilingi bilioni saba na Yanga shilingi bilioni labda saba au sita. Hizi ni gharama kubwa sana na ni kodi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Wizara na siku ya Wizara ya Fedha, tutashika shilingi. Hizi kodi zifutwe na zitawarahisishia hivi vilabu kuweza kujiendesha. Kama vilabu hivi leo kwenye upande wa michezo vijana wengi ambao hawakusoma wapo kwenye michezo na ndiyo sehemu yao ya ajira. Wale vijana waliosoma ambao hawajapata ajira Serikalini wapo kwenye michezo. Kwa hiyo, hii *industry* inabeba vijana wengi sana ambao hawana ajira kwenye mfumo rasmi, lakini ndiko ambako wanapata fedha na kuendesha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijaonesha nia ya dhati ya kuvisaidia au kuisaidia sekta hii ya michezo hasa kutoa *incentives* na kupunguza baadhi ya kodi ili kuweza kuvisaidia vilabu kuweza kuhimili kuajiri hawa vijana na tutapunguza vibaka wengi mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi kama Marekani wanatoa fedha nyingi sana kuisaidia kuanzisha michezo mingi kuwa-*keep* vijana kuwa *busy*. Utaanzisha mchezo huu, mchezo huu yaani kila siku wanaanzisha michezo. Kwa nini? Kwa sababu ya kusaidia vijana wasiharibiwe na masuala ya mihadarati, wasiingie kwenye mambo ya ubakaji na wasiingie kwenye mambo ambayo ni maovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata *stability* ya nchi inaimarishwa zaidi kwenye michezo. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri mwondoe kodi kwenye masuala ya michezo, wekeni *incentives* hivi vilabu viweze kupambana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hata mkatangaza utalii kupitia taasisi zenu mkasema Ligi Kuu ya Tanzania, bingwa atapata shilingi bilioni tano kutoka katika mashirika yenu. Mkatenga shilingi bilioni kumi kutoka Serikalini ambazo zikapitia kwenye hiyo sekta ikaenda ku-*invest* kwenye michezo, bingwa wa Tanzania akachukua shilingi bilioni tano, nafasi ya pili akachukua shilingi bilioni tatu, nafasi ya tatu akachukua shilingi bilioni mbili na wengineo wakapata hela. Hizo fedha zinazisaidia vilabu vyetu kusajili wachezaji imara, kulipa mishahara bora, lakini pia itasaidia Taifa letu kutangazika ndani ya Afrika na duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaona mataifa makubwa kama Nigeria, Brazil na Cameroon yametangazwa kwa sababu ya michezo. Kwa hiyo, ni lazima tuwekeze huko na Serikali iwe na nia ya utayari ili tuweze kupata watalii wengi. Tunaona Rwanda wanakwenda kutangaza Uingereza, wameweka fedha nyingi kwenye timu ya *PSG*. Nini *impact* kutangaza nchi yao? Wanapata watalii kwenye Rwanda. Sisi vilabu vyetu vya Simba na Yanga vinacheza mashindano makubwa, lakini hawaja-*invest* mapema. Kama wange-*invest* hivi vilabu vingeweza kufika fainali, vingeweza kuchukua ubingwa na vinaweza kuitangaza hii nchi na hivyo watalii wanaokuja kuongezeka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikwambie mfano mdogo, timu ya Taifa ya Tanzania walipokuwa wanacheza kule Ivory Coast walipokuwa wakiimba ule Wimbo wa Taifa la Tanzania na siku hiyo kulikuwa kuna mechi kati ya Zambia na Tanzania, watu wakajua kumbe tuna wimbo unaofanana na Tanzania. Hata wa Afrika Kusini walijua, lakini zaidi ya miaka 60 watu walikuwa hawajui kuwa Wimbo wa Taifa la Tanzania unafanana na nchi gani, lakini leo wimbo wetu umefahamika kwenye nchi nyingi kwamba Tanzania, Zambia pamoja na *South Africa* wana wimbo unaofanana, hii ni kwa kupitia michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuwekeze kwenye michezo, tukifanya hili tutaweza kulisaidia Taifa letu kupata watalii wengi, watalii hawa watakwenda kukaa kwenye hoteli hizo, watu watawekeza kwenye hoteli na uchumi wa nchi yetu utakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia mfano mdogo, kutokana na hii ligi kuu leo kuna vibanda umiza vingi mtaani, tayari kuna ajira pale, wenye nyumba wanapangisha nyumba zao kwa ajili ya watu kwenda kuangalia mpira, jezi zinauzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali isamehe kwanza hizi kodi, iweke *incentives* kwenye vilabu vyetu ili kuhakikisha kwamba inainua uchumi wa vilabu vyetu ambavyo ndivyo vichochezi vya ajira kwa vijana wetu ambao wanaanzia miaka 12, 13, 20 na 30 ambalo ndilo kundi kubwa la Watanzania…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Gulamali, muda wako umekwisha.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, usisahau mwaliko wa tarehe 25 Mei pale Dar es salaam, Uwanja wa Taifa, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi, ajiandae Mheshimiwa Malleko na ajiandae Mheshimiwa Festo.

**MHE. CASATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya michezo ambalo ni jambo muhimu. Mimi ukiacha pongezi nitazungumzia mambo matatu; nitazungumzia mpira wa miguu, *media and entertainment industry* na pia nitazungumzia mchezo wa riadha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza na mimi napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo amekuwa anatuongoza katika kuleta hamasa kubwa kwenye michezo. Kama alivyosema Mheshimiwa Gulamali

kwamba ile hamasa ya kuchangia timu zikipata magoli na kununua magoli imeleta hamasa kubwa. Yeye ni mwanadiplomasia namba moja na sisi tunafanya diplomasia ya uchumi. Siku ya mambo ya nje nitalieleza hili zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kinaitwa *sport diplomacy* ndicho ambacho Mheshimiwa Rais amekifanya. Kwanza kwa kuweka mazingira bora katika michezo na kwa kuwa *champion* wa kuhakikisha kwamba *AFCON 2027* inachezwa hapa. Kama nilivyosema hapa wakati nampa taarifa Mheshimiwa Gulamali kwamba ile *African League,* michezo mikubwa ambayo walikuwa wanashirikisha *super eight* na ambayo Simba ilishiriki uzinduzi wake ulifanyika hapa Tanzania, ile yote ni hamasa ambayo Mheshimiwa Rais ameijenga kwa kushirikiana na wasaidizi wake. Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, mtani wangu kutoka Songea, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma (Mwana FA), Katibu Mkuu Bwana Msigwa ambaye nimewahi kufanya naye kazi siku za nyuma na Naibu Katibu Mkuu Bwana Suleiman Serera, kijana kabisa na mchapakazi, wote hawa wanamsaidia Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kwamba mambo haya yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitapongeza vilabu vya Simba na Yanga kwa kushiriki kwenda robo fainali katika Klabu Bingwa Afrika. Pia wachambuzi wa michezo na wasemaji wa vilabu vyetu wamekuwa wakileta hamasa kubwa, pamoja na wachezaji na mashabiki kwa kutazama na kufuatilia mchezo mpira wa miguu viwanjani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nawapongeza *Azam TV* kwa kuonesha michezo ya ligi kuu, michezo ya *FA* na kwa kuonesha ligi ya Kenya ambayo nayo imeanza kuleta hamasa. Juzi hapa *derby* ya wenzetu maarufu kama *derby* ya mashemeji *FC Leopard* na Gor Mahiya ilikuwa na hamasa kubwa kama sehemu ya hamasa ambayo imeletwa na *Azam Tv. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nitumie nafasi hii kuwapongeza *CRDB* kwa kuthubutu na kufadhili Kombe la *FA* na

hapa nitoe wito kwa benki nyingine. Ninafahamu *NBC* wanadhamini ligi kuu, *CRDB* wamekuja kwenye *FA,* niwaombe *TFF* wawashawishi pia *NMB* waje kudhamini kwenye kitu kilichokuwa kinaitwa Kombe la Taifa ambalo timu za mikoa zilikuwa zinashiriki kama sehemu ya kuleta hamasa na kuendelea kukuza mchezo wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze uwekezaji mkubwa uliofanywa kwenye viwanja. Sasa hivi tuna takribani viwanja vitano ambavyo mpira unaweza kuchezwa usiku. Niwaombe *TFF* na Bodi ya Ligi pamoja na pongezi hizi, kwa sababu sasa tuna viwanja ambavyo timu zinaweza kucheza usiku, basi watengeneze ratiba ambayo itapunguza timu kucheza saa nane mchana. Kwa hali yetu ya hewa kwa kweli kucheza saa nane mchana kwa nchi ya *tropical* kidogo inaleta shida. Uingereza na Ulaya wanaweza kucheza mchana kwa sababu ya hali ya hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema pongezi hizo sasa nataka nitoe ushauri. Mchezo wa mpira umekuwa na hamasa kubwa sana na umekuwa na mchango mkubwa sana katika uchumi wetu na kwa sababu hiyo basi, tunayo kila sababu ya kutokuchukulia kikawaida kawaida. Siku ambayo Simba na Yanga wanacheza watu wanatoka Bujumbura, Kigali na Mombasa, vilevile watu kutoka mikoa mbalimbali wanasafiri kwenda kushuhudia mpira pale uwanja wa Taifa. Watu hawa watasafiri, watapanda magari. Maana yake ni kwamba magari yatajaza mafuta na kwa sababu hiyo Serikali itapata *fuel levy,* lakini kule wanakokwenda mama ntilie, vibanda umiza kama tulivyosema kina *Ujugu Arena* watanufaika. Ni mambo ambayo kwa kweli ni uchumi mkubwa. Kwa hiyo, kama huu ni uchumi mkubwa ni lazima tuwe na misingi imara ya kuusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa ushauri wangu, soka letu linaendelea kupiga hatua na uwekezaji unakuja. Mimi ningeshauri kwa sababu mambo mengi tunajifunza kutoka Ligi Kuu ya Uingereza basi katika huu uwekezaji Serikali iwe na utaratibu au kuwe na kitu kama *regulatory authority* ambayo itakuwa inaratibu uwekezaji na kuwe na mwendelezo wa namna

ya uwekezaji. Pia Serikali itupatie taarifa katika muktadha mzima wa mambo ya uwekezaji, kwamba utaratibu ukoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Uingereza huwezi kukuta mtu mmoja au kampuni moja inaweza kumiliki timu mbili kwa sababu itaondoa ule ushindani. Kwa hiyo, mimi rai yangu hapa niiombe Serikali isikae mbali katika masuala ya uwekezaji, ihakikishe kwamba kunakuwa na utaratibu ambao upo *very clear* kwa sababu huu ni mchezo ambao una mvuto na ambao ni uchumi na pia ni mchezo ambao unatushikamanisha. Kwa hiyo, hilo ni jambo la muhimu sana kwenye uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani, kwamba leo hii unaona tu kwamba Gwambina mara imegeuka kuwa *Mufindi United,* mara imegeuka kuwa labda *Kilolo United.* Hapana, pawe na utaratibu mzuri. Hii ni kwa nia njema kabisa kusudi mchezo huu uendelee kuwa na uchumi na kuchangia vipato vya mtu mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ninaona ni muhimu sana kuwekeza ni katika sekta ya uamuzi. Amezungumza vizuri hapa mama yangu Mheshimiwa Sekiboko kwamba waamuzi wetu ni binadamu, kweli wanakosea. Kwa hiyo, ipo sababu ya kuwajengea uwezo ili waweze kwenda kushiriki pia kuchezesha hizo mechi nyingine za kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata kwenye mechi za hapa nyumbani kuna kitu mimi nimekiona hivi karibuni ambacho ukiangalia zaidi inawezekana tu ni mwamuzi kutokuwa eneo la tukio wakati mchezo unaendelea na hii ni *physical fitness* tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja nilimwona yule dada ambaye huwa anachezesha mechi kubwa pale Karume saa saba mchana anafanya *jogging,* anatengeneza *fitness* yake. Sasa ndiyo matokeo yake unakuta kadi nyekundu mechi ya Yanga na Coastal mara imekuja kufutwa. Goli la Maxi Nzengeli kati ya Yanga na Ihefu *infact* halikuwa goli, goli la *Tabora United* na Simba lilikuwa goli. Kwa hiyo, unakuta kitu ambacho

kinajitokeza ni kuwa goli sio goli na sio goli ni goli. Sijui kama mmenielewa hapo, yaani ambapo ni goli si goli, ambapo si goli ni goli. Sasa hii kidogo inavunja hamasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni kuhusu *media and entertainment*. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumchagua mtu ambaye ni wa burudani na sanaa, Mwana FA. Ukiangalia katika *media and entertainment* kulingana na *PWC* kufikia mwaka 2023 mapato ya *media and entertainment industry* yatafikia *1.2 billion*, kama trilioni tatu na kitu hivi, lakini je, kipi kinakwenda kwa wasanii? Tumeambiwa kuhusu mambo ya mirabaha, lakini vipo vitu kama hizi *gadgets*, yaani kwenye *media and entertainment industry* unapata hela kwa kutumia *app* na kwa ku-*download*. Sasa tukitumia hivi vitu je, kuna *percent* inakwenda kwa wasanii? Kwa hiyo tuweke utaratibu ambao utawezesha kwenye hizi *gadgets,* iwe *flash disk*, iwe simu hizi za *android* ama iwe sijui ni *laptop, a certain percent* itengwe iende *COSOTA* ili kama nilivyosoma jana kwenye Mwanaspoti, Mama yake Ngwea kuna ka-*percentage* anakapata pale. Kwa hiyo, hii itasaidia kukuza muziki wetu, sanaa yetu na kukuza na taaluma hii ya *media and entertainment industry. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho kabisa nilisema nitasema kuhusu mchezo wa riadha. Ninashauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii tuwekeze kwa akina Simbu na wenzao. Kwa mfano mbio kama *Boston Marathon, New York Marathon* na *London Marathon* nilishawahi kusema hapa, yaani *while on road,* wakati wale wanariadha wanakimbia kuna zaidi ya watazamaji milioni mbili wanatazama. Sasa *imagine* una wanariadha watatu ama wanne wanashiriki *Boston Marathon* wamevaa hapa imeandikwa Tanzania, unakuwa umeshatangaza nchi yako kwa kiwango na umevutia watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii uwekezaji wake si mkubwa sana, utawekeza kwa mwanariadha, kwa kocha wake, kwa kocha wake wa viungo, kwa mtu wake wa lishe na kwa mtu mmoja wa *sport psychology*. Baadaye na sisi tunakuwa kama wenzetu Wahabeshi, Eritrea na Kenya. Niwaombe *TTB*, *TANAPA* na Ngorongoro shirikianeni na Wizara ya Michezo ili tuwekeze pia

katika huo mchezo wa riadha na kupitia mchezo ule tutavutia watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameshaonesha dira na mwitikio mkubwa katika masuala ya michezo basi tushirikiane wote na kuwa kitu kimoja na mwisho wa siku wote kwa pamoja tutainua Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na Mwenyezi Mungu atubariki sote, abariki sekta ya michezo, utamaduni na sanaa, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Malleko, ajiandae Mheshimiwa Sanga.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana ambayo ndiyo inakonga nyoyo za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu mpedwa Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amekuwa ndiye mwanamichezo namba moja, ameweza kuiboresha sekta hii ya michezo, ameongeza bajeti na ameweka msukumo mkubwa sana, ndiyo maana hadi sasa mnaona namna sekta hii ya michezo inafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nikiacha kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu pamoja na watu wote kwenye Wizara hii kwa namna ambavyo wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo nitaanza hoja yangu kwa kuangalia katika michezo ya kubashiri *(sport betting)*. Tulipitisha katika Sheria ya Fedha hapa mwaka 2020 kwamba Wizara hii ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ipatiwe asilimia tano ya yale mapato yanayotokana na michezo hii ya kubashiri, lakini mpaka sasa fedha hiyo inatolewa kwa kusuasua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mwanakamati na tunajua kazi kubwa ambayo inafanywa na Wizara hii, tunashauri Serikali itafute namna ya kuitoa fedha hiyo kwa wakati, ikibidi tuibadilishe sheria hiyo ili fedha hizo ziwe zinaletwa kila tarehe 15 ya mwezi unaofuata na ije kwa mtiririko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hii inakwenda kwenye maendeleo ya michezo. Tunajua fedha hii inakwenda kuwasaidia wachezaji wetu wa Timu ya Taifa ya miguu ya wanaume. Jukumu la kutunza timu hii linahitaji gharama kubwa sana. Sasa kama hii fedha haitatolewa kwa wakati jukumu lile la msingi haliwezi kutimizwa vizuri. Kwa hiyo, tunashauri fedha hii iletwe kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kuligusia siku hii ya leo, wote tunajua kuwa Rais wetu mpendwa, Mama Samia Suluhu Hassan ndiye mwanamichezo wa kwanza Tanzania na amesukuma sana ajenda hiyo. Tumemsikia pia Mheshimiwa Waziri wakati anasoma taarifa yake ya bajeti hapa, amekuja na *slogan* ya kwamba tutakwenda kwenye Kombe la Dunia na *slogan* tutakayokwenda nayo itakuwa ni twende *World Cup 2030* pamoja na Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linaanza kufanyiwa kazi sasa na litakwenda kwa miaka sita. Tukianza kwa kipindi hiki cha mwaka 2024 mpaka 2030 tutakuwa tumefanya jambo kubwa sana na tutakuwa tumejiandaa vizuri. Tunajua jambo hili likikamilika na likaenda kwa namna tunavyotaka itakuwa ni *royal tour* nyingine, maana jambo hili litakwenda kuitangaza Tanzania, lakini si tu kuitangaza Tanzania bali pia litawapa vijana wetu ajira, kwa maana wachezaji wetu wakishakwenda kucheza katika timu hizo huko juu kwenye kombe la dunia hawawezi kurudi kama walivyokuwa. Ina maana watapanda viwango na wataajiriwa nje ya nchi. Hatuwezi kufanya hili jambo kama tusipokuwa na fedha ya kutosha. Tunashauri fedha ya kutosha itengwe ili tuweze kuwakilisha jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limesemwa na Mheshimiwa Waziri hapo ni namna ya kukibidhaisha Kiswahili. Ninamshukuru Mheshimiwa Palamagamba amesemea namna ambavyo sisi Tanzania tunapaswa kuliweka hili jambo vizuri. Nashukuru Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wametenga vituo 100 na kazi hii watawapa *diaspora.* Hili ni jambo kubwa sana la kujivunia kwa sababu tunakwenda kukibidhaisha Kiswahili na kitakwenda duniani kote. Basi nilikuwa ninashauri tuweze kutenga fedha kwa ajili ya kuwapa mafunzo wale watu wa *diaspora* ili waweze kutoa mafunzo katika hizo nchi 100 au katika hivyo vituo 100 ambavyo vimetengwa kwa ajili ya kufundisha Kiswahili. Hili litatuwezesha zaidi kuwapa ajira ndugu zetu hawa wa *diaspora* na kuendelea kukibidhaisha Kiswahili chetu huko duniani na hatimaye Kiswahili hiki kiweze kutumika kama lugha maalumu katika Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninapenda kuwapongeza sana Mama Ongea na Mwanao. Wasanii hawa wakiongozwa na Mwenyekiti wao Steve Nyerere, Katibu wao Monalisa pamoja na wanachama wote wamefanya kazi kubwa sana kwa kuwafikia Watanzania. Tumeona wamekuja na viatu vya Mama Samia (Mama Samia Nivishe Kiatu). Wamewafikia watoto ambao hawana fedha au wazazi wao hawana fedha ya kuwanunulia wanafunzi hao viatu vya shule. Hili ni jambo kubwa sana la kujivunia. Si hivyo tu, wamekuja pia na baiskeli ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan. Jamani baiskeli hii inakwenda kuwasaidia wale watoto wenye ulemavu ili nao waweze kwenda shuleni bila usumbufu wowote. Tunapongeza sana kampeni hii nzuri na hawa wasanii wa Mama Ongea na Mwanao kwa namna ambavyo wanajituma na kufanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri Wizara itafute namna ili katika ile mikopo ya wasanii watu hawa waweze kupewa fedha ili iweze kuwasaidia kufanya majukumu yao. Tunawashukuru pia *COSOTA*. Tumeona ni namna gani wameweza kuzilinda kazi za wasanii na ubunifu wa kazi hizo. Wameweza kukusanya na zaidi kugawa mirabaha kwa wasanii hawa. Hata hivyo bado wasanii wanateseka. Bado kuna *smartphone* na *computer* ambazo

zinatumika kufanya kazi hizo na hawa watu wanaotumia hawalipi kodi na hawalipi ushuru wowote. Basi tunashauri *smartphone* na *computer* nazo kulipiwa ushuru ili hizo fedha ziende kwenye ule mfuko na kuwasaidia hawa wasanii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kulisemea siku ya leo ni kuhusu kuongeza bajeti, maana bajeti ya mwaka huu pia inatasaidia kuongeza au kumalizia ujenzi wa viwanja vyetu vya mipira na kwamba inakwenda kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ongezeko kubwa sana kwenye bajeti hii, lakini itaenda kufanya matumizi yake ya kawaida. Tuna mashindano ya *CHAN*, haya mashindano ya *CHAN* ni ile *AFCON* inayochezwa na wachezaji wa ndani. Wakipata fedha wakawasaidia wachezaji wa ndani, wanaweza kwenda kukuza kiwango chao cha uchezaji na kuwa-*promote* wachezaji wetu wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona hapa ndugu zetu Yanga wakishangiliwa, lakini wakumbuke kwamba Simba ndiyo Taifa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Tanzania, Uganda na Kenya ndiyo wenyeji katika Mashindano ya *AFCON*. Kwa hiyo, fedha hizo hazitoshi kuandaa *CHAN*, tunaomba waongezewe fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, mimi nilibahatika kwenda Ivory Coast kwenye mashindano ya *AFCON*. Tuliona namna gani yale mashindano yaliandaliwa vizuri na sisi tunahamasisha na tunashauri Serikali iweze kuongeza fedha katika bajeti inayokuja ili yale mashindano yaweze kuandaliwa vizuri. Tuliona hamasa ilikuwa ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hamasa tu, walikuwa wanaimba wimbo wa kuitambulisha nchi yao na sisi tuweze kufanya maandalizi haya mapema, tukifanya hivyo hamasa hii itatujengea... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther ahsante, ni kengele ya pili hiyo.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja kwa 100%. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo. Mheshimiwa Sima, ujiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye bajeti ya Michezo Fungu Namba 96. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ninaipongeza Serikali na Mheshimiwa Rais kwa *transformation* kubwa ambayo anaifanya kwenye sekta ya michezo na sekta mbalimbali. Wewe ni shahidi kwamba leo tunavyozungumza bajeti yetu ya Wizara ya Michezo ime-*raise up* kutoka shilingi bilioni 34 hadi shilingi bilioni 285, haijawahi tutokea kwenye nchi yetu. Hii ni kazi njema ambayo imefanywa na Wizara na Mheshimiwa Rais, hii ni *alert,* ni *green light* kwamba tuna makusudi ya dhati kuhakikisha kwamba michezo inaendelea nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mambo machache ya kuzungumza na la kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, *you guys* mnafanya kazi nzuri sana ambayo sisi kama wafuasi na wadau wa michezo nchini tunapongeza kile ambacho mnakifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina pongezi za kipekee kwa watu wa BASATA na Dkt. Mapana. Dkt. Mapana popote pale alipo, mimi ninaku-*salute* kwa sababu umetuliza kelele za wasanii na Serikali, kelele za wasanii na Wizara na kelele za mambo mengi sana. Kwa kweli umetumia akili nyingi sana za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuifanya BASATA ionekane ni sehemu ya kukimbiliwa na wasanii na ni sehemu salama kabisa kwenye kazi za wasanii. Hongera Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Dkt.

Mapana, hongereni sana kwa kazi ambayo mmeifanya kwa sababu kwa kweli kabla ya Wizara hii kuwa hivi nakumbuka kulikuwepo na kelele nyingi sana BASATA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwenye pongezi, ninawapongeza *Dar Young African,* ninawapongeza kwa ubingwa hata kama wametoka. Sisi ni *Simba Sports Club* lazima tu-*appreciate* kwa kile ambacho wamekipata, mashindano yoyote lazima yawe na mshindi. Kwenye mizani wanasema mashindano hukomesha ushindi, kwa hiyo, niseme wazi kwamba ninawapongeza sana *Dar Young African*, lakini pia nampongeza *Engineer* Hersi kwa kazi nzuri aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa mpira kuna kitu cha kujifunza kwa *Engineer* Hersi. Kuna kitu ambacho najifunza, kwenye mpira mojawapo ya kitu kikubwa ni *communication*. Anajitahidi sana kwenye hilo jambo kwamba *organization* yake inajitahidi kufanya vizuri kwenye *communication*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu uko kwenye mambo matatu na jambo la kwanza, Mheshimiwa Waziri, sisi kama nchi tunakwenda kwenye *AFCON*. Nakupongeza, bajeti ya mwaka huu ninaona kabisa mmekusudia, karibu shilingi bilioni 250 zinaenda kwenye maendeleo. Huu ni mkakati wa wazi kwamba mnaenda kujenga viwanja na *facilities* kwa ajili ya kufanikisha *AFCON*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ushauri wangu ni ule ule, *we have that room* ya sisi kama Wizara kukaa na Wizara zingine. Mheshimiwa Waziri tuna kitu kinaitwa *CSR (Cooperate Social Responsibility)*. Tuna makampuni na tuna migodi katika nchi hii inachota dhahabu, inachota *tanzanite,* almasi na inachota vitu vingi kwenye Taifa letu. Mheshimiwa Waziri, tukiamua kuitumia vizuri ile migodi kwenye *CSR* tu, Mheshimiwa Waziri unapata fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarudia tena mfano wangu, Zambia wakati wa Rais Kaunda, aliamua kuchukua *cooper belt*

na migodi yote ambayo inahusika na *cooper belt*, *CSR* yake yote ilielekezwa kwenye viwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umesikia kelele nyingi za Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba *CSR* hazifanyi vizuri kwenye halmashauri zetu, *CSR* zinapigwa. Mheshimiwa Waziri hiyo ni *room* nzuri sana ya kumshauri Mheshimiwa Rais. Ni *room* nzuri sana ya kuongea na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, *at least*, hata tukipata *50 percent* ya *CSR*, tukaielekeza kwa makusudi kabisa kwenye kujenga miundombinu ya kusababisha *AFCON* iweze kuchezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisubiri sana fedha za Serikali ambayo muda mwingine kwa sababu ni *cash budget*, inategemeana na makusanyo, Mheshimiwa Waziri tutakwama.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Nakushauri *CSR* ni sehemu nzuri sana ya kupata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, tuna magawio mengi ambayo tunayapata kutoka kwenye mashirika mbalimbali kutokana na mapato tunayoyapata...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, kuna Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Sanga, pamoja na mchango wake mzuri na ninaungana na yeye, hata sisi Kamati ya TAMISEMI, kuna baadhi ya halmashauri zimetenga fedha za *own source* kwa ajili ujenzi wa viwanja. Kwa hiyo, nakubaliana na wewe na tunazo *source* nyingi ambazo zinaweza zikatumika kwa ajili ya kujenga viwanja kwa ajili ya *AFCON*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninakubaliana na dada yangu, *CSR* ni hela ambayo iko *clear*, unaipata vizuri. Ni ushauri tu kwa Mheshimiwa Rais na mamlaka ili muweze kupata hiyo fedha hata *50 percent* tu inawatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemshauri Mheshimiwa Waziri kwenye suala la gawio. Magawio huwa yanatolewa mengi sana kwenye mashirika mbalimbali. Tuombe hata *50 percent* ya magawio, yanaweza yakatusaidia, tutamuumiza sana Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndugu Gerson Msigwa akiwa anasugua kichwa kila siku atapata wapi fedha. Hii fedha hii iko *straight* mzee, unaipata moja kwa moja, fedha ya gawio na *CSR,* lakini *betting* nimeshakwambia hakuna *sports betting* duniani ambayo itaendelea kama mpira haupo. Mpira ndiyo unasababisha *betting* iwepo, *betting* lazima iendelee kuchangia. Sisi kama nchi tuna jambo letu kuelekea *AFCON*, lazima tuvae mkanda na ni lazima haya mambo tuyaamue kama Taifa, tunaamua haya kwa muda wa miaka mitatu, sisi kama nchi tunaamua haya mambo tuyasimamishe, tufanye shughuli hii ambayo inatupeleka kwenye heshima ya dunia sasa kwenye soka hili ni jambo langu la lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna ile *issue* ambayo mlikuja nayo, kwanza, nalipongeza Bunge. Mheshimiwa Waziri amesoma hapa bajeti yake, Bunge lilifanya vizuri sana kwenye mabadiliko ya sheria mwaka 2022 kwenye ukusanyaji wa hili hakimiliki kupitia *COSOTA*. Kwa kweli imefanya vizuri sana katika yale mambo 25 ambayo Wizara ilileta mbele ya Bunge, tukapitsha yale mambo karibu 13 ambayo yalipita, yameleta *impact*. Tumefanya makusanyo ndani ya miezi minne toka Septemba, 2023 hadi Aprili, 2024 shilingi milioni 600. Hii inaonesha kabisa kwamba kuna kitu tukiamua kukifanya kwa mkanda yaani tukitoa *full support* kwenye Wizara, wanaweza wakafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Serikali, kuna vitu ambavyo bado vimesalia, kuna *issue* kama *computer, photocopy machine, scanners* na simu, tunahitaji *some percentage* tu ili tuweze kufanikisha wasanii wetu wapate hizo fedha. Wasanii

wako hapo nje, sisi hizi simu tunatumia, tunacheza muziki na tunaweka vichekesho, lakini hizi simu lazima zi-*support* kazi za wasanii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweka vitabu humu kwenye simu, tunaangalia *tv*, tunafanya nini, lazima zi-*support* kazi za wasanii wetu. Naliomba Bunge na Wizara, hakikisheni hili jambo mnalileta mbele ya Bunge, sisi Waheshimiwa Wabunge tuko tayari kuhakikisha kwamba tuna-*facilitate* na Wizara mkiamua, tusogezeni mbele kwa sababu tumeshaona, tulijaribu mambo 13 tulivyokuwa nayo, yameleta matunda ya shilingi milioni 600 ndani ya miezi minne. Sasa hivi tuleteeni hayo mengine tuweze kukamilisha na wasanii wetu wa Tanzania wapate hizo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja tunayo kubwa kwa sababu nchi yetu ilishaingia kwenye Mkataba wa *Ben and Trips Agreement* ambao ulisaniwa kati ya nchi za Malawi, Ghana na Kenya na wenzetu wameshafanya, siyo jambo geni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda simu *(smart phone)* kule Kenya, wana zaidi ya 1.5%, Malawi wana asilimia tano na Ghana wana 20%. *Computer* wana 1.5% na ukienda Malawi wana asilimia tano. Sisi Tanzania tukiamua, tukaweka *2.5 percent* au *three percent*, tunakusanya hela ya kutosha na tuka-*support* kazi za wasanii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana na naiomba Wizara hili jambo leteni mbele sisi tuendelee kusonga nalo mbele kwa sababu litasaidia kwenye makusanyo na hasa hasa hakimiliki za wasanii wetu ili waweze kupata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu lingine nimezungumzia suala la udhamini/uendeshaji wa ligi yetu. Tuna vilabu vikubwa hapa nchini vya Simba na Yanga. Uwekezaji unaendelea, taratibu za kiuwekezaji zinaendelea, tunaipongeza Serikali. Kuna wakati mwingine tunakuwa na maneno makali kwa sababu tunaona kama mchakato umekwama, kwa sababu kuna hivi vilabu vinaendelea kwenye *transformation,* Simba, Yanga na vilabu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kwa sababu suala la uwekezaji wa mpira na nchi yetu hasa hasa *East Africa* tumeonesha wingi na mwitikio mkubwa kwenye suala la soka na kwa sababu vilabu vyetu vinafanya vizuri, tunaiomba Serikali kwenye uwekezaji wa hivi vilabu, wafungue milango iwe mipana kwa ajili ya uwekezaji. Milango iwe mipana, wawekezaji wawe wengi kwenye hivi vilabu ili viweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani, niseme mchakato wa Klabu ya Yanga na mchakato wa Klabu ya Simba umekwama kwa muda mrefu. Wawekezaji wamekuwa wakitoa fedha, wanajitahidi na muda mwingine sisi kama mashabiki kwa sababu ya matamanio, tumekuwa tukitoa maneno makali kwenye vilabu hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali sasa iweze kuruhusu mchakato uweze kukamilika na iweze kufungua dirisha la uwekezaji mpana zaidi kwenye soka letu nchini ili vilabu hivi viweze kufanya vizuri kama ambavyo ukienda *Manchester United,* unakuta kwamba wawekezaji ni wengi ndiyo maana timu inasonga mbele na zingine zinafanya hivyo.

Kwa hiyo, tunaiomba pia Serikali iangalie jinsi gani ya ku-*facilitate* hii michakato iweze kukamilika hususani kuhakikisha kwamba upana wa uwekezaji kwenye vilabu vyetu unaweza kuwa mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo yalikuwa ya kwangu, lakini mwisho kabisa ni kwamba tunatamani sana kuona viwanja kama cha Dodoma kinaanza kujengwa. Kiwanja cha Dodoma kijengwe kwa sababu watu wengi wamekuwa wakiulizia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niseme jambo moja, Mheshimiwa Waziri, timu ya Taifa tumpunguzie kazi Mzee Majaliwa ya kwenda kuitisha kila siku *harambee,* tuanze kuchangisha ili timu ya Taifa iweze ku-*survive*, hakuna kanuni inayotuzuia timu ya Taifa kuwa na mdhamini, ruhusuni mchakato wa udhamini kwenye timu ya Taifa. Timu yetu iweze kupata

mdhamini, angalau iwe na uwezo wa kuwa na *facility* ya kifedha au *incentives* ili wachezaji wetu waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mambo mengi, lakini niseme kabisa timu ya Taifa ni ngao yetu, lazima turuhusu watu waweze kuidhamini na iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana na niwatakie kila la kheri. Ninaunga mkono hoja kwa 100% na ninawapongeza sana Wizara ya Michezo, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoka Shirikisho la Sanaa za Maonesho, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma ambao ni Kamati ya Siasa kutoka Muheza, Mkoa wa Tanga, karibuni. *(Makofi)*

Tukirudi jioni panapo majaaliwa, ataanza Mheshimiwa Khadija Aboud, Mheshimiwa Edwin Swalle, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said na Mheshimiwa Hamisi Taletale. Sasa namwita Mheshimiwa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru na namshukuru sana Mwenyezi Mungu ametujalia na amenijalia nimemaliza ibada yangu ya Umrah vizuri, nimerejea salama, namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa faraja kubwa kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni mwezi wa pili tu hapa wakati tunachangia Taarifa ya Kamati yetu ya Elimu, Utamaduni, Sanaa na Michezo, nilisema kuhusiana na mashaka yangu kwenye maandalizi ya *AFCON* hasa uwepo wa viwanja. Hivi tunavyozungumza na sisi

Wanakamati tumeshuhudia zimetolewa fedha zaidi ya shilingi bilioni 286 kwa ajili ya kujenga uwanja mzuri wa michezo wa Kimataifa pale Arusha na tumeshuhudia mkandarasi akikabidhiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mashaka kabisa ninajua kazi itafanyika vizuri na viwanja vingine vitajengwa kwa dhamira hiyo hiyo ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba eneo hili la michezo linafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea na mchango wangu, nimeona Mheshimiwa Waziri katika wageni wake wote, ukiwaacha wanafamilia pamoja na timu ya Wizara, amealika wasanii. Ni jambo zuri sana, lakini nilitamani sana uwaalike na wachezaji wa zamani ambao walilipa Taifa hili heshima ya kwenda *AFCON* ya Lagos mwaka 1980 na wachezaji hao wa mpira wa miguu wapo. Tunajua Peter Tino ambaye alifunga goli la kuiwezesha timu ya Taifa kwenda Lagos yupo, Leodgar Tenga, Aldoph Rashid na Mohamed Mkwesha yupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa bahati mbaya nitoe pole kwa wanafamilia wa mchezaji Jellah Mtagwa ambaye ametangulia mbele ya haki, ndiyo alikuwa *captain* wa timu ya Taifa ambayo ilikwenda Lagos mwaka 1980.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nayasema haya? Tunaelekea kwenye *AFCON,* tuna *CHAN* na tuna *AFCON,* tunahitaji hamasa hii ya hao wachezaji ambao walifanya kazi yao kwa morali bila kuwa na ujira mkubwa, wakaifanya kwa nia njema, wapo! Hawa wanaweza kuwa kichocheo kikubwa cha kusaidia Taifa hili, Watanzania na wachezaji wengine kuona umuhimu wa mashindano ya *AFCON* tunayoyaandaa ya mwaka 2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri bado hajachelewa kuwaalika wachezaji hawa na sisi kama Bunge tukawapa heshima hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumeshuhudia kazi kubwa ya kuwashirikisha na kuhamasisha vilabu, vyama vya michezo na mashirika ya michezo inayofanywa na Wizara. Mafanikio makubwa yameonekana, leo tunao vijana wengi wamepata ajira ndani na nje ya nchi, kazi hii imefanyika vizuri sana, lazima tuwapongeze wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona vilabu vimefanya kazi nzuri. Mheshimiwa Waziri, nakupongeza na nawapongeza sana Baraza la Michezo la Taifa kwa usimamizi mzuri kwenye eneo hili la michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilabu vimefanya vizuri, tunaiona ligi yetu imekuwa na hamasa kubwa pamoja na changamoto zinazojitokeza. Kipekee kabisa nawapongeza sana *Dar Young African,* wameonesha mfano mzuri siyo tu kwa sababu ya kuchukua makombe mara tatu au mara 30, lakini kwa sababu ya menejimenti nzuri ya uongozi wa *Engineer* Hersi pamoja na *GSM*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii menejimenti nzuri na wenzetu Pamba wamepanda, wameonesha uwezo mzuri, wameonesha kwamba sasa na sisi tunataka kuwa washindani, tuko ligi kuu, wameamua kwenda kujifunza namna ambavyo Yanga wameweza kufanikiwa. Hii siyo vibaya tukamwambia kaka yangu Mheshimiwa Kanyasu pamoja na kwamba timu yake inasuasua, hapa tatizo ni menejimenti. Ni vizuri sana na wao wakajua wanakwama wapi kuweka menejimenti nzuri, timu zetu ziweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzetu akifanya vizuri tujifunze, hatuna sababu ya kuanza kulalamika, watani, nini, Hapana, menejimenti ni nzuri na ndiko mahali pekee ambako sisi kama Watanzania tunapaswa kuwaunga mkono wenzetu wa *Dar*

*Young African*, wamefanikiwa kwenye suala la menejimenti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie timu ya Taifa, kama kuna eneo Serikali tunatakiwa kuwekeza leo ni eneo la timu ya Taifa. Tutakuwa na miundombinu ya viwanja na kila kitu lakini kama bado hatujawa na wachezaji wazuri wa timu ya Taifa na kama hatujaweza kuisimamia timu yetu ya Taifa, hatuna sababu ya kuwa na mashindano ya *AFCON* hapo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ivory Coast wametuonesha mfano mzuri, *bench marking* zuri sana iko kwa wenzetu wa Ivory Coast. Nianze tu kwa kuangalia hapa, Ivory Coast walikuwa na kocha wa kigeni, lakini walivyoanza kusuasua wakamuondoa, wakawa na kocha mzawa, amefanya kazi nzuri mpaka wamechukua Kombe la *AFCON*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema haya? Nataka kuwaomba sana Serikali, ni wakati muafaka wa kuwatumia wazawa. Tunajua kabisa kocha tuliyenaye Hemed Morocco, ni kocha bora na ana uwezo, mara zote ambapo hawa wageni wanashindwa, tunampa yeye kazi hii. Kwa nini tusimpe mkataba Hemed Morocco akaisimamie timu hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyo vipimo vya kumpima, tunakwenda kwenye *CHAN*, tumpime kwenye *CHAN* kama anaweza kufanya vizuri kabla ya kwenda *AFCON*, lakini tukiacha hivi akawa anaendelea na timu bila kumpa mkataba tutakuwa hatujafanya jambo lililo jema. Nataka tuamini kupitia wazawa kwa kuangalia mfano wa wenzetu wa Ivory Coast na wamefanikiwa, ni imani yangu tunaweza kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, pia tunapaswa tuwapongeze sana *TFF*. Shirikisho la Mpira wa Miguu, wamefanya kazi nzuri, ndiyo wameilea timu hii mpaka sasa. Serikali inawajibika moja kwa moja kwa timu hii, lakini walezi wakuu wamekuwa Shirikisho la Mpira la *TFF*. Rais wa *TFF* na Katibu Mkuu wamefanyaka kazi nzuri kwa ajili ya kuilea timu hii ya Taifa. Sasa

mzigo huu inapaswa ifike wakati kwenye bajeti hii, tutenge fedha na fedha iwepo ya kutosha kwa ajili ya timu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwatue mzigo wenzetu wanaolea timu hii, timu ya Taifa ni jukumu la Serikali. Serikali iwajibike na timu ya Taifa na kwa kuwa sisi tunataka mafanikio na Mheshimiwa Rais ameonesha nia njema kwa ajili ya kuhakikisha michezo inakua nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutumie fursa hii kwa ajili ya timu yetu ya Taifa iwe nzuri. Tutenge fedha ya kumwezesha kocha afanye *scouting*. Azunguke mikoa yote kutafuta wachezaji. Tunajua wachezaji wapo, lakini mpaka tufike mwaka 2027 lazima tuandae wachezaji wa rika mbalimbali na wa kutosha ili tuweze kuwa na timu nzuri ambayo itahamasisha hata vilabu vyetu kuwa na wachezaji wazuri. Mathalani, ukiwa na wachezaji wawili kutoka katika kila mkoa, una wachezaji 60, ukachuja kupata wachezaji 30, tutakuwa na timu bora ambayo hatukutarajia kuwa nayo. Jambo hili linaweza kutuweka mahali pazuri na kuwa katika maandalizi ambayo yanastahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili la michezo kuna jambo muhimu sana la kufanya. Wenzangu wamezungumza vizuri sana, leo viko vilabu vina *suffocate* na kupata wakati mgumu wa kuweza kujiendesha. Sasa kama vilabu vinapata wakati mgumu wa kuweza kujiendesha na wadhamani ni hao hao wanatoa kiwango hicho kidogo, ninaamini na ninadhani huko mbele tunakoelekea viko vilabu vitakuwa vinashindwa kujiendesha na ligi yetu inaweza kuwa ngumu kuliko tunavyofikiri, ikabaki kuwa na vilabu vikuu vichache ambavyo vina uwezo wa kuweza kujiendesha na ligi ikakosa mvuto, kwenye eneo hili lazima Serikali tuone umuhimu wa ligi yetu hii ili kuona namna ya kuisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, nafahamu iko tozo ya hakimiliki kwa wasanii, kazi kubwa ni kuwasaidia wasanii, hasa wabunifu na wasanii wetu wadogo ili kuweza kuhakikisha kazi zao zinakuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa umefika wakati wa kuhakikisha tozo hii ya *blank tape levy* ili tuweze kuiangalia hii sheria vizuri kama bado ina tija ama imepitwa na wakati kwa sababu tunakoelekea sasa hivi tuko kwenye sayansi na teknolojia. Wasanii wetu anafanya kazi yake hawezi kwenda kusubiri ku-*perform* kwenye majukwaa ili waweze kumlipa, maana yake atafanya kazi yake lakini zile *softcopy* au *software* itatumika kuhakikisha kwamba wasanii hao wanapata kile kiasi ambacho wanastahili kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuiomba Serikali irudi tena ikatazame sheria hii ambayo tuliitunga na sasa kwa wakati huu bado ina tija hiyo? Kwa sababu wakati tunakoelekea maana yake sheria hii itapitwa na wakati na wasanii wetu watakosa uwezo kabisa wa kazi zao hizi kuwapa manufaa wao. Kazi zao hizi zitakuwa sasa ni kazi ambazo hazina manufaa na ndiyo utawakuta sasa barabarani wanatembea na *compact disc (cd)*, msanii anauza *cd*, ni fedheha. Kwa nini msanii auze *cd* wakati tayari tunajua kabisa sisi mifumo yetu imekaa vizuri. Msanii akifanya kazi yake inaingia kwenye mfumo, maana yake anapata malipo, yale malipo anayoyapata yanamsaidia na yanampa *courage* ya kuweza kufanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ninakushukuru sana, nadhani eneo langu nililokuwa nataka kulizungumzia ni hili. Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, kuna mabadiliko ya wachangiaji wa jioni, tutaanza na Mheshimiwa Edwin Swalle, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Hamisi Taletale na Mheshimiwa Khadija Aboud.

Sasa nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa nilimtaja Mheshimiwa Edwin asubuhi, lakini kuna dharura ya Mheshimiwa Francis Ndulane kwa hiyo ataanza yeye halafu atakuja Mheshimiwa Swalle.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Wizara yetu ya Michezo, Utamaduni na Sanaa.

Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya ya uwekezaji katika sekta ya michezo hasa upande wa mpira wa miguu, amewekeza fedha nyingi katika ku-*support* timu yetu ya Taifa ya wanaume ya wakubwa, lakini hata zile za vijana, lakini pia hata kwenye *women football* pia amewekeza sana na ndiyo maana tumepata mafanikio makubwa katika sekta hii ya michezo hasa mpira wa miguu hadi timu yetu ndani ya miaka michache tumecheza fainali mbili za *AFCON,* kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia hata kwenye hamasa kwenye viilabu vyetu vikubwa vya Simba na Yanga vilipokuwa vinashiriki kwenye mashindano ya Kimataifa vimekuwa chagizo muhimu katika kuhakikisha vilabu hivi vinashiriki kwa mafanikio makubwa. Sisi wote ni mashahidi hapa nchini tumeshuhudia fedha zilitolewa kadiri timu zetu zilivyokuwa zikifanya vizuri kwa

hakika amefanya mambo makubwa sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia napenda kukupongeza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo lakini pia na Mheshimiwa Naibu wako na kwa kweli Mheshimiwa Rais hakukosea kuwaweka kwenye nafasi hizo kwa sababu hapo nikikuangalia kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro mtani wangu ni mbobezi kwenye sekta ya mchezo wa mpira wa miguu. Najua *statistics* na *CV* zako kwenye mpira wa miguu, nina imani tutakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niliangalia Mheshimiwa Naibu wako yupo vizuri kwenye mambo ya sanaa kwa hiyo nina hakika hiyo Wizara Mheshimiwa Rais amewapanga kwa makusudio maalumu kuhakikisha kwamba malengo ya nchi yetu yakufukia maendeleo ya kiwango cha juu katika sekta ya sanaa na michezo yanafika katika kiwango cha juu, lakini pia nampongeza Katibu Mkuu kwa kazi nzuri na ambayo imeonesha matunda makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi niseme kutokana na uwekezaji wa wawekezaji wetu pia kwenye vilabu vyetu kwa kuanzia na muwekezaji Mohamed Dewji kwenye klabu ya Simba na *GSM* kwenye klabu ya Yanga kwa kweli vikiungana na malengo ya Mheshimiwa Rais wetu yameleta mafanikio makubwa katika medani ya soka na kwa kweli tumejionea wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani mpira fedha, mpira ni fedha, lazima kuwepo na uwekezaji na ndiyo maana umekuta hata sasa kutokana na ubora wa *national team* zetu zote, ubora wa vilabu vyetu vya Simba na Yanga ambavyo vimetuwakilisha pale mashindano ya Kimataifa kwa kweli vimetupeleka mbele sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo vilabu vyetu vya Simba na Yanga vinasoma katika *rank* za juu kabisa hapa Tanzania na kutokana kwamba vilabu vyote hivi sasa vimefanikiwa kufanya

vizuri hata zile hadithi za wageni kusindikizwa kwenye mahoteli wakifika hapa zimetoweka, zile kamati za roho mbaya zimekufa na matokeo yake sasa vilabu vyetu vinasoma katika *rank* ya juu kabisa Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Simba ni ya saba kwenye *ranking* za *CAF,* Yanga ni ya 13 kwenye *ranking* za *CAF,* kwa kweli tunawapongeza sana viongozi wa Simba na Yanga, lakini wawekezaji pia tunawapongeza. Miaka miwili iliyopita nilisema kwamba kama hakuna uwekezaji kwenye vilabu kwenye maeneo matatu muhimu ya uendeshaji wa timu basi mafanikio yatakuwa ni magumu na nilitolea mfano kwa klabu ya Simba ambayo kimsingi tangu mwaka 2017 mwekezaji Mohamed Dewji alipoingia kwenye klabu ya Simba amewekeza kwa fedha yingi sana kwenye klabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2017/2018 nilikuwa nasoma takwimu za klabu ya Simba Mohamed Dewji aliwekeza jumla ya shilingi bilioni tatu kwa kuanzia, lakini leo tumeshuhudia msimu huu amewekeza jumla ya shilingi bilioni 21 na mwakani tayari taarifa zinasoma kwamba atawekeza shilingi bilioni 24. Kwa hiyo ni uwekezaji mzuri na ambao unakwenda kuleta matunda ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maneno maneno mengi yanazungumzwa Mohamed Dewji haitaki timu, Mohamed Dewji hivi na vile, lakini kwa hakika Mohamed Dewji amejitahidi kuwekeza hasa ukizingatia kwamba anao mtaji kwa sababu ni tajiri namba moja hapa nchini kwa kweli tunakokwenda ni kuzuri, kwa hiyo, ninaomba wanasimba na wanamichezo wote kwa ujumla tuige mfano wa Mohamed Dewji katika kuwekeza kwenye mpira wa miguu ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kwa vilabu vingine kama vitawekeza kama alivyoweka Mohamed Dewji sina mashaka ndani ya miaka michache ijayo tutashuhudia bingwa wa Afrika kwa mashindano ya vilabu atatoka nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningependa niseme kwamba ukienda pale Simba sasa hivi wachezaji wote wanalipiwa bima, tena bima ambayo ni ya uhakika, hata ikitokea kuna *injury* yoyote mchezaji anapelekwa hadi nje ya nchi kwenda kutibiwa, kwa hiyo, huu uwekezaji siyo wa kubeza, tuendelee kuwashikilia wawekezaji wetu kwenye vilabu katika kuhakikisha kwamba tunapata mafanikio kwa kuanzia na klabu ya Simba, Simba oyee. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Oyee.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikimaliza kuongelea habari hizo nakwenda kwenye upande wa sanaa. Katika siku zilizopita tulikuwa na ndugu yetu Hayati Ruge Mutahaba, aliwekeza sana kwenye sanaa ya mziki na alikuwa na taasisi inaitwa *THT*. Hii taasisi ilikuza vipaji vya wasani wetu wa muziki, lakini hivi karibuni nimeona tasnia ya muziki imeshuka, ninaomba Serikali iwekeze katika eneo hili na kuwaleta wawekezaji wengi wa aina ya Hayati Ruge Mutahaba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahala pepa peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukipata hii tansia yetu ya muziki itarudi kwenye *chart. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwenye soka, tuwekeze kwenye soka la vijana. Ningekuomba Mheshimiwa Waziri angalau kila mkoa kuwe na kituo cha maendeleo ya vijana, tutafute shule katika kila mkoa angalau moja tuwekeze katika maendeleo ya michezo na sanaa kwa ujumla wake ili tuhakikishe kwamba mambo yanakwenda sawa sawa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane ahsante.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia vile vituo vya kukuzia vipaji ambavyo vimefanya vizuri vimetoa wachezaji wengi kwenye timu ya Taifa navyo tuviendeleze, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Francis Ndulane kawahi ndege sasa.

Mheshimiwa Swalle, ajiandae Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said na ajiandae Mheshimiwa Taletale.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuwa mchangiaji wa pili mchana huu wa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwanza niungane na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia tangu asubuhi kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuleta hamasa na mageuzi makubwa katika soka la Tanzania, lakini sio soka tu hata katika michezo mbalimbali ambayo nchi yetu umeanza kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu mmoja alikuwa anatania anasema Mheshimiwa Rais amekuwa ni suluhu ya kila kitu, kwa sababu kwenye majimbo ya Waheshimiwa Wabunge miradi mingi inakwenda vizuri, ukitazama kwenye uchumi tumepewa hapa takwimu uchumi umeanza kukua vizuri na kwenye michezo Mheshimiwa Rais kapeleka timu yetu ya Taifa kwenye mashindano ya *AFCON*. Haya ni mambo makubwa ambayo hatuwezi kuyabeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitumie pia nafasi hii kuwashukuru sana watu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na ni-*declare interest* kwamba mimi ni mdau wa michezo, ni mdau wa michezo kwa sababu si tu kwamba nacheza mpira na riadha, lakini pia mimi nimekuwa nikiratibu *Swalle Cup* katika Jimbo la Lupembe tangu nimeanza Ubunge mwaka 2021 mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie *Swalle Cup* ya mwaka jana Ofisi hii au Wizara hii ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo walinitumia Mheshimiwa Naibu Waziri kuja kuifunga na ilikuwa *Swalle Cup* bora kuliko sherehe za ushindi wa Yanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Michezo, mimi kama Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wengi tunajua na tunamfahamu sana Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro ni mtu makini, mnaokumbuka Mheshimiwa Waziri alitusaidia wakati fulani kuongoza msafara wa kurejesha ndege hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata kwenye hili Ila kusaidia nchi yetu kuwa na sifa ya kuandaa mashindano ya *AFCON* 2027 mimi nafahamu kwamba haikuwa kazi rahisi, Mheshimiwa Waziri na timu yako kwa kufuata maelekezo ya Mheshimiwa Rais mmefanya kazi nzuri sana tunawapongeza hongereni sana na tunayo imani kubwa kwamba mtafanya vizuri na *In ShaaAllah* Mwenyezi Mungu siku moja Tanzania ishiriki Kombe la Dunia kama Mungu akipenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ndugu yangu Mwana FA (Mheshimiwa Hamis Mwinjuma) kama nilivyosema mwaka jana wakati wa fainali ya *Swalle Cup* niliandika barua Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ninaamini Mheshimiwa Waziri kwa nafasi yako ulimtuma Mheshimiwa Naibu wako kuja Lupembe kushuhudia vipaji vya vijana kwenye soka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akiwa kule Mheshimiwa Naibu Waziri alisema vizuri sana, kwanza alieleza kazi kubwa ambayo Wizara inafanya, lakini pili mimi nilikuwa sijui kama Mwana FA ni mtaalamu wa *scouting* ya kuchagua vijana wenye vipaji. Katika ile fainali alifanikiwa kuona vijana wawili wazuri na kuwasema hao wanafaa kwenda mbele, hivi ninavyosema kijana Nebukedreza Gadau na Ronald Benson Chatanda wanakipiga soka kwenye timu nzuri hapa nchini, wameanza kupata mshahara, hongera sana Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hii yote ni kwamba Wizara hii inaonesha ipo karibu na Watanzania na mimi nitoe wito Mheshimiwa Waziri mipango ya Wizara hii ni mizuri sana kama ambavyo nimesema Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro sisi tunaamini

wewe ni mzee wa mipango na ninakumbuka Mheshimiwa Naibu Waziri akiwa Jimboni Lupembe alining'ata sikio, leo nikuibie siri kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aliniambia Mheshimiwa Swalle Mheshimiwa Waziri wangu ni mtu wa mipango sana, hata ule ubora wa timu ya Taifa alikupongeza sana Mheshimiwa Waziri, hongera sana kwa kazi nzuri sisi kama Waheshimiwa Wabunge tunakuunga mkono tunakutakia kila la kheri kwenye Wizara hii ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Lakini pia nimpongeze ndugu yangu Gerson Msigwa Katibu Mkuu wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mkoani Njombe watani wanamwita mzee wa kibegi cha fedha za mama, nampongeza sana Katibu Mkuu - Mheshimiwa Msigwa, kwa kutoa hamasa na kuwa karibu na wanamichezo, lakini pia kwa jinsi ambavyo umekuwa karibu kutoa hamasa kwa wachezaji kwenye makambi na kuhamasisha wadau kuchangia soka hapa nchini. Nakupongeza sana kwa niaba ya wananchi wa Lupembe tunasema hongera muendelee kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maeneo maeneo mawili ya ushauri kwa ajili ya Wizara hii muhimu ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, jambo la kwanza naomba nichangie mahususi kuhusu umuhimu wa vipaji vya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu hapa nchini kumekuwa na watu wengi wenye vipaji vya muziki, Mwana FA (Mheshimiwa Hamis Mwinjuma) ni mmoja wapo ya watu ambao ni wataalamu na wenye vipaji vya muziki. Kama tungewalinda wanamuziki wetu vizuri, wanamuziki wetu wengi wangekuwa na maisha mazuri, wangekuwa na fedha za kutosha, wangetoa ajira, wangechangia kodi ya Serikali na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kumekuwa kuna kuzembea kwenye kulinda haki za wasanii wetu. Nakumbuka mwaka 2022 nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo tulijadili juu ya kuweka wigo wa kusaidia wasanii wetu kupata huu mrabaha

kwenye sanaa na wakapendekeza vifaa mbalimbali viongezwe kodi au viwekwe kodi kwa ajili ya kusaidia wasanii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaruhusu kwamba tuweke tozo kwenye *cd* lakini leo hii *cd* Watanzania wengi hawatumii *cd* tukaweka tozo kwenye vitu kama *sim card*, leo hii watu wengi hawatumii *sim card* na kila Mtanzania hata mimi kwenye simu yangu hii jioni napiga nyimbo za wasanii wanaofanya kazi kubwa, wanatumia muda wao na vipaji wanahitaji kulindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo langu sisi Waheshimiwa Wabunge hatufanyi matamasha wala mikutano bila muziki, imefika wakati tuwasaidie wasanii hawa na wao wakue katika uchumi. Kwa hiyo, ninaunga mkono hoja za Wabunge wenzangu wengi kwamba Mheshimiwa Waziri utakavyokuja ku-*wind up* hapa tuambie kabisa mmejipangaje kuhakikisha kwamba kwenye sheria ya mwaka huu kwenye kodi vifaa hivi vya *smartphone*, vifaa hivi vya *computer* vinakwenda kuongeza angalau kidogo tozo kusaidia wasanii wetu wa muziki hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muziki huu upo duniani, ni biashara kubwa watu wengi ni matajiri sana na hapa kwetu imefika wakati ni lazima sasa tuwalinde wasanii wa Tanzania. Mimi Lupembe ninao wasanii wakina *Buki boy* wapo Lupembe wanapiga muziki, akina *Masai the Don* wanapiga muziki na wao walindwe kwenye sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu kwa wasanii mkishapata mrabaha mkumbuke pia kurejesha kwenye jamii kama ambavyo kina Steve Nyerere na Taasisi yao ya Mama Ongea na Mwanao wanavyokwenda kwenye jamii na wasanii nyie mkipata huu mrahaba msisahau kutoa sehemu ya mali zenu kwenye jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Swalle. Mheshimiwa Mwanakhamis, ajiandae Babu Taletale

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kunijalia kwa siku ya leo na jioni hii kuchangia bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayowafanyia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu katibu Mkuu na menejimenti yote ya Wizara hii ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, kwa kweli Wizara inafanya kazi kubwa sana, mimi ni Mjumbe wa Kamati na najua ninachokifanya, kwa kweli siku zote Wizara hii ilikuwa inaonekana na Wizara ya chini kabisa na ni duni, lakini leo Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wanafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shairi linasema ni upande wapi wema pale upandwapo ukamea. Msanii alisema aupande wapi wema, pale utakapopandwa ukamea, mmea huu ni mti na mti huu lazima umwagiliwe maji. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mama Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mmea huu ameupanda kwa mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mama Samia amewapandia mmea wasanii wetu wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia ameupanda mmea huu kwa vijana wetu wachezaji wa mipira, amefanya kazi kubwa sana, ilikuwa tunasema ni Wizara ya Utamaduni tu, lakini wapi inakamatwa haijulikani, walikuwa wanasema ni Wizara ya Michezo, wapi inashikika haikamatiki kwa sababu ilikuwa haina bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo Mheshimiwa Mama Samia amechukua nguvu zake zote, amewapelekea vijana wake. Niwaombe Watanzania, vijana wa Watanzania mmea huu tusiuache, tuumwagie maji umee tunufaike zaidi, kidogo unakitunza na kikubwa unakitunza. Huu mmea ni mkubwa kwa hiyo tuutunzeni kwa nguvu zetu sote vijana wa Tanzania, wasanii pamoja na wanamichezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwapongeze wasanii, wanafanya kazi kubwa sana, wanaiingizia nchi yetu pesa za kigeni, lakini tumefikia muda utamaduni wetu wa Kitanzania tunauweka pembeni, tunakwenda zaidi na utamaduni wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shairi msanii anasema; "Kitendawili tega, tega kitegueni, una kijungu cha pwaga hakina moto jikoni." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizungumza lugha hii niliyoizungumza mimi hakuna anayejua nini msanii huyu alikusudia au shairi hili limekusudia nini, lakini leo unawakuta wasanii wetu wanazungumza kila kitu fahasha, hawabakizi kitu. Kwa kweli hatujui nyuso zetu tunazipeleka wapi, vijana wengi sasa hivi ni matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani waimba taarabu walikuwa wanavaa kawaida, kama ni mwanaume atavaa kanzu yake na koti na baraghashia na kubazi yake, lakini leo mwimba taarabu mwanaume lazima kidole akiweke hivi, kisuruali kimebana hakitambuliki, hakijulikani. BASATA wako wapi? Na kama sheria hii ni nyepesi iletwe Bungeni tuirekebishe, vijana wetu wengi wanapotea. Hatukatai kuimba, kuimba sasa hivi usanii, ni fedha, ni biashara kama biashara nyingine na kuna nyimbo unaweza ukaimba huwezi ukamkandia msanii kwa sababu unajua kile kivazi kavaa cha usanii, lakini kuna mambo mengine yamezidi ya maadili mabovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kubaya, vijana wetu wengi wameharibika. Sisi ni wazazi matumbo yanatuuma, usanii tunaujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msanii alisema anaitafuta lulu, lakini alifikiri lulu iko kwenye mbuyu au akaichimbe kumbe akasema lulu iko chini ya bahari, nitaipataje kule lulu kuizamia, alikwenda kutafuta mtungi ule wa gesi akavaa viatu na miwani akaizamia lulu, alipoipata lulu ile akasema jamani kumbe lulu nimeipata ni mfano wa yai tena lililo na maji ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hujui nimesema nini, wala hufahamu mimi nilichokizungumza, lakini leo msanii anakwenda kuimba mambo mazito yasioeleweka. Msanii anakwenda anaimba nyimbo inakataliwa Zanzibar hii isiimbwe, inarudi huku inahalalishwa. Kwa kweli tunakwenda kubaya, BASATA lazima wasimamie vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwanakhamis. Mheshimiwa Babu Taletale, ajiandae Mheshimiwa Malapo na ajiandae Mheshimiwa Khadija Aboud.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwanza mimi leo nimekuja na pongezi kubwa na nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Sita, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Rais ametuonesha kwamba yeye ni mwanamichezo namba moja nchini. Mheshimiwa Rais ametuonesha kwa vitendo kwamba dhamira yake ya kutaka michezo ikue anafanya kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikaa hapa kwenye Bunge la Bajeti lililopita, tulitazama na tukajadili bajeti ya Wizara ya Michezo tuliletewa shilingi bilioni 34 nukta kadhaa, lakini leo Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ameleta bajeti ambayo tunaona kabisa ni zaidi ya shilingi bilioni mia mbili na themanini na zaidi, ukisema yule chawa bora hata uwe chawa, uwe kunguni, lakini kwa anachokifanya Mama Samia sijui tusemeje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Rais ambaye ameamua kuupiga mwingi kwenye michezo, naenda kuipongeza Wizara ya Michezo, Wizara ambayo

katika nchi yetu ndiyo inayoleta amani, inaleta utulivu. Kiukweli Wizara ya Michezo safari hii imepata watu wanaoiongoza barabara. Yule ndugu yangu pale Mngoni na ndugu yangu pale wa Kidigo, hongereni sana. Mimi najisikia raha nikiwatazama maana yake naona ile ajira ambayo nilikuwa nikiihangaikia huko nyuma imepata madereva thabiti na mwalimu thabiti Mama Samia akiiongoza barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama unaweza kuipongeza Wizara ya Michezo, lazima uipongeze na Kamati ya Michezo. Hapa kidogo sisi Wajumbe tujimwambafai. Mimi kama mjumbe hii Wizara ya Michezo tumeweza kuwashauri. Nampongeza Mwenyekiti wetu dada yangu Mheshimiwa Husna Sekiboko, hongera sana. Tumeweza kuishauri Wizara iongeze bajeti na leo hii tunazungumza tupo ndani ya historia kubwa ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi leo hii tunaonekana watu wazito kwa sababu ya kile kinachoendelea kwenye Wizara ya Michezo. Huko nyuma tulikuwa tunaonekana kama Wizara inazingua, lakini hakukuwa na watu madhubuti, namba moja haikuwa anaitazama vizuri, nani kama Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo niendelee tena kuipongeza taasisi kama *TFF,* leo hii *TFF* wanachokifanya, akija mtu akamponda Ndugu Karia, akija mtu akaiponda *TFF*, sisi wote tutawaona wendawazimu kwa sababu tunaona mabadiliko ya michezo. Leo hii *TFF* imeenda kuishauri Wizara ya Michezo ijenge viwanja vya kisasa na tunaona vinakuja. Leo hii yule Rais wa *TFF* amekwenda kufanya *maneuver* kule. Sisi Watanzania tunakwenda kupokea *AFCON* ndani ya Tanzania, nani kama Karia? Tunatakiwa tuongee vitu, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, lakini siku hizi mnyonge hanyongwi mpaka apewe haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akina mama wakipewa madaraka wanaweza, kwenye Kamati yetu tulielekeza Wizara, huyu bosi wa BMT hatutaki akaimu tunataka awe kiongozi maridhawa. Dada yangu kutoka BMT pale hongera sana, yule ni mwanamichezo hasa. Unaposifia akina mama maana yake pia unamsifia mama

namba moja wa hii nchi. Unaposifia akina mama na pia tunasifia mama zetu nyumbani. Yule dada pale anaupiga mwingi sana, hongera sana dada yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niende kidogo kuzungumzia maslahi ya wasanii. Tukianza kuzungumzia wasanii, wasanii siyo maskini. Tulikaa na Bunge tukatengeneza sheria ya kutengeneza hii *blank tape levy* ili iweze kwenda kuwasaidia wasanii, lakini kilichotokea ni kidogo. Mimi nashauri kwa kile ninachokiona na kwa *experience* yangu ambayo ninaiona, kama kwenye hii *blank tape levy* tukiweza kuangalia hizi simu janja na tukasema tusimamie simu janja, watu wengi humu ndani tuna simu nyingi janja kuliko hata *flash, disk* au *cd* tuangalie tunaweza kukusanya vipi kodi kwenye simu janja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tukilisimamia maridhawa wasanii wataona faida yao, hata sisi na mimi pia ni *publisher* ningepata mchele wangu kwenye maisha yangu ya baadaye mtoto wangu Tatiana naye atapata pesa yake kulingana na kile baba yake alichopigania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliseme hili tunampongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, kwa upande wa viwanja, wenzetu wana-*football* wanakwenda ku-*enjoy*. Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba utakaposimama wakati unamaliza, nakukumbusha kidogo ulifunga safari mpaka kwenye viwanja vya *Tanganyika Packers* pale Kawe, ukaenda kukagua vile viwanja na ukatuonesha kwamba muda wowote unatujengea na *dome*. Mimi nililalamika hapa juzi, sasa hivi waganga Tanga wamepungua mvua hazifungwi, wasanii wanacheza *show* kwenye viwanja ambavyo viko wazi, tuwe wa kweli, watu wanataka kufanya *show* ndani ya *dome*. Kaka yangu, mtani wangu nakuomba tena najua kutoka Songea kuleta dawa ya kuzuia mvua mpaka Dar es Salaam mbali, lakini watu wanaiangalia Dar es Salaam, wanaiangalia Dodoma kama Toronto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Mama Samia ameleta mwendokasi, watu wakiangalia *show* hapa au wakiangalia *show*

Dar es Salaam, sisi tunaokaa Morogoro tutapanda treni pale ya mwendokasi Ngerengere kufika mpaka Dar es Salaam. Tunaomba utujibu maswali yetu, lini kiwanja, wanasema *dome* itakuwa tayari na sisi tujitambie. Tumekuona ukienda kufanya uzinduzi, upembuzi yakinifu. Tunataka utuambie umepembua nini, umeyakinisha nini maana hapa inabidi tuongee Kiswahili sanifu kwa sababu unajua leo tunazungumzia Wizara yenye Kiswahili chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye eneo la Kiswahili…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** …Aya! muda umeisha?

**NAIBU SPIKA:** Ee, umezungumzia waganga wengi. *(Kicheko)*

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono hoja.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malapo, ajiandae Mheshimiwa Khadija Aboud.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu na Michezo, tumekuwa tukifanya kazi kwa pamoja na Wizara hii chini ya Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, kaka yangu Mheshimiwa Hamis, Katibu Mkuu wetu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeiona dhamira ya Rais na Serikali kwa ujumla katika Wizara hii. Mwaka uliopita tulilalamika

kwa kiasi kikubwa kuonesha ni kwa namna gani Wizara hii imepewa fedha kidogo, ilipewa fedha shilingi bilioni 35 tu, lakini mwaka huu wa fedha tunashukuru na tumefurahi sisi kama Wajumbe wa Kamati na pia nafikiri Bunge zima limeona kwamba kutoka shilingi bilioni 35 sasa hivi tunaongelea bajeti ya Wizara hii imefika ama imetengewa shilingi bilioni 285, ni ongezeko kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rai kwa Serikali, tunaomba fedha hizi ambazo zimekadiriwa kupelekwa kwenye Wizara hii zipelekwe ili yale ambayo yamekusudiwa kufanyika yafanyike. Mheshimiwa Waziri wetu na Naibu Waziri kila siku wamekuwa wakituambia hii Wizara ni Wizara ya raha, maana yake inaleta raha kwa wananchi katika mambo mbalimbali, wanaopenda muziki wanakwenda huko, wanaopenda ngoma za asili wanakwenda huko, sisi tunaopenda mpira hasa wa timu ya Yanga basi tunashabikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kila mtu anapata kile anachokitaka kwenye eneo lake ambalo yeye anaona linamfurahisha, wa mpira atafanya, wa muziki atakwenda, wa ngoma za asili atakwenda. Kwa hiyo, mimi rai yangu kwa Serikali, kwa sababu bajeti imeongezeka kwa kiasi hicho kikubwa, isiongezeke kwenye makaratasi iongezeke kwa fedha kutolewa ili zikafanye yale ambayo yamekusudiwa ili Wizara hii vile vipaumbele, kuna ujenzi wa viwanja mbalimbali ambavyo vitatumika kwenye *AFCON* mwaka 2027 basi vikajengwe, haviwezi kujengwa kama Serikali isipopeleka fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niongelee suala la viwanja vya michezo katika halmashauri zetu, hapo zamani, siyo zamani, nisiseme hapo zamani kama mimi ni wazamani sana, lakini kikawaida tulikuwa tunaona kwenye halmashauri maeneo ya wazi yanatengwa. Yale maeneo ya wazi tulikuwa tunaona watoto wanacheza na wanajifunza michezo mbalimbali, lakini sasa hivi jambo la kusikitisha maeneo mengi ya wazi Serikali imefanyia mambo mengine matokeo yake ni nini? Watoto wanashindwa kupata sehemu ya kuweza kujifunza michezo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa rai yangu, Serikali hii Wizara yetu ya Michezo ikishirikiana na TAMISEMI ikishirikiana na Wizara ya Ardhi waone kuna umuhimu wa kutenga maeneo kwa ajili ya kuendeleza vipaji kwa ajili ya michezo. Yale maeneo yakishatengwa yakipimwa yawekewe utaratibu wa kutokutumika kinyume na hayo matarajio ambayo tumeyategemea kwa sababu mpira wa miguu ulivyo hauwezi ukampata mchezaji asipoanza kujifunza tangu mtoto, anajifunza wapi ikiwa maeneo yote Serikali imefanyia mambo mengine? Mpira wa miguu vyovyote iwavyo mtoto hawezi kuchezea ndani tofauti na *game* kwenye simu kwamba atakaa kwenye kochi atacheza, anatakiwa akacheze uwanjani, akacheze eneo la wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi rai yangu Wizara yetu hii ya Michezo ikishirikiana na TAMISEMI ikishirikiana na Wizara ya Ardhi waone kabisa kuna umuhimu wa kutoa mwongozo kwenye halmashauri zetu hasa yale maeneo ambayo wanakuwa wanapima viwanja vipya basi waweke maeneo ya wazi na maeneo yale yasitumike kwa shughuli nyingine yoyote isipokuwa kukuza vipaji vya watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naiomba Serikali, sisi kule Mtwara hatuna kiwanja kikubwa cha mpira wa miguu ama viwanja vya michezo vya Serikali. Tunaomba Serikali ione umuhimu katika bajeti zijazo kututengea fedha wakatujengee uwanja kama wanavyojenga sehemu zingine, kama wanavyojenga hapa Dodoma, kama wanavyojenga Arusha, kama wanavyojenga Dar es Salaam, basi na kule kwetu Mtwara waone umuhimu wa kwenda kujenga uwanja huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina suala moja linalonisikitisha na kunihuzunisha, sasa hivi kamari nchini kwetu yaani tunataka tuone kama ni jambo la kawaida sana, ni jambo ambalo halipaswi kufuata sheria ni jambo ambalo lipo. Mimi natambua kwamba hiyo kamari kwa namna moja au nyingine inaongeza kodi ya Serikali, lakini kila kitu lazima kiwekewe utaratibu. Sasa hivi hali iliopo ukienda kwenye vijiji vyetu yaani yale madude ya kamari sijui wanayaitaje yale yamejaa mengi kuliko hata huduma ya maji inavyopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wanatoroka shule, watoto wanajifunza tabia mbaya, watoto wanafanya mambo ya ajabu ili wapate fedha wakacheze kamari. Sasa naiomba Serikali ione umuhimu wa kuwekea makatazo na kuwekea *limitation* mambo haya yafanyike kwa muda ambao ni sahihi na kwa watu ambao ni watu wazima, lakini sasa tukiacha mambo hayo yaendelee kufanyika kama hivi yanavyofanyika, ndio kila siku tutakuja tunajilaumu hapa maadili yameshuka, lakini wakati yanashuka tunayaona yanashukaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hicho kipengele cha kamari naomba kifanyiwe kazi ili kusudi kisiathiri vizazi vyetu. Kwa sababu sasa hivi watoto wanaona kupata hela ni jambo rahisi rahisi tu, hafikirii kama anatakiwa ajishughulishe kwa namna yoyote. Watu wana-*bet* hata mtu yuko kazini anatakiwa atumikie umma yeye ana *bet* tu. Sasa haya mambo tusipoyaangalia kwa jicho la tatu yataligharimu Taifa letu…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nimpe Taarifa mchangiaji kwamba anachokisema ni dhahiri. Sasa hivi hata *dropout* ya baadhi ya wanafunzi wa sekondari inatokana na wao kutoka shuleni wanatoroka, wanakwenda kufanya *betting* kwenye vibanda. Kwa hiyo, Serikali lazima iangalie hii kwa kina ili isipoteze kizazi chetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malapo.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea Taarifa hiyo, nafikiri Serikali imesikia na ione umuhimu wa kufanyia kazi ili tuepukane na mambo haya kwa maendeleo ya watoto wetu na kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la mwisho kabisa, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amesema jamii ya Kitanzania bado haiamini kama michezo ni uchumi na michezo ni ajira. Jamii kwa upande mwingine inaamini Serikali inapaswa iwekeze, itoe elimu na ihamasishe watu wafanye michezo na wazazi waone kwamba michezo hii hususan mpira wa miguu na michezo mingine ni ajira na inaweza ikamtoa mtoto kupata kipato, lakini pia kuongeza uchumi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Khadija Aboud, ajiandae Mheshimiwa Khadija Taya, Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Matiko.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuipongeza Wizara hii kwa juhudi mbalimbali wanazofanya kuhakikisha sekta hii inakua katika nyanja zake zote, pia nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wasaidizi wake wote katika kuhakikisha Wizara hii na fani zake zote inasonga mbele na inaleta tija kwa wananchi na kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu napenda nijikite kwenye lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ni rasilimali, uchumi, bidhaa, ajira na utambulisho wa Taifa letu. Napenda kuwapongeza wote waliochukua juhudi mbalimbali za kuhakikisha Kiswahili kinakua hapa duniani na kinatambulika duniani na *UNESCO* kuitambua, sasa hivi nchi mbalimbali zinaendelea kuanzisha mafunzo ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila kinachoelea kimeundwa. Pia kila vinavyong’ara vimegharamiwa, kwa maana hiyo Kiswahili kimegharamiwa na kimeundwa. Nawapongeza wote waliotoa mchango kuhakikisha Kiswahili kimefika hadi hii leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka jana nilisema na nimewataja wengi katika sekta ya utangazaji pamoja walimu mbalimbali waliokistawisha Kiswahili huko duniani. Kwa mfano Bwana Ramadhani Ali wa *Radio Prague Czechoslovakia* na baadaye akaenda *Radio Deutsche Welle* na *Radio Berlin International.* Mheshimiwa Profesa Haroub Othman alianzisha Idhaa ya Kiswahili China, hao ni wachache tu. Vilevile sikuwasahahu akina mama Muhaiminna Fasil Sauti ya *Radio - America,* Umulkher Mohammed - *Deutsche Welle,* Zeyana Seif *BBC*, ni wengi. Ninatoa mfano kwamba kuna watu walijitolea nguvu zao na wakati wao kuhakikisha Kiswahili kinapaa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyosema kuwa Kiswahili ni lugha ya Pwani kwa maana ya neno Swahili lenye maana ya Pwani, kwa maana hiyo watu walioingia kwenye Pwani wakaungana kwa pamoja wakatengeneza maneno ndiyo ikapatikana lugha ya Kiswahili zikiwemo na lugha zetu za asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa, tumetohoa maneno mengi kwenye lugha mbalimbali za kigeni (Kiingereza, Kireno, Kijerumani, Kifaransa, Kijapani, Kigiriki, Kiitaliano, Kituruki, Kihindi). Kihindi chenyewe kuna Kibujurati, Hindu na Punjabi, hicho ndicho kihindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema sasa hivi kumetokea istilahi mpya za Kiswahili ambazo zinatungwa, lakini nyingine hazifuati utaratibu, kwa sababu utaratibu wa kutafuta hizi istilahi ni lazima hili neno la Kiswahili liwe halipo kwenye lahaja zetu za Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano, sasa hivi kuna neno linaitwa “guruguru,” wamelitafsiri kwamba ni ngurumo, sasa hili ngurumo si lipo na ndilo lipo duniani kote linatumika, kuna haja ya kuleta tena mambo ya maguruguru kwenye ngurumo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kiporo kinajulikana dunia nzima kwa wanaosoma Kiswahili, leo kuna neno “bario” tunakwenda wapi? Ndiyo ninasema kwamba hii lugha yetu iwe nyepesi na inayoweza kusomesheka, kuzungumzika na kuandikika ndipo soko

litakua, vinginevyo tutakimbiwa, watakwenda kutafuta maeneo yanayofundisha lugha kwa wepesi na kwa urahisi. Kwa sababu wengine wanachotaka ni kuzungumza na kufahamu tu, hawataki kufanya mitihani, sasa hao wanaotaka kujua kuzungumza, kozi za miezi miwili, miezi mitatu, soko hili litatuponyoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tukiendelea kujaza maneno tu, mengine kama ya kichokozi, hata ukiyatamka unaona taabu. Nasema taratibu zifuatwe katika kuongeza haya maneno.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Baraza la Kiswahili la Taifa, kuna mjumbe mmoja tu kutoka BAKIZA. Nashauri watakapounda tena waongeze idadi ya wajumbe, wachukue kwenye sekta ya utamaduni wawaongeze, kama haiwezekani wanapoandaa haya maneno kwa sababu hii ni lugha ya Taifa waongeze uwakilishi, siyo kukaa kikundi cha watu wachache wakatafuta maneno tu wanajaza, hii lugha tutaipotosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninakitetea Kiswahili na nitakipambania Kiswahili kama watangulizi wetu walivyoanza kukitetea, kwa sababu tunapotoa maneno tutaacha maneno gani wakati Kiswahili hiki kanuni - Kiarabu, Kiswahili, Kihindi; taabani - Kiarabu, Kiswahili, Kihindi; wilaya – Kiarabu; jeshi – Kiarabu; askari - Kiarabu, babu, dobi, kanakana ni Kihindi, ni lugha ya Pwani. Sasa tutakapoanza kila siku tunabadilisha maneno tutajikuta siyo Kiswahili tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba kwa lugha yetu ya Kiswahili wakalimani, walimu, waandishi wa vitabu wajengewe uwezo na waongezewe bajeti ya fedha ili kuweza kumudu lugha mbalimbali za Kimataifa ili kuweza kukamata hili soko la Kiswahili kwa upande wa ajira. Tuna tatizo sana la changamoto ya ajira, soko la ualimu linahitajika, ukalimani na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuongeza hapa nikiachia mambo ya Kiswahili, nataka niseme vitu vifuatavyo na nianze na suala la kuweka kumbukumbu kwenye tunu zetu za Taifa. Wizara mnajitahidi, mnaweka lakini kwenye fani za nyimbo za hamasa na nyimbo za kizalendo, kwa mfano Wimbo wa Taifa,

Wimbo wa Tanzania Tanzania, tunataka kuwasha Mwenge, Tazama Ramani, waweke kumbukumbu za nani alitunga hizi nyimbo, kikundi gani kiliimba, mwaka gani wimbo huo ulipatikana ikiwemo jina la Tanzania. Kwa sababu sasa hivi historia inapotoshwa, kikundi cha nne kinaimba inakuwa wimbo ndiyo wa kwake, lakini kumbe maskini aliyeutunga amekwishakufa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aboud, ahsante.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Khadija Taya, wajiandae Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru tena na tena kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara yetu au Wizara yangu rasmi ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali kabisa naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uhai na afya japo sauti yangu leo imekauka kidogo, lakini si haba namshukuru *Allah* nimefika hapa nilipofika, kwa hiyo, namshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, kusema kweli nimeelemewa, wasanii tumeelemewa kwa mambo anayofanya Mheshimiwa Rais katika Wizara hii, sijui asiyeshukuru ni kafiri na asiyeshukuru kwa kidogo hawezi kushukuru kwa kikubwa na sasa tunashukuru kwa kikubwa na kwa kweli Mheshimiwa Mama Samia, Mwenyezi Mungu akujalie mwaka 2025 mitano tena. Vijana wako, wasanii na wanamichezo tutakuzungumzia Mama Samia. Mama Samia umehamasisha michezo na leo hii hata mtoto wangu ambaye alikuwa hawazi *football* anapenda mpira sana kwa sababu ya Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hamasa yake ya kuwapa vijana shilingi milioni tano, shilingi milioni kumi imeleta chachu sana katika mpira wetu na *sports* zetu za nchi hii. Kwa hiyo, naomba nikushukuru sana mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Wizara kwa kweli imebarikiwa sana, imebarikiwa kwa sababu ina viongozi wenye weledi, kusikiliza, kutambua changamoto na kuzitatua, wenye kufahamu undani ambapo Kaka yangu pale Mheshimiwa Mwana FA (Hamis Mwinjuma) amekuwa kwenye sanaa hii kwa muda mrefu. Pia ana ufahamu mzuri sana wa mambo ya sanaa na amekuwa msaada mzuri sana katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna wakili msomi pale, kaka yangu Dkt. Ndumbaro kwa kweli tunakushukuru sana kwa uelewa wako na kwa namna gani unavyomuachia kijana wako kutoa mawazo. Nina uhakika kuna mambo mengi sana unamsikiliza kwa sababu ukiamini ana *experience* na utaalamu wa kutosha. Kwa hiyo, naomba nikushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze kwa mikakati ambayo mmeiweka. Tunaanza kwenda kuona hii Wizara inakwenda kufanya kazi kwa namna gani. Kwanza, kwa kuongeza bajeti tayari mmeonesha nia ya dhati ya hii Wizara kwenda kufanya kazi nzuri ambayo inakwenda kukomboa vijana wetu, inakwenda kuondoa tatizo la ajira. Kwa sababu katika sanaa vijana wengi tulijiajiri na wengine wamejiajiri kwa sasa na kuna maeneo mengi tofauti tofauti kupitia sanaa hii, watu wanajiajiri.

Kwa hiyo, kukuza Wizara hii kwa hiyo bajeti naomba sana nikuombe Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu hizi pesa zitoke zote. Tunakuomba shilingi milioni 285 zitoke zote kwa 100% kwa sababu mikakati inaonekana, mambo yanaonekana. Basi ikifika mwakani katika bajeti tuambiwe asilimia kubwa ya pesa hizi imeweza kutoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niendelee kuipongeza Wizara hii kwa mkakati wa viwanja vipya na mikakati

ya kuendeleza maadili yetu. Wameamua sasa kurudi nyuma na kuanza kufundisha masuala ya maadili. Mimi naomba mwende kuwafundisha maadili wasanii wetu kwa sababu gani nasema mje kufundisha wasanii wetu? Ni kwa sababu sasa maadili yanaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama alivyosema mama yangu Mheshimiwa Mwanakhamis pale, nyimbo zenye matusi zimekuwa zikiimbwa hadharani, nyimbo zenye maneno ya ajabu sana zimekuwa zikiimbwa. Niwaambie ukweli kabisa kutoka moyoni, Kaka yangu Babu Tale leo nakusemea, yeye ni msimamizi wa wasanii, lakini anavyosikiliza hizo nyimbo hawaambii hizi nyimbo hazina matamshi mazuri. Pia hapo hapo nyumbani kwake hakuna *bongo fleva* inayosikilizwa na mtoto wake, hakuna *bongo fleva* inayosikilizwa na mtoto wa Babu Tale, lakini watoto wetu huko mtaani ambao hawana wazazi wa kuwasimamia..

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, watoto ambao hawana wazazi wa kuwasimamia wanaweza kuharibika kwa sababu ya miziki ambayo tunaitoa sasa hivi haina lugha nzuri, haina tafsida nzuri. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Babu Tale.

**TAARIFA**

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa Dada yangu na msanii wangu, maana Mheshimiwa Keisha mimi ndiyo msanii niliyemtoa, hata huko nyuma kama alikuwa akiimba kwa maadili mimi ndiye nilikuwa nikimweleza maadili. Kwa hiyo, anatakiwa akubali kwamba mimi ni meneja wake wa kwanza, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Keisha.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa yake ninaipokea kwa sababu ni kweli alikuwa ni meneja wangu, lakini alinifundisha niimbe; "Nipe zawadi ya pendo lako, *honey,* sina mwingine zaidi yako ewe *baby." (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Keisha.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nyimbo ambayo naimba hakuna neno hata moja ambalo mtoto hawezi kusikiliza, lakini sasa hivi wasanii wake wanaimba nyimbo ambazo watoto wetu wakiimba tunaona aibu pale nyumbani kwetu. Kwa hiyo, maadili yale umeyasahau sasa hivi uko kibiashara zaidi, kwa sababu ndiyo biashara inataka hivyo tunasema. Kwa hiyo, Taarifa yako ninaipokea, lakini ujumbe umekufikia Mheshimiwa Babu Tale.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Wizara yake kwa kutoa mikopo. Hii mikopo imekwenda kufanya kazi nzuri sana, imekwenda kuwasaidia wasanii wengine ambao tayari walikuwa wanakwenda kwenye mihadarati. Leo hii wana uwezo wa kuchukua mikopo katika Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezzo na wakaweza kurudisha vipaji vyao na tunawaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa na takwimu nilizonazo hapa ni kwamba mikopo au madeni sugu ya watu waliokopa kabla ya kutambulisha benki ilikuwa ni shilingi milioni 259. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kusema mikopo hii ipitie benki. Baada ya mikopo hii kupitia benki, sasa hivi *CRDB* kuna shilingi milioni 23 tu ambao ni watu 11 wakati mwanzo ilikuwa ni watu 26 waliokuwa na madeni sugu. Vilevile *NBC* hakuna mdaiwa sugu hata mmoja. Hongereni sana na hii inaonesha ni jinsi gani ambavyo Serikali inafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe rai kwa wasanii wenzangu, waendelee kukopa, lakini wakumbuke kulipa kwa sababu mikopo hii inakwenda kuwasaidia wasanii wengine. Wao wanaporudisha huu mfuko ndiyo unaweza kwenda kufanya kazi vizuri kwa ajili ya kusaidia wengine. Kwa sababu benki peke yake

imeweza kutoa *3.1 billion* na mfuko umeweza kutoa shilingi bilioni moja.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija, ahsante.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hii ni hatua nzuri sasa hivi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija, ahsante.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul, wajiandae Mheshimiwa Matiko na Mheshimiwa Shabiby.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi na mimi nichangie bajeti ya Wizara yetu ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa jinsi ambavyo amekuwa akitulinda kila mmoja wetu, hata tunapopitia kwenye matatizo, Mwenyezi Mungu ana namna zake za kutulinda. Ninamshukuru kwa afya ambayo ametupatia, lakini kwa jinsi anavyoendelea kulinda Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama niseme leo kwa ujasiri kwamba Watanzania tuna sababu ya kuwaombea viongozi wetu, tuna sababu ya kumuombea kila mmoja wetu, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wasaidizi wake na Serikali yake kwa dhamana ambayo wanayo mikononi mwao kuwatumikia Watanzania, wanapitia mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata mimi nilipopitia namshukuru Mungu kwamba amenipa uvumilivu, siyo rahisi na sijategemea kusema na sijategemea hata leo kwamba ni hoja yangu, nawashukuru kwa maombi yenu wale Watanzania wenye nia njema, viongozi na Wabunge wenzangu. Ninaamini kwamba

maombi ya Watanzania ndiyo yananifanya niendelee kusimama na kufanya majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeendelea kuwa mtulivu, nimepisha vyombo vya uchunguzi wamalize kazi yao, *then* tutajitokeza tutasema ukweli. Siku ya leo nimesimama niendelee na kazi za Kibunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa upendo wake, ameniamini kama binti yake, amenituma kwenye maeneo mengi sana kwa majukumu ambayo amenipa. Ninamshukuru kwa jinsi ambavyo ni mama mvumilivu, msikivu, mwenye upendo, mzalendo anayependa Watanzania. Mheshimiwa Rais, Mungu aendelee kukulinda, Watanzania kazi yetu ni kuendelea kukuombea. Wananchi wa Babati hatuna deni na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maendeleo ambayo tumefanyiwa katika Jimbo letu ni miradi ambayo miaka mingi hatujawahi kuiona. Chini ya Mama Samia, Mji wetu wa Babati kwa miradi ambayo tumefanyiwa ningeeleza siku nzima na kila Mbunge angeweza kueleza, miradi ni mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara hii ya Michezo, ninakupongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa unayofanya, wewe ni Kaka yangu, nimefanya kazi na wewe, ni kiongozi ambaye unajua kuunganisha watu na kushirikisha watu. Mheshimiwa Waziri, Wakili Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro ndiyo maana Wizara hii hata Mheshimiwa Rais amekuelewa na amekuongezea bajeti kutoka shilingi bilioni 30 mpaka zaidi ya shiingi bilioni 200. Wewe na Naibu Waziri pamoja na timu nzima na watendaji wenzako hongereni sana na mnafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana mimi sina wasiwasi katika bajeti yao. Ninafahamu kwamba kwa ongezeko la bajeti hii yale mambo mengi ambayo yalikuwa hayajatimizwa, chini ya Mama Samia na uongozi huu Mheshimiwa Waziri na timu yako

yatakwenda kutimizwa. Hongereni sana kwa ongezeko la bajeti.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesimama kwa jambo moja tu mahsusi ambalo natamani kulisema. Ningeweza kuchangia kila eneo, lakini niruhusu nichangie jambo moja tu mahsusi. Mheshimiwa Waziri, sera yetu hii ya maendeleo ya michezo inataka michezo iwe jumuishi na taasisi zishiriki. Wewe unafahamu maana umenifundisha hayo na umenielekeza hayo, tumehubiri pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wetu wa Babati ni miongoni mwa halmashauri chache ambazo zimetekeleza Sera ya Maendeleo ya Michezo kwa vitendo. Halmashauri, Ofisi yetu ya *RAS* chini ya Mkuu wa Mkoa na timu nzima ya Wana-Manyara tumejenga uwanja wa *Tanzanite* pale Manyara na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuja kuzima Mwenge wa Uhuru katika Mji wetu wa Babati mwaka jana. Pamoja na ule uchanga wa miundombinu, lakini alikubali kuileta Tanzania Babati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa alifahamu kwamba Manyara ni sehemu ya Taifa lake, lakini Manyara kuna jambo wamefanya. Mheshimiwa Rais pamoja na timu yake wali-*appreciate* wakatuzimia Mwenge pale Babati. Tuliwapokea pamoja na mapungufu yetu ya kihoteli na kimiundombinu, lakini mkatuvumilia mkawa pamoja na sisi. Mheshimiwa Rais tunakushukuru na Serikali tunaishukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri, Kombe la *FA* chini ya udhamini wa *CRDB* mlituletea, mkatushirikisha kwamba fainali mtafanyia kwenye Mkoa wetu wa Manyara. Naomba niwashukuru sana hii nia ni njema. Niishukuru *TFF* chini ya Rais Karia, mlijitokeza wenyewe mkasema tunakuja Manyara na tuliwapokea kwa upendo. Tulijua ni upendo ule ule wa Mama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu unaendelea juu ya Wana-Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wana-Manyara wamefanya kazi kubwa. Nimpongeze Mkuu wetu wa Mkoa, Dada yetu Queen. Pia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tunakushukuru kwa kutuletea Mheshimiwa Queen ambaye ni *RC* anayeshuka kule chini, anazungumza na watu wake na wilaya zake. Amehamia na timu yake Babati Mjini chini ya *DC* wetu Lazaro Twange, Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Abdulrahman Kololi, Madiwani, Mkurugenzi wetu Ndugu Pendo, timu nzima pamoja na wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanza maandalizi ya kupokea ugeni huu, lakini ghafla jana tumaini la Wana-Babati na Wana-Manyara lilififia baada ya kuona kwamba fainali hizi sasa zimepelekwa sehemu nyingine. Naomba nieleweke wazi kwa sababu nimejifunza Watanzania wengi wetu tunaweza tukawa tunatengeneza maneno ambayo hata mtu hajasema, sina tatizo kupelekwa fainali hizo popote, tatizo langu ni moja tu Mheshimiwa Waziri, Wana-Manyara walipojiandaa tulienda pale tuka-*reallocate* bajeti zetu, tukachukua hela za halmashauri na wadau tukawekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia watu wamekopa na wameweka mali-kauli bidhaa wafanye biashara, lakini tumaini lao limefifia. Mimi naelewa kwamba *TFF* walikuwa wana nia njema kabisa na hata kuhamisha ninaamini wana nia njema kabisa kwa sababu wametaja sababu za kimiundombinu kwamba ule uwanja ukamilike. Nikuhakikishie Mheshimiwa Waziri mpaka jana timu yetu ya *engineers* walikuwa uwanjani wakipambana *deadline* ya terehe 28 Mei kwa Manyara.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Pauline Gekul, mwaka 1985 Mheshimiwa Mkuchika aliileta Simba ikacheza Mbulu kwenye Uwanja wa Julius Nyerere na iliwezekana. Mimi nadhani Mheshimiwa Waziri ana haja ya kutoa kauli ili Wana-Manyara na majirani zake wakaelewa kuhusiana na kuhamishwa kwa fainali hii. Hii ilikuwa taarifa yangu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, napokea Taarifa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchana wa leo Wabunge wa Mkoa wa Manyara ilibidi tukae tuangalie *messages* ambazo tunapokea kwa wananchi wetu, hali si nzuri na taharuki ni kubwa. Hawana tatizo kuondoa hiyo fainali, mmeondoa katika dakika za mwisho, tumepambana lakini mmeondoa na sasa wananchi wako kwenye taharuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu Mheshimiwa Waziri kupitia *TFF* njooni basi mfanye mashindano mengine makubwa katika mkoa wetu katika ule uwanja. Hatuna ubaya kabisa, asiyeshukuru kwa dogo hata kikubwa hashukuru. Mheshimiwa Karia, Rais wa *TFF* nakushukuru lakini tunaomba sasa ili ule upendo wa Wana-Mayara na ile kiu ya kuona timu kubwa zikicheza pale na uwekezaji tuliofanya mtuletee mashindano pale ili tuwafute machozi na maumivu ambayo wananchi wetu kwa sasa wanayapitia. Kupitia *messages* ambazo tunazo kwa kweli hali si nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nina imani na Serikali na Mheshimiwa Waziri naamini utalitolea ufafanuzi kwa sababu kwenye barua ya *TFF* wamezungumzia pia suala la usalama. Wana-Manyara wanauliza usalama upi? Basi tutoe ufafanuzi kwa sababu tunaishi kwa amani na kazi zinafanyika. Kama ni usalama wa kimichezo kauli yako Mheshimiwa Waziri itatusaidia. Nikuombe kauli yako tu kabla mwaka huu haujaisha fanyeni jambo kwa ajili

ya Wana-Manyara ambao wamejitokeza kujenga ule uwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara hii wanafanya mambo makubwa sana katika mji wetu wa Babati. Wanajenga hata *center* kwa ajili ya kuwafundisha vipaji mbalimbali kwa sababu wanafahamu Mkoa wa Manyara ni miongoni mwa mikoa ambayo inatoa wanamichezo wa aina mbalimbali hususani riadha, mpira wa miguu na kadhalika. Mheshimiwa Waziri *motivation* yetu ni hizo timu kubwa zije pale ku-*devote our resources*, wadau kujenga ule uwanja na heshima ambayo Serikali imetupa na ninyi basi msituvunje moyo, mtusaidie katika hilo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipatia fursa na mimi kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ambayo Serikali ikiamua kuwekeza kwa kupeleka fedha nyingi sana itaenda kuinua uchumi wetu. Wizara hii ni kiini kimojawapo cha kuweza kutangaza utalii wetu. Nitaenda kuchangia katika maeneo yote ya michezo, sanaa na utamaduni kulingana na muda utakavyo niruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na michezo; tumekuwa na programu ya mashindano ya michezo katika shule za msingi kwa maana ya UMITASHUMTA, sekondari UMISSETA na vyuoni UMISAVUTA. Sasa sijui kama Serikali imeshafanya tathmini kuweza kuona mashindano haya yameleta tija gani katika Taifa kwa maana ya kwamba wanashiriki michezo mbalimbali. Mashindano

haya yameweza kutoa vipaji vipi ambavyo vimetuwakilisha kitaifa na kimataifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania leo tukisimama hapa katika *angle* ya michezo hatuwezi tukajitanabaisha kwamba Tanzania tunajulikana kwa michezo fulani. Kwa mfano nchi zetu jirani hapa za Kenya na Ethiopia nilikuwa hata naangalia michezo na mambo yanayoendelea, wenyewe wamejitanabaisha kwenye riadha, sisi Tanzania tunasikika wapi? Maana yake hatupo kabisa ambapo tunaelekea zaidi ya sasa hivi tunavyoenda enda kwenye *football.* Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kweli kwa jinsi alivyowekeza sasa hivi walau kwa hizi *bonus* alizozitoa kwenye michezo kwa maana ya *football* tuna afadhali, ingawa hatufiki kule kabisa tunakotakiwa kufika, nikataka nijue kama Serikali imeshafanya tathmini mtatueleza hapa na kama hamjafanya mkafanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mashindano haya ambayo tunaendesha ya UMITASHUMTA, UMISSETA na UMISAVUTA yamekuwa na tija? Kama hayana tija na kuna sehemu yana-*fail* ni sehemu gani ili tuweze kurekebisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mashindano yangetumika vizuri tungeweza kuwa na vipaji maana yake mashindano yale yana michezo mbalimbali siyo *football* tu ambayo imesheheni kwenye ripoti ya Waziri hapa. Yana *football*, *netball*, *basketball*, *volleyball*, *handball,* mitupo mbalimbali, *long jump and short jump, swimming* na kila kitu, lakini hapa tuna-*concentrate* kwenye mpira wa miguu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kushauri tu na nilivyokuwa nikiongea hapa Serikali tuanze. Najua mna mikakati mbalimbali ambayo kutekelezeka ni muda mrefu. Tuanzishe mwendelezo wa vipaji vinavyoibuliwa kwenye UMITASHUMTA tuwe na shule maalumu ya michezo ya shule ya msingi. Wakishaibuliwa wale wapelekwe pale kuwepo na *scholarship,* msisubiri ambayo mmeitunga sasa hivi ya kujenga kila halmashauri au kila wilaya tuanzishe saa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shule moja tu inatosha tuwe na shule maalumu ya michezo ya sekondari. Sasa hivi tuna Chuo cha Maendeleo cha Malya tu, Chuo cha Maendeleo tayari ni *advanced level,* tunavyokuwa tunawapata kwenye UMITASHUMTA waende kwenye shule maalumu ya shule ya msingi, tunapokuwa tunawapata kwenye UMISSETA wapelekwe kule. Mwisho wa siku tutakuwa na vipaji mbalimbali kwenye *discipline* mbalimbali za michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo pia litaenda kupelekea kuendeleza miundombinu ya michezo na *sport center.* Mimi nilishasema mara kadhaa hapa kutumia *CSR* kwenye halmashauri zenye uwezo au mapato ya ndani tuwe na *sport center* kwenye kila halmashauri ambapo haya mashindano yakifanyika yaweze kwenda kufanyikia pale ili yawe na *sport facility* kwa hii michezo yote. Sasa hivi UMITASHUMTA na UMISSETA inafanyika, ukienda viwanja wanavyochezea vinasikitisha sana, haitoi taswira nzuri wala kuweza kuendeleza vipaji vile. Hili linawezekana, pelekeni miongozo, shirikianeni na TAMISEMI na Wizara ya Ardhi watenge na waweze kuwa na viwanja ambavyo ni stahiki kwa kuanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Waziri Mkuu aliongea hapa siyo tu kutengwe nafasi kwa ajili ya *jogging,* tunajua kuna *jogging clubs* nyingi sana Tanzania sasa hivi zimeanzishwa. Pia tunajua katika kukimbia na michezo mingine ni afya kwa Taifa letu kwani tutapunguza hata magonjwa na imekuwa kwamba inakuwa ina-*contradict* na magari kuwekwa pembeni watu waweze kukimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tulikuwa Rwanda, wenzetu wale wamejenga *night running tracks* kwa usiku. Kwa nini tusijenge Tanzania kwenye majiji na miji tuwe na *night running tracks* ambapo Watanzania wakitoka kazini usiku wataenda, wataweza kukimbia bila kusababisha *congestion* kwingine na ajali zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye ujenzi wa barabara hii sasa katika wilaya na kwingineko kwa nini tusitenge eneo? Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi uko hapa, mnapojenga barabara

zetu tengeni eneo la watu waenda kwa miguu ambapo mtaliweka kiasi wakimbiaji watakuwa wanakimbia pale na wataondoa *congestion* za magari kuwekwa pembeni ili watu waweze kukimbia na kufanya mazoezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukifanya hayo tutaendelea si tu kwa afya ya Watanzania, lakini tutaibua vipaji mbalimbali. Watanzania wanariadha na wenye vipaji mbalimbali vya michezo ni wengi sana, lakini Serikali pamoja na kushirikiana na wadau hatujaweza kuwekeza vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho pia nimekuwa nikiongelea hapa ni kuhusu kujenga *arenas.* Mmeainisha lakini hatuoni mipango mikakati. Wenzetu wa Rwanda na naendelea kufanya *reference* pale pia, *BK Arenas* ile ina *capacity* ya watu 10,000. Wamewekeza pale dola milioni 104 lakini *return on investment* ni ajabu kubwa sana, lakini ni kitega uchumi tosha. Pale kuna michezo mbalimbali ya kidunia na Afrika inafanyika kama *basketball, volleyball, tennis, concert* mbalimbali na *conference* mbalimbali zinafanyika pale na wanapata mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashindwa nini kuchukua hata *joint venture?* Wenzetu walikuwa na *Rwanda Housing Authority* na kampuni moja kutoka Turkey wakajenga. Tanzania tunashindwa kufanya hii *joint venture* na watu wengine tukajenga *arenas* ambazo ni za maana kabisa? Ile ni ya watu 10,000 kwa *East Africa* lakini kwa Afrika, Senegal wana *arena* yenye *capacity* kubwa ambayo inachukua watu 25,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunashindwa nini Tanzania? *We have all it takes* na watu wetu wanapenda michezo. Hebu tuamue, tumempata Rais ambaye ana *political will* ya kuendeleza michezo. Tunakwama wapi kuhakikisha kwamba tunamtumia Rais huyu mwenye *political will* ya kujenga michezo tumpe mipango mikakati ya kuendeleza michezo Tanzania, atoe fedha ili tuweze kuwekeza kwenye michezo mbalimbali na siyo *football* peke yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, mwezi ujao tarehe tisa watu wa *basketball under 18* wanaume kwa wanawake wanaenda Rwanda kushiriki *zone five*. Wale watu huwa wanajichangisha changisha. Wameleta *proposal* Serikali muweze kuwasaidia *only 57 million shillings,* mnashindwa wapi? Wakienda Uganda wakashinda wataenda *South Africa* kushiriki Ligi ya Afrika, wakishinda wataenda Ligi ya Kidunia, *57 million shillings* wekezeni hata kwenye *basketball* tusijiwekeze tu kwenye *football.* Watanzania sasa hivi wameamka kwenye michezo mbalimbali kama vile riadha, *basketball, netball* na *volleyball.* Tuwekeze na huko pia kuibua vipaji mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitakuwa sijatenda haki kuhusu *issue* ya Sekondari ya Orkeeswa ambayo iko Monduli. Mwekezaji yule Ndugu Peter Luis amejitoa sana, amejenga viwanja vya *basketball* zaidi ya tisa kwa shule ya msingi na sekondari ambavyo vinaibua vipaji vya watoto wetu mbalimbali. Pia amekuwa akikusanya Watanzania yuko kule kwenye jamii ya kimasai anakusanya Watanzania kuweza kuibua vile vipaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali tusimchukue yule kama *role model* tutafute na wadau wengine kwenye mikoa yetu mbalimbali ambao wanaweza wakajenga viwanja walau tuwe na kiwanja kimoja cha *basketball* cha maana cha kubeba watu hata 500 mpaka 1,000 katika mikoa yetu ambapo tutaweza kuendeleza michezo ya *basketball? (Makofi)*

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa.

**TAARIFA**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumwongezea Taarifa mchangiaji anayechangia vizuri. Tanzania tuko polepole sana katika kupokea mawazo mapya. Kuna *NGO* moja ilijitolea hapa kujenga *arena,* ilikuwa inataka

kufanya hapa na Kenya, lakini Kenya wamewapokea kwetu bado tuna mbwayambwaya, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeipokea, lakini pia kuna *Premier Bet* wamejenga viwanja Zanaki, wamejenga viwanja pia pale Kigamboni na wanataka wajenge hapa Dodoma. Tuwatumie hawa tutoe ardhi, tusi-*by time*. Wakiwa wanatokea washirikiane na Waziri wa Ardhi muweze kutoa viwanja.

*(Hapa kegele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja.

**NAIBU SPIKA:** *Basketball* imekwisha kazi kaa chini. *(Kicheko)*

Tunao wageni waliopo Bungeni jioni hii, tumepokea wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni walimu 41 kutoka *Songea Boys.* (Makofi)

Wapo pia maafisa watano kutoka Klabu ya Yanga Idara ya Wanachama, Mashabiki na Matawi. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wachezaji wawili wa zamani kutoka *TFF* Ndugu Boniface Pawasa na Ndugu Jonas Lunyamila. *(Makofi)*

Kuna wageni watatu kutoka *Tanzania Golf Union* na pia wapo wagebi kutoka Shirikisho la Sanaa za Ufundi na Meja Mstaafu na Mwandishi wa Vitabu vya Historia Ndugu Minael Hossana Mdundo, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wanafunzi 70 wa Chuo cha Mipango na Maendeleo ya Vijijini kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Shabiby, ajiandae Naibu Waziri.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza niwashukuru ndugu zangu wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza mimi nataka niwaombe tu na huwa naongea siku zote na Waziri pamoja na Naibu Waziri kwamba pale Gairo, CCM imejenga uwanja mzuri wenye *pitch* nzuri ambayo inakubalika kimataifa na ule uwanja unachezewa na ligi kuu. Umeshachezewa na *Fountain Gate* na *Mtibwa Sugar,* lakini tunaomba ile misaada mnayotoa sehemu nyingine ya kuweka zile zulia kwa maana ya majani bandia basi mtupatie pale Gairo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni Uwanja wa Dodoma; Uwanja wa Dodoma umezungumzwa siku nyingi toka Hayati Magufuli na sasa hivi pamoja na kuwa unajengwa, lakini naona *speed* yake ni ndogo na Dodoma ni eneo muhimu, lakini naona sasa kama mnataka kuanza kulisahau. Viwanja hivyo vingine vya Arusha vijengwe ni sawa eneo linalofaa la Arusha na sehemu nyingine, lakini mwongeze *speed* kwenye uwanja wa Dodoma. Watu wengi walikuwa wanasubiri hiyo ahadi, lakini mpaka leo dalili zake siyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ninachotaka kuongea najua dakika nilizopata ni chache, lakini Wizara na Bodi ya Filamu mimi sioni kitu gani kinachofanyika kizuri kwenye filamu. Niwapongeze wanatunga *story* nzuri, wasanii wako vizuri, lakini hizi filamu za Kitanzania sasa hivi zimekuwa zinaiga sana mambo ya nje. Sasa hivi sasa filamu za Tanzania zimekuwa zinafundisha uganga wa kienyeji na uchawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kila filamu ya Tanzania lazima awepo mganga, mchawi na msukule. Sasa mimi hapa sijielewi, hii ni moja ya kusaidia kufundisha watu uchawi na uganga au ni filamu ambazo zinafundisha maadili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiondoa maadili, lakini basi wenzetu wa Ulaya kule mkiiga utakuta *robot* linaongea, *robot* linafanya hivi au teknolojia iko hivi. Sasa ninyi mara msukule katokea hapa, mara msukule kaja sijui kafanyaje, sasa hii kitu gani? Maana yake lazima tuongee ukweli kwamba mnawaharibu watu kisaikolojia. Watu wengi wanaharibika *psychologically* hapa Tanzania ni kwa ajili ya vitu kama hivyo vya hovyo hovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukamkuta mtu sasa hivi anashinda kwa mganga kwa sababu ameona kwenye filamu kumbe hata uchawi nao upo na mtu anafanikiwa. Ukienda watoto wadogo hawa nao wanaharibika. Sasa hivi hawa watoto wanaoangalia filamu wote mjue kabisa kwamba mnaandaa wachawi na waganga wa baadaye na ndiyo ukweli huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninyi Wizara msipokuwa makini na ninyi Bodi ya Filamu hii kazi yenu ya kila sinema ya Tanzania 90% ni mganga wa kienyeji, mchawi na msukule. Sasa muangalie hii kitu ni bora isiwepo kabisa kama *style* ndiyo hii ya kufundisha watu uchawi na ndiyo maana Watanzania wengi sasa hivi badala ya kufanya kazi, hawafanyi kazi wamekuwa tu wanashinda kwenye mitandao, wanashinda huku, wanakuwa wambeya, wanakuwa hivi kwa sababu hakuna vitu vya maana ambavyo vinawafundisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake akienda labda ku-*relax* aangalie filamu za kibongo kama watu wa vijijini kule hawezi kuangalia sinema za Ulaya wala wapi kwa sababu wakati mwingine lugha kidogo inakuwa lugha gongana kidogo. Sasa akiingia kwenye filamu za Kitanzania anaona hapa mtu alikuwa anashida, akaenda kwa mganga, akafanikiwa. Sasa unategemea nini hapa kama siyo kufundisha uchawi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba, leo sina mambo mengi sana, lakini Bodi ya Filamu na Wizara muangalie haya masuala, yanaharibu watoto. Juzi juzi hapa kuna mtoto mmoja aliumwa alikuwa anaongea na mtu wa saikolojia pale Muhimbili, akaambiwa huyu mtoto wako ameangalia sinema ya kutisha.

Mara mtoto analia anamtaja jirani fulani ananiroga, fulani ananiita. Yule mtu wa Muhimbili pale akamwambia akasema, huyu mtoto anaangalia sinema za kutisha, za uchawi. Akamfanyia *counselling* yule mtoto akatulia, lakini walishaanza kumwitia wachungaji, mashekhe, mara huyu ana pepo na mara huyu ana nini, kumbe pepo lenyewe limetokana na kuangalia sinema za kutisha za uchawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Bodi ya Filamu wawe makini na kuonesha sinema za uchawi kwa sababu wanaharibu watoto kisaikolojia na wanaharibu hata watu wazima. Hata hapa kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanakwenda kwa waganga kwa ajili ya kuangalia angalia hizo picha zenu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro na Naibu wake Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Katibu Mkuu Bwana Gerson Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Suleiman Serera pamoja na timu ya wataalamu kutoka Wizarani na taasisi zinazosimamiwa na Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu leo utajikita kwenye umuhimu wa kuhifadhi na kuendeleza tamaduni na sanaa zetu ambazo ni urithi wetu wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ya Tanzania imebarikiwa kuwa na utajiri wa tamaduni na sanaa mbalimbali kutoka katika makabila zaidi ya 120 yaliyoko nchini. Kila kabila hapa nchini lina sanaa, tamaduni na desturi zake za kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Wizara ya Utamaduni ihakikishe inazitafuta tamaduni zetu kutoka kwenye makabila yetu na kuziandika na kuzihifadhi kwa njia ambayo

itaendeleza urithi wetu huu wa kitamaduni. Hii ni kutokana na ukweli kwamba ujio wa utandawazi unaelekea kuvuruga tamaduni zetu za asili. Kwa kuweka haya mambo kwenye kumbukumbu zetu, hii itahamasisha vijana wetu kuwa na upendo na kujivunia tamaduni za makabila yetu na ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ikitekeleza haya, tamaduni za makabila yetu yatajulikana kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine, hivyo basi kuwapa watoto wetu fursa ya kujifunza na kufahamu asili yao.

Mheshimiwa Naibu Spika kwenye kutekeleza hili, ni vyema Wizara ikatumia teknolojia za kisasa kuhifadhi na kutawanya tamaduni zetu kwa wadau mbalimbali na dunia kwa ujumla. Tamaduni zetu zikiwa kwenye maandishi, itavutia watu kutoka maeneo mengine duniani kuja kujifunza vitu vyema vya makabila yetu. Kwa yale mazuri tunayofanya kama Waafrika, hii itatujengea heshima ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishauri Wizara iweke msisitizo kwenye kuendeleza sanaa zinazoundwa kwa utaalamu mkubwa na mikono ya watu wetu kutoka kwenye makabila mbalimbali. Kwa mfano, Wamakonde wako vizuri sana kwenye uchongaji wa vinyago. Kuna makabila mengine yako vizuri sana kwenye ufinyanzi na uchoraji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa kupitia kwenye sanaa hizi tunaweza kuonesha na kuhifadhi tamaduni zetu kwa njia ya kuvutia na ya kipekee. Vilevile sanaa hizi zinaweza kuwa ni chanzo kizuri cha mapato na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Awamu ya Kwanza Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema; "Tamaduni za watu wetu ni hazina ya thamani ambayo inapaswa kulindwa kwa nguvu zote." Kwenye hili, mimi naungana naye kwa 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kulijalia Taifa baraka zake katika nyanja mbalimbali za ustawi wa kijamii, kichumi, kiplomasia, kiuchumi, kisiasa na mshikamano wakati wote kwa kweli ametuepusha na majanga mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na wananchi wa Jimbo langu la Mbulu Mjini kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi ilivyotekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2020 hadi 2025 kwa kweli yapo mambo mengi sana yametekelezwa hususani miradi ya maendeleo iliyoshindikana kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wakuu wote wa Wizara kwa kwa jinsi walivyotekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge na Wajumbe wote kwa jinsi walivyochakata taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa maslahi ya kuibua, kukuza na kuendeleza sekta ya michezo pamoja na kuleta mafanikio katika tasnia ya michezo ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali itoe fedha zote zinazoombwa kwenye bajeti ya Wizara hii muhimu sana, pia tunaiomba Serikali iangalie upya utaratibu wa kuandaa mafunzo ya walimu wa michezo katika shule zetu za sekondari nchini na tunaiomba Serikali iainishe majukumu ya maafisa michezo kwenye Mabaraza ya Madiwani katika halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tayari tuna kamati ya michezo ngazi ya wilaya, Serikali itoe waraka wa kuundwa kwa kamati za michezo katika halmashauri zote kuanzia vijiji, kata na tarafa ili washiriki mpango kazi wa sekta ya michezo wenye kalenda ya michezo kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hivi sasa kuna michezo mingi ya aina mbalimbali Serikali iangalie utaratibu wa kuwepo kwa siku ya vipaji katika kila hamashauri nchini ili viongozi wa vilabu na vyama vya michezo wapate fursa ya kujua vijana wenye uwezo na kuwaendeleza kupitia vilabu vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono kwa 100%.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha ombi langu kwamba katika michezo ya *AFCON* sisi Manispaa ya Iringa kwa hadhi yetu Kimataifa ya kuwa na chifu ambaye ana historia kubwa duniani Chifu Mkwawa, ambaye umaarufu wake ulisababisha Wajerumani kuchukua fuvu lake. Kabila hili bado linatamaduni imara kama mila na desturi, lakini pia tuna ngoma za utamaduni wa kihehe ambayo tunaomba kutumbuiza kwenye mashindano hayo ya *AFCON*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaomba kupata fursa ya kutumbuiza katika michezo ya mpira kama *Ndondo Cup,* lakini sisi pia tuna ligi kama hizo na ikiwezekana pia Iringa inafanya vizuri kwenye mbio za magari, lakini pia tuna mbuga za wanyama za Ruaha, tunaweza kupewa fursa ya kuwakaribisha *Ruaha National Park.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa vituo vya sanaa na utamaduni, kijengwe Iringa kwa kuwa ndiyo lango la utalii Kusini. Hivyo uwepo wa kituo hicho utasaidia kuimarisha utalii Kusini na kuutangaza utalii wetu na utamaduni wetu Kimataifa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Niabu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nianze kwa kumshukuru

Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na kutuwezesha kukutana leo hapa kwenye Bunge lako hili Tukufu kwa ajili ya kujadili hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, inayohusu bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama yangu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani kubwa ambayo bado anayo kwangu kijana wake ya kumsaidia kazi katika sekta ya utamaduni, sanaa na michezo, nikimsaidia Dkt. Damas Ndumbaro. Kutokana na mambo mengi makubwa anayoyafanya Mheshimiwa Rais hapa kwenye michezo tunamwita mwanamichezo namba moja na msanii namba moja kwa vile anasimamia maslahi ya wanamichezo na wasanii wa nchi hii kuliko wakati wowote mwingine kwenye historia ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatuna la kumlipa isipokuwa kumshukuru, kumpongeza na kumsaidia kazi ambayo ametupa na kumwombea Mungu ampe maisha marefu na asimbadilishe moyo wake wa huruma na upendo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, bosi wangu. Dkt. Ndumbaro mimi hata simwiti Waziri tena, namwita mwalimu kila wakati kwa sababu naamini miongoni mwa kazi kubwa anazozifanya pamoja na kuisimamia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, ni kutuingiza darasani wote tuliopo chini yake na kutufundisha mambo mbalimbali kuhusiana na utawala hasa katika sekta hizi ambazo tunazisimamia. Ahsante sana Mheshimiwa Ndumbaro, tunaendelea kujifunza kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Gerson Msigwa na Naibu Katibu Mkuu – Dkt. Suleiman Serera, wakurugenzi na watendaji wakuu wa taasisi zote zilizoko chini ya Wizara hii pamoja na wafanyakazi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Spika na wewe unayelisimamia Bunge hili siku ya leo na Bunge lako

zima kwa ujumla kwa miongozo na kuisimamia Serikali kwa namna ya kirafiki ambayo inalenga tu kuwaletea maendeleo Watanzania na kuwarahisishia maisha, kama ambavyo Mheshimiwa Rais amekuwa akielekeza siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwetu linawakilishwa na Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo. Nichukue fursa hii kipekee kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii dada yangu Mheshimiwa Husna Sekiboko, Makamu Mwenyekiti - Mheshimiwa Mussa Sima na wajumbe wengine wote kwa kazi nzuri wanayoifanya na miongozo na maelekezo wanayotupa. Ninaamini yale ambayo tunalenga kuyafikia kwa usimamizi wa Kamati hii na uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Wizara hii itayafikia maono ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wenzangu wa Muheza kwa kuniunga mkono, kunivumilia ninapokuwa kwenye majukumu ya kitaifa, hali kadhalika kusimama na mimi ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kuiletea maendeleo yanayoistahili Muheza. Niwahakikishie kwamba Muheza wana Mbunge na tutafanya kazi bega kwa bega ili kuhakikisha kwamba yote tuliyokubaliana wakati tunaimba *iyena iyena* tunayafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa japo si kwa umuhimu ninaishukuru familia yangu, mke wangu Helga na watoto wangu Maleeka, Ayan na Imad kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kunitia moyo, kunipenda na kunivumilia ninapokuwa kwenye majukumu ya kimataifa, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye kufafanua hoja kadhaa zilizoletwa na Waheshimiwa Wabunge tangu asubuhi ya leo. Kwanza, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango mingi ya kujenga, ni takribani yote. Katika michango yote hakukuwa na mchango wowote ambao haukuwa wa kujenga ndani yake, ninawashukuru sana kwa hoja zenu Mheshimiwa Sima, Mheshimiwa Cosato Chumi, Mheshimiwa

Esther Malleko, rafiki yangu Bigwa – Kisaki Hamisi Taletale, Mheshimiwa Swalle, Mheshimiwa Khadija Taya na Mheshimiwa Festo Sanga kuhusiana na tozo ya hakimiliki . *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama msanii nimeimba kwa miaka 22 na kusema kweli natamani mazingira ambayo yanatengenezwa sasa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan yangekuwepo enzi hizo wakati naanza kuimba. Naamini maisha yangu yangekuwa tofauti sana na yalivyo leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu yeye ndiye aliyelisema mara ya kwanza kabisa wazo hili la kuanzisha tozo ya hakimiliki mwezi Mei, 2022 alipohudhuria *show* ya msanii maarufu wa *Hip Hop,* Sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais aliielekeza *COSOTA* kuanzisha tozo hii ambayo si mpya duniani na inafanyika kote kwa kufuata mchakato rasmi ambao unatakiwa ikiwemo kuja Bungeni ili kuhakikisha tozo hii inaanzishwa kwa mujibu wa sheria za nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiufupi tozo hii ya hakimiliki inachokifanya ni kutoza kodi ya mara moja vifaa vyote ambavyo vinaweza kurudufu kazi za sanaa vinapoingizwa nchini, yaani vinavyorudufu kazi ya sanaa, lakini wasanii hawawezi kufaidika tena, kwa mfano msanii wimbo wake ukinukuliwa kwenye *cd* na akapewa mtu mwingine, mtu wa kwanza ndiye anakuwa ameununua na msanii amefaidika, lakini mtu anayekwenda kupewa ile *cd* hafaidiki tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kinachofanyika ni vyombo na vifaa vyote ambavyo vinaweza kunukuu/kurudufu kazi za sanaa vinakuwa *charged* tozo ya mara moja vinapoingizwa nchini na fedha ile pamoja na mambo mengine inakwenda kuwasaidia wasanii kwa mfumo wa mirabaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tozo ile ilipoanza kufanya kazi mwezi wa tisa mwaka jana, *TRA* ambao ndio wakusanyaji wetu wameweza kukusanya jumla ya shilingi 636,096,726.40. Kwa ulinganisho mara ya mwisho ambapo mirabaha inagawiwa kwenye nchi hii ilikuwa mwaka 2022 na ilikuwa ni ya miaka mitatu mfululizo yaani mwaka 2019, 2020 na 2021 na fedha zilizogawiwa kwa wasanii zilikuwa shilingi milioni 395.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa miezi sita hii ambayo tozo hii ya hakimiliki imekuwa ikifanya kazi imeweza kukusanya shilingi milioni 636 na ushee namba ambayo ni kubwa sana. Nikuhakikishieni kwa hali ninavyoiona, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge walivyopendekeza hapa kama tutaongeza vifaa tutakuwa na mirabaha ambayo itavunja rekodi kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema ukweli mimi mwenyewe kama msanii ninatamani vifaa vyote ambavyo vinaweza kurudufu kazi za sanaa viweze kuwa *charged* na tozo hii ambayo kwanza ni 1.5% tu, hata mnunuzo mwenyewe hawezi kui-*feel* hiyo *pinch*. Kwa hiyo, tozo hii itawasaidia wasanii, itaongeza ajira na pia inaingiza kodi kwa Serikali na inaongeza mzunguko wa fedha nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaahidi Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwenye jambo hili kwa hisia kubwa kwamba tunafanya kazi kwa kushirikiana na wenzetu Wizara ya Fedha ambao walikubali Sheria ya Fedha Namba Tano irekebishwe mwaka 2023 ili kuongeza kanuni hii ya kuruhusu vifaa hivi kukatwa tozo hii. Kwa hiyo, la kutengeneza kanuni mpya lilikuwa kubwa zaidi kuliko hili la kuongeza vifaa viwili/vitatu kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamependekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie kwamba si muda mrefu mtasikia habari za mabadiliko haya ambayo mmeyapendekeza. Niwahakikishie pia utayari wa kisiasa wa Mheshimiwa Rais unashuka kwetu wasaidizi wake kwenye Wizara zote na tutafanya kama ambavyo Bunge hili linapendekeza kwa faida ya wasanii wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limesemwa ni suala la maadili kwenye kazi za sanaa. Mheshimiwa Mwanakhamis amesema kuhusu usimamizi wa maadili na amelisema kwa hisia kubwa. Mheshimiwa Mwanakhamis halisemi tu hili jambo akiwa humu Bungeni, lakini hata nikikutana naye huko kwenye *corridor* ananitolea mifano ya nyimbo na kunizomea nazo utadhani mimi ndiye niliyeziimba, lakini nimhakikishie kwamba BASATA ipo macho, iko kazini na hatua nyingi zinachukukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri asubuhi, ukurasa wa 96 inaeleza kabisa kwamba; "Baraza limeandaa mwongozo wa uzingatiaji wa maadili katika kazi za sanaa ambao ulizinduliwa rasmi tarehe 3 Novemba, 2023 na kupata idhini ya matumizi. Lengo la mwongozo ni kuhakikisha wadau wenyewe wanashiriki kuhakiki kazi zao wakati wa maandalizi ili tusiwape hasara ya kuzizuia na kuzifungia zitakapotoka zikiwa zimekiuka maadili." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mwanakhamis kwamba na sisi tuna watoto na wadogo zetu, tusingependa nyimbo ambazo zinakiuka maadili ya Mtanzania ziwafikie, hakuna wanachojifunza zaidi ya uhuni. Kwa hiyo, tunafanya kazi kwa karibu kabisa na BASATA ili kuhakikisha kwamba tunalisimamia hili. Adhabu nimezotolewa, zinatolewa na zitaendelea kutolewa. Kama nilivyosema, kwamba BASATA ipo macho na iko kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanya kazi ya kuwaelimisha wasanii kuhusiana na aina ya *content* ambazo zinatakiwa kuwa kwenye sanaa zao. Hali kadhalika tunahakikisha kwamba tunalinda maadili kwa kuchukua hatua kali pale ambapo inabidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililosemwa ni kuhusiana na ujenzi wa *arena*. Mheshimiwa Babu Tale na

Mheshimiwa Esther Matiko wamelisema hili kwa nguvu nyingi. Niwahakikishie kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa malizia.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** ... upembuzi yakinifu umekwishafanyika. Tunazo ekari 12 pale *Tanganyika Packers,* tumeshaanza mchakato wa kupata uwekezaji kupitia utaratibu wa *PPP* ili tujenge *arena* na Babu Tale aache kusumbua waganga. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa namna ambavyo umetuendeshea mjadala wa bajeti yetu kwa siku hii ya leo. Ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kutokana na ripoti yao ambayo wameiwasilisha leo na mapendekezo 11 ambayo wametupatia sisi kama Wizara kwa ajili ya kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba tumepokea mapendekezo hayo na tunaiahidi Kamati kwamba tutayafanyia kazi kama ambavyo tumekuwa tukifanyia kazi mapendekezo waliyotupatia siku za nyuma na hatimaye kupata mafanikio katika kuiendesha Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge 17 wamesimama na kutoa hoja mbalimbali. Hoja nyingi zilikuwa ni kuisifia Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na utendaji wake mzuri ndani ya miaka yake mitatu hasa katika sekta ya utamaduni, sanaa na michezo na sehemu ya pili wametoa ushauri kwa Wizara katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa kwa mikono miwili na kwa unyenyekevu mkubwa Wizara tumepokea ushauri wote ambao Waheshimiwa Wabunge 17 wameutoa katika siku hii ya leo. Tutaufanyia kazi katika kuhakikisha kwamba sekta ya utamaduni, sanaa na michezo inatendewa haki na inasonga mbele. Kuna maeneo mahususi ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyaongelea nami napenda niyatolee ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni uenyeji wa Tanzania katika mashindano ya *AFCON* 2027. Waheshimiwa Wabunge wamepongeza kwa sisi kuwa wenyeji kwa pamoja na jirani zetu Kenya na Uganda. Wametoa rai kwamba tutangaze fursa kwa Watanzania, tujenge miundombinu ya michezo na muhimu zaidi tuwe na timu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunasema Mheshimiwa Rais aliagiza *AFCON* hii ije kwa lengo la kutoa fursa mbalimbali zikiwemo fursa za kiuchumi kwa Watanzania. Watanzania wenye uwezo ndio muda sasa wa kujenga hoteli na ni muda sasa wa kuwekeza katika usafiri ili wageni wetu watakapokuja tuweze kuwapa kile wanachokistahili. Wanaofanya biashara za utalii ndio watakaonufaika zaidi, wanaotoa huduma za afya ndio muda wao sasa, wanaotoa huduma za chakula wajue *AFCON* hii Mheshimiwa Rais ameileta kwa niaba yao, fursa hizo lukuki ni kwa niaba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye miundombinu tumeshaona, tayari mkandarasi yuko *site* kule Arusha kwenye Uwanja wa Samia Suluhu Hassan, uwanja ambao utakuwa ni wa kisasa kuliko uwanja wowote Afrika Mashariki na Kati, uwanja utakaochukua watu 30,000 na uwanja ambao umetengenezwa kwa kuangalia mandhari ya Kitanzania ikiwemo umbile la *Tanzanite* na Mlima Kilimanjaro. Hii ni dhamira safi ambayo Mheshimiwa Rais ameionesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Dodoma tayari mchakato wa kumpata mshauri mwelekezi umeanza, muda wowote atapatikana na uwanja wa Dodoma utajengwa kama ambavyo

ule wa Arusha utajengwa na ndiyo maana bajeti hii katika miradi ya maendeleo imetoka kutoka shilingi bilioni 12 mwaka jana kwenda kwenye shilingi bilioni 250 ili kuhakikisha kwamba viwanja hivi vinaweza kujengwa. Kwa hiyo, kwenye maendeleo ya michezo hatuna shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaunda kamati ya wadau ili kuhakikisha kwamba suala la *AFCON* linanyooka. Hii ni uhakika kwamba Serikali ipo makini. Kamati ile inaongozwa na Mwenyekiti Leodgar Tenga, mtu makini na mzoefu ambaye amebobea katika uongozi na utawala wa michezo na ambaye anaheshimika ndani na nje ya nchi hii, tunaamini atatutendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme kitu kimoja, wengi wana shaka na timu ya Taifa. Niwahakikishie Watanzania kwamba tunaunda timu ya Taifa ambayo itaweza kufanya vizuri katika *AFCON* ya mwaka 2027. Kuanzia sasa tumeshaanza kuwekeza sana katika UMITASHUMTA na UMISSETA. Mheshimiwa Esther Matiko amesema hapa, sasa hivi kuanzia mwaka huu kila UMITASHUMTA itatengeneza timu ya Taifa ya *under 17. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaweka makocha wataalamu wa ndani na nje na si kwenye *football* pekee, tunaongelea michezo yote. Mheshimiwa Esther anajua kwamba mimi ninacheza *basketball* kama yeye na ninacheza *golf* kama Mheshimiwa Tendega. Kwa hiyo, tutaangalia michezo yote, si *football* peke. Pia kwenye UMISSETA tunakwenda kutengeneza timu ya *under 20* inayotokana na UMISSETA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaenda kutengeneza timu ya *under 23* ambayo tutaiweka kwenye makundi matatu, kundi la kwanza ni wachezaji ambao wanacheza kwenye ligi zetu mbalimba za hapa ndani na kundi la pili ni wachezaji ambao wana vipaji, lakini hawapo kwenye ligi. Tumekwishaongea na JKT, tunawachukua hawa wachezaji tunawapeleka kambi mbalimbali za JKT na huko shughuli yao ikawe mpira na kundi la tatu la *under 23* ni wale ambao ni *diaspora* yaani wako nje ya nchi. *Diaspora* wetu wengi wana miaka 22 mpaka 17. Tunataka tuwaunde hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizi timu tatu zinakwenda kulelewa na Serikali chini ya BMT. Hapa tunafanya vitu viwili, kwanza tunakwenda kupata timu itakayoweza kushiriki vizuri *AFCON 2027,* pia tunaanza safari ya Tanzania kwenda Kombe la Dunia mwaka 2030. Katika kampeni ambayo tumeipa jina Twende na Mama Samia *World Cup 2030,* tunaamini miaka hii sita kuanzia sasa mpaka mwaka 2030 wakati Mheshimiwa Rais anamaliza muda wake wa uongozi tunaipeleka Tanzania. Mheshimiwa Rais anakwenda kuacha alama nyingine. Mheshimiwa Esther Matiko tuwe pamoja kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais Samia, imedhamiria kufanya kweli katika michezo na ndiyo maana tumeivuta *AFCON*. Hii miundombinu tunayoijenga itatuwezesha kuwa na mashindano mengine makubwa hapa katikati kabla ya Mheshimiwa Rais hajamaliza muda wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imeongelewa hapa Sera ya Michezo. Ni kipaumbele chetu kufanya mabadiliko ya Sera ya Michezo kwa sababu kwa kiasi kikubwa imepitwa na wakati, lakini muhimu zaidi ambacho nataka tukiweke kwenye hiyo ajenda mpya ya Sera ya Michezo ni ukweli kwamba sasa hivi michezo ni ajira na michezo ni uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, timu zetu ambazo ni za *premier league* hususani Simba, Yanga na Azam zinaajiri wachezaji na zinalipa mshahara mpaka wa shilingi milioni 42. Humu ndani hakuna Mheshimiwa Mbunge anayelipwa mshahara wa shilingi milioni 42 lakini wachezaji sasa hivi wanalipwa hela hiyo. Hii inaamaanisha kwamba michezo ni ajira na michezo ni uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunakwenda kufanya mapitio na mabadiliko ya Sera ya Michezo ili kuhahakikisha kwamba tunaakisi uhalisia wa sasa katika sekta ya michezo, lakini tunatumia sekta ya michezo kutengeneza ajira nyingi zaidi kama ambavyo Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025 imetuagiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge na hasa nimkumbushe Mheshimiwa Esther Matiko kwamba ilani hiyo ndiyo ambayo Watanzania waliichagua na kuipenda mwaka 2020. Kwa hiyo, lazima tuitumikie ili tuweze kufika vizuri zaidi. Nikupongeze Mheshimiwa Esther Matiko kwa kuwa na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, hizi ni dalili nzuri, kwa sababu ukiona mawingu, ujue mvua imekaribia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umakini wa Serikali ya Mama Samia, Serikali ya Awamu ya Sita katika michezo unaonekana pia kwenye juhudi zake za kufufua Mfuko wa Maendeleo ya Michezo ambapo siyo tu ameufufua, lakini pia ameupa fedha asilimia tano zinazotokana na *sports betting*. Sasa unaona dhamira hiyo ya Mheshimiwa Rais kuweza kufufua Mfuko wa Maendeleo wa Michezo. Mfuko huo umefufuka na unafanya kazi kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imesemwa hapa Serikali iwekeze kwenye michezo, lakini niwaambie Serikali iko *serious* kwenye michezo. Tunapoongea sasa hivi, kuanzia Julai Mosi mpaka Aprili mwaka huu timu 15 za Taifa zimewezeshwa kutokana na Mfuko wa Maendeleo wa Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize hapa, siyo timu za soka, ni timu mbalimbali. Moja ya kati ya timu ilikuwa ni timu ya gofu ya wanawake. Mheshimiwa Tendega wewe ni mcheza gofu, hata timu ya gofu imewezeshwa. Sasa hivi timu ya *Tembo Warriors* imewezeshwa iko Misri, timu ya kuogelea imewezeshwa. Tumesema hapa tuwezeshe wanariadha, wanariadha wanawezeshwa na mfuko huu wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ya CCM siyo Serikali ya maneno, ni Serikali ya vitendo. Tunaposema timu za Taifa ni mpaka timu za Taifa za riadha wanawezeshwa na wanaweza kufanya vizuri kama tunavyosema na kama tulivyodhamiria. Mheshimiwa Tunza Malapo amesema hapa kwamba tuna kansa kubwa sana ya uvamizi wa viwanja vya michezo, viwanja vingi vya michezo. Takwimu zinasema 70% ya viwanja vya michezo na

maeneo ya wazi ambayo yametumika kwa watoto kufanyia michezo yamevamiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara na kama Serikali tumeshaongea na Wizara ya Ardhi na tumekubaliana katika sera mpya ya ardhi inayokuja maeneo ya michezo na maeneo ya wazi yanapewa hadhi kama maeneo ya hifadhi. Kwa hiyo, halmashauri haitakuwa na mamlaka ya kutwaa tena maeneo hayo ili tuyalinde, tuweze kuendeleza michezo kwa afya yetu, lakini kwa kujenga ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uwekezaji kwa vilabu, mwaka 2017 kupitia Kanuni ya Sheria ya Michezo, Gazeti la Serikali Na. 422 la mwaka 2017 iliongeza kifungu cha 18(a) ambacho kiliruhusu wawekezaji kuwekeza katika sekta mbalimbali za michezo. Kumekuwa na maneno mengi, kumekuwa na malalamiko mengi na leo Mheshimiwa Festo Sanga ameleta hoja hapa, Serikali hii ni sikivu, tumepokea hiyo hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sababu jambo hili linahusisha wadau wengi, siyo wadau wa soka peke yake hata michezo mingine yote, niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba katika mwezi wa sita tutaitisha kikao na wadau wote wa michezo kuijadili kanuni hiyo na tupate mapendekezo yao, namna bora ya kuboresha kifungu hicho na miongozo hiyo ili uwekezaji katika michezo uwe na tija zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imejipanga na iko kwenye mchakato wa kupata mdhamini wa timu ya Taifa *(Taifa Stars)*. Kampuni moja ya *1XBET* imejitokeza kudhamini timu ya Taifa na siyo tu *Taifa Stars*, hata zile timu ndogo za *under 23*, *under 20* na *under 17*. Tuko kwenye maongezi hayo, tunajadili mkataba huo, tutaupeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na endapo ataupitisha basi tutaweza kusaini mkataba huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imeongelewa kwa uchungu sana hapa kwamba hivi sasa inajitokeza kama mtu mmoja au taasisi moja inamiliki timu zaidi ya moja hivyo kuathiri ushindani wa haki katika michezo. Kwenye hili naomba kutoa agizo kwa Baraza la

Michezo Tanzania, ndani ya wiki moja waniletee taarifa ni timu gani au taasisi gani za michezo zinamilikiwa na zaidi ya mtu mmoja ili tuondoe changamoto hiyo ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeisema na kuleta ushindani wa haki katika sekta ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema hapa Mheshimiwa Pauline Gekul ambaye mimi nilipata bahati ya kufanya naye kazi akiwa kama Naibu Waziri wangu katika Wizara ya Katiba na Sheria. Naheshimu sana uwezo wake wa kufikiri, kuweka hoja mezani na kuwapigania Wana-Babati katika kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja aliyoileta ni ya msingi kwamba *TFF* wamebadilisha mechi ile jana kutoka Babati kwenda Zanzibar na sababu zilizotolewa ni za msingi, hatuwezi kuzibeza lakini hatuwezi kukataa kwamba mabadiliko hayo yameleta athari kwa Wana-Babati na Wana-Manyara. Hivyo, naiagiza *TFF* ikae kikao na uongozi wa Mkoa wa Manyara, wajadili namna ya kupunguza kadhia hizo ambazo Wana-Manyara wamezipata, lakini muhimu zaidi namna ya kuwapa Wana-Manyara mchezo mwingine wowote katika siku za hivi karibuni ili Wana-Manyara na Wana-Babati hawa wafurahie matunda ya juhudi zao katika kujenga uwanja pale Babati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninahakikisha katika tukio litakalopangwa nitajitahidi kama siyo mimi basi Naibu Waziri tuweze kuhudhuria na kuwaunga mkono Wana-Babati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali ya Awamu ya Sita ambayo inatambua nguvu za wananchi na inawaunga mkono. Wana-Babati na Wana-Manyara tunawahakikishia Serikali yenu iko na ninyi katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Watanzania, tumekusudia kabisa kwa dhati kuinua sekta ya michezo, sanaa ya utamaduni kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amesema. Katika sekta ya utamaduni niseme jambo moja tu, Kiswahili ndiyo

lugha ya saba kwa ukubwa duniani, inaongelewa na watu zaidi ya milioni 500, ni lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni lugha rasmi ya *SADC* na ni lugha rasmi ya Maziwa Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nimesema hapa tuna vituo 44 vya kufundisha Kiswahili, vituo 28 vikiwa nje ya nchi. Katika mwaka huu wa fedha tumejipanga kufungua vituo 100 kwa kushirikiana na *diaspora*. Lengo hapa siyo tu kukikuza Kiswahili, lengo pia ni kutoa fursa za ajira kwa Watanzania ambao tunawaita *diaspora*, wako nje wanafanya kazi, wanazalisha na maokoto wanayopata huko nje wanakuja kuwekeza hapa nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tuko na vita yetu ya kuhakikisha kwamba Kiswahili kinakuwa lugha rasmi ya Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini kuiongoza Wizara hii katika muda huu. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe Naibu Spika, Mbunge wa Ilala na mshabiki maarufu sana wa *Simba Sports Club* kwa namna ambavyo umetuongozea Bunge letu kwa siku hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Kamati chini ya uongozi shupavu wa Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima almaarufu Mzee wa Muungano kwa namna ambavyo wametuongoza kufikia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Songea Mjini, hao ndiyo waajiri wangu, hao ndiyo wamenituma kuja huku Bungeni, niwaahidi nitaendelea kuwawakilisha vyema na kutetea maslahi ya Wana-Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa namna ambavyo ananisaidia kutekeleza majukumu katika Wizara hii, ameifanya kazi yangu ya kuwa Waziri kuwa nyepesi zaidi, nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa msaada wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Katibu Mkuu - Ndugu Gerson Partinus Msigwa, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naishukuru familia yangu, ikiongozwa na mke wangu Bi. Flora ambaye toka asubuhi yuko pale kwenye Jukwaa la Spika akiniunga mkono katika kuwatumikia Watanzania, akiambatana na mwanangu Raphael, nawashukuru sana kwa kuja kuungana na mimi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA - KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 96 - Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Recourses Management Division*………..………Sh. 7,405,479,000

**MBUNGE FULANI:** *(Hakutumia kipaza sauti)*.

**MWENYEKITI:** Sijaona orodha hapa, sasa usibishane na Kiti, wewe toa hoja tu, usibishane na Kiti. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, sina lengo la kushika shilingi bali nitataka ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunakua tulishuhudia ni kwa jinsi gani mila na desturi zilivyokuwa zikitumika kuuenzi utamaduni wetu, kwenye matamasha mbalimbali na hasa shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba kwa sasa hivi teknolojia inakua kwa kasi sana kitu ambacho kinasababisha vizazi vyetu, kwa maana ya watoto wetu kupoteza na kutotambua kabisa tamaduni na mila zetu na zaidi kujielekeza kwenye mila na tamaduni za magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikataka kujua na katika wasilisho la Waziri hakuainisha kabisa kuonesha kwamba kuna mkakati madhubuti wa kuendelea kuuenzi utamaduni wetu, tamaduni hizi zikienziwa zinaweza kuwa kama chanzo cha utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba inauenzi utamaduni huu na kuweza kuhifadhi vizazi na vizazi na kuelimisha Watanzania kwa kuanzisha siku maalumu ya tamaduni ya kitaifa ambapo kutakuwa na mashindano ya kitaifa kwa kuunganisha makabila mbalimbali ambayo yataenda kushindana kulingana na

tamaduni zao kwa maana ya ngoma, nyimbo za asili, vyakula vya asili na mambo mengine mengi ili tuweze kuhifadhi historia hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini mkakati wa Serikali kuanzisha siku hii ya kitaifa ambayo itaambatana na maonesho na itakuwa inaadhimishwa kwa kuzunguka mikoa yote Tanzania? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Esther kwa hoja yake hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha bajeti tumetoa ufafanuzi mzuri sana kwamba jambo la utamaduni, mila na desturi zetu kwanza liaanzia kwenye familia. Hivi sasa wengi tunaamini kwamba ni jambo la Serikali, tuanze kwenye familia, tukianza kwenye familia ndipo tunakua nalo. Kila familia ikiwa na maadili na ikajali utamaduni wetu, nchi nayo itakuwa na maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara tunafanya nini? Moja, tumesema kwenye kitabu cha hotuba, tunatoa elimu ya utamaduni, mila na desturi kupitia vipindi vya redio na televisheni. Tumesema bayana kwenye kitabu cha hotuba, tunatumia fedha nyingi kutoa elimu hiyo, inawezekana watu hawasikilizi lakini tunakwenda mpaka kwenye mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu siku ya utamaduni, tunayo, kila mwaka tunafanya tamasha la utamaduni ambalo linashirikisha mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani. Mwaka jana limefanyika mkoani Njombe ambapo masuala ya elimu, mila, ngoma na maonesho mbalimbali yamefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ilishiriki mwaka jana. Kwa hiyo, iliwakilisha Bunge maana yake Bunge lina taarifa hiyo. Mwaka huu yatafanyika Mkoa wa Ruvuma na yatazunguka mikoa yote.

Mheshimiwa Esther ukitaka tutaleta kule Kanda Maalum, nayo tufanye mwaka unaokuja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Kifungu hicho kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…….….….Sh. 598,446,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*………………Sh. 689,951,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*…..Sh.263,699,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*..…....Sh.332,086,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*…………....…………Sh.273,751,000
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*……………….....……….Sh.377,836,000
Kifungu 1008 – *Legal Service Unit*…………………..……..Sh.260,685,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*….....…Sh.318,128,000
Kifungu 6001 – *Culture Development Division*……*Sh.2,708,039,000*
Kifungu 6004 – *Sports Development*……….....……….Sh.3,963,766,000
Kifungu 6005 – *Arts Development Division*………..….Sh.9,935,733,000
Kifungu 7003 – *Information Services*………...........................……….Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. MONICA MWAGA - KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 96 - Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Kifungu 6001 – *Culture Development Division*..........Sh.5,500,788,000
Kifungu 6004 – *Sports Development*………………...Sh. 250,590,000,000
Kifungu 6005 – *Arts Development Division*…………....Sh. 2,100,000,000
Kifungu 7003 – *Information Services*............................................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. MONICA MWAGA - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati yako ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa hoja Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Fungu 96, kwa mwaka 2024/2025 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwamba Bunge likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Wote wameafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hongera sana wewe na Naibu wako, Katibu Mkuu na timu yote ya Wizara yako kwa namna ulivyojieleza na namna ulivyoweza kupata pesa nyingi kama hizi kwa maendeleo ya michezo kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Tunakushukuru sana na tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwekeza zaidi kwenye michezo na tupate wachezaji bora zaidi wa kuwakilisha kwenye vilabu vyetu vya ndani na hatimaye wakapata ajira kwenye vilabu vya nje.

Sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.00 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 24 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*